# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Tatu – Tarehe 4 Aprili, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Leo ni kikao cha tatu cha Mkutano wetu wa Kumi na Tano.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, AJIRA, KAZI VIJANA NA WAZEE NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Taarifa

ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti wa UKIMWI) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU:** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema la kudharau na kulidhalilisha Bunge.

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. STEPHEN KIGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, swali la kwanza linakwenda ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunaanza na Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 19

### Posho za Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI** aliuliza:-

Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa hupata posho shilingi elfu ishirini kwa mwezi kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kazi kubwa wanayoifanya:-

Je, ni lini Serikali itaongeza posho kwa Wenyeviti hao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, tafadhali.

**MHE. MWITA M. WAITARA-NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS-TAMISEMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji katika shughuli za maendeleo. Hata hivyo, kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Mitaa, vitongoji na Wajumbe wa Serikali za Vijiji pamoja na Wajumbe wa Mitaa za mwaka 2014 zilizotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na. 322 na Na. 323, sifa zinazomwezesha mkazi wa

Mtaa, Kijiji na Kitongoji kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Serikali za Mitaa ni pamoja na kuwa na shughuli halali inayomwingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalipa posho ya Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kwa kutumia asilimia 20 ya mapato ya ndani inayorejeshwa na Halmashauri kwenye ngazi za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kiasi hicho kinategemea hali ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri yanayokusanywa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mkakati uliopo ni kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo katika vyanzo vya mapato vilivyopo kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ili kujenga uwezo wa kulipa posho kwa viongozi hao. Aidha, viwango vya posho inayolipwa vinatofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine kulingana na uwezo wa kifedha uliopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Apolinary, swali la nyongeza.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi mara ya pili kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji hawana ofisi za kufanyia kazi. Je, ni lini Serikali itawajengea ofisi za kufanyia kazi?

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa wana wajumbe wanaosaidiana nao katika kazi za utendaji wa kazi za kila siku. Je, ni lini Serikali itawapa posho wale wajumbe?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba ku-*declare* kwamba mimi pia ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa mstaafu. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anaulizia kuhusu Ofisi za Serikali za Mitaa. Sasa hivi tunaenda kwenye Bunge la Bajeti na mpango wa kujenga ofisi za mitaa, vijiji na vitongoji ni mpango wa halmashauri husika. Kwa hiyo kama kuna upungufu mkubwa, tunatarajia kwamba halmashauri hizo na vijiji watakuwa wameweka kwenye bajeti yao ili waweze kuleta kwenye Bunge lako Tukufu iweze kupitishwa na waweze kujenga ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anaulizia juu ya posho, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi ni kwamba posho za wenyeviti na wajumbe wao zinapatikana kwenye halmashauri husika kulingana na vipato vyao. Kwa hiyo kama kuna sababu ya kulipa posho tofauti na ilivyo kwa Wenyeviti wa Mitaa hili nalo pia lilifanyiwa kazi kwenye ngazi ya chini ya halmashauri husika kulingana na mapato yao, kama wana uwezo wataendelea kuwalipa.

Hata hivyo, sifa ya msingi ya kugombea kama ilivyo kwenye uchaguzi mwezi wa Kumi wajumbe hawa na Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji wanajua wanapaswa kufanya kazi ya kujitolea. Kwa hiyo tunatarajia kwamba watafanya kazi kama ambavyo waliamua kugombea na kupata nafasi hizo kama kuna uwezo wa posho watalipana, kama haupo wafanye kazi kama ambavyo waliamua kugombea nafasi hizo.

**SPIKA:** Wizara ya Maji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Allan Joseph Kiula.

Na. 20

**Utafiti wa Vyanzo vya Maji Jimbo la Mkalama**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Pamoja na mambo mengine, Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano imelenga kuongeza asilimia za upatikanaji wa maji vijijini.

(a) Je, lini Serikali itafanya utafiti wa vyanzo vya maji katika Jimbo la Mkalama ili kuwa na uhakika wa rasilimali hiyo?

(b) Je, lini Serikali itatoa fedha za kutosha kuwapatia maji safi wananchi wa Jimbo la Mkalama?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshiimwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, lenye kipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/ 2019, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetenga kiasi cha shilingi milioni 450 kwa ajili ya kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo kame ya Mikoa ya Singida, Mwanza, Tabora na Shinyanga. Utafiti huo utahusisha pia Wilaya ya Mkalama ambapo shilingi milioni 50 zitatumia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utafiti unaotarajiwa kufanyika, Serikali imekua ikitekeleza miradi mbalimbali ya maji katika Vijiji vya Ndunguti, Kinyangiri, Ipuli na pia inatekeleza miradi ya uchimbaji wa visima 24 katika maeneo mengine tofauti. Ili kuhakikisha miradi hii inakamilika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.36 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiula, tafadhali.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa tena nafasi. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza ikiwemo kushukuru ziara ya Makamu wa Rais ambaye alibaini ubadhirifu wa mradi wa Nyahaa, natumaini Wizara inaendelea kulifanyia kazi suala hilo. Swali la kwanza, je, Serikali iko tayari kuongeza fedha za utafiti hususan katika

maeneo yasiyo na miradi mikubwa kama ile iliyopitiwa na maji ya Ziwa Victoria au mkopo wa India ikiwemo Mkalama ili kuweza kupata vyanzo vya uhakika vya maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili je, ni kweli Serikali inatekeleza miradi hiyo na pesa hizo zilitengwa, je ni lini *certificate* za wakandarasi zitalipwa ili kazi iweze kuendelea kwa sababu kazi kule imesimama kutokana na wakandarasi kutokulipwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Allan Kiula Mbunge wa Jimbo la Mkalama kwa kazi nzuri sana anayoifanya katika jimbo lake. Kubwa ni kuhusu suala zima la utafiti, sisi kama Serikali tunautambua umuhimu wa suala zima la utafiti hasa katika sekta ya maji kwa sababu italeta mapinduzi makubwa. Nataka nimhakikishie sisi kama Serikali hatutokuwa kikwazo kuongeza fedha za utafiti kadiri bajeti itakavyokuwa imeruhusu katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na tafiti ambazo zitaruhusu kufanya mapinduzi katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu suala zima la madai ya wakandarasi hususan katika miradi ya jimbo lake. Utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha, tukubali tulikuwa na madai zaidi ya bilioni 88 ya wakandarasi lakini tunashukuru Wizara ya Fedha ijumaa imetupa zaidi ya bilioni 44 kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi *certificate* zao na wametupa *commitment* ndani ya mwezi huu wa nne watatupa bilioni 44 zingine kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi fedha zao.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge apate nafasi ya kuwasiliana na sisi katika kuhakikisha tunamlipa mkandarasi wake ili aweze kuendeleza miradi ya maji katika Jimbo lake la Mkalama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

Na. 21

**Kutenga Bajeti ya Miradi ya Maji– Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Baada ya Serikali kukamilisha usanifu wa mradi wa maji wa vijiji 57 kwenye kata 15 Wilayani Kyerwa:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwenye Bajeti ya 2019/2020 ili miradi hiyo ianze kutekeleza Ilani ya CCM ya kumtua mama ndoo kichwani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la watu wa Kyerwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa vijiji 57 kwenye kata 15, Wilayani Kyerwa ni miongoni mwa miradi mikubwa ya maji ambayo Serikali ina mpango wa kuitekeleza ili kuhudumia wananchi wengi. Mradi huu unalenga kuhudumia watu takriban 282,000 waishio kwenye vijiji hivyo utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa mradi huu umekamilika na imeonekana kuhitaji kiasi kikubwa cha fedha. Hivyo, Serikali inafanya jitihada za kutafuta fedha za kutekeleza mradi huu wa kimkakati *(Strategic Water Project).*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate tafadhali.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa hatua ambayo imefikia kwenye usanifu, lakini niombe kuuliza maswali mawili

ya nyongeza. Kwa sababu ya hali ngumu kwa wananchi wa Jimbo la Kyerwa hasa hasa kwenye vijiji ambavyo vinaguswa na mradi huu, je, Serikali iko tayari kwenye bajeti ya 2019/2020 kutenga angalau kiasi kidogo ili mradi huu uweze kuanza wakati Serikali inaendelea kutafuta hela kubwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna miradi ambayo iko katika Kata ya Mabira, Lukulaijo na kwenye Kijiji cha Kageni miradi hii imeshaanza lakini wakandarasi wamekuwa wakienda kwa kusuasua kwa sababu bado *certificate* zao hazijalipwa. Je, Serikali iko tayari kuwalipa wakandarasi hawa ili waweze kukamilisha hii miradi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Bilakwate, mimi binafsi nilipata nafasi ya kwenda katika jimbo lake, nimeona kazi kubwa anayoifanya katika jimbo lake pamoja na wananchi wake. Sasa nataka nimhakikishie sisi kama Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo kwa wananchi wa Kyerwa kupata maji safi salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Spika, tumefanya tathmini ule mradi ni fedha nyingi sana, lakini tunatambua maji ni uhai na hayana mbadala. Sasa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ukikosa ziwa la mama, la ngombe unanyonya, sisi tupo tayari kufanya njia mbadala katika kuhakikisha wananchi wake wa Kyerwa wanapata maji safi na salama ili waweze kuishi katika eneo lake. Kikubwa na cha msingi kabisa nimwombe kutokana na kuna miradi ambayo inaendelea katika jimbo lake, tukutane baada ya saa saba ili tuangalie ni namna gani tunamsaidia katika kuhakikisha fedha zile tunazilipa wananchi wake waweze kupata maji safi.

**SPIKA:** Ahsante sana lakini ziwa la mama ni tamu.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini. Mheshimiwa Malocha endelea kwa niaba yake.

Na. 22

**Kipande cha Barabara Eneo la Hifadhi ya Katavi**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.n. y. MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI)** aliuliza:-

Tunaishukuru Serikali kwa kutujengea barabara ya lami kutoka Mpanda –Sumbawanga:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kipande cha kilomita 86 eneo la Hifadhi ya Katavi kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga hadi Mpanda yenye urefu wa km 245 ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2009. Serikali kwa kutumia fedha za ndani imekamilisha ujenzi wa kilometa 188.5 kwa kiwango cha lami sehemu za Sumbawanga - Kanazi, (kilometa 75), Kanazi - Kizi - Kibaoni (kilometa 76.6) na Sitalike – Mpanda (kiolometa 36.9)

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua umuhimu wa

kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Katavi kwa barabara ya lami, hivyo ujenzi wa sehemu iliyobaki kati ya Kizi - Lyamba Lya Mfipa - Stalike (kilometa 86) utaanza mara moja kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malocha nilikuona.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Eneo hilo la kilometa 86 ni eneo korofi na liko katikati ya mbuga ya wanyama, wakati mwingine kama gari zinasafiri inafika gari inakwama katikati ya mbuga, jambo ambalo ni hatari kwa raia ambao watakuwa wamepanda basi hilo. Je, Serikali ituambie imetilia umuhimu gani kuliko kusema kwamba itakapopata fedha kwa sababu jambo hili ni muhimu mno kuliko, naomba majibu ya Serikali katika suala hilo, ni lini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nashukuru Serikali kwa ujenzi wa daraja la Mto Momba ambalo linaunganisha mikoa mitatu. Nataka kuuliza baada ya ujenzi wa daraja hilo ni lini sasa Serikali itatenga pesa kwa ajili ya upembuzi yakinifu, kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, barabara inayounganisha mikoa mitatu, Mkoa wa Songwe, Rukwa na Katavi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii ambayo nimetoka kujibu swali lake kwa sababu utagundua kwamba asilimia 65 ya barabara hii baada ya usanifu tulifanya ujenzi na ujenzi ulizingatia maeneo korofi zaidi. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sehemu hii iliyobaki bado ina maeneo changamoto wakati fulani. Sisi kama Serikali tumeendelea kutenga fedha ili kushungulikia

maeneo haya korofi. Hata katika mwaka huu wa fedha unaoendelea tumekuwa na fedha za kutosha kuhakikisha maeneo korofi wakati wowote tunayapa umuhimu wa kuyafanyia matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa eneo hili watakuwa mashuhuda wa kuona kwamba wakati wote tunahakikisha kwamba barabara hii inapitika wakati tunajiandaa kwa ajili ya kuitengeneza katika kiwango cha lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira kwa vile sehemu kubwa ya barabara tumeitengeneza hii sehemu ndogo iliyobaki tutakwenda kuitengeneza kwa kiwango cha lami. Tumeweka mapendekezo katika bajeti hii inayokuja kama Bunge lako litatupitishia na Serikali ikapata fedha tutakwenda na hatua ya mwisho kuikamilisha barabara hii.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu barabara hii inayopita katika Daraja la Mto Momba, Mheshimiwa Mbunge anafahamu na nimetembelea eneo hili, ujenzi wa daraja umekamilika kwa sehemu kubwa na sasa tunaweza kupita mto huu. Mheshimiwa Mbunge anafahamu barabara hii ni ndefu sana ukitoka Momba mpaka uje Majimoto na mimi nimeliipita. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeiweka kwenye mpango wetu mkakati kwa maana ya sasa kufanya usanifu baada ya kukamilisha sehemu ya Mto Momba ambayo ni korofi ili sasa tuweze kuitazama kwa ajili ya kuitengeneza katika kiwango cha lami. Kwa hiyo, tuvute subira Serikali ikipata fedha tutakamilisha barabara hii.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Susan Kiwanga.

Na. 23

**Ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Mlimba – Madeke**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Barabara kutoka Ifakara hadi Mlimba mpakani mwa Mkoa wa Njombe (Madeke) ni kero kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Mlimba:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ifakara – Mlimba – Taweta - Madeke yenye urefu wa kilometa 220.22 inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Njombe katika Kijiji cha Madeke. Barabara hii ni ya changarawe na udongo ambapo sehemu kubwa inapitika vizuri isipokuwa maeneo yanayohitaji kuimarishwa ili nayo yapitike wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imeshakamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara kutoka Ifakara Kihansi (km 126) ikiwa ni hatua ya awali ya kuanza mipango ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Hatua hiyo itawezesha kuunganisha sehemu ya barabara hiyo na kipande cha barabara ya lami yenye urefu wa kilometa 24 kilichojengwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba. Kufuatia kukamilika kwa hatua hiyo, Serikali imeanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 kipande kilichobaki kati ya Mlimba hadi Taweta

kimewekwa kwenye mpango ili kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Serikali itaendelea kutenga fedha za matengenezo ili barabara hii iweze kupitika wakati wote wa mwaka wakati fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami zinatafutwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga, tafadhali.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimepokea majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa upembuzi yakinifu umeshafanyika kuanzia Ifakara mpaka Kihansi; na kwa kuwa barabara hiyo hakuna kabisa sehemu ambayo unaweza ukapata changarawe kwa sababu upande wa kulia ni bonde oevu na upande wa kushoto ni Udzungwa. Je, Waziri husika yupo tayari kuongea na Waziri mwenzake wa Maliasili ili wakandarasi hao wanaotengeneza hiyo barabara ingawaje kwa kiwango cha changarawe waweze kupata kifusi au moramu katika eneo ambalo watalitenga kwenye eneo la Udzungwa? Nasema hivyo kwa sababu ni udongo tupu na hii barabara inabomoka kwa muda mfupi sana na wananchi wanapata tabu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa pale Mlimba Mjini, *TARURA* kwa bajeti zao wanasema wataweka angalau kilometa 1 kiwango cha lami lakini kuna mita 500 za *TANROADS* zinazopita kwenda pale mjini. Je, *TANROADS* sasa wako tayari kwenye ile barabara yao pale Mlimba Mjini hizo mita 500 kuunganisha na ile lami ya Kihansi, Mlimba Mjini ili *TARURA* wanapofanya kazi yao kusiwepo na kipande kingine cha vumbi pale Mlimba Mjini, kwenye mji wa Mlimba?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Mbunge, Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda

kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Kiwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu tulipata nafasi ya kutembelea barabara hii na changamoto ya kupata changarawe ili kuifanya barabara iwe bora zaidi tuliizungumza na tulikuwa tumefanya mazungumzo na wenzetu upande wa Maliasili. Hata hivyo, kwa vile amelisema tena hapa nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya mazungumzo ili tuweze kupata kibali cha kifusi ambacho kitafanya barabara hii matengenezo yake yawe imara.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la kipande cha mita 500, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nalichukua ili niweze kulielekeza upande wa wenzetu wa *TANROADS,* Mkoa wa Morogoro ili kilometa 1 itakayotengenezwa na *TARURA* iwe na muunganiko mzuri na hizi mita 500, hii nimelichukuwa.

**SPIKA:** Ahsante. Huo ndiyo mwisho wa kipindi cha maswali, leo tuna ratiba ya mambo mengi sana, ndiyo maana inabidi tujaribu kuchunga muda kidogo. Tutakuwa na taarifa za Wenyeviti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Kamati ya UKIMWI, Kamati ya Bajeti na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani mara tu baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, inabidi niokoe muda kadri inavyowezekana. Wageni wetu nitawatangaza baadaye kidogo endeleeni kuwa nasi. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

## TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUDHARAU NA KUDHALILISHA BUNGE LINALOMKABILI MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB)

**SPIKA:** Hoja za Kamati, naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na

Madaraka ya Bunge, Mwenyekiti tafadhali. Karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa watakaotaka kuchangia hoja hiyo nipate majina mapema vinginevyo nitafunga dirisha, Mwenyekiti una robo saa tu ya kuwasilisha.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hii ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu suala la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema la kudharau na kudhalilisha Bunge.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 2 Aprili, 2019, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema alipokuwa akichangia Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Halima James Mdee aliyekuwa amepatikana na hatia mbele ya Kamati ya Maadili kwa kufanya kitendo cha kudharau, kukejeli na kudhalilisha Bunge, alinukuliwa pamoja na mambo mengine akisema yafuatayo, nanukuu: ***"****Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa vipindi viwili, nathibitisha Bunge hili ni dhaifu."* Mwisho wa kumnukuu Mheshimiwa Lema.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kauli hiyo, mamlaka ya Kiti yaliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 74(1)(a) na (b) na Kanuni ya 4(1)(a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ilielekezwa kuwa Mheshimiwa Lema afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kuhojiwa kuhusiana na tuhuma hizo. Mheshimiwa Lema aliitwa na aliitikia wito.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Mheshimiwa Godbless Lema kufika kwenye Kamati alitoa ombi la ruhusa ya kumleta Wakili. Kamati ilitafakari na kuona kuwa Mheshimiwa Lema ni Mbunge mzoefu wa vipindi viwili na pia aliwahi kuhojiwa na Kamati hii anajua fika kuhusu haki ya kuambatana na Wakili wake lakini hakuja naye. Kamati ilijadili na kuona kuwa Shahidi hakuwa amepanga kuwa na Wakili.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Kamati ilipata mashaka juu ya uaminifu wa Shahidi kwani mnamo tarehe 9 Machi 2016, aliwahi kuiomba Kamati impe muda wa kutafuta Wakili kuhusiana na tuhuma dhidi yake za kufanya vurugu Bungeni siku ya tarehe 27 Januari 2016. Siku hiyo Kamati ilikubali ombi lake na ilimtaka afike tarehe 11 Machi 2016. Kitu cha ajabu ni kuwa Mheshimiwa Lema hakurejea kwenye Kamati na wala hakutoa sababu ya kushindwa kufika. Kwa hali hiyo, Kamati ilikosa imani naye na iliamua kuyakataa maombi yake.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mahojiano Mheshimiwa Lema aliieleza Kamati kuwa anaunga mkono maoni yaliyotolewa na Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Mheshimiwa Halima James Mdee ambao Kamati iliwakuta na hatia kwa kulidhalilisha Bunge. Kwa hali hiyo, Kamati iliona naye ametenda kosa hilo kwa mujibu wa Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura 296 pamoja na Kanuni ya 74(1)(a) na (b) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi wake, Kamati ilirejea Katiba, Sheria, Kanuni, maamuzi mbalimbali ya awali ya Bunge pamoja na *video* iliyomrekodi Mheshimiwa Lema akizungumza. Kamati ilijiridhisha kuwa Mheshimiwa Lema alitamka kwa makusudi maneno kuwa Bunge ni dhaifu akilenga kulidhalilisha Bunge. Kamati ilitilia maanani na kuutafakari kwa kina ushahidi wa Mheshimiwa Lema mbele ya Kamati ikiwemo wa kukiri kosa, Kamati iliona Mheshimiwa Lema ametenda kosa la kudharau na kudhalilisha Bunge hivyo ilimtia hatiani. Kitendo alichofanya Mheshimiwa Lema ni cha kupigwa vita ili kulinda hadhi na heshima ya Bunge ambalo ni chombo kinachowakilisha wananchi tunaowaongoza.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema (Mb) kwa Kitendo cha kudharau na kudhalilisha Bunge.

KWA KUWA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA, mnamo tarehe 2 Aprili, 2019 Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema alipokuwa akichangia Hoja ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri lililokuwa linamkabili Mheshimiwa Halima James Mdee alinukuliwa akilieleza Bunge kuwa yeye ni Mbunge wa vipindi viwili na anathibitisha kuwa Bunge hili ni dhaifu;

NA KWA KUWA, Kiti kwa mamlaka yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kilimpeleka Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa ajili ya uchunguzi wa kauli yake iliyoonekana kudharau, kufedhehesha, kudhalilisha na kushusha heshima ya Bunge kwa kuliita dhaifu;

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa siku ya tarehe 3 Aprili, 2019 kufanya uchunguzi wa shauri hili ambapo ilibaini kuwa Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kwa kutamka maneno yenye kudharau mamlaka ya Spika, kukejeli na kudhalilisha heshima ya Bunge na kudhalilisha Bunge na shughuliza Bunge katika kipindi ambacho Bunge lilikuwa linajadili kuhusu tuhuma za namna hiyohiyo zilizofanywa na Mheshimiwa Halima James Mdee;

NA KWA KUWA, kwa kuzingatia kuwa Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema hii ni mara yake ya pili kuitwa mbele ya Kamati ya Maadili ambapo mara ya kwanza alitiwa hatiani kwa makosa ya kudharau Bunge na mamlaka ya Spika kwa kufanya vurugu Bungeni tarehe tarehe 27 Januari, 2016 na alipewa adhabu kwa kusimamishwa kuhudhuria vikao vyote vya Mkutano wa Tatu wa Bunge kuanzia tarehe 30 Mei, 2019 siku ambayo Azimio hilo lilitolewa;

NA KWA KUWA, kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema amekutwa na hatia ya kuvunja Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kwa kutoa kauli za kudharau na kudhalilisha Bunge ambapo Kamati imemtia hatiani;

NA KWA KUWA, akiwa mbele ya Kamati Mheshimiwa Godbless Lema hakujutia kosa lake na wala kuomba radhi kwa kitendo chake cha kudharau Bunge bali aliendelea kusisitiza kuwa Bunge hili ni dhaifu jambo ambalo linadhihirisha kuwa alidhamiria kutenda kosa hilo la kudharau mamlaka ya Bunge na Wabunge;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema ambaye ni Mbunge mkongwe kwa vipindi viwili anao uelewa mkubwa wa taratibu za kikanuni za namna Bunge linavyoendeshwa, hivyo kwa kitendo alichofanya ni ukosefu wa heshima kwa mamlaka ya Bunge na Wabunge na kutokuwa na uwajibikaji wa pamoja;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema asimamishwe kuhudhuria Mikutano mitatu ya Bunge kuanzia tarehe ya Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia sehemu hiyo;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema Mbunge asimamishwe kuhudhuria Mikutano mitatu ya Bunge kuanzia tarehe ya Azimio hili

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba linakubaliana na kupitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

# TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUDHARAU NA KUDHALILISHA BUNGE LINALOMKABILI MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri linalomkabili Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) la kudharau, kukejeli, kufedhehesha, kudhalilisha na kulishushia heshima Bunge kwa lugha isiyostahili, kinyume na Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 *[The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296].*

1.2 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 2 Aprili, 2019 kwa Mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, uliiagiza Kamati ninayoiongoza kukutana kwa ajili ya kushughulikia suala la tuhuma za kudharau, kukejeli, kufedhehesha, kudhalilisha na kulishushia Bunge heshima linayostahili zinazomhusu Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb). Katika maelekezo hayo uliitaka Kamati kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hizo na kutoa ushauri.

## 2.0 CHANZO CHA SHAURI LINALOMKABILI MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB)

2.1 **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 2 Aprili, 2019 katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge na wakati wa mjadala wa Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge unaendelea, kuhusu shauri la kudharau na kudhalilisha Bunge lililokuwa linamkabili Mhe. Halima James Mdee (Mb), Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) aliruhusiwa kuchangia, alisimama na kuanza kutoa mchango wake. Katika mchango huo alinukuu maneno ya

Mhe. Halima James Mdee yaliyompongeza Prof. Mussa Assad Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ifuatavyo:- **Nukuu**

***"...kitendo cha CAG cha kusema kwamba hali sio nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni kitendo cha kijasiri na nina imani kwamba wanaoongoza huo muhimili watakuwa wavumilivu hawatafikiria kumuita kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu, kwa sababu kweli ni dhaifu. Roho ya mwenendo wa nchi unategemea uimara wa Bunge, sasa amesema Bunge ni dhaifu ni kweli na mimi kama Mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo".***

Baada ya kunukuu maelezo hayo, Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) aliendelea kueleza kuwa, yeye amedumu Bungeni kwa vipindi viwili na kuwa anathibitisha kwamba Bunge ni dhaifu. Kwa maneno yake alieleza:-**Nukuu**
***"Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa vipindi viwili nathibitisha Bunge hili ni dhaifu".***

Kiti kilielekeza kuwa, mjadala uliokuwepo Bungeni ulihusu kitendo cha Mhe. Halima James Mdee (Mb). kudharau na kudhalilisha Bunge. Kiti kiliendelea kueleza kuwa, kwa kuwa na yeye ameeleza kuwa anao uthibitisho kuwa Bunge ni dhaifu anatakiwa afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili ifanye uchunguzi wake.

2.2 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelekezo hayo ya kiti, hivyo, Mhe. Godbless Jonatahan Lema (Mb) alipatiwa Hati ya Wito kwa mujibu wa Kifungu cha 15 na 16 cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296 ili afike mbele ya Kamati kujibu tuhuma zinazomkabili. Hati ya Wito ilimtaka Shahidi kutoa maelezo juu ya kuhusika au kutohusika kwake na tuhuma zinazomkabili na kama ikibainika kuwa alihusika aeleze ni kwa nini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) na 33(1) na (3) vya Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296. Vifungu hivyo vinakataza kufanya kitendo ambacho Mhe. Godbless Lema alituhumiwa kufanya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA SHAURI

3.1 **Mheshimiwa Spika,** katika Waraka wako ulioelekeza kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ulirejea Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Kwa urahisi wa rejea Kanuni inaeleza: **Nukuu**

***4 (1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo:-***

(a) ***Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya Haki,Kinga na Madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika***;

(b) ***Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika.***

3.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Hati ya Wito iliyotolewa kwa shahidi, Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) alitakiwa kueleza kuhusu kitendo chake cha kukiuka masharti ya Kifungu cha 26(e) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura, 296. Kifungu hicho kinaeleza kwamba, mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo atafanya kwa makusudi kitendo chochote chenye kudharau shughuli za Bunge au mtu anayeendesha shughuli za Bunge.

3.3 **Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia suala hili, Sekretarieti ilirejea nyaraka mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(ii) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura ya 296;

(iii) Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016;

(iv) Picha ya *video* inayomuonesha Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) na Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*; na

(v) Hukumu za Mashauri mbalimbali yaliyowahi kuamuliwa na Bunge *(case law).*

## 4.0 HOJA ZA MSINGI *(ISSUES)*

4.1 **Mheshimiwa Spika,** ili Kamati iweze kufanya uchambuzi wa malalamiko yaliyotolewa ilijielekeza katika kupata majibu ya maswali yafuatayo:

(a) Je, ni kweli kwamba Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) alitamka kauli zilizolalamikiwa kukejeli, kudharau, kufedhehesha, kudhalilisha na kulivunjia Bunge heshima?

(b) Ikiwa alitamka kauli hizo, je, Kauli hizo zinaonesha kudharau, kukejeli, kufedhehesha, kudhalilisha na kulishushia Bunge heshima linayostahili; na

(c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?.

4.2 **Mheshimiwa Spika,** tarehe 3 Aprili, 2019 Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) alifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kujibu tuhuma zilizokuwa zimeainishwa kwenye Hati ya Wito aliopewa. Mhe. Lema alifika mbele ya Kamati kwa maelekezo ya kiti yaliyotolewa tarehe 3 Aprili 2019 ukumbini ambapo Mhe. Lema alikuwepo na alitekeleza maelekezo kama alivyotakiwa. Aidha, alipofika mbele ya Kamati Mhe, Lema aliieleza Kamati kuwa alikuwa tayari kutoa utetezi wake.

4.3 **Mheshimiwa Spika,** mara baada ya Mh. Godbless Lema kufika kwenye Kamati alitoa ombi la ruhusa ya kumleta wakili. Kamati ilitafakari na kuona kuwa, Mhe. Lema ni Mbunge mzoefu wa vipindi viwili na pia aliwahi kuhojiwa na Kamati hii anajua fika kuhusu haki ya kuambatana na Wakili wake lakini hakuja naye. Kamati ilijadili na kuona kuwa Shahidi hakuwa amepanga kuwa na wakili.

4.4 **Mheshimiwa Spika,** Halikadhalika, Kamati ilipata mashaka juu ya uaminifu wa Shahidi. Mnamo tarehe 9 Machi 2016 aliwahi kuiomba Kamati impe muda wa kutafuta wakili kuhusiana na tuhuma dhidi yake za kufanya vurugu Bungeni siku ya tarehe 27 Januari 2016. Siku hiyo Kamati ilikubali ombi lake na ilimtaka afike tarehe 11 Machi 2016. Kitu cha ajabu

ni kuwa, Mhe. Lema hakurejea kwenye Kamati na wala hakutoa sababu ya kushindwa kufika. Kwa hali hiyo, Kamati ilikosa imani naye na iliamua kuyakataa maombi yake.

4.5 **Mheshimiwa Spika,**
Katika mahojiano mbele ya Kamati Shahidi alihojiwa iwapo alitamka maneno yanayolalamikiwa kudharau, kukejeli, kufedhehesha, kudhalilisha na kulishushia Bunge heshima inayostahili. Mhe. Lema alikiri kuwa ni kweli alitamka kuwa alieleza yafuatayo:-

***"Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa vipindi viwili nathibitisha Bunge hili ni dhaifu".***

4.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliangalia ushahidi wa video iliyochukua matukio ya ukumbini inayomuonesha Mhe. Lema akichangia. Aidha, Kamati ilipitia Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. Hivi vyote vilimuonesha na kumnukuu Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb), wakati akichangia kuhusu Shauri la Mhe. Halima James Mdee (Mb) la kudharau na kulidhalilisha Bunge. Katika maelezo hayo Mhe. Lema alionekana na kunukuliwa akisema kuwa yeye ni Mbunge wa vipindi viwili na anathibitisha Bunge hili ni dhaifu.

4.7 **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijiridhisha bila kuacha shaka yoyote kwamba Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) alitamka maneno hayo. Kamati ilizingatia kukiri kwake, *Hansard* na ushaidi wa *video*.

4.8 **Mheshimiwa Spika** baada ya kujiridhisha kuwa Mhe. Godbless Jonathan Lema alitamka kuwa ***Bunge ni dhaifu.*** Kamati ilijelekeza katika kujibu hoja ya pili kwamba, ikiwa alitamka kauli hizo, je! Kauli hizo zinaonesha dharau, kejeli, kufedhehesha, kudhalilisha na kulishushia Bunge heshima inayostahili?.

4.9 **Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi ushahidi huu, Kamati ilifanya utafiti kwa kuangalia maana ya neno **"dhaifu"**. Katika Kamusi Kuu ya Kiswahili ambayo imeidhinishwa na Baraza la Kiswahili Tanzania (TIE) na Baraza la Kiswahili la Taifa

Kenya (KICD) iliyotafsiri neno “**dhaifu”** kuwa ni ***isiyokuwa thabiti kiafya; nyonge; yenye kutokuwa na mashiko; goigoi; legevu; hafifu; isiyo imara, sahihi, thabiti; kiumbe kama vile mtu au mnyama asiye na nguvu; dhuli****.*

4.10 **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, Kamusi ya Visawe: *Swahili Dictionary of Synonyms (East African Educational Publishers* Toleo la 2014) imetafsiri neno” **dhaifu**” kuwa ni ***hafifu, nyonge, gonjwa; goigoi; legevu; dhalili; hakiri; fifi; duni; ghofi; uchwara; fisadi; tule; baya; ovu; shakii; harabu; thakili; potovu; chui; jahili; katili.***

4.11 **Mheshimiwa Spika**, katika tafsiri zote hizo neno dhaifu ni neno linalodhalilisha na kushusha hadhi ya mtu, kitu au taasisi inayolengwa. Tafsiri hizo zinatoa maana na mtazamo hasi kwa jambo, kitu, mtu at taasisi inayozungumzwa.

4.12 **Mheshimiwa Spika**, Shahidi alisisitiza katika ushahidi wake kuwa alipopewa nafasi ya kuzungumza alikatishwa na kiti isivyo halali na kuwa, hakupewa muda wa kuendelea na mchango wake. Alieleza zaidi kuwa, angepewa fursa hiyo angeweza kulishawishi Bunge kukubaliana naye kuwa Mhe. Mdee hakutenda kosa kwa maneno aliyotumia na pengine Bunge lingeweza kumuunga mkono juu ya hoja yake kuwa Bunge ni dhaifu.

4.13 Aidha, katika kusisitiza maelezo yake alieleza kuwa kiti kilikiuka Kanuni ya 5 ya Kanuni za Bunge kwa kuwa kiti kilipaswa kutumia Kanuni ya 63 na 64 ambayo kama ingetumiwa ingewezesha kumtaka Mhe. Lema afute au athibitishe kauli yake.

4.14 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari juu ya ushahidi wake na kuona kuwa shahidi huo hakutafsiri Kanuni kwa usahihi. Kanuni ya 63 inayoongelea kusema uongo Bungeni na 64 inayokataza baadhi ya matendo kufanyika hazingeweza kutumika katika suala lake.

4.15 **Mheshimiwa Spika**,Katika kutafakari hoja hiyo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 5, 72 na 74 ya kwamba kanuni

hizo zinakipa kiti mamlaka ya kusimamia masuala ya utaratibu Bungeni na kuwa uamuzi wa Kiti kuhusu jambo lolote la utaratibu ni wa mwisho. Vilevile Kanuni ya 74 inakipa Kiti mamlaka ya kuelekeza Mbunge yeyote anachangia kwa namna isiyofaa kupelekwa kwenye Kamati ya Maadili.

4.16 **Mheshimiwa Spika**, Katika utetezi wake Shahidi alipoulizwa ni kwa nini hakuomba radhi baada ya kuliita Bunge dhaifu, aliendelea kusisitiza kuwa hakupewa fursa ya kumalizia mchango wake aliokuwa akiendelea nao. Katika kutafakari ushahidi huu, Kamati ilizingatia kuwa kama angekuwa na nia ya kuomba radhi angeweza kufanya hivyo mapema. Kamati iliona kuwa Shahidi hakuwa na nia ya kuomba radhi.

4.17 **Mweshimiwa Spika,** Maelezo ya Shahidi kuwa Kiti hakikumtendea Haki kwa kutomruhusu kuendelea na mchango wake. Kamati ilijielekeza kwenye Kanuni za Bunge ambapo ilirejea Kanuni ya 72 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ambayo imetoa mamlaka kwa Kiti kusimamia shughulli za Bunge kwa namna kitakavyoona inafaa.

4.18 **Mheshimiwa Spika**, shahidi aliendelea kujitetea kuwa msimamo wa Mhe. Halima James Mdee (Mb) kwamba Bunge ni dhaifu ni msimamo wa Kambi ya upinzani hivyo alieleza kuwa asingeweza kwenda kinyume na msimamo wa Kambi. Kamati iliona kuwa ushahidi huo pia hauna mashiko kwa sababu utaratibu wa kuwasilisha maoni ya Kambi upo kwa mujibu wa Kanuni, na Mhe. Gobless Jonathan Lema (Mb) wakati wa mjadala huo hakuwa anachangia kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

4.19 **Mheshimiwa Spika,** baada ya kuchambua ushahidi huo, Kamati inaona kuwa Shahidi amekiuka Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 na Kanuni ya 74 (1)(a) na (b) ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 26 kinaeleza: **Nukuu:**

"**26.** ***Any person shall be guilty of an offence who-***

***(a)N/A***
***(b)N/A***
***(c)N/A***
***(d)N/A***

***(e) does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or to any person presiding at such proceedings commits an offence".***

4.20 **Mheshimiwa Spika,** katika kujibu hoja kwamba Endapo ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake? Kamati ilizingatia masharti ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kinachotoa mamlaka kwa Bunge kupitia Azimio kutoa adhabu kwa Mbunge anayepatwa na hatia ya kukiuka masharti ya Kifungu cha 26.

4.21 **Mheshimiwa Spika** Adhabu zinazotajwa chini ya Kifungu hiki ni kumuonya au kumsimamisha Mbunge husika kufanya shughuli za Bunge kwa kipindi kitakachoamriwa na Bunge. Kifungu hicho kinaeleza:

***"33-(1) Where any Member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such Member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine.***

***Provided that, such period shall not extend beyond the last day of the the session next following that which the resolution was passed or of the session in which the resolution is passed as the Assembly may so determine".***

## 5.0 UZOEFU WA BUNGE KATIKA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA KUDHARAU BUNGE

**Mheshimiwa Spika,** Bunge hili limewahi kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko ya kudharau Bunge ambapo Kamati ya Maadili ilifanyia kazi na kupendekeza na hatimaye Bunge kutoa Uamuzi. Miongoni mwa mashauri hayo ni:

**SHAURI DHIDI YA MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB)**

5.1 **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 2 Januari, 2019 Mhe. Halima James Mdee (Mb) alinukuliwa na alisikika katika mitandao ya kijamii akipongeza kauli za Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika pongezi hizo Mhe. Halima James Mdee alitumia lugha iliyolalamikiwa kuwa ni dharau na yenye kudhalilisha Bunge kinyume na kifungu cha Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 *[The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296 R.E 2015].*

5.2 **Mheshimiwa Spika,** Pongezi za Mhe. Mdee zilitokana na kauli za Prof. Mussa Assad akiwa Nchini Marekani ambapo alisikika na kuonekana kwenye chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa alipokuwa anahojiwa na mtangazaji wa chombo hicho Ndg. Arnold Kayanda. Katika majibu yake kwenye mahojiano hayo, alitoa kauli zinazoashiria kulidharau na kulidhalilisha Bunge.

5.3 **Mheshimiwa Spika,** Katika katika maelezo yake Mhe. Mdee alitamka maneno yafuatayo:-

***"...kitendo cha CAG cha kusema kwamba hali sio nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni kitendo cha kijasiri na nina imani kwamba wanaongoza huo <u>mhimili watakuwa wavumilivu hawatafikiria kumwita kwenye kamati ya maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu, kwa sababu kweli ni dhaifu... roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge...sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli,</u> na mimi kama MBunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo''.***

Mhe. Halima James Mdee (Mb) alifika mbele ya Kamati na alikiri wazi kuwa alitamka maneno hayo yaliyolalamikiwa na Bunge. Kamati ilimtia hatiani na kumpa adhabu ya kumsimamisha kuhudhuria vikao vya Mikutano miwili ya Bunge.

## 6.0 HITIMISHO

6.1 **Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kukushukuru kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kutuamini na kutupa jukumu hili. Napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge na kuhakikisha kuwa heshima yake inalindwa.

6.2 **Mheshimiwa Spika,** kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa Shauri hili. Wajumbe walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe Emmanuel A. Mwakasaka (Mb) – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb) -M/Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani (Mb) - Mjumbe
4. Mhe. Margareth Simwanza Sitta (Mb) - "
5. Mhe. George Malima Lubeleje (Mb) - "
6. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb) - "
7. Mhe. Adadi Mohamed Rajab (Mb) - "
8. Mhe. Almas Athuman Maige (Mb) - "
9. Mhe. Ruth Hiyob Mollel (Mb) - "
10. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha (Mb) - "
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi (Mb) - "
12. Mhe. Allan Joseph Kiula (Mb) - "
13. Mhe. Prosper Joseph Mbena (Mb) - "
14. Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb) - "
15. Mhe. Omar Mohamed Kigua (Mb) - "
16. Mhe. Rose Kamili Sukum (Mb) - "
17. Mhe. Innocent Bilakwate (Mb) - "
18. Mhe. Ali Hassan Omari King (Mb) - "

6.3 **Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kipekee, nawashukuru Ndg. Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa ushauri na ufafanuzi

walioutoa kuhusiana na hoja mbalimbali za kisheria katika shauri hili.

6.4 **Mheshimiwa Spika**, vile vile, nawashukuru Ndg. Seraphine Tamba, Makatibu wa Kamati, Ndg. Joyce Chuma, Mwandishi Mwendesha Ofisi na Ndg. Imelda Ntimba Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati pamoja na Ndg. Mohamed Salum, Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge na Ndg. Munubi Kajobi kutoka Kitengo cha TEHAMA kwa kurekodi kumbukumbu za vikao vyote vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**
3 Aprili, 2019

**AZIMIO LA BUNGE KUHUSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI YA MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB) KWA KITENDO CHA KUDHARAU NA KUDHALILISHA BUNGE**

---

*[Limetolewachini ya Kifungu cha 33(1)] cha Sheria ya Kinga, MadarakanaHakiza Bunge (The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R.E. 2015] na Kanuni ya 54(1)(2)(3) na 74(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

---

**KWA KUWA,** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwakwamujibu wa Katiba, Sheria na KanunizaKudumuza Bunge ambazozilitungwa na Bunge lenyewekwaajili ya kuliongozakatikakutekelezashughulizake;

**NA KWA KUWA,** mnamo tarehe 2 Aprili, 2019 Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) alipokuwa akichangia Hoja ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri

lililokuwa linamkabili Mheshimiwa Halima James Mdee(Mb) alinukuliwa akilieleza Bunge kuwa yeye ni Mbunge wa vipindi viwili na anathibitisha kuwa Bunge hili ni dhaifu;

**NA KWA KUWA,** Kiti kwa Mamlaka yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kilimpeleka Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa ajili ya uchunguzi wa kauli yake iliyoonekana kudharau, kufedhehesha, kudhalilishana kushusha heshima ya Bunge kwa kuliita dhaifu;

**NA KWA KUWA,** Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaasiku ya tarehe 3Aprili, 2019 kufanya uchunguzi wa shauri hili ambapo ilibaini kuwa, Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kwa kutamka maneno yenye kudharau mamlaka ya Spika, kukejeli na kudhalilisha heshima ya Bunge na kudhalilisha Bunge na shughuli za Bunge katika kipindi ambacho Bunge lilikuwa linajadili kuhusu tuhuma za namna hiyo hiyo zilizofanywa na Mhe Halima James Mdee (Mb);

**NA KWA KUWA,** kwa kuzingatia kuwa Mhe. Godbless J. Lema (Mb) hii ni mara yake ya pili kuitwa mbele ya Kamati ya Maadili ambapo mara ya kwanza alitiwa hatiani kwa makosa ya kudharau Bunge na Mamlaka ya Spika kwa kufanya vurugu Bungeni tarehe 27 Januari, 2016 na alipewa adhabu kwa kusimamishwa kuhudhuria vikao vyote vya Mkutano wa Tatu wa Bunge kuanzia tarehe 30 Mei, 2019 siku ambayo Azimio hilo lilitolewa;

**NA KWA KUWA**, kwa mara nyingine tena Mhe. Godbless Jonathan Lema amekutwa na hatia ya kuvunja kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hakiza Bunge, Sura ya 296 kwa kutoa kauli za kudharau na kudhalilisha Bunge ambapo Kamati imemtia hatiani.

**NA KWA KUWA,** akiwa mbele ya Kamati Mhe.Godbless Lema hakujutia kosa lake na wala kuomba radhi kwa kitendo chake cha kudharau Bunge bali aliendelea kusisitiza kuwa Bunge

hili ni dhaifu jambo ambalo linadhihirisha kuwa alidhamiria kutenda kosa hilo la kudharau mamlaka ya Bunge na Wabunge;

**NA KWA KUWA,** Godles Jonathan Lema ambaye ni Mbunge mkongwe kwa vipindi viwili anaouelewa mkubwa wa taratibu za kikanuni za namna ya Bunge linavyoendeshwa hivyo kwa kitendo alichofanya ni ukosefu wa heshima kwa mamlaka ya Bunge na Wabunge na kutokuwa na uwajibikaji wa pamoja;

**HIVYO BASI,** Bunge, liliazimia kuwa Mhe Godbless Jonathan Lema (Mb) asimamishwe kuhudhuria Mikutano mitatu ya Bunge kuanzia tarehe ya Azimio hili;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, linakubaliana na kupitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mhe. Godbless Jonathan Lema (Mb) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**MHESHIMIWA SPIKA NAOMBA KUTOA HOJA**

Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**
3Aprili, 2019

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa uwasilishaji wako. Ninao wachangiaji kadhaa, mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wakati Mwenyekiti wa Kamati anawasilisha taarifa na mapendekezo kwa Bunge pamoja na mambo mengine amesema uamuzi huu unalenga kulinda heshima ya Bunge dhidi ya kudhalilishwa, kuzarauliwa na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, heshima ya Bunge lolote haiwezi kulindwa kwa kuwafukuza, kuwaadhibu, kuwadhalilisha na kuwahukumu Wabunge wake. Heshima ya Bunge lolote inalindwa kwa Bunge kutumia vizuri madaraka yake na kwetu yamewekwa kwenye Katiba, Ibara ya 63(2) mamlaka ya kuishauri na kuisimamia Serikali, kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi, Bunge linalofanya kazi hiyo vizuri ndiyo Bunge lenye heshima kwa wananchi na siyo Bunge la adhabu, siyo Bunge la kudhalilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani nilisahau kusema muda, kwa kawaida huwa tunatumia dakika tano, tano lakini kwa hili nitawapeni dakika kumi, kumi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Katika mazingira kama hayo, mapendekezo ya adhabu zilizotolewa na taarifa yote ya Kamati yasikubaliwe na Bunge hili tukufu ili Bunge liachane na haya ambayo kimsingi badala ya kulinda heshima ya Bunge yanazidi kuendelea kudhalilisha heshima ya Bunge, Bunge lijielekeze kwenye kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko kwenye Bunge la bajeti hakuna....

**SPIKA:** Unajua unaongea na mimi, sasa ukipandisha sana unakuwa unanifokea, ongea taratibu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naongea taratibu na kukuomba kwamba Kanuni 5 ambayo umeapa kuilinda ya Kanuni za Bunge inakutaka wewe Mheshimiwa Spika unapoliongoza Bunge uhakikishe Bunge linazingatia Katiba, Sheria na Kanuni. Kanuni ya 5(3) inakutaka wewe

Mheshimiwa Spika pale ambapo ukiona Mbunge amekiuka utaratibu umtake huyo Mbunge anayekiuka utaratibu ajirekebishe. Vilevile Kanuni ya 8(a) inakutaka uendeshe Bunge hili bila chuki wala upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini kilitokea? Ndiyo maana nasema, mapendekezo yote ya Kamati yanapaswa kutupiliwa mbali na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu za Bunge *(Hansard)* kwa sababu ya muda sitarejea pale ambapo Mheshimiwa Lema alinukuu taarifa ya Kamati juu ya maneno ambayo Mheshimiwa Mdee aliyasema kuunga mkono kauli ya *CAG.* Ila nitanukuu kauli aliyosema Mheshimiwa Lema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kunukuu maelezo yote hayo, Mheshimiwa Lema akasema, mimi ni Mbunge wa Vipindi viwili, nathibitisha Bunge hili ni dhaifu. Mara baada ya Mheshimiwa Lema kunukuu maneno hayo, Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume na kanuni ya 5 (1) ya Bunge, kinyume na kanuni ya 5 (2) ya Bunge, kinyume na kanuni ya 8 (a) ya Bunge akasimama akasema, Mheshimiwa Lema kwa maneno hayo uliyoyasema, nawe unapelekwa kwenye Kamati ya Maadili na ukae na hakuna mchango kwa sababu tunajadili adhabu kuhusu maneno hayo hayo na wewe unasema unayathibitisha. Haya maneno muhimu sana “unayathibitisha.” Nawe utaelekea kwenye Kamati ili ukathibitishe. Nasisitiza “ukathibitishe” vizuri kule.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu Mheshimiwa Naibu Spika alisema ukathibitishe kule; kwa kanuni zetu za Bunge, Mheshimiwa Naibu Spika alipokuwa hapa mezani alipaswa kuongozwa na kanuni ya 63 ya Kanuni za Bunge. Kanuni ya 63 ya Kanuni za Bunge inasema; maana yake hili jambo mlitofautishe kati ya kauli inayotolewa nje ya Bunge na kauli inayotolewa ndani ya Bunge. Kauli zinazotolewa ndani ya Bunge zina kinga ya Kibunge ya Ibara ya 100 ya Katiba, zina kinga ya Kibunge ya Kanuni za Bunge, zina kinga

ya Kibunge ya Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukikubali leo Bunge likapitisha azimio la kumwadhibu Mbunge kwa kauli aliyosema Bungeni kwa kumpeleka Kamati ya Maadili bila utaratibu wa kikanuni, mkipitisha utaratibu huu maana yake mmetengeneza mazingira ya Bunge hili la Bajeti linaloanza leo kwa Hotuba ya Waziri Mkuu Wabunge kuminywa mamlaka na haki yao ya kikatiba ya kuishauri na kuisimamia Serikali, ambalo ndiyo lingelinda heshima ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu ambao ulipaswa kufuatwa ni upi? Ibara ya 61, 63 (1)(a) inaweka makatazo kwa Mbunge, baada ya hapo, inaeleza nini ambacho Mbunge mwingine angefanya. Siyo Mbunge mwingine angefanya, ndiyo kusema kwamba hicho ulichosema siyo sahihi au ni uongo. Ibara ya 63 (5) inasema: "bila kuathiri masharti ya fasiri zilizotangulia za kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli au kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi wake.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Spika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naibu Spika hakufanya hayo, badala yake...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Nawaombeni leo wala kusiwe na taarifa. Tuwaache waseme, watumie dakika zao 10, na wengine nao watasema, watatumia dakika zao 10. Leo sitaki fujo, anayeleta fujo leo, hamna cha taarifa wala nini. Endelea bwana, dakika zako 10.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kama utaratibu huo ungefuatwa, maana yake ama Mheshimiwa Lema angetakiwa afute kauli, au angetakiwa athibitishe hapa Bungeni. Kama angeshindwa kuthibitisha, utaratibu wa adhabu ambao ungefuatwa uko kwenye kanuni ya 63 (9) ambapo adhabu pekee zilizotajwa kama ni kosa la kwanza, vikao visivyozidi 10 kama ni kosa la pili, vikao visivyozidi 25 na kadhalika. Adhabu zimetajwa hapa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa adhabu ungekuwa tofauti na ilivyopendekezwa na Kamati, asingesimamishwa mikutano mitatu kwa mapendekezo mnayotoa ambayo ni kinyume kabisa na utaratibu, isingekuwa namna hii na utaratibu usingekuwa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa nasimama kusisitiza hili na nayasema haya na naomba taarifa ya Kamati isikubaliwe. Kwa sababu kama taarifa ya Kamati ikikubaliwa; Mheshimiwa Lema alikata rufaa baada ya uamuzi wa Naibu Spika kabla Kamati ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge haijakaa. Alitumia haki ya kikanuni, kanuni ya 5 (4) akapeleka taarifa ya rufaa kwa Katibu, kama kanuni inavyosema, akaeleza nimesema hoja moja tu ya kasoro za jambo zima kama nitakuwa na muda nitakwenda kwenye nyingine, alikuwa na hoja tatu; akakata rufaa kabla. Akaenda mbele ya Kamati ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge akaiambia Kamati, nimekata rufaa ipo kwa Katibu, nakala ya rufaa hii hapa. Kamati ikasema hatujapokea rufaa, hatuko tayari kuipokea kutoka kwako, sisi tunaendelea mbele. Kimsingi Kamati ilikuwa imesha-*shape* uamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi ya haki, kwa kauli zako za jana tayari ulishatoa hukumu kabla ya Kamati kufanya kazi. Huu mchakato mzima ukiendelea, ni mchakato ambao ni batili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama uamuzi ukishafanywa na Bunge, hakuna mahali popote pengine pa kukata rufaa isipokuwa Mahakamani na Mahakama inaminywa kwa Sheria ya Kinga Haki na Bunge kushughulikia mambo ambayo

yameamuliwa na Bunge. Sasa kama tukipitisha huu uamuzi leo, maana yake tuna-*pre-empty* Kamati ya Kanuni. Tuahirishe hii taarifa isijadiliwe kabisa, Kamati ya Kanuni ikakae kwanza kabla ya uamuzi wa Bunge ili taratibu za kikanuni zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nijielekeze kwenye eneo lingine haraka haraka. Amehukumiwa kwa kosa la kudharau Bunge wakati siyo kosa lake. Kwa kosa hilo, Ibara ya 33 kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kinasema: "*Where any member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct Speaker to reprimand*..." ungeweza wewe mwenyewe Spika kuamua kumwonya, kungeweza kuwa na adhabu ya onyo, lakini naendelea mbele. Kwa hiyo, kama Spika ukiamua kuondoa misingi yoyote ya mazingira ya kuonea au nini, unaweza kumpa onyo tu.

Mheshimiwa Spika, sentensi inaendelea, kama ukiamua kutoa *suspension: suspend him from service of the Assembly for such period as it may determine.* Sheria inaendea mbele inasema, sikilizeni: "*provided that, such period shall not extend beyond the last day of the session next following that which the resolution was passed or of the session in which the resolution is passed as the Assembly may so detrmine.*"

Mheshimiwa Spika, sheria imeweka ukomo wa kiwango cha adhabu kinachoweza kutolewa. Ninyi taarifa yenu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika ninyi taarifa yenu ya Kamati imekiuka sheria, imekiuka Katiba, imekiuka mambo yote ya msingi isikubalike.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika ahsante sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa sababu mko wengi na mmeshaamua, kama mnataka kuamua, ninyi muamue kwenye Mahakama ambayo ninyi wenyewe ndio walalamikaji, ninyi wenyewe ndio watoa hukumu na kila kitu Mheshimiwa Spika na hatimaye mtaendelea kulidhalilisha Bunge kwa haya mnayoyafanya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kama muda wangu umeisha. Kama bado, niendelee.

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi tafadhali. Dakika kumi pia.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye azimio hili la Kamati ya Maadili ya Bunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani walitoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Mbona mmeanza kukimbia tena? Mmeshaingia baridi?

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikupongeze kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu, unatuongoza vizuri kama Wabunge....

**SPIKA:** Hapana, mtu yeyote asifanye fujo. Anayetoka atoke. Mtu yeyote asifanye fujo. Leo Bunge hili litaendeshwa kisayansi. Msiwe na wasiwasi. Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI**: Mheshimiwa Spika, sawasawa. Wewe ndio kiongozi, tumekuchagua na wewe ndio mwenye mamlaka ya kuweza kupanga taratibu zote za Bunge.

**SPIKA:** Namwambia *Serjeant-at-arms,* habari ya watu kutoka hapo nje mara sijui Waandishi wa Habari na nini, marufuku! Anayetaka sijui kuongea ongea nini, nje ya geti.

**MHE. MARIAM N. KISANGI**: Sawasawa.

**SPIKA:** Anayetaka kuongea, aongee humu ndani. Naomba *Serjeant-at-arm* awe macho hapo. Endelea Mheshimiwa Mariam.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, nia yako ni njema. Unapomwambia mtu yeyote ambaye amelikosea Bunge kumpeleka kwenye Kamati ya Maadili, kwa maana nyingine ulikuwa unawasaidia watu hawa kwa sababu Kamati ya Maadili siyo Kamati ya kuadhibu mtu tu, bali ni Kamati ambayo inazingatia maelezo ambayo mtu anatoa; na pale anapoomba msamaha, Kamati hii haiwezi kuacha kumsamehe.

Mheshimiwa Spika, lakini watu wanapokuja kwenye Kamati ile na kuendeleza ubabe na kuendeleza maneno yasiyofaa, ile Kamati, sisi ni Wabunge lakini pia tunao uwezo wa kufikiri na kuangalia nini kinachoendelea katika maisha na taratibu za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge leo ni mhimili. Mhimili wa Bunge unaunganisha viongozi mbalimbali wa Kitaifa wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika mwenyewe na viongozi mbalimbali. Sasa inapotokea mtu akasimama akasema kwamba Bunge ni dhaifu, hatuwezi kukubali.

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge tumepata taabu kugombea leo hii kuja kuwawakilisha wananchi hapa. Leo hii akili zote hazipo, ziko Majimboni. Tunapofika hapa Bungeni tukasema dhaifu, ina maana sisi dhaifu? Siyo sawa. Serikali yetu, Wabunge ndio tunaopitisha Bajeti, ndio tunaopitisha miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, leo katika Mkoa wa Dar es Salaam miradi yote muhimu; mwendokasi, barabara nane, miradi kibao imeenda, kazi yote hiyo na Mbunge, iweje leo Bunge hili liambiwe kuwa ni dhaifu? Hiyo haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio hilo. Nasema yote yaliyopendekezwa kwenye Kamati ni sawa sawa. Tuchukulie pia hili Bunge kuna watu mbalimbali wanakuja kujifunza humu ndani ya Bunge. Tunao vijana huko juu, wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo Vikuu, wanakuja kujifunza katika kwenye Bunge hili, tafiti mbalimbali zinafanyika katika Bunge hili, leo anatokea mtu huko anakuja kusimama kwamba Bunge hili ni dhaifu, sisi tukubaliane naye! Hatuwezi kukubali, tunaungana nawe Mheshimiwa Spika, lazima Bunge letu sasa liwe na nidhamu. Wabunge tuwe na nidhamu, tuangalie mazingira gani ambayo unaweza ukaongea maneno gani.

Mheshimiwa Spika, upotokaji wa maadili unazidi kuwa mkubwa ndani ya Bunge. Kwa maana hiyo, azimio hili la Kamati iwe fundisho sasa kwa Wabunge wengine na viongozi wengine walio nje au ndani ya Bunge kwamba wauheshimu mhimili wa Bunge. Bunge linafanya kazi kubwa sana na linapitisha mipango mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nitoe angalizo kwa Waheshimiwa Wabunge wetu vijana, kama Mheshimiwa Godbless Lema, sisi tunawategemea vijana, sisi ni watu wazima, umri unaenda, tutafika sehemu itabidi tuwaachie vijana hawa waendeleze nchi yetu. Leo Mbunge anasimama anaongea maneno yasiyofaa ndani ya Bunge, anatuambia nini sisi kama wazee ambao tunawatarajia wao tuwape nafasi hizi waendeleze Taifa hili? Je, viongozi kama hawa tukiwapa nafasi wataliacha salama Taifa letu kwa utovu huu wa maadili?

Mheshimiwa Spika, tumekumbana na hii hali kwa muda mrefu, sasa umeamua na sisi tuko tayari kuku-*support,* hatuwezi kukubali kwamba Bunge liwe mtu anasimama

anatukana anafanya hivi na hivi kisha anaachiwa. Hiyo haikubaliki hata kidogo. Lazima taratibu za Bunge zifanywe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuambiwa huyu Godbless Lema kwamba yeye amekosea aliambiwa siku moja kabla kulikuwa na masaa 24 kwa mtu huyu kutafuta njia mbalimbali za kutubu na kuomba msamaha kwa kosa lake. Bunge kuna taratibu mbalimbali kwa mujibu wa kanuni. Kuna hoja binafsi, kuna kumwandikia Spika, kuna kumwomba Spika, lakini Mbunge huyu hakutaka kufanya taratibu yoyote ya kutaka kujinusuru na kuona kwamba labda kauli ile niliitoa kwa bahati mbaya aweze kupata msamaha.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tulimwomba sana; je, kijana wetu huwezi kujutia hilo tatizo lako? Kwa mapenzi makubwa. Anasema mimi nimekubali, kama kufungwa nitafungwa, nimefungwa sana, jambo ambalo siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili la Bunge na niwaombe Wabunge wenzangu kwamba sasa ifike sehemu awe Mbunge gani kama ulivyoongea kwamba awe Mbunge wa Chama gani, bila kujali Chama, wote kwa pamoja tuzingatie nidhamu na maadili ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mariam Kisangi. Anafuata Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii iliyoko mezani inayomhusu Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Godbless Lema.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Haki, Kinga na Maadili ya Bunge ipo kisheria ndani ya Bunge na ipo kikanuni. Kabla ya kuanza kazi ya Kamati hii tulipewa *instruments*; tulipewa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, tulipewa Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge, lakini pia tulipewa Katiba ya nchi hii ili Kamati hii itende haki.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inafanya kazi kwa kanuni ya Nyongeza ya Nane, kanuni ya 4 inayotaka; na naomba kwa faida ya Bunge hili ninukuu, inasema: "Kamati ya Haki na Maadili ya Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na Madaraka ya Bunge, yatakayopelekwa kwake kwenye Kamati hii na Spika.

(b) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika."

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Godbless Lema chimbuko lake lilitokana na kesi ya Mheshimiwa Profesa Assad aliyetamka maneno kuhusu dharau na kuliteremsha hadhi Bunge, akisema Bunge hili ni dhaifu. Suala hilo lilishadidiwa na Mheshimiwa Halima Mdee aliyasema pia yeye ni Mbunge mzoefu na ana hakika Bunge hili ni dhaifu. Mheshimiwa Godbless Lema alishadidia zaidi naye akasema kwamba yeye ni Mbunge mwenye vipindi viwili, naye anashadidia kwamba Bunge hii ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, kisheria Mheshimiwa Godbless Lema aliunganishwa na kesi ambayo aliikuta. Kwa hiyo, akathibitisha kwamba naye pia anafanya kosa hilo hilo kwa ushahidi alionao yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, ulimleta Mheshimiwa Godbless Lema aje athibitishe kwenye Kamati kwamba anao ushahidi wa kutosha kwamba Bunge hili ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, neno "shahidi" linatumika kwa ajili ya Wabunge wanaokuja kwenye Kamati. Shahidi huyu alipofika kwetu alithibitisha kwamba naye bado anaamini kwamba Bunge ni dhaifu. Kwa hiyo, anakiri kwamba alifanya kosa hilo na alithibitisha na bado aling'ang'ania kwamba ni kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, msemaji aliyetangulia hapa, ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika, ame-*quote* kifungu cha sheria ambacho hajui kwamba tulikitumia au hatukukitumia. Tunatumia sheria mara nyingi kwa watu ambao hawahusiki. Ali-*quote* kifungu cha 33 na ange-*quote* na cha 26 pia cha Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge, lakini sisi tunatumia sana kanuni hizi kwa ajili ya Wabunge ambao ni wanachama wa Bunge hili na angekwenda kwenye kifungu cha 74 kingemsaidia zaidi kupata majibu, kwa nini Mheshimiwa Lema amechukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, nami kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wengine, ningependa kusoma kanuni ya 74 (4) wale wenye kanuni za Kudumu za Bunge, inasema hivi: "Bunge linaweza kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na Kamati ya Haki Maadili ya Madaraka ya Bunge kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyekiuka masharti ya kanuni hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile kanuni ya 74 kifungu kidogo cha (5) inasema: "bila ya kujali masharti ya fasili ya (4) ya kanuni hii, Bunge linaweza kumchukulia hatua nyingine za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kumsimamisha kazi Mbunge yeyote atakayetenda kosa chini ya kanuni hii." Kwa hiyo, kanuni aliyojielekeza Mheshimiwa Mnyika sidhani kama aliamini kwamba tuliitumia sisi.

Mheshimiwa Spika, nini maana ya kazi ya Kamati hii? Sisi katika Kamati ya Maadili, tuko pale kwa ajili ya kutumia Kanuni, kusahihishana Wabunge, kwa Wabunge ambao umewaleta wewe kwenye Kamati yetu. Hata hivyo, huyu Mheshimiwa Lema ambaye ni shahidi wa mwisho kwa suala hili, alipokuja kwetu hakuonesha hata kidogo kujutia kosa alilolifanya alithibitisha kwamba amelifanya na tulipompa nafasi ya mwisho aseme, akasema moja nawaombeni kabisa kabisa msinihurumie. Narudia, tulipompa ruhusa aseme chochote kwamba sisi tunataka kumtia katika hatia kwa sababu amevunja kanuni kwa kulidhalilisha Bunge kwamba Bunge hili ni dhaifu, akasema, naiomba Kamati hii isinionee huruma na wala isinipe msamaha. Sasa sisi tulibaki na jambo

la kushangaa sana Mheshimiwa Lema tulipotaka, unamwambia Hakimu wewe Hakimu usinihurumie mimi na wala usinisamehe, wewe hukumu.

Mheshimiwa Spika, imetupa tabu sana, tukafikiria makosa ya nyuma ya Mheshimiwa Lema. Mheshimiwa Lema huyu alipoitwa mara ya kwanza kwa kudharau Bunge kule Dar es Salaam alisema naomba nikatafute Wakili na alipopewa fursa hiyo hakurudi tena. Kwa hiyo jana alipokuja alikuwa na wazo hilo kwamba naomba mnisamehe nikatafute Wakili, lakini tulipomwambia wewe unaweza kujitetea, akaongea mambo mengi sana ya kujitetea, lakini sio kujitetea ili asamehewe, ya kusema mambo mabaya kuhusu Bunge ili Bunge halina uwezo na uwezo wa Spika si, alisema maneno mengi kwenye Kamati ile na akatuma salamu tukwambie Mheshimiwa Spika kwamba unavyoendesha Bunge sio vizuri na tulivyomwambia aeleze hasemi lolote la maana akijaribu kusema kwamba mimi nathibitisha kwamba Bunge hili ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimtia hatiani kwa adhabu ambayo azimio limeomba na mimi naunga mkono adhabu hii ya mikutano mitatu na kwa kweli Kamati ingeomba zaidi mikutano zaidi ya mitatu iliyoombwa sababu kubwa ya kumpa mikutano mitatu ni kwamba Bunge linakaribia mwisho, tumetaka awepo kwenye Mkutano wa mwisho wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Msemaji wa mwisho Mheshimiwa Mlinga, hayupo tumalize Mwenyekiti wa Kamati. Kumbe yupo, endelea Mheshimiwa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami naomba niweke maneno yangu machache. Katika Bunge hili baada ya kuapishwa huwa tunapewa vitabu vya kanuni, sasa kwa bahati mbaya Wabunge wengi huwa hawavisomi hivi vitabu vya kanuni, wanasoma mistari michache ambayo wao wanaona

wameilewa, lakini hawafanyi jitihada za kuelewa kanuni zote zilizoandikwa katika kitabu hiki cha kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba nisome kanuni ya 72, Sehemu ya Sita inasema hivi:

*"Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa, utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho."*

Mheshimiwa Spika, hili Bunge ni la kwako, hizi kanuni ndio zinazokulinda tafadhali asikuchezee mtu yeyote kazi unayoifanya ni nzuri sana na Wabunge tunailewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeomba kuchangia kwa kuwa juzi nilichangia kuhusu Kamati hii ya Madili lakini jana wakati naingia katika viwanja vya Bunge katika lile geti la usalama kwenye kamera pale kwenye sehemu ambayo tunapekuliwa nilikutana na Wabunge wawili Mbunge mmoja anaitwa Haonga na mwingine wa Mbeya simkumbiki jina lake, nitalikumbuka baadaye, walinizodoa sana, walinitukana sana.

Mheshimiwa Spika, nakupa tu taarifa hii, kwa kuwa mimi kijana nikawaambia kuwa wafanye haya mambo wakiwa katika viwanya Bunge, wakithubutu kufanya nje ya viwanja vya Bunge watakuja kuwasimulia ndani nitakachowafanya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, juzi nilisema kuwa katika hili Bunge tuna viongozi wetu. Sisi wa Chama cha Mapinduzi tuna viongozi wetu usipohudhuria vikao vitatu unaandikiwa barua, uki-*misbehave* unaitwa kwenye Kamati za Chama, hawa wenzetu viongozi wao wanapokutana, wakimaliza suala la kuchangishana hamna jambo lingine, kuwa mbunge ahudhurie kwenye vikao asihudhurie lwake, inafika kipindi mpaka Mbunge anafukuzwa Ubunge, kiongozi wao hajui. Kiongozi wao mwenyewe ukihesabu katika vikao vinavyozidi 150 kwa mwaka anavyohudhuria hata vikao hata 20 havifiki. Kwa hiyo hawa wenzetu hawana viongozi. Kwa hiyo ifike

mahali tubadilishe hizi kanuni Kiongozi wa Kambi Rasmi Bungeni asipohudhuria vikao kadhaa na yeye mwenyewe aenguliwe, wapewe hata *CUF*. Leo hii tujiulize *CUF* kwa nini hawasimamishwi, *CUF* kwa nini hawa-*misbehave* Bunge? *CUF* kwa nini hawatoi kauli chafu? Kwa nini ni wao tu? Kuna chama cha *ACT* humu kwa nini hayawakuti, ni wao tu CHADEMA?

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mfano Mheshimiwa Lema wakati anafanya utumbo wake juzi na kiongozi wake wa Kambi ya Upinzani yupo, hafanyi kitu ananyamaza tu na mimi nilisema, kwa hiyo tubadilishe hizi kanuni hawa viongozi wao wawajibike kwa mambo wanayowafanya Wabunge wao. Tabia mbaya za viongozi wa upinzani, kwanza la utoro, hata ukifanya tathmini ya mahudhurio ya Wabunge wa Upinzani ni nusu ya vikao na ni nusu ya Wabunge, Wabunge wengi. Mheshimiwa Lema siku ambayo unamsikia anazungumza ndio kaingia Bungeni, lakini siku zote hayupo. Anakuja humu kwa ajili ya *interest* zake na ukiona kaingia ujue ana jambo lake binafsi, sio jambo la watu wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, ndio maana ulisema kuwa ukiweka masuala yako binafsi katika Bunge hili, lazima utaharibikiwa, sehemu, acha ya huyo, kuna Mbunge mwingine wa *ACT* anazunguka huko mitandaoni, anasema anawasainisha wananchi ili wakatae maazimio ya Bunge. Siku moja nitakuja kuwaambia, anayofanya ana *interest* yake binafsi, sio kama ya jamii kama wanavyojua. Siku moja nitawaambia wananchi na wataelewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tunasema, Bunge letu linaenda vizuri na ndio maana maendeleo yanapatikana, barabara zinajengwa na miradi mikubwa inafanyika na wageni wanakuja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja ya Kamati.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati uhitimishe kwa

dakika chache sana kama tano hivi tuweze kusonga mbele na mambo ya maana zaidi. Karibu sana Mwenyekiti, tafadhali.

**EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kupewa nafasi ya kuhitimisha hii hoja. Labda kuja jambo moja ambalo amelisema Mheshimiwa. Kuna hili ambalo alikuwa analizungumzia Mheshimiwa Mnyika la kunukuu Ibara ya 63, lakini pia akanukuu kanuni ya 5 na amenukuu kanuni hizi ili kujaribu kutafuta uhalali kwamba ametumia vifungu na kujaribu kutaka kuonesha jamii au hata wananchi kwa ujumla wadhani kwamba ulichokifanya pengine umekiuka Katiba au kifungu chochote cha kanuni, kitu ambacho si kweli.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 74, kanuni ya 72(1) inakupa mamlaka ya kuangalia amani na utulivu Bungeni, ninaomba kwa ridhaa yako nisome 72(1) inasema:

*"Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa, utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho."* Hii ni kanuni ya 72(1) ya kanuni zetu za Kudumu za Bunge.

Kanuni ya 74(1) inasema:

*"Spika anaweza kutaja jina la Mbunge kwamba amedharau mamlaka ya Spika na kisha kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikiwa*

*(a) kwa maneno vitendo, Mbunge huyo anaonesha dharau kwa mamlaka ya Spika; au*

*(b) Mbunge huyo atafanya kitendo chochote cha makusudi au Mbunge yoyote anayeongoza shughuli hiyo."*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho Mheshimiwa Lema alikifanya hapa. Kwa hiyo, hakuna mahali popote ambapo umekiuka kanuni yoyote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lema jana alisema kitu cha ajabu sana, kwamba yeye alichokisema humu Bungeni na kipo kwenye *hansard* cha kudhalilisha Bunge na kuliita dhaifu ni msimamo wa Kambi ya Upinzani na leo tunaweza kuthibitisha kwa jinsi walivyoweza kutoka wote hapa, kumbe kweli wao msimamo wao ni kulidhalilisha, kulidharau Bunge. Kwa mantiki hiyo, kwa kuwa tayari tumeshamtia hatiani Mheshimiwa Lema kwa kutohudhuria Mikutano mitatu ya Bunge, Waheshimiwa wengi wote wameweza kuunga mkono pia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako Tukufu liweze kupokea taarifa hii ya Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, lakini pia kuridhia azimio la adhabu ya Mheshimiwa Lema ambayo imependekezwa na Kamati ya Haki Kinga na Mamlaka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa jukumu langu mimi ni kuwahoji kuhusu mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, kwa hiyo Mheshimiwa Godbless Lema anafungiwa na Bunge hili kutohudhuria Mikutano mitatu ijayo ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, niongeze yafuatayo: ndugu zangu wapo watu ama kwa malezi au kwa makuzi ni tatizo na baadhi yao ni aina ya hawa watu kama huyu ambaye tunampa adhabu leo. Hatuwezi sisi kumkunja samaki mkavu, ni ngumu sana lazima twende nae vile alivyo. Kanuni hizi zilipotungwa na wengi hawajui, wengi wa Wabunge wapya kina Mnyika wanakuja wanasomasoma kanuni hapa. Hizi

kanuni Mheshimiwa Mwakyembe yupo hapa ndio tulifanya kazi ya kuzitunga mwaka 2007 mimi nikiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakyembe akiwa mjumbe wangu na wajumbe wengine hawapo hapa hivi sasa. Tunazijua mwanzo mwisho, kwa nini kitu gani kiliwekwa wapi, kwa sababu gani na kwa namna gani.

Kufundisha kanuni hapa wala haisadii na baadhi ya ujeuri unatokana na kanuni yetu *assumption* yake ilikuwa ni kanuni kwa Waheshimiwa, ni kanuni zinazoangalia mwenendo wa Waheshimiwa kwa hiyo zimekaa kiheshimiwa heshimiwa. Unapokuwa na Mbunge yupo chini ya kiwango cha Waheshimiwa haikuwa matarajio. Hasa utampata wapi, Mbunge unaropoka hovyo, unasema hovyo, mimi sijali kupigwa risasi, mimi sijali, sasa aliyesema anakupiga risasi nani? Hapa kuna risasi hapa. Mbunge anaenda mahali pa wenzake, mwenzetu mbona unasema maneno ambayo wenzako hatukuelewi, anasema wala msinihurumie, hebu nishughulikieni. Yaani yeye mwenyewe anaomba ashukughulikiwe, kanuni hazikutarajia kama tunakutana. Yaani anafungiwa Mikutano mitatu kuanzia Mkutano huu ndio maana yangu mimi, ndio mapendekezo ya Kamati ya Maadili. Kwa hiyo sijakosea, katika hilo, kuanzia huu na mingine miwili itakayofuata.

Kwa hiyo tuna watu ambao mtu anasema msinionee huruma wala msinisamehe, hivi wewe ungekuwa wewe unafanyaje, mnakaa mnatoka nje, mnatoka nje kufanya nini? Mwenzenu kasema hataki huruma wala asisamehewe, halafu ninyi mnamfuata nje, hakuna umoja, yeye mwenyewe hataki kuhurumiwa, hii haisadii na wanafanya haya wakijua kanuni zetu zina adhabu ndogo ndogo, tulishatoka huko, tulishavuka, Bunge hili limekwenda kulingana na aina ya ukorofi uliopo. Ndio maana yule mwingine wiki iliyopita ilikuwa Mikutano miwili, huyu mitatu na mwingine akiingia hivyo hivyo tunakwenda tu. Sasa hivi mtaona wengine tunakutana nao 2020.

Sasa kwa kuwa tumeshaamua nishauri tu jambo moja au mawili kwamba huko aliko Mheshimiwa Lema akiropoka

jambo ambalo litavunja hadhi na heshima ya Bunge, atarudishwa tena maadili na hicho kimoja kilichobaki huwezi kujua na haya yanatokana na kwamba huyu mtu ana uhakika kabisa kwamba pale Arusha Mjini hachaguliki, ana hakika kabisa. Niliwahi kusema hapa Arusha *deserves better, you can't have this kind of* Arusha, haiwezekani, anajua. Sasa mtu akishajua kabisa hali ndio hiyo, anakuwa yaani na yale niliyosema jana na nini basi taabu.

Wewe ukope milioni 600 katika miaka minne umelipa mbili, katika mwaka mmoja unatakiwa ulipe milioni 400 utazilipaje? Utaacha kupata matatizo kidogo kichwani, lazima utachanganyikiwa kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, demokrasia ni kusikilizana, ni vizuri mnapopata nafasi ya kusema na ninyi mkapata nafasi ya kusikiliza wenzenu ndio demokrasia hiyo. Demokrasia ambayo tumezoea kuiona hapa ya wewe unasema, halafu ukishasema mnatoka nje, hamsikilizi wenzenu, sijui ni demokrasia ya wapi hiyo.

Kwa hiyo pamoja na maamuzi tumeshayafanya hayo ni maamuzi ya Bunge kuhusu Lema. Sasa maamuzi yangu mimi kama Spika kwa mamlaka mlishataja kanuni ya 5 na kadhalika, hawa waliotoka nje *Sergeant-at-arms* kwa siku ya leo marufuku kurudi hapa ndani. Kwa leo tarehe 4 Aprili, 2019, wote waliotoka asirudi hata mmoja, maana si wamechangua kutoka, wakae huko huko, huo ndio uamuzi wangu.

Katibu tunaendelea

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Muongozo wa Spika.

**SPIKA:** Tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

**SPIKA:** Hoja za Serikali kwa sababu ya muda sasa tunamkaribisha Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kutoa hotuba yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshimi na tahadhima karibu sana. *(Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti za Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyeko ziarani Mkoani Mtwara, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uongozi wao makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa juhudi

na maono yao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali zinaleta manufaa kwa tija ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuboresha utendaji Serikalini, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Mwaluko Aidan Kabudi (Mb.), kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni matumaini yangu kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi tunaowawakilisha walifikwa na misiba ya ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, Taifa lilikumbwa na maafa kutokana na ajali za vyombo vya majini na nchi kavu. Ajali hizo ziligharimu maisha ya watu, kusababisha majeruhi na uharibifu wa mali. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliopata majeraha na azipumzishe roho za marehemu mahala pema, amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohammed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mwanasheria Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na umakini mkubwa. Ni imani yangu kuwa mtaendeleza hekima na weledi mlionao katika kuongoza Bunge kuisimamia Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, nimpongeze Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa namna wanavyolisaidia Bunge letu kutekeleza majukumu yake ipasavyo *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru watumishi wote wa umma kwa kutekeleza majukumu yao na kukamilisha kuandaa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge Viti Maalumu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji); Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kujitoa kwao katika kutekeleza majukumu na ushirikiano mkubwa wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni Bibi Maimuna K. Tarishi (Waziri Mkuu na Bunge); Bwana Andrew W. Masawe (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Bibi Dorothy A. Mwaluko (Sera, Uratibu na Uwekezaji); na wafanyakazi wote kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Washirika wetu wa Maendeleo, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi na Taasisi za Dini kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kujenga uchumi wa viwanda ili kufikia azma ya kuwa na Taifa lenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono. Niwapongeze kwa kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi wakati mimi Mbunge wao nikitekeleza majukumu ya kusimamia utendaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimshukuru mke wangu mpendwa, Mary Mbawala na familia yangu kwa ujumla kwa utulivu wao wakati wote ninapokuwa nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru sana kwa upendo wanaoendelea kunionesha na kunitia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo na Bajeti wa Mwaka 2019/2020. Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020 yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2019/2020 ambao ni wa nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka kwa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia mwaka (2016/2017 – 2020/2021). Dhima ya Mpango huo ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu unatekelezwa sanjari na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi

(CCM) ya Mwaka 2015 – 2020; Ahadi za Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na zile alizozitoa katika hotuba yake ya kuzindua Bunge hili mwezi Novemba, 2015. Vipaumbele vya mpango wa mwaka 2019/2020 ni kuendelea kuimarisha msingi wa uchumi wa viwanda; kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; kuendelea kuboresha mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji; na kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo ya Bajeti ya mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Umeme wa Maji ya Mto Rufiji (*Stiegler's Gorge*), ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa (*SGR*), barabara pamoja na kukuza sekta ya anga. Utekelezaji wa miradi hiyo na miundombinu wezeshi ya kiuchumi una lengo la kufungamanisha ukuaji wa sekta hizo na sekta nyingine hususan za kibiashara, kilimo na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuimarika kwa sekta hizo kutachochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla wake. Nitoe rai kwa Wabunge wenzangu, wafanyabiashara na wajasiriamali, viongozi na watendaji wa serikali, taasisi za dini, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo na wananchi wote kwa ujumla, kuiunga mkono Serikali katika kutekeleza Mpango huu ili kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano. Mwezi Juni 2018 wakati akizindua Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II), Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema, ninanukuu, "Tumekuwa wakimya na hatuelezi kwa kina masuala tunayofanya. Niwaombe basi viongozi wenzagu wa Serikali, kila tunapopata nafasi tuseme mambo yanayofanyika. Tusipofanya hivyo yanayosemwa yataonekana kuwa kweli." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, bila kumung'unya maneno katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka mitatu kazi kubwa tena ya kihistoria imefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na ya kijamii kwa ujumla. Hivyo, niungane na Mheshimiwa Rais kuwakumbusha viongozi na watendaji wakuu Serikalini kuwa tunalo jukumu kubwa la kuhakikisha umma wa Watanzania unafahamishwa kuhusu shughuli zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na mafanikio makubwa yanayopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamepatikana mafanikio mengi ambayo wananchi wamepaswa kufahamishwa. Aidha, Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira ya dhati ya kisiasa katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Halikadhalika, ameweza kuhakikisha dhamira hiyo ya kujenga uchumi imara usiyo tegemezi inaenea kwa viongozi wengine, watendaji na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kuendelea kukua na kuimarika kwa uchumi ambao unachochewa na jitihada za Serikali za kuwekeza kwenye miundombinu ya usafirishaji ikiwemo ujenzi wa barabara, reli, viwanja vya ndege sanjari na kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme. Aidha, kuimarika kwa Shirika la Ndege Tanzania ni sehemu ya mafanikio hayo, ambapo Serikali inafanikisha ununuzi wa ndege sita mpya ikiwemo Dreamliner Boeing 787. Ununuzi wa ndege hizo umesaidia kuitangaza nchi, kuongeza mapato ya Serikali, kuongeza fursa za ajira kwa vijana na kuwa kichocheo ya sekta nyingine kama vile kilimo, utalii, mifugo na uvuvi na madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa reli ya kisasa (*SGR*) kutoka Dar es Salaam-Morogoro na kutoka Morogoro-Makutupora Dodoma unaendelea vizuri na kwa kasi ya kuridhisha. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wake wa Elimumsingi Bila Malipo. Mpango huo umesaidia

kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa ambao pengine wangekosa fursa ya kupata elimu kutokana na kushindwa kulipa ada na michango mingine isiyokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, hii imejidhihirisha kutokana na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi kutoka milioni 1.57 mwaka 2015 hadi milioni 2.08 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 35.2. Kwa mwaka 2019 uandikishaji ulikuwa milioni 1.58. Kutokana na takwimu hizi ni dhahiri kuwa kwa sasa watoto wote wanaofikia umri wa kwenda shule wanaandikishwa bila kikwazo chochote.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima, kuongeza bajeti ya dawa kutoka Shilingi Bilioni 31 mwaka 2015/2016 kufikia Shilingi Bilioni 270 mwaka 2018/2019. Ongezeko hilo linaongeza upatikanaji wa dawa muhimu kufikia asilimia 96 katika mwaka 2018/2019. Aidha, tiba za kibingwa zinatolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali mpya za Rufaa za Benjamini Mkapa pamoja na Mloganzila. Hospitali hizo zinatoa huduma za kibingwa zikiwemo upasuaji wa moyo, ubongo na uti wa mgongo ambazo awali zilikuwa zinapatikana nje ya nchi na kuigharimu Serikali fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuanza kwa ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwenye Bonde la Mto Rufiji (*Stiegler's Gorge*) pamoja na kuendelea na kazi ya kusambaza umeme vijijini. Mafanikio haya na mengine yatafafanuliwa kwa kina na Wizara husika wakati watakapokuja hapa kuwasilisha bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya nne ya Serikali ya Awamu ya Tano, ni bajeti inayolenga kukamilika kwa kiasi kikubwa yale tuliyowaahidi wananchi wakati Chama cha Mapinduzi (CCM) kikiomba ridhaa ya kuongoza Dola katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Kwa msingi huo, nisisitize kwamba, sekta na taasisi zote Serikalini zikamilishe utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. Kwa kasi ambayo Serikali yetu inaonesha na mafanikio

makubwa yaliyopatikana katika kipindi hichi cha zaidi ya miaka mitatu, ni matarajio yetu kuwa ahadi zilizotolewa kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 zitakamilishwa ifikapo mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi. Kama nilivyotangulia kueleza kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuimarisha uchumi na mafanikio yanaonekana. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2018, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Ukuaji huu wa uchumi umechangia kutoa ajira na kuongeza mapato ya Serikali yaliyowezesha ujenzi wa uboreshaji wa miundombinu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 4.0 Januari, 2018 hadi asilimia 3.0 Januari, 2019. Kiwango hiki cha chini cha mfumuko wa bei kimetokana na kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha na kujenga misingi na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuwa na mapato endelevu kwa ajili ya kugharamia matumizi yake. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia jukumu lake la msingi la kutafuta mapato kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi na kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za umma kupitia bajeti za Serikali inayowasilishwa hapa Bungeni mwezi Juni 2019.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) katika mwaka 2016/2017, umeonesha kuwa Halmashauri 166 kati ya Halmashauri 188 zimepata hati safi na kwa asilimia 90, Halmashauri 16 zimepata hati zenye mashaka ikilinganishwa na Halmashauri 32 mwaka 2015/2016. Matokeo hayo yanaonesha kuimarika kwa usimamizi wa fedha pamoja na

uwajibikaji wa watendaji na viongozi wenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nazielekeza Halmashauri zote nchini kuendelea kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha zinazopelekwa katika Halmashauri hizo ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inalingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, suala la Vitambulisho vya Wajasiriamali Wadogo. Kwa kutambua umuhimu wa wajasiriamali wadogo nchini katika kuchangia pato la Taifa na kukuza uchumi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa vitambulisho 670,000 kwa ajili ya wajasiriamali wadogo ambao mitaji yao haizidi shilingi milioni nne kwa mwaka. Lengo la kutoa vitambulisho hivyo vyenye kugharimu Sh.20,000 kwa kila kimoja ni kuwatambua, kuwaandalia maeneo ya kufanya biashara bila usumbufu wowote na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 10 Machi 2019, jumla ya vitambulisho 496,221 sawa na asilimia 74 vilikuwa vimegawiwa kwa wajasiriamali wadogo katika mikoa yote nchini. Aidha, tangu kuanzishwa kwa utaratibu huo, Serikali imeshakusanya shilingi bilioni 9.9. Naendelea kusisitiza kwamba viongozi na watendaji wote katika Serikali za Mitaa kuwapatia ushirikiano wa kutosha wajasiriamali wadogo na kutowabughudhi kwenye maeneo wanamofanyia biashara zao.

Mheshimiwa Spika, hali ya siasa. Kwa ujumla hali ya kisiasa na demokrasia imeendelea kuimarika nchini. Katika mwaka 2018/2019, zilifanyika chaguzi ndogo za Wabunge katika majimbo 10 na Madiwani katika kata 231 kwenye maeneo mbalimbali nchini. Majimbo yaliyoshiriki uchaguzi hayo ni Buyungu, Korogwe, Monduli, Ukonga, Liwale, Serengeti, Simanjiro, Ukerewe, Babati Mjini na Temeke. Katika chaguzi hizo, Wagombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM) walishinda majimbo yote na kata 230 ambapo CHADEMA walishinda Kata moja. Nichukue fursa hii, kuvipongeza vyama

vyote vilivyoshiriki katika chaguzi hizo na kipekee nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa ulioupata katika chaguzi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeendelea kusimamia na kukuza mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa ili kudumisha amani, utulivu na mshikamano uliopo katika nchi yetu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Sheria ya Vyama vya Siasa Namba.5 ya mwaka 1992, Sura ya 354 imefanyiwa marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji na hivyo kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya saba kwa sheria hii kufanyiwa marekebisho tangu kutungwa kwake mwaka 1992 kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika. Nitoe wito kwa Vyama vya Siasa nchini kuendesha shughuli zao za kisiasa kwa kuzingatia matakwa ya sheria hiyo ili kuwa na uwazi, uwajibikaji, kudumisha amani na kukuza demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kuelimisha umma kuhusu utekelezaji wa sheria hiyo, kusimamia vyama vya siasa nchini na kuhakikisha vinajiendesha kama taasisi. Vilevile, itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019. Serikali inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019 ambao ni uchaguzi wa sita tangu kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1994 chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Hivi sasa, Serikali imekamilisha zoezi la uhakiki wa maeneo ya utawala ambayo yatashiriki kwenye uchaguzi huo katika Halmashauri zote 185. Lengo la uhakiki huo ni kujiridhisha na usahihi wa maeneo hayo kwa idadi na majina ili kufanikisha maandalizi ya bajeti na mahitaji mengine muhimu ya uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi zitakazotumika kusimamia uchaguzi huo mwezi Oktoba, 2019. Nitoe wito kwa wadau mbalimbali na wananchi kujiandikisha na kujitokeza kwa wingi katika upigaji kura ili waweze kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Oktoba, mwaka huu wa 2019. Serikali kwa upande wake itaendelea kuhahakisha kunakuwepo na mazingira salama na tulivu kwa kipindi chote cha uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza maandilizi ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga kura pamoja na uhakiki wa Vituo vya Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka 2020. Hadi sasa, Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura zimeandaliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 792 na Na. 793 ya tarehe 28 Desemba, 2018.

Aidha, uhakiki wa vituo vya kuandisha wapiga kura nao umekamilika, ambapo kwa upande wa Tanzania Bara vimeongezeka kutoka 36,549 vilivyokuwepo mwaka 2015 hadi kufikia vituo 37,407 mwaka 2018, sawa na ongezeko la vituo 858. Kwa upande wa Zanzibar vimeongezeka vituo 27 kutoka 380 vya mwaka 2015 hadi kufikia 407 mwaka 2018. Natoa wito kwa wananchi wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha mara zote zoezi hilo litakapoanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Bunge limetimiza wajibu wake wa Kikatiba na kikanuni kwa kufanya mikutano mitatu na huu ukiwa wa nne. Katika mikutano hiyo, masuala mbalimbali yamejadiliwa na kutolewa ufafanuzi na Serikali ikiwemo hoja za Kamati za Kudumu za Bunge. Aidha, jumla ya maswali ya msingi 374 yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali yakijumuisha pia maswali ya nyongeza 978.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, maswali ya msingi 19

pamoja na moja la nyongeza yaliulizwa na kujibiwa. Vilevile Miswada ya Sheria ya Serikali 12 iliwasilishwa, pia imejadiliwa na kuridhiwa na Bunge kuwa Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Maazimio ya Bunge matatu pamoja na Itifaki za Kimataifa nne ziliridhiwa na kupitishwa na Bunge kwa utekelezaji wa Serikali. Ni matumaini ya Serikali kwamba Bunge lako Tukufu litaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi Kikatiba la kutunga Sheria na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 Ofisi ya Bunge itafanya ukarabati katika Ukumbi wa Bunge na Ukumbi wa Msekwa, kusimika mitambo ya Studio ya Bunge na kuboresha miundombinu mingine ya Ofisi zake ikiwa ni pamoja na Usimikaji wa mitambo ya usalama katika majengo la Bunge na kukamilisha ujenzi wa nyumba za viongozi wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuona kuwa haki inatendeka nchini. Ili kutekeleza dhamira hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa kufanya maboresho ya kiutendaji kwa vyombo vya maamuzi ikiwemo Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, jumla ya mashauri 231,927 yalifunguliwa katika Mahakama zote nchini hadi Februari, 2019. Kati ya hayo mashauri 224,950 sawa na asilimia 96 yamesikilizwa na kutolewa hukumu. Ufanisi huu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa Majaji 21 wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu. Vilevile, kukamilika kwa miundombinu muhimu ya Mahakama imewezesha kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha huduma ya Mahakama inayotembea ikiendesha shughuli zake kwa kutumia magari maalum katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya Mahakama. Huduma hii imesaidia kuongeza kasi ya Mahakama kusimamia haki kwa kutumia mifumo rafiki ya utoaji haki nchini.

Aidha, Mahakama nchini zimeanza kutekeleza utaratibu wa kutoa nakala za hukumu bure kwa wananchi kupitia huduma ya Posta Mlangoni ambapo hadi Februari 19, jumla ya nakala 5,942 zimeshatolewa. Katika mwaka 2019/ 2020, Serikali itawajengea uwezo watumishi wa Mahakama, kuimarisha mifumo yao ya utoaji haki na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhamishia shughuli zake Jijini Dodoma tangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atoe tamko la Serikali kuhamia Dodoma tarehe 23 Julai, 2016. Mpango huo unatekelezwa kwa awamu mbalimbali zinazojumuisha uhamisho wa watumishi, ujenzi wa makazi na miundombinu, uboreshaji wa huduma za jamii na ujenzi wa Mji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika awamu hizo, jumla ya watumishi 8,883 wa Wizara na Taasisi za Serikali wameshahamia hapa Dodoma. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kuhakikisha watumishi waliobaki wanahamia Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi za awali za Wizara 23 ikiwemo jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umekamilika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Julai, 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikabidhi hati miliki 64 za viwanja kwa Mabalozi wote wanaowakilisha nchi zao hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Kibalozi hapa Jijini Dodoma. Niendelee kutoa wito kwa Mashirika ya Kimataifa na Mabalozi wakamilishe kuhamishia Ofisi zao Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 Serikali itaendeleza ujenzi wa Mji wa Serikali na Jiji la Dodoma kwa kuimarisha huduma za jamii, miundombinu ya masoko, barabara, mfumo wa majisafi, afya na majitaka. Natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika Jiji la Dodoma kwenye maeneo niliyoyataja kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Jiji letu la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa Sekta Binafsi ili iweze kutoa mchango uliokusudiwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa Sekta Binafsi inashiriki ipasavyo katika maendeleo ya Taifa letu kwa kutengeneza ajira, kuongeza uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha malengo haya, Serikali inachukua hatua mbalimbali za makusudi za kuboresha Sheria na mifumo ya kodi, kuimarisha miundombinu pamoja na kuendeleza mazungumzo na makundi mbalimbali ya wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa.

Mheshimiwa Spika, mathalan, tarehe 22 Januari, 2019 Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokutana na wadau wa Sekta ya Madini alitoa maelekezo kwa viongozi na Watendaji wa Serikali kuhakikisha kuwa wanachukua hatua za kukuza Sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Februari, 2019, mimi mwenyewe nilikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa lengo la kujadiliana kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika Mkutano huo, niliambatana na viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi na kutatua kero mbalimbali zinazowasibu wafanyabiashara hao.

Aidha, Serikali inafarijika kupata mrejesho kutoka Sekta Binafsi kwamba mahusiano ya pande hizi mbili yanaendelea kuimarika. Natoa wito kwa viongozi na Watendaji wote wa Serikali kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki kwa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa uwekezaji katika kujenga uchumi wa nchi yetu, Serikali imeendelea kutoa uzito katika uwekezaji ambapo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania alichukua hatua ya kuhamishia masuala ya uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu na kuteua Waziri wa Nchi kushughulikiwa masula ya uwekezaji. Vilevile Mheshimiwa Rais amekihamishia Kituo cha Uwekezaji nchini kuwa chini Ofisi ya Waziri Mkuu. Hatua hizo zitasaidia kuimarisha uratibu wa masuala ya uwekezaji nchini na kuhakikisha kwamba changamoto mbalimbali zilizopo zinashughulikiwa kwa ufanisi ili kuwezesha nchi yetu kuvutia zaidi mitaji ya uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha na kuvutia wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi ili wawekeze hapa nchini kwetu. Katika kuhamasisha na kuhakikisha uhamasishaji huo na uwekezaji kutoka nje, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi mbalimbali zikiwemo Ofisi za Balozi zetu za Nje na Balozi za nje zilizoko hapa nchini, kiliandaa na kuendesha makongamano na semina mbalimbali zilizowalenga wawekezaji kutoka ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji huo umefanikisha kuvutia uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za kimkakati. Hadi kufikia Februari mwaka huu 2019, jumla ya miradi mipya 149 ilisajiliwa na Kituo cha Uwekezaji. Kati ya miradi hiyo, miradi 104 sawa na asilimia 72 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani, miradi 38 sawa na asilimia 26 inamilikiwa na wawekezaji kutoka nje na miradi mitatu sawa na asilimia 2.01 ni ya ubia. Miradi hiyo inatarajia kuwekeza mitaji ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.84 na kuzalisha ajira mpya 15,491.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kuvutia uwekezaji hapa nchini, hali ya uwekezaji imeendelea kuimarika ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Ripoti mbalimbali za uwekezaji duniani zinaonesha kuwa Tanzania imeongoza kwa kuvutia uwekezaji kati ya nchi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Uwekezaji ya Dunia (*World Investment Report*) ya mwaka 2018, inayotolewa na

Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(UNCTAD)* inaonesha kuwa Tanzania imevutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.18, ikifuatiwa na Uganda Dola za Marekani bilioni 0.7 na Kenya Dola za Marekani bilioni 0.67.

Mheshimiwa Spika, taarifa nyingine ya "*The African Investment Index* 2018 inaonesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 13 kati ya nchi 54 za Afrika katika kutoa fursa za masoko na vivutio vya uwekezaji. Vilevile, taarifa ya *"Where to Invest in Africa"* ya mwaka 2018, inaonesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya saba kati ya nchi 52 zinazovutia zaidi kwa uwekezaji Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Watanzania kuchangamkia fursa zinazojitokeza kutokana na ukuaji wa uchumi, maendeleo ya kijamii na pia uwekezaji wa Sekta ya Umma Kwenye miundombinu kwa kuthubutu kuwekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji wa biashara ikiwemo kutekeleza mapendekezo ya mpango kazi jumuishi wa kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini; kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria yake ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2017/2018 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 imeendelea kuimarika kutokana na hali nzuri ya mvua katika maeneo mengi ya nchi, kuongezeka kwa tija na uzalishaji. Uzalishaji wa mazao ya chakula umefikia tani milioni 16.89 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni 13.57. Hivyo, nchi ina ziada ya chakula ya tani milioni 3.32 na mazao yote. Hii ni hatua mzuri na ya kujivunia kwani usalama wa chakula ndiyo usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Juni 2018, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili. Programu hiyo inalenga kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo kwa maana

ya mazao, mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza pato la wakulima hususan wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha na usalama wa chakula na lishe.

Mheshimiwa Spika, ikiwa sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kilimo wa kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili, Serikali inaimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kuwa benki mama inayoongoza mipango inayolenga kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi hapa nchini. Lengo la Serikali ni kuifanya benki hiyo ya kilimo Tanzania kuwa benki ya mfano na ya kisasa katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kutoka kilimo cha mazoea cha kujikimu kwenda katika kilimo cha kibiashara na uzalishaji wenye tija katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari 2019, Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini imetoa mikopo ya shilingi bilioni 100.7 ikilinganishwa na shilingi billioni 10 ya mwaka 2017. Mikopo hiyo, imewanufaisha zaidi ya wakulima na wafugaji milioni moja nchi nzima. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania tayari imeshafungua ofisi mbili za Kanda Jijini Dodoma na Jijini la Mwanza. Rai yangu kwa Menejimenti ya Bodi ya Benki ya Kilimo Tanzania ni kwamba kamilisheni ufunguzi wa ofisi zilizopangwa kwa wakati ili kutatua changamoto za upatikanaji wa pembejeo; na miundombinu duni ya uzalishaji, usafirishaji, uchakataji wa mazao na masoko zinazokabili wakulima wadogo nchini.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao makuu ya kimkakati yakiwemo chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku umeimarika kutokana na juhudi zinazofanywa na Serikali ikiwemo kuimarisha ushirika. Kwa mfano, uzalishaji wa zao la pamba uliongezeka kutoka tani 132,934 mwaka 2017/ 2018 hadi kufikia tani 222,039 mwaka 2018/2019 wakati uzalishaji wa zao la Kahawa uliongezeka kutoka tani 45,245 hadi kufikia tani 65,000 mwaka 2018/2019. Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa mazao hayo na mengine kwa kuwa ndiyo mhimili wa kutoa malighafi za kuendesha viwanda na

yana mnyororo mpana wenye fursa ya kutoa ajira nyingi na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Uzalishaji wa zao la chikichi. Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya kununua mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Aidha, uzalishaji mdogo wa zao la chikichi ni miongoni mwa sababu za kushindwa kujitosheleza kwa mahitaji ya mafuta ya kula hapa nchini. Kutokana na changamoto hiyo, Serikali imeamua kuweka nguvu kubwa kwenye uzalishaji wa mazao za mbegu za mafuta ili kuondokana na utegemezi na kuokoa matumizi ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeanza kuimarisha kilimo cha zao la chikichi hususan katika Mkoa wa Kigoma ili kusaidia upatikanaji wa mbegu bora za chikichi. Lengo ni kuzalisha na kusambaza kwa wakulima miche ipatayo milioni 20 katika kipindi cha miaka minne (2018/2019 hadi 2021/2022). Vilevile, Serikali imeamua kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kihinga, Mkoani Kigoma kuwa Kituo cha Utafiti wa Mbegu Bora za Chikichi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maamuzi haya ya Serikali yameanza kuzaa matunda. Mathalan, hadi Februari, mwaka huu 2019, Kituo cha Kihinga kimezalisha miche 4,747 ambazo zimefanyiwa uoteshwaji wa awali. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imepanga kuzalisha miche ya chikichi milioni tano. Ni matarajio ya Serikali kwamba usimamizi mzuri wa mkakati huo wa miaka minne utalisaidia Taifa kuondokana na uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje, kutengeneza fursa mbalimbali za ajira na kuwaongezea kipato wakulima wa chikichi.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kwa zao la chikichi ni kuwa wazalishaji wakubwa kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki ambao kwa sasa nchi inayozalisha kwa wingi chikichi Afrika Mashariki ni nchi ya Burundi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali ilianzisha Dawati la Sekta Binafsi kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji katika Sekta mbalimbali za Mifugo na Uvuvi. Lengo la Serikali ni kuongeza uwekezaji wenye tija utakaowezesha wafugaji na wavuvi kuongeza kipato, kuzalisha malighafi za kutosha za viwandani na kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba Sekta ya Mifugo na Uvuvi inakua na mnyororo mpana na ongezeko la thamani kwa kutoa kipaumbele katika ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao hayo ya mifugo na uvuvi. Hadi sasa, viwanda 99 vya kusindika mazao ya mifugo vimeanzishwa vikiwemo viwanda 17 vya nyama, 76 vya maziwa na 6 vya ngozi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuweka msisitizo katika kuwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika uwekezaji kwenye viwanda, kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu na kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii imeendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa na kuongeza ajira. Mathalan, idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2018 imeongezeka na kufikia watalii milioni 1.49 ikilinganishwa na watalii milioni 1.33 walioingia nchini mwaka 2017. Vilevile, mapato yatokanayo na utalii yameongezeka na kufikia Dola za Marekani bilioni 2.43 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 2.19 mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 7.13.

Mheshimiwa Spika, katika kutangaza vivutio vya utalii, mwaka 2018/2019, Serikali imeanzisha *channel* ya utalii ijulikanayo kama *Tanzania Safari Channel* ili kuvutia Watanzania na wageni kutoka Mataifa mbalimbali kutembelea vivutio vyetu. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha *channel* hiyo kwa kuipatia wataalam, vifaa na

vitendea kazi stahiki. *Channel* hii itaendeleza taswira ya sifa nzuri ya Tanzania ya Kimataifa sambamba na kuongeza thamani katika mnyororo mzima wa biashara ya utalii hapa nchini. Nafurahi kuwajulisha kwamba, jana tumepokea watalii 333 kutoka nchi mbalimbali duniani walioingia na Meli yao kubwa ya kitalii iliyoko kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya utalii kwa kuhamasisha na kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuendeleza sekta hiyo ya utalii. Aidha, sanjari na kutangaza utalii, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ikiwemo usafiri wa anga, meli, barabara ili kuvutia watalii wengi zaidi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda; sote tunatambua kwamba dhima ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu wetu. Katika kipindi cha miaka mitatu ya kutekelezwa azma hii, Serikali inaridhika kuona hamasa na uthubutu wa Watanzania kwa kushirikiana na nchi rafiki kuhamasika na kuwekeza katika ujenzi wa viwanda. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda hapa nchini. Vipaumbele ni katika viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini, viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi na kuendelea kubainisha maeneo ya viwanda katika mikoa yote na kuendeleza maneo maalum ya uwekezaji; *EPZ* na *SEZ* pamoja na Kongani za viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ya Serikali ni kuinua uchumi wa wananchi kwa kuwawezesha kupata mitaji ya kufanyia kazi zao. Katika kufanikisha malengo hayo, Serikali kupitia *SIDO* imeendeelea kuratibu Mfuko wa Wafanyabiashara wa Wananchi *(National Enterpreneurship Development Fund).* Katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.74 ilitolewa ambapo mikopo 520 yenye thamani ya shilingi milioni 788

ilitolewa kwa wanawake na mikopo 493 yenye thamani ya shilingi milioni 958.8 ilitolewa kwa wanaume.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza azma ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020/2025 kwa kuongeza uwekezaji katika viwanda, Serikali inaendelea kuandaa mipango kabambe ya miji na kuhakikisha maeneo yanatengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda lakini pia katika mpango kabambe wa miji 17 iliyokamilika na ile inayoandaliwa jumla ya hekari 127,859 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Vilevile kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji wa Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Kilosa, Serikali imetanga hekta 2,710 za ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo. Pia mamlaka za upangaji zimeagizwa kuzingatia utengaji wa asilimia 10 ya kila eneo la mpango kabambe wa mji kwa ajili ya uwekezaji wa kibiashara na viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Serikali imeandaa mwongozo wa tathmini ya mazingira kimkakati ambao utawezesha mpango wa uchumi na viwanda kufanyiwa tathmini namazingira ya kikakati. Katika maboresho ya Kanuni yaliyofanyika, yanampa Waziri mwenye dhamana ya mazingira mamlaka ya kutoa vibali vya muda kwa ajili ya miradi ya uwekezaji kwenye sekta ya viwanda na hivyo kuboresha taratibu za uwekezaji wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuhuisha, kuboresha na kutekeleza sera, sheria, taratibu na mikakati ya maendeleo ya viwanda, biashara pamoja na masoko hususani kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini, kuimarisha na kusimamia mfumo wa biashara ya ndani, kutumia kikamilifu fursa za masoko yenye unafuu wa kodi na usio wa kodi. Vilevile Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Taasisi zinazohusika na maendeleo ya viwanda na kuhamaisha uanzishaji wa maendeleo ya viwanda vidogo hasa vile vya kati na vikubwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini; kwa kutambua umuhimu wa sekta ya madini na mchango wake katika kukuza uchumi, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutoa kipaumbele katika kulinda rasilimali za madini na kuhakikisha zinawanufaisha Watanzania wote. Katika hilo tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuelekeza mamlaka za Serikali kutunga Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili, Na.5 ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili na Nchi, Na.6 ya mwaka 2017 pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura Na.123. Katika hili, ninayo nafasi pia ya kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge mlioridhia kuipitisha Sheria hii ambayo sasa inafanya kazi na inaleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kutoa kipaumbele kwa wachimbaji wadogo kwa kuwapatia maeneo ya uchimbaji, kuwakopesha zana za uchimbaji, kuwapatia utaalam na matumizi ya tekonolijia katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Aidha, Serikali inashughulikia kero zinazowakabili wachimbaji wadogo ili waweze kuendesha shughuli zao za uchimbaji mdogo na kunufaika na rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Spika, mfano wa utekelezaji wadhamira hiyo nzuri ya Serikali ni kitendo cha Mheshimiwa Rais kukutana na kufanya mazungumzo na wachimbaji wadogo mwezi Januari, 2019m Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuwasikiliza na kutatua kero zao. Vilevile Mheshimiwa Rais aliekeleza kufutwa kwa kodi ya nyongeza ya thamani na kodi ya zuio kwa wachimbaji wadogo, maelekezo ambayo tayari yameshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kufutwa kwa kodi na tozo hizo, kunatarajiwa kupunguza utoroshwaji wa madini, kuwatambua wachimbaji wadogo kupitia maoko ya madini yatakayoanzishwa na kuwapunguzia gharama za uendeshaji wa shughuli zao za uchimbaji mdogo mdogo. Hatua hiyo pia itaongeza wigo wa mapato kwa nchi kwa kuwa sasa madini yatauzwa katika utaratibu unaotambulika rasmi hapa hapa

ndani ya nchi. Rai yangu kwa wachimbaji wote wadogo, endeleeni kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali katika kutekeleza majukumu yenu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali iteendelea kukuza soko la ndani la madini kwa kuvutia wawekezaji na kuhamasisha shughuli za uongezaji wa thamani ya madini nchini. Pia mkazo utawekwa katika kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa masoko ya madini yenye ushindani mkubwa ili kudhibiti utoroshaji wa maliasili hiyo. Aidha, Serikali itaendelea kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo wa madini ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo, huduma za utafiti, teknolojia, mitaji na masoko.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati; dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa viwanda sambamba na kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme unatosha na upatikanaji wa umeme huo uwe ni wa uhakika na wa bei nafuu. Kwa kutambua hilo, Serikali inatekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji wa umeme yenye lengo la kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na ukuaji wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba mwaka 2018, niliungana na Mheshimiwa Dokta Mustapha Madoul, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, kushuhudia uwekaji saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme wa *megawatts* 2,100 katika ya Shoirika la umeme Tanzania *(TANESCO)* na Kampun ya *JV Arab contrators Elsewaid electric* ya Misri. Mradi huo unaotarajiwa kukamilika mwaka 2021/2022 utawezesha ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuhakikisha upatikanaji wa umeme tena kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari 2019, uwezo wa jumla ya mitambo kuzalisha umeme nchini umeongezeka kutoka takribani *megawatts* 1,205 mwaka 2015 hadi kufikia *megawatts* 1,614 mwaka 2019. Ongezeko hilo limewezesha kuwa na umeme wa ziada na wastani wa zaidi ya *megawatts* 300.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza kwa mafaniko makubwa mpango wa usambazaji wa umeme vijijini. Katika mwaka 2018/2019, vijiji 511 vimeunganishwa na umeme. Aidha, tangu kuanza kwa usambazaji wa umeme vijiji tayari 5,746 vimeunganishwa umeme kati ya vijiji 12,268 vilivyopo nchini sawa na takribani asilimia 47 ya vijiji vyote na uwekaji wa umeme huu haungalii ubora wa nyumba. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekelezaji miradi ya uzalishaji umeme wa maji na kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu ambapo vijiji vyote vitakavyosalia vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, huduma za kiuchumi; sekta ya ardhi; rasilimali ardhi ina umhimu wa pekee katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na uzalishaji mali. Kutokana na umuhimu huo, Serikali inachukua hatua madhubuti za kuiendeleza rasilimali hii kwa kuipanga vizuri, kuipima na kuimilikisha kwa Taasisi na wananchi mmoja mmoja kama inavyopaswa. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa mwaka 2013 - 2033 ambapo jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 263 katika Wilaya 45 imeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro, Wizara za kisekta zimeanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais tarehe 15 Januari, 2019. Maelekezo hayo ni pamoja na kurasimisha vijiji 351 vilivyokuwemo kwenye hifadhi za misitu na mapori tengefu yaliyokosa sifa pamoja na kufuta jumla ya hekari 121,032 za ranchi na mashamba yaliyotelekezwa. Hatua hizi zimewezesha wananchi kupata ajira na pia kupata sehemu za kufanyia shughuli zao za kilimo, ufugaji na makazi.

Mheshimiwa Spika, kupitia mradi wa mikopo ya nyumba unaosimamiwa na Benki kuu ya Tanzania, Serikali imeshusha riba ya mikopo inayotolewa kwa wananchi kwa Mabenki na Taasisi za fedha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 7.5 na jumla ya wananchi 4,174 wamenufaika na mikopo inayotolewa na Benki ya Taasisi hizi za fedha. Aidha, Mfuko

wa Mikopo Midogo Midogo ya Nyumba ulio chini ya Benki Kuu umeongezewa mtaji wa Dola za Marekani milioni 18 ambapo Taasisi za Fedha tano zimepatiwa mtaji wa shilingi bilioni 13.87 kwa ajili ya kukopesha wananchi wa kipato cha chini kwa masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa 2013 - 2033 ikiwemo kupima, kupanga, kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini na kutekekeleza program ya kurasimisha makazi katika miji mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulinda hifadhi na vyanzo vya maji ili kuleta manufaa endelevu kwa Taifa na pia kuhimiza kilimo na ufugaji wenye tija utakaoleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, barabara; lengo la Serikali ni kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami ili kuimarisha na kurahisisha mawasiliano ya usafiri na usafirishaji wa watu, bidhaa na mazao mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2019 jumla ya kilomita 266.78 za barabara kuu na za mikoa zimekamilika na kilomita 392.2 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Halikadhalika, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja matano katika Mto Lukuledi kule Lindi, Mara Mkoani Mara, Sibiti (Singida), Momba, Rukwa na Songwe na Mlalakuwa (Dar es Salaam) na ujenzi wa madaraja nane unaendelea katika sehemu mbalimbali nchini. Ujenzi wa miradi hii, utatoa fursa mbalimbali kwa wananchi kupata ajira pamoja na kupata soko kwa bidhaa na mazao wanayoyalima.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa miradi ya barabara inayolenga kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa barabara kuwezesha mradi wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji kwa kiwango cha changarawe kutoka Ubena Zomozi mpaka Selous kilomita 177.6 na ukarabati wa barabara ya kutoka Kibiti kupitia Mloka mpaka Selous yenye urefu wa kilometa 201. Miradi mingine ni pamoja na ujenzi wa barabara kutoka

Tabora kwenda Mpanda, kilometa 370; Makutano–Natta–Mugumu–Loliondo, kilometa 239; Loliondo–Mto wa Mbu, kilometa 213; na barabara ya Kidatu–Ifakara–Lupilo kwenda Malinyi kupitia Londo mpaka Lumecha yenye urefu wa kilometa 464.

Mheshimiwa Spika, kuondoa Msongamano wa Magari Jijini Dar es Salaam; Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kuondoa msongamano wa magari kwenye Jiji la Dar es Salaam, ili kurahisisha usafiri na usafirishaji na kuchochea shughuli za kiuchumi. Miradi iliyokamilika ni ujenzi wa barabara ya juu ya Mfugale na barabara za mlisho. Miradi inayoendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni:-

Ujenzi wa Barabara za juu kwenye makutano ya Ubungo (Ubungo *interchange);* Upanuzi wa barabara ya Kimara Mwisho mpaka Kiluvya ya kilometa 19.2 kutoka njia mbili za sasa na kuwa njia nane; Daraja Jipya la *Salender* na Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka awamu ya pili na ya tatu. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa mikoa ambayo haijaunganishwa na barabara kuu za lami.

Mheshimiwa Spika, suala la vivuko; katika mwaka 2018/2019, Serikali imekamilisha ujenzi wa vivuko viwili vipya vya Magogoni mpaka Kigamboni na Kigongo mpaka Busisi. Aidha, ujenzi wa vivuko vipya vinne vya Kayenze–Bezi, Nyamisati–Mafia, Nkome-Chato–Muharamba na Bugolora mpaka Ukara unaendelea. Vilevile, Serikali imekamilisha ukarabati wa kivuko cha *MV*.Pangani II kiko Pangani) na ukarabati mkubwa wa vivuko viwili vya *MV*.Sengerema (Mwanza) na *MV*.Kigamboni (Dar es Salaam) na *MV*. Utete kule Rufiji unaendelea. Serikali pia, imekamilisha ujenzi wa maegesho ya Bwina (Geita), Lindi–Kitunda kule Lindi pia taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya Nyamisati–Mafia, Mkoani Pwani, Kayenze-Bezi (Mwanza) na Mlimba-Malinyi kule Morogoro zenyewe zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege; katika kuimarisha usafiri wa anga nchini, Serikali inakamilisha ujenzi wa Jengo la Tatu la abiria katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Jijini Dar es Salaam. Jengo hilo ambalo hadi kufikia Februari, 2019 ujenzi wake umefikia asilimia 95.5, litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka pindi litakapokamilika mwaka 2019. Jengo hilo linatarajiwa kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu cha utalii kwa kuwezesha watalii wanaoingia nchini kuelekea katika maeneo mbalimbali ya vivutio vyetu na Nchi jirani katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Mheshimiwa Spika, mpango huo wa kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu cha utalii unakwenda sambamba na maboresho ya Shirika la Ndege la Tanzania. Lengo ni kuhakikisha watalii wanaoingia nchini wanakuwa na usafiri wa uhakika kufikia vivutio vyetu na kuelekea katika nchi za jirani. Kwa kufanya hivyo, shughuli za kiuchumi nchini zenye kufungamana na utalii hususani ajira, huduma, biashara na usafirishaji zitaimarika na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhamira ya kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kisasa, Serikali inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato. Lengo la Serikali ni kulifanya Jiji la Dodoma ambalo ndilo Makao Makuu ya Nchi kuwa kitovu cha mawasiliano na maeneo mengine nchini. Kwa sasa kazi inayoendelea ni kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja kuendana na hadhi na mahitaji ya Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa viwanja vingine vya ndege vya Songwe, Kigoma, Sumbawanga, Shinyanga, Tabora, Mtwara, Songea, Nachingwea, Lindi, Iringa na Musoma ambavyo viko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, sekta ya reli; ujenzi wa awamu ya kwanza wa Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam hadi

Morogoro umefikia asilimia 42.8 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Novemba, 2019. Halikadhalika, ujenzi wa awamu ya pili wa reli hiyo ya kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora Jijini Dodoma umefikia asilimia 6.07. Hadi sasa Mradi kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora umeshaajiri wafanyakazi wazawa wapatao 6,335 sawa na asilimia 90 ya wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi wa reli mpya ya kisasa, Serikali katika mwaka 2018/2019, imeendelea na kazi ya kuboresha, kujenga na kukarabati miundombinu ya reli ya kati kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenye uzani wa paundi 80 kwa yadi kati ya Stesheni ya Dar es Salaam na Isaka, Tabora-Uvinza kwenda Kigoma na mpango endelevu ni kutoka Uvinza mpaka Msongati ili kuunganisha na nchi jirani za Burundi na Rwanda. Aidha, kazi ya ukarabati wa reli ya Tanga–Arusha imekamilika kwa sehemu ya Tanga mpaka Same kilometa 199. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali inaendelea na kazi ya ujenzi wa reli ya kisasa, ukarabati na ujenzi wa reli ya kati na nyingine ikiwemo ya Tanga, Arusha ili kuimarisha huduma za usafirishaji wa mizigo na abiria kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, sekta ya bandari. Katika mwaka 2018/2019 kazi ya kuboresha Bandari ya Dar es Salaam kupitia mradi wa *Dar es Salaam Maritime Gateway* inaendelea vizuri. Lengo la Serikalini ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri wa majini na kuiwezesha kushindana na bandari nyingine katika ukanda huu. Kazi za kuboresha gati namba moja hadi gati namba saba na ujenzi wa gati jipya la kuhudumia meli za magari zimekamilika kwa asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kumaliza changamoto ya usafiri kwa njia ya maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kutekeleza azma hiyo, Septemba, 2018 Serikali iliingia mikataba minne na Kampuni ya KTMI ya Jamhuri ya Korea

kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya za kisasa Ziwa Victoria, chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria na Mv Butiama.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa meli mpya itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo na magari madogo 200 utafanywa na kampuni ya KTMI kwa kushirikiana na SUMA JKT. Aidha, ujenzi na ukarabati wa meli hizo utakwenda sambamba na kujenga uwezo wa wataalam wetu wa ndani katika tasnia ya ujenzi na ukarabati mkubwa wa meli kwa kushirikiana na kampuni zitakazotekeleza ujenzi huo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali itasimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika na ukarabati mkubwa wa meli za MV Liemba, MV Umoja na MV Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Ninayo furaha kubwa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka wa fedha 2018/2019 Zanzibar imeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kupitia utekelezaji wa awamu ya tatu ya ujenzi, huduma kwa wateja zinaanza kupatikana Jun, 2019. Matumizi ya huduma za Mkongo kwa upande wa Zanzibar yatachochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kuinua kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, sambasamba na Mkongo wa Taifa, Kituo cha Data cha Taifa kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi hasa katika kuongeza ukusanyaji wa mapato Serikalini. Hadi kufikia Desemba 2018, kituo kimeweza kuunganisha wateja 79 ambapo taasisi na Idara za Serikali ni 56 na taasisi binafsi 23. Uhamasishaji unaendelea kwa kuunganisha taasisi nyingi zaidi ili kuendelea kukuza usalama na kupunguza gharama za uendeshaji wa miundombinu ya TEHAMA hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuhakikisha kunakuwepo udhibiti wa kutosha katika mawasiliano, Serikali ilipokea mfumo wa kusimamia mawasiliano wenye uwezo wa kubaini takwimu mbalimbali

zinazopita katika mtandao ya mawasiliano. Mfumo huo pamoja na mambo mengine utasaidia kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika Sekta ya Mawasiliano kwa kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha, sanjari na kudhibiti matumizi mabaya ya mtandao kwa kugundua mawasiliano ya ulaghai.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma hiyo katika Makao Makuu ya Wilaya zote hapa nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha taasisi na wateja wengine kuunganishwa na Kituo cha Data cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu. Serikali inatekeleza kwa mafanikio makubwa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo wenye lengo la kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania mwenye umri wa kwenda shule anapata haki ya kupata Elimumsingi bila kikwazo cha ada na michango mingine isiyokuwa na tija. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu Serikali imetumia shilingi bilioni 711.22 kuteleza mpango huo. Katika mwakawa fedha 2018/2019, Serikali tayari imeshatoa shilingi bilioni 166.44 hadi Februari, 2019 kwa ajili ya kutekeleza mpango wa Elimumsingi Bila Malipo hapa nchini. Utekelezaji wa mpango huo umeongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za msingi na sekondari nchini kote.

Mheshimiwa Spika, sambasamba na utekelezaji wa Elimumsingi Bila Malipo, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na washirika wa maendeleo imeboresha miundombinu ya shule za awali na msingi ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa 6,521 kwa shule za msingi na hivyo kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka 119,647 vilivyokuwepo mwaka 2017 hadi 126,168 Februari, 2019, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Kwa upande wa shule za sekondari vyumba 2,499 vya madarasa vimejengwa na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka 40,720 mwaka 2018 hadi 43,219 kufikia Februari, 2019. Aidha, madarasa 2,519 yako katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Taifa letu linajenga uchumi ulio imara, jamii inayoheshimu na kufuata misingi ya uwajibikaji na ubunifu, Serikali pamoja na mambo mengine imeendelea kuwekeza katika elimu ya juu. Serikali imeendelea kuhakikisha Watanzania wote wenye sifa wanapata elimu ya juu kwa kupewa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Katika mwaka 2018/2019, shilingi bilioni 412.4 zimetolewa kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Hatua hiyo imeongeza idadi ya wanufaika wa mikopo hiyo kufikia wanafunzi 119,214 kutoka wanafunzi 98,300 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa wigo wa utoaji elimu nchini unapanuka, hivyo ili kulinda ubora wa elimu yetu nazielekeza mamlaka zote zinazohusika na usimamizi na udhibiti wa ubora wa elimu zitekeleze majukumu yao ipasavyo ili kulinda kiwango chetu kwa kutoa miongozo na kufanya kaguzi za mara kwa mara katika ngazi zote za shule.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji. Upatikanaji wa maji vijijini. Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kwa kujenga miradi ya maji ili kusogeza huduma hizo karibu zaidi na wananchi. Hadi Februari, 2019, jumla ya miradi 65 ya maji vijijini ilikamilishwa ambapo wananchi milioni 25.36 waishio katika vijiji hivyo wamenufaika. Kutokana na kukamilika kwa miradi hiyo, hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka kutoka asilimia 58.7 Julai, 2018 kufikia asilimia 64.8 Februari, 2019. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali itaendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa na kukamilisha miradi mingine 482 iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwenye Halmashauri zetu kote nchini.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji mijini. Serikali imetekeleza miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ili kuongeza upatikanaji wa huduma za maji na salama kwa wananchi walio katika miji hiyo. Hadi Februari, 2019, upatikanaji wa maji safi na salama katika Jiji la Dar es Salaam

na maeneo mengine yanayohudumiwa na DAWASA umeshafikia asilimia 85.

Mheshimiwa Spika, katika Miji Mikuu ya Mikoa upatikanaji wa huduma za maji imefikia wastani wa asilimia 80. Aidha, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miji ya Kitaifa upatikanaji wa huduma ya maji imefikia wastani wa asilimia 64. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kukamilisha miradi mbalimbali ya maji pamoja na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria mpya ya huduma za maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya. Miundombinu ya huduma za afya. Ujenzi wa uchumi wa viwanda unakwenda pamoja ujenzi wa Taifa lenye watu wenye afya, tena afya bora wanaoweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi husika. Kwa msingi huo, Serikali inaimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kujenga, kukarabati na kuvipatia mahitaji muhimu vituo vyote vya kutolea huduma za afya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha azma hiyo, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kutoka vituo 7,678 mwaka 2017 hadi 8,119 mwaka 2018, sawa na ongezeko la vituo 441. Ongezeko hilo limesaidia kusogeza huduma ya afya karibu zaidi na wananchi na hivyo kupunguza kwa kasi kubwa vifo vya mama na watoto na watoto wachanga pamoja na kuboresha afya za wananchi wetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa hospitali. Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali tano za mikoa ambayo ilikuwa haina hospitali kabisa za rufaa. Katika miradi hiyo jumla ya shilingi bilioni 6.5 zimetolewa kwa Mikoa mipya ya Songwe, Katavi, Njombe, Geita na Simiyu. Vilevile Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali 67 katika Halmashauri mbalimbali ambapo jumla ya shilingi bilioni 100.7 sawa na shilingi bilioni 1.5 kwa kila Halmashauri zimetolewa na kazi zinaendelea katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, Serikali itaboresha zaidi miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa miundombinu hiyo, kuendelea na ujenzi Hospitali za Rufaa za Mikoa isiyokuwa na hospitali pamoja na kuendelea na ujenzi Hospitali za Wilaya katika Halmashauri ambazo hazina hospitali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini unakwenda sambamba na upatikanaji wa dawa na vifaa na vifaa tiba. Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini sasa imefikia asilimia 96.7 kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa, Serikali imefunga mashine mpya za *X-ray* 11 katika Hospitali za Mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Simiyu, Mji wa Magu, Mikoa ya Chato, Singida, Nzega, Njombe, Bukoba, Amana na Mpanda. Vilevile, Serikali imekamilisha kuweka mashine za *MRI, CT- SCAN, Digital X-ray mashine, Modern Ultrasound Mashine* na vifaa vya wodini vyenye thamani ya shilingi bilioni 12 katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma za afya za kibingwa. Serikali imeimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Hospitali ya Benjamin Mkapa. Huduma za kibingwa zinazotolewa ni upandikizaji wa figo, upasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo, upasuaji wa mishipa ya fahamu na upandikizaji wa nyonga pamoja upandikizaji wa vifaa vya kusaidia usikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma hizi za kibingwa ambazo awali zilikuwa zinapatikana nje ya nchi

pekee umepunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Junuari, 2019 kulikuwa na wagonjwa 38 waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi ikilinganishwa na wagonjwa 114 katika kipindi hicho kwa mwaka 2019. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaimarisha huduma za kibingwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali za Magonjwa Maalum kwa kuendelea na ujenzi wa majengo ya kutolea huduma, kusimika mitambo ya uchunguzi pamoja na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa wanawake na watoto. Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 mpaka mwaka 2021/2022. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeanzisha Kamati 3,605 za ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi mbalimbali. Kati ya hizo, Kamati 1,289 zimeanzishwa katika ngazi za Kata na Kamati 2,313 katika ngazi za mtaa na kijiji.

Mheshimiwa Spika, lengo la Kamati hizi ni kuhakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama kwa wanawake na watoto katika jamii yetu hapa nchini. Aidha, uanzishaji wa Kamati umeongezeka kutoka Kamati 7,383 mwaka 2017 hadi Kamati 10,988 mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 48.83. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha utaratibu wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ulioanza mwaka 2017 hadi 2022.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa wazee. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa wazee nchini wanapata matibabu kupitia vitambulisho vinavyowawezesha kupata matibabu bure. Katika mwaka 2018/2019, wazee 247,771 wamepatiwa kadi za matibabu bure. Juhudi hii imewezesha wazee waliopata vitambulisho vya matibabu bure kuongezeka kutoka wazee 213,025 mwaka 2015/2016 hadi kufikia wazee 1,042,329 mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la wazee 829,304. Serikali itaendelea kuwatambua wazee

wote nchini na kuhakikisha kwamba inawapatia vitambulisho ili wazee wote hapa nchini wapate matibabu bure.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa watu wenye ulemavu. Mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikataba inayohusu haki na huduma kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Na.9 ya mwaka 2010. Sheria hiyo pamoja na masuala mengine inamtaka kila mwajiri mwenye waajiriwa kuanzia 20 kuwa na watumishi wenye ulemavu wasiopungua watatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kutoa chakula, matibabu, malazi, ushauri nasaha na mafunzo ya stadi za kazi kwa wanafunzi wenye ulemavu katika vyuo vya Singida na Yombo Jijini Dar es Salaam. Vilevile, Serikali imewezesha upatikanaji wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufikia huduma mbalimbali bila vikwazo. Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na viti mwendo, fimbo nyeupe, magongo ya kutembelea, viti maalum vya kuogea, miwani maalum, kofia pana, vifaa vya kukuzia maandishi, mafuta kinga kwa ajili ya watu wenye Ualbino na mashine za kuchapia maandishi ya nukta nundu kwa wasioona.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeratibu maadhimisho ya siku za watu wenye ulemavu ili kuondoa unyanyapaa miongoni mwa jamii ikiwa ni pamoja na siku ya fimbo nyeupe, siku ya viziwi na siku ya watoto wenye ulemavu. Katika maadhimisho hayo, elimu ya kutowanyanyapaa watu wenye ulemavu huwa inatolewa. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu uundwaji wa Kamati za watu wenye ulemavu ambapo Kamati 26 zimeshaundwa katika mikoa yote Tanzania Bara, ngazi ya Halmashauri Kamati 140, ngazi ya Vijiji Kamati 5,024 na ngazi ya Mitaa Kamati 2,284.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu, Serikali imekamilisha uundaji wa Baraza jipya la Ushauri la Taifa kwa watu wenye ulemavu baada ya lile lililopita kumaliza muda wake. Ni matarajio ya Serikali kwamba Baraza hilo litaendelea kutekeleza majukumu

yake na kuishauri Serikali kuhusu huduma kwa watu wenye ulemavu hususani masuala ya afya, ajira, miundombinu pamoja na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itafanya mapitio ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Na.9 ya mwaka 2010 ili iweze kwenda na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, kukusanya maoni na mapendekezo ya uendeshwaji wa Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu pamoja na kuratibu uendeshaji wa shughuli za Baraza la Ushauri la Taifa kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na usalama. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba hali ya amani, usalama na utulivu nchini inaimarika. Katika mwaka wa 2018/2019, Serikali imelitumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania kusaidia mamlaka za kiraia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali kama vile uokoaji wa watu na mali zao pamoja na ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Mtumba hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi Tanzania limeendelea kushiriki kwenye misheni za kulinda amani nchini chini ya mwamvuli wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Misheni hizo ni kama vile *MINUSCA* huko Jamhuri ya Afrika ya Kati *(CAR), MONUSCO* Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)*, *UNAMID* - nchini Sudan, *UNFIL* – nchini Lebanon, *UNISFA* huko Abyei na *UNIMISS* nchini Sudan Kusini.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Jeshi letu pamoja na vyombo vingine vya usalama katika misheni hizo za amani, umeendelea kuvipatia uzoefu, kuongeza maarifa na mbinu mbalimbali za kijeshi na kiintelijensia. Aidha, vyombo vyetu vimeendelea kujifunza matumizi ya vifaa vya kisasa na kuanzisha au kuimarisha mahusiano ya kijeshi na nchi nyingine zinazoshiriki kwenye misheni hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, Serikali itaendelea kuimarisha hali ya ulinzi na usalama,

kuendelea kutoa fursa za mafunzo kwa vyombo vya ulinzi na usalama, kuvipatia vifaa na zana za kisasa na kuendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka.

Mheshimiwa Spika, nguvukazi ya vijana ni mhimili muhimu katika kuiwezesha nchi yetu kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Vijana imewezesha vikundi vya vijana 755 ambavyo vimepatiwa mikopo ya shilingi bilioni 4.2 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya vijana.

Aidha, imeibua bunifu 31 za Vijana katika sekta ya sayansi na teknolojia. Kati ya hizo, bunifu 11 zimefanyiwa tathmini ya kisayansi na kwa sasa ziko katika hatua mbalimbali ikiwemo kuwekwa kwenye kiota atamizi *(incubator)* kabla ya hatua ya majaribio ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, bunifu nyingi zimefanyika nchini kama vile kifaa cha kupimia matatizo ya moyo, kiti maalum cha kuhudumia watoto wenye usonji, mfumo wa kuwasha na kuzima taa za nje ya ndege kwa kutumia simu ya mkononi, mguu wa ndege kwa ajili ya matumizi ya kufundishia vyuoni na gari linalotumia mfumo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, Serikali itaendelea kuwawezesha vijana kimitaji kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, mapato ya ndani ya Halmashauri na Programu za kukuza ujuzi.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa nguvukazi ya Taifa hususan vijana ni muhimu katika kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Hivyo basi, Serikali inatekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi inayolenga kuwapatia vijana ujuzi stahiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi kwa kujiajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, jumla ya vijana 32,563 wamewezeshwa kupata mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa. Hii inahusisha vijana 18,800 waliopata mafunzo ya ujuzi wa kilimo kwa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba pamoja na vijana 2,720 waliopatiwa mafunzo ya ufundi kwa fani mbalimbali pamoja vijana 10,443 waliopatiwa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kwa fani za ufundi wa magari, useremala, uashi, upishi, huduma za vyakula na vinywaji, ufundi umeme, uchomeleaji, ufundi bomba, uchongaji vipuri na ushonaji nguo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri, kuajiriwa na stadi za kazi kwa vijana 46,950 katika fani mbalimbali. Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza vijana kote nchini kuchangamkia fursa za mafunzo haya kwa kuwa ni nyenzo muhimu kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa fursa za ajira umeendelea kuwa agenda ya kipaumbele ya Serikali ya Awamu ya Tano. Suala hilo, limezingatiwa katika sera, mipango na programu zote za maendeleo ya Kitaifa na kisekta. Hadi kufikia Februari, 2019, jumla ya ajira 221,807 zimezalishwa nchini kote.

Mheshimiwa Spika, kati ya ajira hizo, ajira 146,414 sawa na asilimia 66 zimetokana na utekelezaji wa miradi ya Umma mikubwa ya ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi kama vile ujenzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa reli za kisasa, ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji, umeme, ujenzi wa Mji wa Serikali hapa Jijini Dodoma, uimarishaji wa Shirika la Ndege Tanzania pamoja na ajira za moja kwa moja katika Utumishi wa Umma. Aidha, ajira 75,393 ambazo ni asilimia 34 ya ajira zilizozalishwa zimetokana na uwekezaji katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan Waajiri na Wafanyakazi, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo pamoja na Vyama vya Kiraia itaendelea kutekeleza programu zinazowezesha kuibua fursa zaidi za ajira.

Mheshimiwa Spika, utulivu na amani mahali pa kazi ni nguzo muhimu kuwezesha uzalishaji na tija katika maeneo mbalimbali ikiwemo viwandani na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa kutambua ukweli huu, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ili kuwezesha mazingira yanayopelekea kazi za staha pamoja na uwepo wa amani na utulivu mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya kaguzi 2,516 zimefanyika zikihusisha kaguzi za kawaida 2007, kaguzi maalum 382 na kaguzi za ufuatiliaji 127. Vilevile, jumla ya Amri Tekelezi 455 zilitolewa kwa waajiri na waajiri 16 walifikishwa Mahakamani kwa kukiuka Sheria za Kazi. Jumla ya shilingi milioni 285 zilitozwa kama adhabu kwa Waajiri waliopatikana na hatia. Aidha, jumla ya Waajiri 414 na Wafanyakazi 2,572 walielimishwa kuhusu Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi kwa kusimamia uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi Mahali pa Kazi. Katika mwaka 2018/2019, Mabaraza 116 yameundwa na Mabaraza 110 yamepewa elimu kuhusu wajibu na majukumu yao na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi. Aidha, katika kuimarisha mahusiano mema miongoni mwa viongozi wa vyama vya wafanyakazi, vikao tisa vya maridhiano vilifanyika kwa lengo la kusuluhisha migogoro ya kivyama na viongozi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inasimamia na kuratibu ajira za wageni nchini kwa kutumia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya mwaka 2015. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya vibali vya kazi 8,703 vilitolewa, jumla ya maombi 974 yalikataliwa na maombi 1,701 yalipewa msamaha. Aidha, katika kusimamia na kuratibu Huduma za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira Nchini, jumla ya maombi 20 ya wakala yamepatiwa usajili na maombi matatu yamekataliwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria za kazi ili kuwezesha utulivu mahali pa kazi na hivyo kuchochea uwekezaji na ukuzaji wa uchumi. Hii itahusisha kufanya kaguzi

za kazi, kufanya mapitio na marekebisho ya sheria na kufanya utambuzi wa wadau wanaotekeleza shughuli za kukomesha utumikishwaji wa watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imeanza utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya Mwaka 2018 kwa kuunganisha Mifuko ya *LAPF, GEPF, PSPF* na *PPF* na kuanzisha mfuko wa pamoja *PSSSF*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho hayo, Serikali imeshalipa madeni yote ya wastaafu wa *PSSF, PSPF* wa mwaka 2017/2018 wapatao 9,971 yenye thamani ya Shilingi bilioni 818.39. Hatua hii ni kubwa kwa kuwa imeweza kutatua kero za wastaafu ambazo zilidumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Desemba, 2018, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania ambapo alielekeza kila Mfuko wa Pensheni uendelee kutumia kikotoo chake cha zamani katika kipindi cha mpito cha miaka mitano ijayo. Katika kutekeleza maagizo hayo, *PSSSF* kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi imeandaa Mpango Kazi wa namna ya kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha mpito (2019 – 2023) ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa jumla ya wastaafu 81,525 wa mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa kushirikiana na Shirikisho la Wafanyakazi ili kuwezesha kupata kanuni ambazo zitakidhi matarajio ya wafanyakazi wa Sekta ya Umma na Binafsi na kuhakikisha kwamba mifuko inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Masuala Mtambuka. Kwa wale ambao mnatumia vitabu, Masuala

Mtambuka mjielekeze ukurasa wa 74 wa Kitabu cha Hotuba kilichoko Mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inaendelea kutekeleza majukumu yake ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwa ni pamoja na kuelimisha Umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria. Aidha, Serikali imeendelea kujenga uelewa kwenye Taasisi za Umma na kuweka mfumo thabiti wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu ili kupata matokeo yaliyo bora zaidi katika vita dhidi ya Rushwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji mzuri wa Mkakati huo na juhudi zinazofanywa na TAKUKURU na wadau wengine nchini, katika kupambana na rushwa, rushwa sasa imepungua. Katika upimaji wa hali ya rushwa uliofanywa na mashirika ya Kimataifa yameonesha Tanzania kufanya vizuri miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano, ripoti ya taasisi ya *Transparency International* ya mwaka 2018, Tanzania imeshika nafasi ya pili baada ya Rwanda kwenye mapambano dhidi ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu katika Sekta zote kwa mfumo jumuishi na msisitizo ukiwekwa kwenye mfumo wa mrejesho kwa wadau kama nguzo muhimu ya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati huu. TAKUKURU pia itaendelea kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea na tuhuma mpya zitakazojitokeza pamoja na kuendesha mashauri yanayoendelea Mahakamani na mashauri mapya yatakayofunguliwa Mahakamani. Aidha, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 itahuishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mapambano dhidi ya uzalishaji, uuzaji, usambazaji na utumiaji dawa za kulevya. Aidha, Serikali imeendelea kubaini mtandao wa waingizaji wa dawa hizo hapa nchini na

kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahalifu hao. Kutokana na juhudi hizo, mwezi Septemba, 2018, nchi yetu ilipata heshima kubwa ya kuandaa Mkutano wa Mwaka wa Wakuu wa Vyombo Vinavyopambana na Dawa za Kulevya Afrika *(HONLEA AFRICA)* uliofanyika Jijini Dar es Salaam. Kupitia mkutano huo, vyombo vyetu vya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya viliweza kubadilishana mbinu, uzoefu, kupeana mikakati ya kukabiliana na changamoto ya dawa za kulevya pamoja na kubadilishana taarifa kuhusu kadhia hiyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Januari, 2019, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola imefanikiwa kukamata watuhumiwa 11,617 wakiwa na dawa za kulevya za aina mbalimbali kama vile *heroin, cocaine*, bangi na mirungi. Aidha, ekari zaidi ya 59 za mashamba ya bangi ziliteketezwa nchini katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma, Kagera na Mara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa waraibu wa dawa za kulevya, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa kutumia dawa ya *Methadone* katika Mkoa wa Dar es Salaam na vituo vipya katika Mikoa ya Dodoma, Mwanza na Mbeya. Aidha, kufikia Januari 2019, watumiaji wapatao 6,500 wanapata huduma za tiba ya *Methadone* katika vituo vilivyopo hapa nchini, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa waraibu wanaopatiwa matibabu hawarejei tena kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha azma hiyo, Serikali imetenga shilingi billion mbili kwa ajili ya ukuzaji ujuzi wa vijana hawa. Mpango huo utawahusisha vijana ikiwa ni pamoja na wale walioachana na matumizi ya dawa za kulevya. Vijana hawa watapelekwa viwandani na sehemu mbalimbali za kazi kwa lengo la kukuza ujuzi wao na baadaye waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevya zina athari kubwa kwa ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo,

napenda kurejea wito wangu kwa Watanzania wote kuunga mkono jitihada za Serikali katika mapambano haya kwa kutoa taarifa kuhusu watu wote wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya nchini. Aidha, rai yangu kwa waraibu ambao wamepatiwa ujuzi kujiunga kwenye vikundi vidogo vidogo ili waweze kupatiwa mikopo na hivyo kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 – 2022/2023 ambao unalenga kuzuia maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na UKIMWI hapa nchini. Tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Tatu wa Taifa uliomaliza muda wake Juni, 2018 umeonesha kwamba vifo na maambukizi mapya ya UKIMWI yameanza kupungua. Kutokana na tathmini hiyo, ulifanyika utafiti *(Tanzania HIV Impact Survey)* mwaka 2016/2017 katika ngazi ya kaya ambao umeonesha kwamba kiwango cha maambukizi ya VVU kwa Tanzania Bara kimeshuka kutoka asilimia 5.1 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 4.8 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto ya Watanzania wengi kutojua afya zao na idadi kubwa ya WAVIU kutokuwa kwenye mpango wa matunzo na matibabu. Pamoja na dawa za *ARV* kutolewa bure, inakadiriwa kuwa takriban WAVIU 500,000 hawapati dawa hizo. Nitoe rai kwa wadau wote nchini kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha watu kupima na kujua hali zao za maambukizi ya VVU. Katika hili idadi kubwa ya wanaume huwa hawapimi na wanaopima sehemu kubwa ni wanawake. Aidha, kwa wale watakaokutwa na maambukizi waingizwe kwenye mpango wa matibabu mapema iwezekanavyo na WAVIU wanaotumia dawa za kufubaza waendelee kutumia dawa hizo pasipo kuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali na wadau mbalimbali wakiwemo wa ndani na nje wameendelea kuchangia Mfuko maalum wa Kupambana na Kudhibiti UKIMWI nchini *(AIDS Trust Fund)* ili kuondokana na utegemezi wa wafadhili. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018 Mfuko uliweza

kukusanya shilingi milioni 884. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 750 zilitolewa na Serikali na shilingi milioni 114 zimekusanywa kutoka kwa wadau kupitia matembezi ya hiari na harambee. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika bajeti yake kwa kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI ili kufikia lengo la 90 tatu ifikapo mwaka 2020. Lengo la Mkakati huo ni kwamba hadi kufikia mwaka 2020, asilimia 90 ya Watanzania wote wawe wameshapima na kujua hali zao za maambukizi. Asilimia 90 ya waliopima VVU na kugundulika kuwa wana maambukizi waanze kutumia dawa za *ARV,* ili kufubaza na asilimia 90 ya watu wanaotumia dawa za kufubaza wawe wameshafubaza VVU.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Kikanda za Afrika Mashariki, *SADC*, Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa na Mashirika yake katika masuala ya usimamizi wa maafa kwa kufanya mafunzo ya vitendo na mazoezi ya pamoja ya kukabiliana na maafa. Vilevile, Serikali imetoa elimu kuhusu usimamizi wa maafa kwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu jirani zetu wa Msumbuji, Malawi na Zimbabwe walipata maafa yaliyosababishwa na kimbunga kikali kiitwacho Idai. Maafa hayo yalisababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa miundombinu na mazingira na watu wengi kukosa makazi katika nchi hizo. Kutokana na athari hizo, Serikali ilitoa msaada wa dharura wa kibinadamu wa tani 214 za chakula, tani 24 za madawa mbalimbali na vifaa vya kujihifadhi. Tumwombe Mwenyezi Mungu awajalie afya njema wale wote waliopata majeraha na azipumzishe mahala pema roho za Marehemu. Amina.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za kuimarisha mifumo ya kufuatilia mienendo ya majanga na utoaji wa tahadhari ya awali ili kujenga jamii iliyo salama na stahimilivu. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa mipango yote ya maendeleo

katika sekta mbalimbali inazingatia vihatarishi vya maafa na hivyo, kuipunguzia gharama kubwa za kukabili na kurejesha hali ya madhara yakitokea.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni matokeo ya mahusiano ya kihistoria ya pande zote mbili. Hivyo, hatuna budi kuuheshimu na kuulinda muungano wetu ili uendelee kudumu kwa faida ya watu wetu. Katika kuimarisha Muungano wetu, Serikali zote mbili zimeendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoukabili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika tarehe 21 Januari, 2019 kiliridhia utozwaji wa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kwa kiwango cha asilimia sifuri (0%) kwenye umeme unaouzwa na Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na kufuta malimbikizo ya deni la kodi ya *VAT* lililofikia shilingi bilioni 22.9 kwa Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* kwenye umeme uliouzwa na *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio haya yanayoendelea kupatikana katika utatuzi wa kero za Muungano, naomba nirudie kutoa wito wangu kwa Watanzania kuendelea kudumisha Muungano wetu ambao ni tunu na mfano wa kuigwa barani Afrika na dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kuimarika na kuendeleza mahusiano mema baina yake na Mataifa mengine na pia Mashirika ya Kikanda na Kimataifa duniani. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kutokana na jitihada hizo, Tanzania imeendelea kuwa nchi rafiki kwa Mataifa yote duniani. Aidha, Serikali imeshiriki katika mikutano na majukwaa mbalimbali muhimu ya Kikanda na Kimataifa na kutetea maslahi ya nchi ikiwemo kutoa ufafanuzi pale ambapo baadhi ya watu wa ndani na nje wenye nia mbaya na Tanzania walipojaribu kupotosha ukweli wa hali halisi ya hapa nchini na kuchafua taswira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi za Serikali ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini

mwa Afrika *(SADC)* uliofanyika mwezi Agosti 2018 nchini Namibia ulimteua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na kwa kuendelea kutekeleza kwa ukamilifu wajibu na heshima aliyopewa na wakuu wenzake wa nchi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za *SADC* Makamu Mwenyekiti ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa mwaka unaofuata. Hivyo, mwezi Agosti mwaka huu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli anatarajiwa kuchukua nafasi ya Uenyekiti wa *SADC* katika Mkutano Mkuu wa Nchi na Serikali za *SADC* utakaofanyika Jijini Dar es Salaam hapa Tanzania. Napenda kutumia nafasi hii kuwasihi wale wote wanaohusika na maandalizi ya mkutano huu mkubwa utakaofanyika mwezi wa Nane mwaka huu na muhimu kutekeleza jukumu hilo kwa bidii, weledi na ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkutano huu utawaleta nchini Wakuu wa Nchi na Serikali, Mawaziri, Maofisa Waandamizi, Wawakilishi wa Jumuiya za Wafanyabiashara, Waandishi wa Habari na wengineo kutoka Nchi 15 Wanachama wa *SADC.* Hii ni fursa muhimu sio tu kwa Serikali bali pia kwa sekta binafsi nchini kujiandaa kuwapokea wageni hawa kwa malazi, usafiri, chakula na utalii. Nitoe wito kwa Watanzania kujipanga vyema na kuchangamkia fursa zitakazoambatana na ujio wa wageni kwenye mkutano huo.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu Sera ya Mambo ya Nje ni mtambuka na ni mwendelezo wa sera ya ndani ya nchi katika nyanja na maeneo mbalimbali ya kiuchumi na jamii. Kwa kuzingatia muktadha huo nitumie fursa hii kuwasisitiza mabalozi wetu wa nje kuendelea kutafuta mitaji na uwekezaji hususan katika miradi ya kipaumbele, masoko mapya ya bidhaa zetu, kutangaza fursa za utalii, kutafuta fursa za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali itahakikisha utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi unaendelea kupewa kipaumbele cha kutosha ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Taifa ya *Diaspora*, kuendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda, kuimarisha ujirani mwema na mahusiano na Taasisi za Kimataifa, kupigania mfumo wa haki na utawala, siasa na uchumi wa kuunga mkono juhudi za kulinda amani na utulivu duniani kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, michezo; kwa wale wenye kitabu wanaofuatilia kupitia kitabu wafungue ukurasa wa 71 ndio unazungumzia suala la michezo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba imepita takribani miaka 39 tangu nchi yetu ishiriki kwa mara ya mwisho michuano ya mpira wa miguu katika nchi za Bara la Afrika maarufu *AFCON.* Hata hivyo, kusubiri huko kulikoma tarehe 24 Machi, 2019 baada ya vijana wetu wa *Taifa Stars* kupata ushindi mnono wa mabao matatu bila majibu dhidi ya jirani zetu wa Uganda. Ushindi huo unaipeleka Taifa *Stars* katika *AFCON* 2019 huko nchini Misri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwahamasisha watanzania kujitokeza kwa wingi kesho tarehe 5 katika Uwanja wa Taifa kwa ajili ya kuishangilia timu yetu ili ishinde kwa mabao mengi na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga katika hatua inayofuata. Mchezo wa kesho ni timu ya wanawake ya Taifa ambayo kesho inacheza na Congo. Viingilio vya mchezo huo vimepunguzwa mno kwa mfano kiingilio cha kesho kwa wanawake ni Sh.500 tu na wanaume ni Sh.1,000. Lengo ni kutoa fursa kwa wanawake na Watanzania wote kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yetu pale uwanja wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa riadha, timu yetu hivi sasa inashiriki michezo ya riadha nchini Rwanda, ni maratajio yetu kwamba timu hiyo ya riadha itarejea nyumbani na medali za kutosha na tunawatakia ushiriki mwema na mafanikio katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kupongeza wachezaji na viongozi wa benchi la ufundi la uhamasishaji na ushindi, mashabiki na Watanzania wote kwa kutimiza ndoto yetu ya muda mrefu ya kushiriki michuano hiyo mikubwa kabisa Barani Afrika. Nitoe wito kwa viongozi, wachezaji na Walimu kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye michezo iliyotangulia ili kujiweka sawa na michuano ya mwezi Juni, 2019 huko nchini Misri. Napenda mtambue kwamba lengo letu ni kwenda kushindana na sio kushiriki. Niwatakie maandalizi mema na mafanikio katika michuano hiyo inayokuja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nchi yetu inaendelea vyema na maandalizi ya mashindano ya mpira wa miguu kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 Barani Afrika *(AFCON U17)* yatakayoanza Aprili, 2019. Katika mazungumzo niliyofanya na viongozi wa Serikali na vyama mbalimbali vya michezo nchini vikiongozwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu wamenihakikishia kwamba maandalizi ni mazuri na timu yetu kwa sasa ipo nchini Rwanda kwa mazoezi zaidi kwenye mashindano yanayoendelea na leo usiku saa 10.30 wanacheza mechi nyingine na wenyeji Rwanda.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serengeti *Boys* itaibuka na ushindi walau katika michezo yake miwili tu katika mashindano hayo, itakuwa imekata tiketi ya kushiriki mashindano ya dunia huko nchini Brazil kwa vijana wa umri huo. Hii inatokana na ukweli kwamba kila kundi linatoa timu mbili ambazo zitaiwakilisha Bara la Afrika kwenye mashindano hayo ya dunia. Tunaiombea sana timu yetu ya vijana ili iweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuendelea kuipongeza timu yetu ya vijana wenye ulemavu wa akili kwa kuibuka na ushindi wa medali 15 katika michezo maalum ya *Olympic* iliyohusisha riadha na mpira wa wavu huko Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu mwezi Machi, 2019. Mafanikio hayo ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyowahi kupatikana katika nchi yetu kwenye tasnia ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, niipongeze pia timu yetu ya mpira wa miguu ya wanawake ambayo nilishaitaja mwanzo Twiga *Stars* kwa kuibuka mabingwa wa *CECAFA* mwaka 2018 pamoja na kuwa washindi wa kwanza wa mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Bujumbura nchini Burundi mwezi Julai mwaka 2018. Vilevile nawatakia maandalizi mema na ushindi Twiga *Stars* katika mchezo huo ambao nimeutaja kesho katika Uwanja wa Taifa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ikiwa ni hatua ya awali ya kufuzu kwa ajili ya michuano ya Olympic mwaka 2020 huko Tokyo, Japan na tuna imani watafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mwanamasumbwi wa Kitanzania Hassan Mwakinyo kwa kuendelea kuwa mfano bora kwenye tasnia hiyo ya masumbwi. Tarehe 23 Machi 2019, Hassan Mwakinyo aliendelea kung'ara katika anga za masumbwi na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania baada ya kumtwanga mpinzani wake Muajentina Sergio Gonzalez huko Nairobi. Nitoe wito kwa vyama vya michezo kuendelea kuwalea vyema wanamichezo hususan vijana ili kuipaisha vyema bendera ya Tanzania kwenye medani mbalimbali za michezo ndani na nje. Huu ni wakati muafaka kwa Watanzania kuthamini michezo na kutambua kuwa michezo ina ajira na vilevile inalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu vilabu vyetu vya mpira wa miguu vimekuwa havifanyi vizuri katika medali za michuano ya Klabu Bingwa Afrika. Hata hivyo, katika msimu wa mwaka wa fedha 2018/2019 Klabu ya Simba ya Dar es Salaam imeweza kututoa kimasomaso baada ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Barani Afrika. Kufanya vizuri kwa Klabu ya Simba kunaongeza uwezekano wa Tanzania kupatiwa nafasi nyingine mbili na kufanya jumla ya vilabu vinne vitakavyoshiriki mashindano hayo makubwa ya vilabu Barani Afrika katika misimu ijayo. Vilevile ushindi wa *Taifa Stars* na Simba una manufaa makubwa kwa nchi yetu yakiwemo kuitangaza vyema nchi yetu na kufungua fursa za ajira kwa vijana wetu wanaojihusisha na soka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie basi fursa hii kuwapongeza sana wachezaji, viongozi, benchi la ufundi na mashabiki wote wa Klabu ya Simba kwa mafanikio hayo makubwa. Niseme tu kwamba tupo pamoja na nyie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwatakie heri maandalizi mema ya ushindi wa timu zetu zote ikiwemo *Serengeti Boys* mashindano ya Taifa ya *AFCON,* Taifa *Stars* katika mashindano ya *AFCON* huko nchini Misri mwaka 2019 na Klabu ya Simba katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Barani Afrika na tunawatakia kila la kheri kwa mchezo wenu mtakaoucheza Jumamosi Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa wanaofuatilia kitabu sasa waende ukurasa wa 85. Wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu, nitoe wito kwa Viongozi, Watendaji na Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Nirejee tena kuwakumbusha kwamba dhamira ya kufikia uchumi wa kati itafikiwa tu iwapo Watanzania tutaweka mbele uzalendo na maslahi mapana ya Taifa letu pamoja na kudumisha misingi ya umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, lengo la uchumi wa viwanda ni kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi jumuishi wenye kupunguza umaskini, kuongeza uzalishaji, ajira na ustawi wa watu wetu na lengo letu litafikiwa la kufungamanisha sekta ya viwanda na sekta nyingine za uchumi ikiwemo biashara, kilimo na utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake Serikali itaendelea kuonyesha uthubutu wa dhamira ya dhati katika kuhakikisha kwamba inatekeleza yafuatayo:-

(1) Kuendelea kupambana na rushwa, ufisadi, uzembe na uvivu sambamba na kuimarisha nidhamu kwa viongozi na watendaji wa ngazi zote katika kuwahudumia wananchi;

(2) Kusisitiza kwa viongozi, watendaji na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, ubunifu na uzalendo katika kujiletea maendeleo yetu;

(3) Wafanyabiashara, wajasiriamali kuendesha biashara zao kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo pamoja na kujenga tabia ya kuona fahari kulipa kodi kwa maendeleo ya Taifa letu;

(4) Kuielekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kujenga mahusiano rafiki na walipakodi wa lengo la kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa walipakodi kuwa taasisi hiyo inatumia nguvu na vitisho katika kudai kodi na kwa sababu hiyo inapelekea kuzorotesha ukusanyaji wa mapato.

(5) Kuendelea kujenga mazingira mazuri na wezeshi ya kufanya kazi, biashara, kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi; na

(6) Kuwahimiza wananchi kutumia ipasavyo haki yao ya kidemokrasia kwa kujiandikisha na kushiriki katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa utaofanyika mwezi wa kumi mwaka huu 2019. Aidha, Serikali itahakikisha mamlaka zinazosimamia uchaguzi huo zinashirikiana vyema na vyombo vyote vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kwamba uchaguzi huo unaendeshwa kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Spika, ni vyema tukatambua kuwa tupo kwenye zama za ushindani wa kiuchumi, kwa msingi huo mafanikio yetu katika zama hizi yatategemea pia ubunifu, tija na uwepo wa ufanisi kwenye miundombinu wezeshi ya kiuchumi inayoendelea kujengwa na Serikali. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuhakikisha inasimamia ipasavyo rasilimali za Taifa ili zielekezwe katika sekta ambazo zitatuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea pamoja na kuhimiri ushindani wa kiuchumi uliopo.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka

wa fedha 2019/2020. Kwa mwaka huu wa 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi 148,886,523,581; kati ya fedha shilingi 86,290,355,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 62,596,168,581 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naliomba pia Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 124,182,587,600 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi 116,573,026,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 7,609,511,600 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea, hongereni sana Bunge zima mmeunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo imefafanua mambo mengi yanayohusu nchi yetu na utendaji wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano na umetuanzishia sasa zoezi zima la kushughulikia bajeti za Wizara mbalimbali ndani ya Serikali kwa hotuba hii ambayo umeitoa, tunashukuru sana. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI MKUU, MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2018/2019 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2019/2020.

**2. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2018/2019 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/2020.

**3. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uongozi wao makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa juhudi na maono yao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali, zinaleta manufaa na tija kwa wananchi.

**4. Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kuboresha utendaji Serikalini, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, na Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Kabudi (Mb.), kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni matumaini yangu kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

5. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, baadhi ya waheshimiwa Wabunge na wananchi tunaowawakilisha walifikwa na misiba ya ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, Taifa lilikumbwa na maafa kutokana na ajali za vyombo vya majini na nchi kavu. Ajali hizo ziligharimu maisha ya watu, kusababisha majeruhi na uharibifu wa mali. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliopata majeraha na azipumzishe roho za marehemu mahala pema. Amina!

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mhe. George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe. Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazofanya.

7. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa weledi na umakini mkubwa. Ni imani yangu kuwa mtaendeleza hekima na weledi mlionao katika kuliongoza Bunge kuisimamia Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, nimpongeze Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa namna wanavyolisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

8. **Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu

Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru watumishi wote wa umma kwa kutekeleza majukumu yao na kukamilisha kuandaa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/2020.

**9. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu); Mhe. Angellah Kairuki, Mbunge Viti Maalumu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji); Mhe. Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira); Mhe. Stella Alex Ikupa, Mbunge Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu) kwa kujitoa kwao katika kutekeleza majukumu na ushirikiano wanaonipa.

**10. Mheshimiwa Spika,** pia niwapongeze Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni: Bibi Maimuna K. Tarishi (Waziri Mkuu na Bunge); Bwana Andrew W. Masawe (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Bibi Dorothy A. Mwaluko (Sera, Uratibu na Uwekezaji); na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**11. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru Washirika wetu wa Maendeleo, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi na Taasisi za Dini kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kujenga uchumi wa viwanda ili kufikia azma ya kuwa Taifa lenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**12. Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono. Niwapongeze kwa kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi, wakati mimi

Mbunge wao nikitekeleza majukumu ya kusimamia utendaji wa Serikali. Kipekee, ninamshukuru mke wangu mpendwa, Mary na familia yangu kwa uvumilivu wao wakati wote ninapokuwa nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru sana kwa upendo wanaoendelea kunionesha na kunitia moyo.

## MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI WA MWAKA 2019/2020

**13. Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/2020 yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 ambao ni wa nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka wa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021). Dhima ya Mpango huo ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu.

**14. Mheshimiwa Spika,** Mpango huu unatekelezwa sanjari na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020; Ahadi za Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na zile alizozitoa katika hotuba yake ya kuzindua Bunge hili mwezi Novemba, 2015. Vipaumbele vya mpango wa mwaka 2019/2020 ni kuendelea kuimarisha msingi wa uchumi wa viwanda; kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; kuendelea kuboresha mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji; na kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango.

**15. Mheshimiwa Spika,** katika Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Umeme wa Maji wa Mto Rufiji (Stiegler's Gorge), ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa (SGR), barabara pamoja na kukuza sekta ya anga. Utekelezaji wa miradi hiyo ya miundombinu wezeshi ya kiuchumi una lengo la kufungamanisha ukuaji wa sekta hizo na sekta nyingine hususan za biashara, kilimo na utalii.

**16. Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuimarika kwa sekta hizo kutachochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi

kwa ujumla. Nitoe rai kwa Wabunge, Wafanyabiashara na Wajasiriamali, Viongozi na Watendaji wa Serikali, Taasisi za Dini, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo, na Wananchi wote kwa ujumla, kuiunga mkono Serikali katika kutekeleza Mpango huu ili kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

**MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO**

**17. Mheshimiwa Spika,** mwezi Juni 2018, wakati akizindua Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II), Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema, ninanukuu,

**"Tumekuwa wakimya na hatuelezi kwa kina masuala tunayofanya. Niwaombe basi viongozi wenzagu wa Serikali, kila tunapopata nafasi tuseme mambo tunayoyafanya...... Tusipofanya hivyo yanayosemwa yataonekana kuwa kweli.'' Mwisho wa kunukuu.**

**18. Mheshimiwa Spika,** bila kumung'unya maneno katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka mitatu kazi kubwa tena ya kihistoria imefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii nchini. Hivyo, niungane na Mheshimiwa Rais kuwakumbusha viongozi na watendaji wakuu wa Serikali kuwa tunalo jukumu la kuhakikisha umma wa Watanzania unafahamishwa kuhusu shughuli zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na mafanikio makubwa yanayopatikana.

**19. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamepatikana mafanikio mengi ambayo wananchi wanapaswa kufahamishwa. Aidha, Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira ya dhati ya kisiasa katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Halikadhalika, ameweza kuhakikisha dhamira hiyo ya kujenga uchumi imara usiyo tegemezi inaenea kwa viongozi wengine, watendaji na wananchi kwa ujumla.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kuendelea kukua na kuimarika kwa uchumi ambao unachochewa na jitihada za Serikali za kuwekeza kwenye miundombinu ya usafirishaji ikiwemo ujenzi wa barabara, reli, viwanja vya ndege sanjari na kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme. Aidha, kuimarika kwa Shirika la Ndege Tanzania ni sehemu ya mafanikio hayo, ambapo Serikali imefanikisha ununuzi wa ndege sita mpya ikiwemo Dreamliner Boeing **787**. Ununuzi wa ndege hizo umesaidia kuitangaza nchi, kuongeza mapato ya Serikali, fursa za ajira kwa vijana na kuwa kichocheo kwa Sekta nyingine kama vile kilimo, utalii, mifugo na uvuvi.

**21.** **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam-Morogoro na Morogoro-Makutupora unaendelea vizuri na kwa kasi ya kuridhisha. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wake wa Elimumsingi Bila Malipo.

Mpango huo umesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa ambao pengine wangekosa fursa ya kupata elimu kutokana na kushindwa kulipa ada na michango mingine. Hii imejidhihirisha kutokana na ongezeko la uandikishaji wanafunzi kutoka milioni **1.57** mwaka 2015 hadi milioni **2.08** mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia **35.2.** Kwa mwaka 2019 uandikishaji ulikuwa milioni 1.58. Kutokana na takwimu hizi ni dhahiri kuwa kwa sasa watoto wote wanaofikia umri wa kwenda shule wanaandikishwa bila kikwazo chochote.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima, kuongeza bajeti ya dawa kutoka Shilingi Bilioni **31** mwaka 2015/2016 kufikia Shilingi Bilioni **270** mwaka 2018/2019. Ongezeko hilo limeongeza upatikanaji wa dawa muhimu kufikia asilimia **96** katika mwaka 2018/2019. Aidha, tiba za kibingwa zinatolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali mpya za Rufaa za Benjamini Mkapa na Mloganzila.
Hospitali hizo zinatoa huduma za kibingwa zikiwemo upasuaji wa moyo, ubongo na uti wa mgongo ambazo awali

zilipatikana nje ya nchi na hivyo, kuigharimu Serikali fedha nyingi.

**23. Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuanza kwa ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme kwenye Bonde la Mto Rufiji (Stiegler's Gorge) pamoja na kuendelea na kazi ya kusambaza umeme vijijini. Mafanikio hayo na mengine yatafafanuliwa kwa kina na sekta husika wakati watakapowasilisha bajeti zao.

**24. Mheshimiwa Spika,** bajeti hii ya nne ya Serikali ya Awamu ya Tano, ni bajeti inayolenga kukamilisha kwa kiasi kikubwa yale tuliyowaahidi wananchi wakati Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikiomba ridhaa ya kuongoza Dola katika Uchaguzi Mkuu Mwaka 2015. Kwa msingi huo, nisisitize kwamba, Sekta na Taasisi zote za Serikali zikamilishe utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020.

**25. Mheshimiwa Spika,** kwa kasi ambayo Serikali yetu imeonesha na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka mitatu, ni matarajio yetu kuwa ahadi zilizotolewa kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 zitakamilishwa ifikapo mwaka 2020.

**HALI YA UCHUMI**

**26. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyotangulia kueleza kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuimarisha uchumi na mafanikio yanaonekana. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2018, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia **6.7** ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia **6.2** katika kipindi kama hicho mwaka 2017.
Ukuaji huu wa uchumi umechangia kutoa ajira na kuongeza mapato ya Serikali yaliyowezesha ujenzi na uboreshaji wa miundombinu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

**27. Mheshimiwa Spika,** mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia **4.0** Januari, 2018 hadi asilimia **3.0** Januari, 2019. Kiwango hiki cha chini cha mfumuko wa bei kimetokana na kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika

masoko ya ndani na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha na kujenga misingi na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuwa na mapato endelevu kwa ajili ya kugharamia matumizi yake. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia jukumu lake la msingi la kutafuta mapato kutoka vyanzo vya ndani na nje na kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za umma kupitia bajeti ya Serikali itakayowasilishwa hapa Bungeni mwezi Juni 2019.

***Usimamizi wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa***

**29.** **Mheshimiwa Spika**, ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika mwaka 2016/2017, umeonesha kuwa Halmashauri **166** kati ya **185** zimepata hati safi sawa na asilimia **90**, Halmashauri **16** zimepata hati zenye shaka ikilinganishwa na Halmashauri **32** mwaka 2015/2016. Matokeo hayo yanaonesha kuimarika kwa usimamizi wa fedha pamoja na uwajibikaji wa watendaji na Viongozi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nazielekeza Halmashauri zote nchini kuendelea kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha zinazopelekwa katika halmashauri hizo ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inalingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

***Vitambulisho vya Wajasiriamali Wadogo***

**30.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa wajasiriamali wadogo nchini katika kuchangia pato la Taifa na kukuza uchumi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa vitambulisho **670,000** kwa ajili ya wajasiriamali wadogo ambao mitaji yao haizidi Shilingi milioni nne. Lengo la kutoa vitambulisho hivyo vyenye kugharimu shilingi **20,000** kwa kila kimoja ni kuwatambua, kuwaandalia maeneo ya kufanya biashara bila usumbufu wowote na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza mapato ya ndani.

**31.** **Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe **10** Machi 2019, jumla ya vitambulisho **496,221** sawa na asilimia **74** vilikuwa vimegawiwa kwa wajasiriamali wadogo katika mikoa yote nchini. Aidha, tangu kuanzishwa kwa utaratibu huo, Serikali imekusanya Shilingi bilioni **9.9**.

Naendelea kusisitiza kwamba viongozi na watendaji wote katika Serikali za Mitaa kuwapatia ushirikiano wa kutosha wajasiriamali wadogo na kutowabughudhi.

**HALI YA SIASA**

**32.** **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla hali ya kisiasa na demokrasia imeendelea kuimarika nchini. Katika mwaka 2018/2019, zilifanyika chaguzi ndogo za wabunge katika majimbo **10** na madiwani katika kata **231** kwenye maeneo mbalimbali nchini. Majimbo yaliyoshiriki uchaguzi ni Buyungu, Korogwe, Monduli, Ukonga, Liwale, Serengeti, Simanjiro, Ukerewe, Babati Mjini na Temeke. Katika chaguzi hizo, Wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) walishinda majimbo yote na kata **230** ambapo CHADEMA walishinda Kata moja. Nichukue fursa hii, kuvipongeza vyama vyote vilivyoshiriki katika chaguzi hizo, na kipekee naipongeza CCM kwa ushindi mkubwa ilioupata katika chaguzi hizo.

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeendelea kusimamia na kukuza mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa ili kudumisha amani, utulivu na mshikamano uliopo katika nchi yetu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Sheria ya Vyama vya Siasa Namba.5 ya Mwaka 1992 Sura ya **358** imefanyiwa marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji na hivyo kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni mara ya saba kwa Sheria hii kufanyiwa marekebisho tangu kutungwa kwake mwaka 1992 kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika. Nitoe wito kwa Vyama vya Siasa nchini kuendesha shughuli zao za siasa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria hiyo ili kuwa na uwazi, uwajibikaji, kudumisha amani na kukuza demokrasia nchini.

**34. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kuelimisha umma kuhusu utekelezaji wa Sheria hiyo, kusimamia vyama vya siasa nchini na kuhakikisha vinajiendesha kama Taasisi. Vilevile, itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010 katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

***Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019***

**35. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2019 ambao ni uchaguzi wa sita tangu kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1994 chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Hivi sasa, Serikali imekamilisha zoezi la uhakiki wa maeneo ya utawala ambayo yatashiriki kwenye uchaguzi huo katika Halmashauri zote **185**. Lengo la uhakiki huo ni kujiridhisha na usahihi wa maeneo hayo kwa idadi na majina ili kufanikisha maandalizi ya bajeti na mahitaji mengine muhimu ya uchaguzi huo.

**36. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi zitakazotumika kusimamia uchaguzi huo mwezi Oktoba 2019. Nitoe wito kwa wadau mbalimbali na wananchi kujiandikisha na kujitokeza kwa wingi katika upigaji kura ili waweze kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Oktoba 2019. Serikali kwa upande wake itaendelea kuhakikisha kunakuwepo na mazingira salama na tulivu kwa kipindi chote cha uchaguzi.

***Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020***

**37. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza Maandalizi ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura pamoja na uhakiki wa vituo vya Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka 2020. Hadi sasa, Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura zimeandaliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. **792** na **793** ya tarehe 28 Desemba 2018.

Aidha, uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura nao umekamilika, ambapo kwa upande wa Tanzania Bara vituo vimeongezeka kutoka **36,549** vilivyokuwepo mwaka 2015 hadi kufikia vituo **37,407** mwaka 2018, sawa na ongezeko la vituo **858**. Kwa upande wa Zanzibar vimeongezeka vituo **27** kutoka **380** vya mwaka 2015 hadi kufikia vituo **407** mwaka 2018. Natoa wito kwa wananchi wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha mara zoezi hilo litakapoanza.

**BUNGE**

**38.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Bunge limetimiza wajibu wake wa kikatiba na kikanuni kwa kufanya mikutano mitatu na huu ukiwa wa nne. Katika mikutano hiyo, masuala mbalimbali yamejadiliwa na kutolewa ufafanuzi na Serikali ikiwemo hoja za Kamati za Kudumu za Bunge. Aidha, jumla ya maswali ya msingi **374** yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali yakijumuisha pia maswali ya nyongeza **978**.

Katika utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, maswali ya msingi 19 pamoja na moja la nyongeza yaliulizwa na kujibiwa. Vilevile, Miswada ya Sheria ya Serikali **12** iliwasilishwa, kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge kuwa Sheria za nchi. Maazimio ya Bunge matatu pamoja na Itifaki za kimataifa nne ziliridhiwa na kupitishwa na Bunge kwa utekelezaji wa Serikali. Ni matumaini ya Serikali kwamba Bunge lako tukufu litaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi kikatiba la kutunga sheria na kuisimamia Serikali.

**39.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Ofisi ya Bunge itafanya ukarabati katika Ukumbi wa Bunge na Ukumbi wa Msekwa, kusimika mitambo ya Studio ya Bunge na kuboresha miundombinu mingine ya Ofisi zake ikiwa ni pamoja na Usimikaji wa mitambo ya usalama katika majengo ya Bunge na kukamilisha ujenzi wa nyumba za viongozi wa Bunge.

**MAHAKAMA**

**40.** **Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuona haki inatendeka nchini. Ili kutekeleza dhamira

hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa kufanya maboresho ya kiutendaji kwa vyombo vya maamuzi ikiwemo Mahakama.

**41. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019 jumla ya mashauri **231,927** yalifunguliwa katika mahakama zote nchini hadi Februari, 2019. Kati ya hayo, mashauri **224,950** sawa na asilimia 96 yamesikilizwa na kutolewa hukumu. Ufanisi huu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa Majaji **21** wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu. Vilevile, kukamilika kwa miundombinu muhimu ya Mahakama imewezesha kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi.

**42. Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeanzisha huduma ya mahakama inayotembea ikiendesha shughuli zake kwa kutumia magari maalumu katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya mahakama. Huduma hii imesaidia kuongeza kasi ya Mahakama kusimamia haki kwa kutumia mifumo rafiki ya utoaji haki nchini. Aidha, mahakama nchini zimeanza kutekeleza utaratibu wa kutoa nakala za hukumu bure kwa wananchi kupitia huduma ya Posta Mlangoni ambapo hadi Februai 2019, jumla ya nakala **5,942** zimetolewa. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itawajengea uwezo watumishi wa mahakama; kuimarisha mifumo ya utoaji haki; na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama nchini.

**SERIKALI KUHAMIA DODOMA**

**43. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhamishia shughuli zake Jijini Dodoma tangu Mheshimiwa Dkt.John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atoe tamko la Serikali kuhamia Dodoma tarehe 23 Julai 2016. Mpango huo, unatekelezwa kwa awamu mbalimbali zinazojumuisha uhamisho wa watumishi, ujenzi wa makazi na miundombinu, uboreshaji wa huduma za jamii na ujenzi wa Mji wa Serikali.

**44. Mheshimiwa Spika,** katika awamu hizo, jumla ya watumishi 8,883 wa Wizara na Taasisi za Serikali wamehamia Dodoma. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kuhakikisha watumishi waliobaki wanahamia Dodoma.

Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi za awali za Wizara 23 likiwemo Jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umekamilika.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** tarehe 30 Julai 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikabidhi hati miliki **64** za viwanja kwa mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Kibalozi Jijini Dodoma. Niendelee kutoa wito kwa Mashirika ya Kimataifa na Mabalozi wahamishie Ofisi zao Jijini Dodoma.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendeleza ujenzi wa mji wa Serikali na Jiji la Dodoma kwa kuimarisha huduma za jamii, miundombinu ya masoko, barabara, mfumo wa maji safi na maji taka. Natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika Jiji la Dodoma kwa lengo la kuchochea maendeleo ya Jiji la Dodoma.

***Maendeleo ya Sekta Binafsi***

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inatekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa Sekta Binafsi ili iweze kutoa mchango uliokusudiwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa Sekta Binafsi inashiriki ipasavyo katika maendeleo ya Taifa letu kwa kutengeneza ajira, kuongeza uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma na kukuza uchumi.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha malengo hayo, Serikali inachukua hatua mbalimbali za makusudi za kuboresha sheria na mifumo ya kodi, kuimarisha miundombinu pamoja na kuendeleza mazungumzo na makundi mbalimbali ya wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa. Mathalan, tarehe 22 Januari 2019, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokutana na wadau wa Sekta ya Madini alitoa maelekezo kwa viongozi na watendaji wa Serikali kuhakikisha wanachukua hatua za kukuza Sekta hiyo.

**49. Mheshimiwa Spika,** tarehe 28 Februari 2019, nilikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa lengo la kujadiliana kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika Mkutano huo, niliambatana na viongozi na watendaji wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi na kutatua kero mbalimbali zilizowasilishwa na wafanyabiashara hao. Aidha, Serikali inafarijika kupata mrejesho kutoka Sekta Binafsi kwamba mahusiano ya pande hizi mbili yanaendelea kuimarika. Natoa wito kwa viongozi na watendaji wote wa Serikali kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki kwa Sekta Binafsi.

***Uwekezaji***

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa uwekezaji katika kujenga uchumi wa nchi yetu, Serikali imeendelea kutoa uzito katika uwekezaji ambapo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichukua hatua ya kuhamishia masuala ya uwekezaji katika Ofisi yangu na kuteua Waziri wa Nchi kushughulikia masuala ya uwekezaji. Vilevile, Mheshimiwa Rais amekihamishia kituo cha Uwekezaji nchini kuwa chini ya Ofisi yangu. Hatua hizo zitasaidia kuimarisha uratibu wa masuala ya uwekezaji nchini na kuhakikisha kwamba changamoto mbalimbali zilizopo zinashughulikiwa kwa ufanisi ili kuwezesha nchi yetu kuvutia zaidi mitaji ya uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

**51. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhamasisha na kuvutia wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi ili wawekeze nchini. Katika kuhamasisha uwekezaji kutoka nje, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi mbalimbali zikiwemo Ofisi za Balozi zetu za Nje na Balozi za nje zilizopo hapa nchini, kiliandaa na kuendesha makongamano na semina mbalimbali zilizowalenga wawekezaji kutoka ndani na nje.

**52. Mheshimiwa Spika,** uhamasishaji huo, umefanikisha kuvutia uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za kimkakati. Hadi

kufikia Februari, 2019 jumla ya miradi mipya 145 ilisajiliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC). Kati ya miradi hiyo, miradi **104** sawa na asilimia **72** inamilikiwa na wawekezaji wa ndani; miradi **38** sawa na asilimia **26** inamilikiwa na wawekezaji kutoka nje na miradi mitatu sawa na asilimia **2.01** ni ya ubia. Miradi hiyo, inatarajia kuwekeza mitaji ya jumla ya Dola za Marekani bilioni **1.84** na kuzalisha ajira mpya **15,491**.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kuvutia uwekezaji nchini, hali ya uwekezaji imeendelea kuimarika ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Ripoti mbalimbali za uwekezaji duniani zinaonesha kuwa Tanzania imeongoza kwa kuvutia uwekezaji kati ya nchi za Afrika Mashariki.

**54.** **Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Uwekezaji ya Dunia (World Investment Report) ya mwaka 2018 inayotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) inaonesha kuwa Tanzania imevutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni **1.18**, ikifuatiwa na Uganda Dola za Marekani Bilioni **0.7** na Kenya Dola za Marekani Bilioni **0.67**.

**55.** **Mheshimiwa Spika,** taarifa nyingine ya "The Africa Investment Index (AII) 2018" inaonesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya **13** kati ya nchi **54** za Afrika katika kutoa fursa za masoko na vivutio vya uwekezaji. Vilevile, taarifa ya "Where to Invest in Africa" ya mwaka 2018, inaonesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya saba kati ya nchi **52** zinazovutia zaidi kwa uwekezaji Barani Afrika. Napenda kutoa rai kwa Watanzania kuchangamkia fursa zinazojitokeza kutokana na ukuaji wa uchumi, maendeleo ya kijamii na pia uwekezaji wa sekta ya umma kwenye miundombinu kwa kuthubutu kuwekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ikiwemo kutekeleza mapendekezo ya Mpango Kazi Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini;

kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji.

## SEKTA ZA UZALISHAJI

### *Kilimo*

#### *Hali ya Upatikanaji wa Chakula*

**57. Mheshimiwa Spika,** hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2017/2018 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2018/2019 imeendelea kuimarika kutokana na hali nzuri ya mvua katika maeneo mengi ya nchi, kuongezeka kwa tija na uzalishaji. Uzalishaji wa mazao ya chakula umefikia tani milioni **16.89** ikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni **13.57**. Hivyo, nchi ina ziada ya chakula ya tani milioni **3.32** za mazao yote. Hii ni hatua nzuri na ya kujivunia kwani usalama wa chakula ni usalama wa nchi.

#### *Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)*

**58. Mheshimiwa Spika,** tarehe 4 Juni 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Programu hiyo, inalenga kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo kwa maana ya mazao, mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza pato la wakulima hususan wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha na usalama wa chakula na lishe.

**59. Mheshimiwa Spika**, ikiwa sehemu ya Utekelezaji wa ASDP II, Serikali inaiimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ili kuwa benki mama itakayoongoza mipango inayolenga kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi nchini. Lengo la Serikali ni kuifanya TADB kuwa benki ya mfano na ya kisasa katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kutoka kilimo cha mazoea cha kujikimu kwenda katika kilimo cha kibiashara na uzalishaji wenye tija katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

**60.** **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari 2019, TADB imetoa mikopo ya shilingi bilioni **100.7** ikilinganishwa na shilingi billioni **10** mwaka 2017. Mikopo hiyo, imewanufaisha zaidi ya wakulima na wafugaji milioni moja nchi nzima. Aidha, TADB tayari imekwishafungua Ofisi mbili za Kanda Jijini Dodoma na Mwanza. Rai yangu kwa Menejimenti na Bodi ya TADB ni kwamba kamilisheni ufunguzi wa ofisi zilizopangwa kwa wakati ili kutatua changamoto za upatikanaji wa pembejeo na miundombinu duni ya uzalishaji, usafirishaji, uchakataji wa mazao na masoko zinazokabili wakulima wadogo nchini.

***Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara***

**61.** **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mazao makuu ya kimkakati yakiwemo chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku umeimarika kutokana na juhudi zinazofanywa na Serikali ikiwemo kuimarisha ushirika. Kwa mfano, uzalishaji wa zao la pamba uliongezeka kutoka tani **132,934** mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani **222,039** mwaka 2018/2019 wakati uzalishaji wa zao la Kahawa uliongezeka kutoka tani **45,245** hadi kufikia tani **65,000**. Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa mazao hayo na mengine kwa kuwa ndiyo mhimili wa kutoa malighafi za kuendesha viwanda na yana mnyororo mpana wenye fursa ya kutoa ajira nyingi na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

***Mkakati wa Uzalishaji wa Zao la Chikichi***

**62.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya kununua mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Aidha, uzalishaji mdogo wa zao la chikichi ni miongoni mwa sababu za kushindwa kujitosheleza kwa mahitaji ya mafuta ya kula nchini. Kutokana na changamoto hiyo, Serikali imeamua kuweka nguvu kubwa kwenye uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ili kuondokana na utegemezi na kuokoa matumizi ya fedha za kigeni.

**63.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeanza kuimarisha kilimo cha zao la chikichi hususan katika mkoa wa Kigoma ili kusaidia upatikanaji wa mbegu

bora za chikichi. Lengo ni kuzalisha na kusambaza kwa wakulima miche ipatayo milioni 20 katika kipindi cha miaka minne (2018/2019 hadi 2021/2022). Vilevile, Serikali imeamua kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kihinga, mkoani Kigoma kuwa Kituo cha Utafiti wa Mbegu Bora za Chikichi.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maamuzi haya ya Serikali yameanza kuzaa matunda. Mathalan, hadi kufikia Februari 2019, Kituo cha Kihinga kimezalisha mbegu **4,747** ambazo zimefanyiwa uoteshwaji wa awali. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imepanga kuzalisha miche ya chikichi milioni 5. Ni matarajio ya Serikali kwamba usimamizi mzuri wa Mkakati huo wa miaka minne utalisaidia Taifa kuondokana na uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje, kutengeneza fursa mbalimbali za ajira na kuwaongezea kipato wakulima wa chikichi.

***Mifugo na Uvuvi***

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaimarisha sekta ya mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali ilianzisha Dawati la Sekta Binafsi kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi. Lengo la Serikali ni kuongeza uwekezaji wenye tija utakaowezesha wafugaji na wavuvi kuongeza kipato, kuzalisha malighafi za kutosha za viwanda na kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba Sekta ya Mifugo na Uvuvi inakua na mnyororo mpana wa ongezeko la thamani kwa kutoa kipaumbele katika ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi. Hadi sasa, viwanda **99** vya kusindika mazao ya mifugo vimeanzishwa vikiwemo viwanda **17** vya nyama, **76** vya maziwa na **6** vya ngozi.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuweka msisitizo katika kuwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika uwekezaji kwenye viwanda; kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Ukanda wa Uchumi

wa Bahari na Bahari Kuu; na kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi.

***Utalii***

**68.** Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii imeendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa na kuongeza ajira. Mathalan, idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2018 imeongezeka na kufikia watalii milioni **1.49** ikilinganishwa na watalii milioni **1.33** walioingia nchini mwaka 2017. Vilevile, mapato yatokanayo na utalii yameongezeka na kufikia Dola za Marekani bilioni **2.43** mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni **2.19** mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia **7.13**.

**69.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza vivutio vya utalii, mwaka 2018/2019 Serikali imeanzisha Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari Channel) ili kuvutia watanzania na wageni kutoka mataifa mbalimbali kutembelea vivutio vyetu. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha Chaneli hiyo kwa kuipatia wataalamu, vifaa na vitendea kazi stahiki. Chaneli hii itaendeleza taswira na sifa nzuri ya Tanzania kimataifa sambamba na kuongeza thamani katika mnyororo mzima wa biashara ya utalii nchini.

**70.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya utalii kwa kuihamasisha na kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuendeleza sekta hiyo. Aidha, sanjari na kutangaza utalii, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ikiwemo usafiri wa anga ili kuvutia watalii wengi zaidi nchini.

***Viwanda***

**71.** **Mheshimiwa Spika,** sote tunatambua kuwa dhima ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu wetu. Katika kipindi cha miaka mitatu ya kutekeleza azma hii, Serikali inaridhika kuona hamasa na uthubutu wa Watanzania kwa kushirikiana na nchi rafiki kuhamasika na kuwekeza katika ujenzi wa viwanda. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeendelea kuhamasisha Sekta

Binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda nchini. Vipaumbele ni katika viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini; viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi; na kuendelea kubainisha maeneo ya viwanda katika mikoa yote na kuendeleza maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZ & SEZ) pamoja na kongani za viwanda nchini.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** moja ya malengo ya Serikali ni kuinua uchumi wa wananchi kwa kuwawezesha kupata mitaji ya kufanyia kazi zao. Katika kufanikisha malengo hayo, Serikali kupitia SIDO imeendelea kuratibu Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi yaani "National Entrepreneurship Development Fund (NEDF)". Katika mwaka 2018/2019, jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni **1.74** ilitolewa ambapo mikopo **520** yenye thamani ya Shilingi milioni **788** ilitolewa kwa wanawake na mikopo **493** yenye thamani ya Shilingi milioni **958.8** ilitolewa kwa wanaume.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** ili kutimiza azma ya kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kuongeza uwekezaji katika viwanda, Serikali inaendelea kuandaa mipango kabambe ya miji na kuhakikisha, maeneo yanatengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Katika mipango kabambe ya miji **17** iliyokamilika na ile inayoandaliwa, jumla ya ekari **127,859** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Vilevile, kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji za Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Kilosa, Serikali imetenga hekta **2,710** za ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo. Pia, Mamlaka za Upangaji zimeagizwa kuzingatia utengaji wa asilimia **10** ya kila eneo la Mpango Kabambe wa Mji kwa ajili ya uwekezaji wa biashara na viwanda.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Serikali imeandaa Mwongozo wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati ambao utawezesha mpango wa uchumi na viwanda kufanyiwa Tathmini ya Mazingira Kimkakati. Katika maboresho ya kanuni yaliyofanyika, yanampa Waziri mwenye dhamana ya mazingira mamlaka ya kutoa vibali vya muda kwa ajili ya miradi ya uwekezaji kwenye sekta ya viwanda na hivyo kuboresha taratibu za uwekezaji wa viwanda nchini.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuhuisha, kuboresha na kutekeleza Sera, Sheria, Taratibu na Mikakati ya Maendeleo ya Viwanda, biashara na masoko hususan kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini; kuimarisha na kusimamia mfumo wa biashara ya ndani; na kutumia kikamilifu fursa za masoko zenye unafuu wa kodi na usio wa kodi. Vilevile, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Taasisi za utafiti zinazohusika na maendeleo ya viwanda na kuhamasisha uanzishaji na maendeleo ya viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati.

***Madini***

**76.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Madini na mchango wake katika kukuza uchumi, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutoa kipaumbele katika kulinda rasilimali za madini na kuhakikisha zinawanufaisha Watanzania. Katika hilo tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuelekeza Mamlaka za Serikali kutunga Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Maliasili **Na. 5** ya Mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Maliasili za Nchi **Na. 6** ya Mwaka 2017 pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini Sura **123**.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia, imeendelea kutoa kipaumbele kwa wachimbaji wadogo kwa kuwapatia maeneo ya uchimbaji; kuwakopesha zana za uchimbaji; kuwapatia utaalamu na matumizi ya teknolojia katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini.
Aidha, Serikali inashughulikia kero zinazowakabili wachimbaji wadogo ili waweze kuendesha shughuli zao za uchimbaji mdogo na kunufaika na rasilimali ya madini.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** mfano mzuri wa utekelezaji wa dhamira hiyo nzuri ya Serikali ni kitendo cha Mheshimiwa Rais kukutana na kufanya mazungumzo na wachimbaji wadogo mwezi Januari 2019, Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuwasikiliza na kutatua kero zao. Vilevile, Mheshimiwa Rais alielekeza kufutwa kwa kodi ya ongezeko la thamani na kodi

ya zuio kwa wachimbaji wadogo maelekezo ambayo tayari yamefanyiwa kazi.

**79. Mheshimiwa Spika,** kufutwa kwa kodi na tozo hizo kunatarajiwa kupunguza utoroshwaji wa madini; kuwatambua wachimbaji wadogo kupitia masoko ya madini yatakayoanzishwa na kuwapunguzia gharama za uendeshaji wa shughuli zao. Hatua hiyo pia, itaongeza wigo wa mapato kwa nchi kwa kuwa sasa madini yatauzwa katika utaratibu unaotambulika rasmi. Rai yangu kwa wachimbaji wote wadogo, endeleeni kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali katika kutekeleza majukumu yenu.

**80. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kukuza soko la ndani la madini kwa kuvutia wawekezaji na kuhamasisha shughuli za uongezaji wa thamani madini nchini. Pia, mkazo utawekwa katika kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa masoko ya madini yenye ushindani mkubwa ili kudhibiti utoroshaji wa maliasili hiyo. Aidha, Serikali itaendelea kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo wa madini ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo, huduma za utafiti, teknolojia, mitaji na masoko.

***Nishati***

**81. Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa viwanda sambamba na kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme ya kutosha, uhakika na nafuu. Kwa kutambua hilo, Serikali inatekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji wa umeme yenye lengo la kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na ukuaji wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

**82. Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba, 2018 niliungana na Mhe. Dkt. Mostafa Madbouly Waziri Mkuu wa Jamhuri ya kiarabu ya Misri kushuhudia uwekaji saini mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme wa MW **2,100** kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya *JV Arab Contractors & Elsewedy Electric* ya Misri. Mradi huo unaotarajiwa kukamilika 2021/2022 utawezesha ujenzi wa

uchumi wa viwanda kwa kuhakikisha upatikanaji wa umeme tena kwa bei nafuu.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwishoni mwa Februari, 2019 uwezo wa jumla wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini umeongezeka kutoka takriban MW **1,205** mwaka 2015 hadi kufikia MW **1,614** mwaka 2019. Ongezeko hilo limewezesha kuwa na umeme wa ziada wa wastani wa zaidi ya MW **300**.

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutekeleza kwa mafanikio makubwa mpango wa usambazaji wa umeme vijijini. Katika mwaka 2018/2019, vijiji **1,782** vimeunganishwa na umeme. Aidha, tangu kuanza kwa usambazaji wa umeme vijijini, tayari vijiji **5,746** vimeunganishiwa umeme kati ya vijiji **12,268** vilivyopo nchini; sawa na takriban asilimia **47** ya vijiji vyote.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji umeme wa maji na kusambaza umeme vijijini Awamu ya Tatu ambapo vijiji vyote vitakavyosalia vitapatiwa umeme.

**HUDUMA ZA KIUCHUMI**

***Ardhi***

**86.** **Mheshimiwa Spika,** rasilimali ardhi ina umuhimu wa pekee katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na uzalishaji mali. Kutokana na umuhimu huo, Serikali inachukua hatua madhubuti za kuiendeleza rasilimali hii kwa kuipanga, kuipima na kuimilikisha kwa taasisi na wananchi kama inavyopaswa. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, (2013 – 2033) ambapo jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 263 katika Wilaya **45** imeandaliwa.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro, Wizara za kisekta zimeanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais tarehe 15 Januari, 2019.

Maelekezo hayo, ni pamoja na kurasimisha vijiji 351 vilivyokuwemo kwenye hifadhi za misitu na mapori tengefu yaliyokosa sifa pamoja na kufuta jumla ya ekari **121,032** za ranchi na mashamba yaliyotelekezwa. Hatua hizi zimewezesha wananchi kupata ajira na pia kupata sehemu za kufanya shughuli za kilimo, ufugaji na makazi.

**88.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mradi wa Mikopo ya Nyumba unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, Serikali imeshusha riba ya mikopo inayotolewa kwa mabenki na taasisi za fedha kutoka asilimia **10** hadi asilimia **7.5** na jumla ya wananchi **4,174** wamenufaika na mikopo inayotolewa na benki na taasisi hizo za fedha. Aidha, Mfuko wa Mikopo Midogo Midogo ya Nyumba ulio chini ya Benki Kuu umeongezewa mtaji wa dola za Marekani milioni **18** ambapo taasisi za fedha tano zimepatiwa mtaji wa shilingi bilioni **13.87** kwa ajili ya kukopesha wananchi wa kipato cha chini kwa masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

**89.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, (2013 – 2033), ikiwemo kupima, kupanga na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini na kutekeleza programu ya kurasimisha makazi katika miji mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulinda hifadhi na vyanzo vya maji ili kuleta manufaa endelevu kwa Taifa na pia kuhimiza kilimo na ufugaji wenye tija utakaoleta maendeleo endelevu.

***Barabara***

**90.** **Mheshimiwa Spika**, lengo la Serikali ni kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami ili kuimarisha na kurahisisha mawasiliano ya usafiri na usafirishaji wa watu, bidhaa na mazao mbalimbali. Hadi kufikia Februari 2019, jumla ya kilomita **266.78** za barabara kuu na za mikoa zimekamilika na kilomita **392.2** zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Halikadhalika, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja matano katika Mto Lukuledi (Lindi), Mara (Mara), Sibiti

(Singida), Momba (Rukwa na Songwe) na Mlalakuwa (Dar es Salaam) na ujenzi wa madaraja **8** unaendelea katika sehemu mbalimbali nchini. Ujenzi wa miradi hii, utatoa fursa mbalimbali kwa wananchi kupata ajira pamoja na kupata soko kwa bidhaa na mazao yao.

**91.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa miradi ya barabara inayolenga kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa barabara kuwezesha mradi wa kuzalisha umeme wa Stiegler's Gorge kwa kiwango cha changarawe kutoka Ubena Zomozi mpaka Selous (**km 177.6**); na ukarabati wa barabara ya kutoka Kibiti – Mloka – Selous (**km 201**). Miradi mingine ni pamoja na ujenzi wa barabara kutoka Tabora – Mpanda (**km 370**), Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo (**km 239**), Loliondo – Mto wa Mbu (**km 213**), na barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (**km 464**).

***Kuondoa Msongamano wa Magari Jijini Dar es Salaam***

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kuondoa msongamano wa magari kwenye Jiji la Dar es Salaam, ili kurahisisha usafiri na usafirishaji na kuchochea shughuli za kiuchumi. Miradi iliyokamilika ni ujenzi wa barabara ya juu ya Mfugale na barabara za mlisho. Miradi inayoendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni Ujenzi wa Barabara za Juu kwenye makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange), Upanuzi wa barabara ya Kimara Mwisho – Kiluvya (**km 19.2**) kutoka njia mbili kuwa nane, Daraja Jipya la Selander na Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya II na III.

**93.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa mikoa ambayo haijaunganishwa na barabara kuu za lami.

***Vivuko***

**94.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Serikali imekamilisha ujenzi wa vivuko viwili vipya vya Magogoni – Kigamboni na Kigongo - Busisi. Aidha, ujenzi wa vivuko vipya

vinne vya Kayenze – Bezi, Nyamisati – Mafia, Nkome - Chato – Muharamba na Bugolora - Ukara unaendelea. Vilevile, Serikali imekamilisha ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II (Pangani) na ukarabati mkubwa wa vivuko viwili vya MV Sengerema (Mwanza) na MV Kigamboni (Dar es Salaam).

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia, imekamilisha ujenzi wa maegesho ya Bwina (Geita) na Lindi – Kitunda (Lindi). Pia, taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia (Pwani), Kayenze - Bezi (Mwanza) na Mlimba - Malinyi (Morogoro) zinaendelea.

***Viwanja vya Ndege***

**96.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usafiri wa anga nchini Serikali inakamilisha ujenzi wa Jengo la Tatu la abiria katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Jijini Dar es Salaam. Jengo hilo ambalo hadi kufikia Februari 2019 ujenzi wake umefikia asilimia **95.5** litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka pindi litakapokamilika Mei 2019.

**97.** **Mheshimiwa Spika,** jengo hilo linatarajiwa kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu cha utalii kwa kuwezesha watalii wanaoingia nchini kuelekea katika maeneo mbalimbali ya vivutio vyetu na nchi jirani katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Mpango huu wa kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu cha utalii unakwenda sambamba na maboresho ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL). Lengo ni kuhakikisha watalii wanaoingia nchini wanakuwa na usafiri wa uhakika kuvifikia vivutio vyetu na kuelekea katika nchi za jirani. Kwa kufanya hivyo, shughuli za kiuchumi nchini zenye kufungamana na utalii hususan ajira, huduma, biashara na usafirishaji zitaimarika na kuwaongezea kipato watu wetu.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza dhamira ya kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kisasa, Serikali inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato. Lengo la Serikali ni kulifanya Jiji la Dodoma ambalo ndilo Makao Makuu ya Nchi kuwa kitovu cha mawasiliano na maeneo mengine

nchini. Kwa sasa kazi inayoendelea ni kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Kiwanja kuendana na hadhi na mahitaji ya Makao Makuu ya Nchi.

**99. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa viwanja vingine vya ndege vya Songwe, Kigoma, Sumbawanga, Shinyanga, Tabora, Mtwara, Songea, Nachingwea, Lindi, Iringa na Musoma ambavyo viko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

***Reli***

**100. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa awamu ya kwanza wa Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro umefikia asilimia **42.8** na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2019. Halikadhalika, ujenzi wa awamu ya pili wa reli hiyo ya kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora Jijini Dodoma umefikia asilimia **6.07**. Hadi sasa Mradi kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora umeshaajiri wafanyakazi wazawa wapatao **6,335** sawa na asilimia **90** ya wafanyakazi wote.

**101. Mheshimiwa Spika,** sambamba na ujenzi wa reli mpya ya kisasa, Serikali katika mwaka 2018/2019 imeendelea na kazi ya kuboresha, kujenga na kukarabati miundombinu ya reli ya kati kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenye uzani wa paundi **80** kwa yadi kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Isaka. Aidha, kazi ya ukarabati wa reli ya Tanga – Arusha imekamilika kwa sehemu ya Tanga – Same (km 199).

**102. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea na kazi ya ujenzi wa reli ya kisasa, ukarabati na ujenzi wa reli ya kati na nyingine ikiwemo ya Tanga – Arusha ili kuimarisha huduma za usafirishaji na biashara kwa ujumla.

***Bandari***

**103. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, kazi ya kuboresha Bandari ya Dar es Salaam kupitia Mradi wa Dar es Salaam Maritime Gateway inaendelea. Lengo la Serikali ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri wa majini na kuiwezesha kushindana na Bandari nyingine katika Ukanda

huu. Kazi za kuboresha gati namba moja hadi gati namba namba saba na ujenzi wa gati jipya la kuhudumia meli za magari zimekamilika kwa asilimia **65**.

**104. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kumaliza changamoto ya usafiri kwa njia ya maji katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kutekeleza azma hiyo, Septemba 2018 Serikali iliingia mikataba minne na Kampuni ya KTMI ya Jamhuri ya Korea kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya ya kisasa ziwa Victoria; chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria na MV Butiama.

**105. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa meli mpya itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria **1,200**, tani **400** za mizigo na magari madogo **200** utafanywa na kampuni ya KTMI kwa kushirikiana na SUMA JKT. Aidha, ujenzi na ukarabati wa meli hizo, utakwenda sambamba na kujenga uwezo kwa wataalamu wetu wa ndani katika tasnia ya ujenzi na ukarabati mkubwa wa meli kwa kushirikiana na kampuni zitakazotekeleza ujenzi huo. Aidha, katika mwaka 2019/2020, Serikali itasimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika na ukarabati mkubwa wa meli za MV Liemba, MV Umoja na MV Serengeti.

## SEKTA YA MAWASILIANO

### *Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano*

**106. Mheshimiwa Spika,** ninayo furaha kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba katika mwaka 2018/2019, Zanzibar imeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kupitia utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya ujenzi. Huduma kwa wateja zitaanza kupatikana Juni 2019. Matumizi ya huduma za mkongo kwa upande wa Zanzibar yatachochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kuinua kipato cha wananchi.

**107. Mheshimiwa Spika,** sambamba na Mkongo wa Taifa, Kituo cha Data cha Taifa kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi hasa katika kuongeza ukusanyaji wa mapato Serikalini. Hadi kufikia Desemba 2018,

kituo kimeweza kuunganisha wateja **79** ambapo Taasisi na Idara za Serikali ni **56** na taasisi binafsi **23**. Uhamasishaji unaendelea kufanyika kwa kuunganisha Taasisi nyingi zaidi ili kuendelea kukuza usalama na kupunguza gharama za uendeshaji wa miundombinu ya TEHAMA nchini.

**108. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine ya kuhakikisha kunakuwepo udhibiti wa kutosha katika mawasiliano, Serikali ilipokea Mfumo wa kusimamia Mawasiliano (TTMS) wenye uwezo wa kubaini takwimu mbalimbali zinazopita katika mitandao ya mawasiliano. Mfumo huo pamoja na mambo mengine utasaidia kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika sekta ya mawasiliano kwa kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao sanjari na kudhibiti matumizi mabaya ya mtandao kwa kugundua mawasiliano ya ulaghai.

**109. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma hiyo katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha Taasisi na wateja wengine kuunganishwa na Kituo cha Data cha Taifa.

## HUDUMA ZA JAMII

### *Elimu*

**110. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatekeleza kwa mafanikio makubwa Mpango wa Elimumsingi bila malipo wenye lengo la kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania mwenye umri wa kwenda shule anapata haki ya kupata elimumsingi bila kikwazo cha ada na michango mingine. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu, Serikali imetumia Shilingi bilioni **711.22** kutekeleza Mpango huo. Katika mwaka 2018/2019 Serikali tayari imetoa Shilingi bilioni **166.44** hadi Februari, 2019 kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo nchini. Utekelezaji wa mpango huo, umeongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za msingi na Sekondari nchini.

**111. Mheshimiwa Spika,** sambamba na utekelezaji wa elimumsingi bila malipo, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na Washirika wa Maendeleo imeboresha miundombinu ya

shule za awali na msingi ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa **6,521** kwa shule za msingi na hivyo kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **119,647** vilivyokuwepo mwaka 2017 hadi **126,168** Februari 2019, sawa na ongezeko la asilimia **5.5**. Kwa upande wa shule za Sekondari, vyumba **2,499** vya madarasa vimejengwa na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **40,720** Mwaka 2018 hadi **43,219** kufikia Februari, 2019. Aidha, madarasa **2,514** yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**112. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha taifa letu linajenga uchumi ulio imara, linajenga jamii inayoheshimu na kufuata misingi ya uwajibikaji na ubunifu, Serikali pamoja na mambo mengine imeendelea kuwekeza katika elimu ya juu. Serikali imeendelea kuhakikisha watanzania wote wenye sifa wanapata elimu ya juu kwa kupewa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Katika mwaka 2018/2019, Shilingi bilioni **412.4** zimetolewa kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Hatua hiyo, imeongeza idadi ya wanufaika wa mikopo hiyo kufikia wanafunzi **119,214** kutoka wanafunzi **98,300** mwaka 2015.

**113. Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa wigo wa utoaji elimu nchini unapanuka. Hivyo, ili kulinda ubora wa elimu yetu ninazielekeza mamlaka zote zinazohusika na usimamizi na udhibiti wa ubora wa elimu zitekeleze majukumu yao ipasavyo kwa kutoa miongozo na kufanya kaguzi za mara kwa mara.

***Maji***

**Upatikanaji wa Maji Vijijini**

**114. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kwa kujenga miradi ya maji sehemu mbalimbali nchini ili kusogeza huduma hiyo karibu zaidi na wananchi. Hadi Februari 2019, jumla ya miradi **65** ya maji vijijini ilikamilishwa ambapo wananchi milioni **25.36** waishio katika vijiji hivyo wamenufaika. Kutokana na kukamilika kwa miradi hiyo, hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka kutoka asilimia **58.7** Julai 2018 na kufikia asilimia **64.8** Februari, 2019. Katika mwaka 2019/2020, Serikali

itaendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa na kukamilisha miradi mingine **482** iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwenye Halmashauri nchini.

***Upatikanaji wa Maji Mijini***

**115.** Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi katika miji hiyo. Hadi Februari 2019, upatikanaji wa maji safi na salama katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine yanayohudumiwa na DAWASA umefikia asilimia **85**.

Katika Miji Mikuu ya Mikoa, upatikanaji wa huduma ya maji imefikia wastani wa asilimia **80**. Aidha, katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa upatikanaji wa huduma ya maji umefikia wastani wa asilimia **64**.

**116.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kukamilisha miradi mbalimbali ya maji pamoja na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria mpya ya huduma za maji na usafi wa mazingira.

***Afya***

***Miundombinu ya Huduma za Afya***

**117.** **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa uchumi wa viwanda unakwenda pamoja na ujenzi wa taifa lenye watu wenye afya bora wanaoweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi husika. Kwa msingi huo, Serikali inaimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kujenga, kukarabati na kuvipatia mahitaji muhimu vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kufanikisha azma hiyo, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kutoka vituo **7,678** mwaka 2017 hadi **8,119** mwaka 2018, sawa na ongezeko la vituo **441**. Ongezeko hilo limesaidia kusogeza huduma ya afya karibu zaidi na wananchi na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga pamoja na kuboresha afya za wananchi wetu kwa ujumla.

***Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali***

**118. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali tano za mikoa ambayo ilikuwa haina Hospitali za Rufaa. Katika miradi hiyo, jumla ya Shilingi bilioni **6.5** zimetolewa kwa Mikoa mipya ya Songwe, Katavi, Njombe, Geita na Simiyu.Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali **67** katika halmashauri mbalimbali ambapo jumla ya Shilingi bilioni **100.5** sawa na Shilingi bilioni **1.5** kwa kila halmashauri zimetolewa.

**119. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaboresha zaidi miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa miundombinu hiyo, kuendelea na ujenzi wa hospitali za rufaa za mikoa isiyokuwa na hospitali pamoja na kuendelea na ujenzi wa Hospitali za wilaya katika Halmashauri ambazo hazina hospitali hizo.

***Upatikanaji wa Dawa na vifaa tiba***

**120. Mheshimiwa Spika;** ujenzi wa vituo vya kutolea huduma ya afya nchini unakwenda sambamba na upatikanaji wa dawa na vifaa na vifaa tiba. Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya nchini imefikia asilimia **96.7** mwaka 2018/ 2019.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa, Serikali imefunga Mashine mpya za X-ray **11** katika hospitali za Ruvuma, Morogoro, Simiyu, Magu, Chato, Singida, Nzega, Njombe, Bukoba, Amana na Mpanda. Vilevile, Serikali imekamilisha kuweka mashine ya MRI, CT-SCAN, Digital X-Ray mashine, Moden Utrasound mashine na vifaa vya Wodini vyenye thamani ya shilingi bilioni 12 katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI). Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa Dawa, vifaa, na vifaa tiba katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya nchini.

***Huduma za Afya za Kibingwa***

**122. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na Hospitali ya Benjamin Mkapa. Huduma za kibingwa zinazotolewa ni upandikizaji figo, upasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo, upasuaji wa mishipa ya fahamu na ubadilishaji wa nyonga pamoja na upandakizaji wa vifaa vya kusaidia usikivu.

**123. Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa huduma hizo za kibingwa ambazo awali zilipatikana nje ya nchi pekee umepunguza gharama za kupeleka wagonjwa wengi nje ya nchi kwa ajili ya matibabu. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Januari 2019, kulikuwa na wagonjwa **38** waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi ikilinganisha na wagonjwa **114** katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017.

**124. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaimarisha huduma za kibingwa katika hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za magonjwa Maalum kwa kuendelea na ujenzi wa majengo ya kutolea huduma, kusimika mitambo ya uchunguzi na vifaa tiba.

***Ulinzi wa Wanawake na Watoto***

**125. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kwa kipindi cha 2017/18 – 2021/2022. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeanzisha Kamati **3,605** za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi mbalimbali. Kati ya hizo, Kamati 1,289 zimeanzishwa katika ngazi ya Kata na Kamati **2,313** katika ngazi ya Mtaa/Kijiji. Lengo la kamati hizi ni kuhakikisha ulinzi na usalama wa wanawake na watoto katika jamii. Aidha, uanzishaji wa Kamati umeongezeka kutoka Kamati **7,383** mwaka 2017/2018 hadi Kamati **10,988** mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia **48.83**. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu wa

utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22).

***Huduma kwa Wazee***

**126.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa wazee nchini wanapata matibabu kupitia vitambulisho vinavyowawezesha kupata matibabu bure.

**127.** Katika mwaka 2018/2019 wazee **247,771** wamepatiwa kadi za matibabu bure. Juhudi hii imewezesha wazee waliopata vitambulisho vya matibabu bure kuongezeka kutoka wazee **213,025** mwaka 2015/2016 hadi kufikia wazee **1,042,329** mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la wazee **829,304**. Serikali itaendelea kuwatambua wazee na kuhakikisha inawapatia vitambulisho vya matibabu bure wazee wote nchini.

***Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu***

**128.** **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2018/2019, Serikali imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikataba inayohusu haki na huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni pamoja na Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na. **9** ya mwaka 2010. Sheria hiyo, pamoja na masuala mengine, inamtaka kila mwajiri mwenye waajiriwa kuanzia **20** kuwa na watumishi wenye ulemavu wasiopungua asilimia **3**.

**129.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeendelea kutoa chakula, matibabu, malazi, ushauri nasaha na mafunzo ya stadi za kazi kwa wanafunzi wenye ulemavu katika vyuo vya Singida na Yombo – Dar es Salaam. Vilevile, Serikali imewezesha upatikanaji wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kuzifikia huduma mbalimbali bila vikwazo. Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na viti mwendo, fimbo nyeupe, magongo ya kutembelea, viti maalum vya kuogea, miwani maalum, kofia pana, vifaa vya kukuzia maandishi, mafuta kinga kwa ajili ya Watu wenye Ualbino na mashine za kuchapia maandishi ya nukta nundu kwa Wasioona.

**130.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeratibu maadhimisho ya siku za watu wenye ulemavu ili kuondoa unyanyapaa

miongoni mwa jamii ikiwa ni pamoja na; siku ya Fimbo nyeupe, Siku ya Viziwi na Siku ya watoto wenye ulemavu. Katika maadhimisho hayo, elimu ya kutowanyanyapaa watu wenye ulemavu ilitolewa. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu uundwaji wa Kamati za Watu wenye Ulemavu ambapo Kamati **26** zimeundwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, ngazi ya Halmashauri Kamati **140**, ngazi ya Vijiji Kamati **5,024** na ngazi ya Mitaa Kamati **2,284**.

**131.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu, Serikali imekamilisha uundaji wa Baraza jipya la Ushauri la Taifa kwa Watu wenye Ulemavu baada ya lililopita kumaliza muda wake. Ni matajio ya Serikali kwamba Baraza hilo litaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kuhusu huduma kwa watu wenye ulemavu hususan masuala ya afya, ajira, elimu na miundombinu pamoja na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu.

**132.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Serikali itafanya mapitio ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya mwaka 2010 ili iweze kwenda na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, kukusanya maoni na mapendekezo ya uendeshwaji wa Mfuko wa Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu pamoja na kuratibu uendeshaji wa shughuli za Baraza la Ushauri la Taifa kwa Watu wenye Ulemavu.

***ULINZI NA USALAMA***

**133.** **Mheshimiwa Spika**, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi kubwa katika kuhakikisha hali ya amani, usalama na utulivu nchini inaimarika. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imelitumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania kusaidia mamlaka za kiraia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali kama vile uokoaji wa watu na mali zao pamoja na ujenzi wa mji wa Serikali katika eneo la Mtumba, Dodoma.

**134.** **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushiriki kwenye misheni za kulinda amani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Misheni hizo ni MINUSCA huko Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR);

MONUSCO Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC); UNAMID nchini Sudan; UNFIL nchini Lebanon; UNISFA huko Abyei na UNMISS nchini Sudan Kusini.

**135. Mheshimiwa Spika**, ushiriki wa Jeshi letu pamoja na vyombo vingine vya usalama katika misheni hizo za amani, umeendelea kuvipatia uzoefu, kuongeza maarifa na mbinu mbalimbali za kijeshi na kiintelijensia. Aidha, vyombo vyetu vimeendelea kujifunza matumizi ya vifaa vya kisasa na kuanzisha au kuimarisha mahusiano ya kijeshi na nchi nyingine zinazoshiriki kwenye misheni hizo.

**136. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao, Serikali imeendelea kudhibiti hali ya ulinzi na usalama nchini kwa kuboresha mazingira ya kuishi askari na kufanyia kazi; kutoa huduma bora za kubaini, kutanzua na kudhibiti uhalifu; kudhibiti vitendo vya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi pamoja na kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kupambana na uhalifu nchini. Hali hii imechangia kupunguza makosa ya kiuhalifu kutoka makosa **37,602** mwaka 2017 hadi kufikia makosa **36,228** mwaka 2018.

**137. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa uhamiaji Serikali inatekeleza kwa mafanikio makubwa awamu ya pili ya Mradi wa Uhamiaji Mtandao, ambayo inahusisha utoaji wa huduma ya Viza pamoja na Vibali vya Ukaazi vya Kielektroniki. Aidha, tarehe 26 Novemba 2018, nilizindua mfumo huo ambao sasa unamuwezesha mteja kufanya maombi yake kwa njia ya mtandao. Mfumo huo, utarahisisha utoaji wa huduma bora za uhamiaji, kuimarisha ulinzi na usalama, kuongeza udhibiti wa wageni wanaoingia nchini, ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi kupitia sekta ya uwekezaji.

**138. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha hali ya ulinzi na usalama, kuendelea kutoa fursa za mafunzo kwa vyombo vya ulinzi na usalama, kuvipatia vifaa na zana za kisasa na kuendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka.

## KAZI, AJIRA NA VIJANA

### *Maendeleo ya Vijana*

**139. Mheshimiwa Spika,** nguvukazi ya vijana ni mhimili muhimu katika kuwezesha nchi yetu kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025. Katika 2018/2019, Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Vijana imewezesha vikundi vya vijana **755** ambavyo vimepatiwa mikopo ya Shilingi Bilioni **4.2** kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, imeibua bunifu **31** za Vijana katika sekta ya sayansi na teknolojia. Kati ya hizo, bunifu **11** zimefanyiwa tathmini ya kisayansi na kwa sasa ziko katika hatua mbalimbali ikiwemo kuwekwa kwenye kiota atamizi (Incubator) kabla ya hatua ya majaribio na uzalishaji.

**140. Mheshimiwa Spika,** bunifu nyingi zimefanyika nchini kama vile: kifaa cha kupimia matatizo ya moyo; kiti maalum cha kuhudumia watoto wenye usonji; mfumo wa kuwasha na kuzima taa za nje za ndege kwa kutumia simu ya mkononi; mguu wa ndege kwa ajili ya matumizi ya kufundishia vyuoni; na gari linalotumia mfumo wa umeme. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuwawezesha vijana kimitaji kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mapato ya ndani ya Halmashauri na Programu ya kukuza ujuzi.

### *Ukuzaji Ujuzi*

**141. Mheshimiwa Spika,** ushiriki wa nguvukazi ya taifa hususan vijana ni muhimu katika kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Hivyo basi, Serikali inatekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi inayolenga kuwapatia vijana ujuzi stahiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi kwa kujiajiri au kuajiriwa.

**142. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, jumla ya vijana **32,563** wamewezeshwa kupata mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa. Hii inahusisha vijana **18,800** waliopata mafunzo ya ujuzi wa kilimo kwa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba pamoja na vijana **2,720** waliopatiwa mafunzo ya ufundi wa fani mbalimbali pamoja vijana **10,443** waliopatiwa

mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kwa fani za ufundi wa magari, useremala, uashi, upishi, huduma za vyakula na vinywaji, ufundi umeme, uchomeleaji, ufundi bomba, uchongaji vipuri na ushonaji nguo.

**143. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri, kuajiriwa na stadi za kazi kwa vijana **46,950** katika fani mbalimbali. Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza vijana kuchangamkia fursa za mafunzo haya kwa kuwa ni nyenzo muhimu kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

***Fursa za Ajira***

**144. Mheshimiwa Spika,** utengenezaji wa fursa za ajira umeendelea kuwa agenda ya kipaumbele ya Serikali ya Awamu ya Tano. Suala hilo, limezingatiwa katika sera, mipango na programu zote za maendeleo ya kitaifa na kisekta. Hadi kufikia Februari 2019, jumla ya ajira **221,807** zimezalishwa nchini. Kati ya ajira hizo, ajira **146,414** sawa na asilimia 66 zimetokana na utekelezaji wa miradi ya umma ya ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi kama vile ujenzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji, umeme, ujenzi wa Mji wa Serikali Jijini Dodoma, uimarishaji wa Shirika la Ndege Tanzania pamoja na ajira za moja kwa moja katika Utumishi wa Umma. Aidha, ajira **75,393** ambazo ni asilimia **34** ya ajira zilizozalishwa zimetokana na uwekezaji katika sekta binafsi.

**145. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan Waajiri na Wafanyakazi, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo pamoja na Vyama vya Kiraia itaendelea kutekeleza programu zinazowezesha kuibua fursa zaidi za ajira.

***Masuala ya Kazi na Wafanyakazi***

**146. Mheshimiwa Spika,** utulivu na amani mahali pa kazi ni nguzo muhimu kuwezesha uzalishaji na tija katika maeneo mbalimbali ikiwemo viwandani na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa kutambua ukweli huu, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za kazi ili kuwezesha

mazingira yanayopelekea kazi za staha pamoja na uwepo wa amani na utulivu mahali pa kazi.

Katika mwaka 2018/2019, jumla ya kaguzi **2,516** zimefanyika zikihusisha kaguzi za kawaida 2007, kaguzi maalum **382** na kaguzi za ufuatiliaji **127**. Vilevile, jumla ya Amri Tekelezi **455** zilitolewa kwa waajiri na waajiri **16** walifikishwa Mahakamani kwa kukiuka Sheria za Kazi. Jumla ya shilingi milioni **285** zilitozwa kama adhabu kwa waajiri waliopatikana na hatia. Aidha, jumla ya Waajiri **414** na Wafanyakazi **2,572** walielimishwa kuhusu Sheria za Kazi.

**147.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi kwa kusimamia uundwaji wa Mabaraza ya wafanyakazi mahala pa kazi. Katika mwaka 2018/2019, Mabaraza **116** yameundwa na Mabaraza **110** yamepewa elimu kuhusu wajibu na majukumu yao na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi. Aidha, katika kuimarisha mahusiano mema miongoni mwa viongozi wa vyama vya wafanyakazi, vikao **9** vya maridhiano vilifanyika kwa lengo la kusuluhisha migogoro ya kivyama na viongozi.

**148.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia, inasimamia na kuratibu ajira za wageni nchini kwa kutumia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Namba.**1** ya mwaka 2015. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya vibali vya kazi **8,703** vilitolewa, jumla ya maombi **974** yalikataliwa na maombi **1,701** yalipewa msamaha. Aidha, katika kusimamia na kuratibu Huduma za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira nchini, jumla ya maombi **20** ya wakala yamepatiwa usajili na maombi matatu yamekataliwa.

**149.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria za kazi ili kuwezesha utulivu mahala pa kazi na hivyo kuchochea uwekezaji na ukuzaji wa uchumi. Hii itahusisha kufanya kaguzi za kazi, kufanya mapitio na marekebisho ya Sheria za Kazi na kufanya utambuzi wa wadau wanaotekeleza shughuli za kukomesha utumikishwaji wa mtoto.

***Hifadhi ya Jamii***

**150. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeanza utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Na.2 ya Mwaka 2018 kwa kuunganisha Mifuko ya LAPF, GEPF, PSPF na PPF na kuanzisha mfuko mmoja wa PSSSF. Kutokana na maboresho hayo, Serikali imelipa madeni yote ya wastaafu wa PSPF wa mwaka 2017/2018 wapatao **9,971** yenye thamani ya Shilingi bilioni **888.39**. Hatua hii ni kubwa kwa kuwa imeweza kutatua kero za wastaafu ambazo zilidumu kwa muda mrefu.

**151. Mheshimiwa Spika,** tarehe 29 Desemba 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na viongozi wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania ambapo alielekeza kila Mfuko wa Pensheni uendelee kutumia kikotoo chake cha zamani katika kipindi cha mpito cha miaka mitano ijayo. Katika kutekeleza maagizo hayo, PSSSF kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi imeandaa Mpango Kazi wa namna ya kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha mpito (2019 – 2023) ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa jumla ya wastaafu **81,525** wa mfuko huo.

**152. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Mhe. Rais kwa kushirikiana na Shirikisho la Wafanyakazi ili kuwezesha kupata kanuni ambazo zitakidhi matarajio ya wafanyakazi wa Sekta ya Umma na Binafsi na kuhakikisha mifuko inakuwa endelevu.

**MASUALA MTAMBUKA**

***Vita Dhidi ya Rushwa***

**153. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inaendelea kutekeleza majukumu yake ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwa ni pamoja na kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria. Aidha, Serikali

imeendelea kujenga uelewa kwenye Taasisi za Umma na kuweka mfumo thabiti wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) ili kupata matokeo yaliyo bora zaidi katika vita dhidi ya Rushwa nchini.

**154. Mheshimiwa Spika,** kutokana na utekelezaji mzuri wa Mkakati huo na juhudi zinazofanywa na TAKUKURU na wadau wengine nchini, tatizo la rushwa limepungua. Katika upimaji wa hali ya rushwa uliofanywa na mashirika ya kimataifa yameonesha Tanzania kufanya vizuri miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano, ripoti ya taasisi ya *Transparency International* ya mwaka 2018, Tanzania imeshika nafasi ya pili baada ya Rwanda kwenye mapambano dhidi ya rushwa.

**155. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) katika Sekta zote kwa mfumo jumuishi na msisitizo ukiwekwa kwenye mfumo wa mrejesho kwa wadau kama nguzo muhimu ya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati huu. TAKUKURU pia, itaendelea kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea na tuhuma mpya zitakazojitokeza pamoja na kuendesha mashauri yanayoendelea mahakamani na mashauri mapya yatakayofunguliwa Mahakamani. Aidha, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 itahuishwa.

***Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya***

**156. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na mapambano dhidi ya uzalishaji, uuzaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Aidha, Serikali imeendelea kubaini mtandao wa waingizaji wa dawa hizo hapa nchini na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahalifu hao. Kutokana na juhudi hizo, Septemba 2018, nchi yetu ilipata heshima kubwa ya kuandaa Mkutano wa Mwaka wa Wakuu wa Vyombo Vinavyopambana na Dawa za Kulevya Afrika (HONLEA AFRICA) uliofanyika Jijini Dar es Salaam. Kupitia mkutano huo, vyombo vyetu vya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya viliweza kubadilishana mbinu, uzoefu, kupeana mikakati ya kukabiliana na changamoto ya dawa za kulevya pamoja na kubadilishana taarifa kuhusu kadhia hiyo.

**157. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Januari 2019, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola imefanikiwa kukamata watuhumiwa **11,617** wakiwa na dawa za kulevya za aina mbalimbali kama vile heroin, cocaine, bangi na mirungi. Aidha, ekari zaidi ya **59** za mashamba ya bangi ziliteketezwa nchini katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma na Mara.

**158. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa waraibu wa dawa za kulevya, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa kutumia dawa ya Methadone katika mkoa wa Dar es Salaam na vituo vipya katika mikoa ya Dodoma, Mwanza na Mbeya. Aidha, kufikia Januari 2019, watumiaji wapatao **6,500** wanapata huduma za tiba ya methadone katika vituo vilivyopo nchini. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa waraibu wanaopatiwa matibabu hawarejei tena kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

**159. Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha azma hiyo, Serikali imetenga shilingi billion mbili kwa ajili ya ukuzaji ujuzi kwa vijana. Mpango huo utawahusisha vijana ikiwa ni pamoja na wale walioachana na matumizi ya dawa za kulevya. Vijana hawa watapelekwa viwandani na sehemu mbalimbali za kazi kwa lengo la kukuza ujuzi wao na baadaye kupatiwa fursa za ajira.

**160. Mheshimiwa Spika,** dawa za kulevya zina athari kubwa kwa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla. Hivyo, napenda kurejea wito wangu kwa Watanzania wote kuunga mkono jitihada za Serikali katika mapambano haya kwa kutoa taarifa kuhusu watu wote wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya nchini. Aidha, rai yangu kwa waraibu ambao wamepatiwa ujuzi kujiunga kwenye vikundi vidogo vidogo ili waweze kupatiwa mikopo na hivyo kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

***Mapambano Dhidi ya UKIMWI***

**161. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza kutekeleza Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi

cha mwaka 2018/2019 - 2022/2023 ambao unalenga kuzuia maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na UKIMWI nchini. Tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Tatu wa Taifa uliomaliza muda wake Juni 2018 umeonesha kwamba; vifo na maambukizi mapya ya UKIMWI yamepungua. Kutokana na tathmini hiyo, ulifanyika utafiti (Tanzania HIV Impact Survey) mwaka 2016/2017 katika ngazi ya kaya ambao umeonesha kwamba kiwango cha Maambukizi ya VVU kwa Tanzania Bara kimeshuka kutoka asilimia **5.1** mwaka 2011/2012 hadi asilimia **4.8** mwaka 2016/2017.

**162. Mheshimiwa Spika,** bado tuna changamoto ya watanzania wengi kutojua afya zao na idadi kubwa ya WAVIU kutokuwa kwenye mpango wa matunzo na matibabu. Pamoja na dawa za ARV kutolewa bure, inakadiriwa kuwa kuna takriban WAVIU **500,000** ambao hawapati dawa hizo.

Nitoe rai kwa wadau wote nchini kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha watu kupima na kujua hali zao za maambukizi ya VVU. Aidha, kwa wale watakaokutwa na maambukizi waingizwe kwenye mpango wa matibabu mapema iwezekanavyo na WAVIU wanaotumia dawa za kufubaza waendelee kutumia dawa hizo pasipo kuacha.

**163. Mheshimiwa Spika,** Serikali na Wadau mbalimbali wakiwemo wa ndani na nje wameendelea kuchangia Mfuko maalum wa Kupambana na Kudhibiti UKIMWI nchini (AIDS TRUST FUND) ili kuondokana na utegemezi wa wafadhili. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2018 Mfuko uliweza kukusanya Shilingi milioni **864**. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni **750** zimetolewa na Serikali na Shilingi milioni 114 zimekusanywa kutoka kwa wadau kupitia matembezi ya hiari na harambee. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika bajeti yake kwa kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI kila mwaka.

**164. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI ili kufikia lengo la TISINI TATU ifikapo mwaka 2020. Lengo la Mkakati huo ni kwamba hadi kufikia mwaka 2020, asilimia **90** ya watu wanaoishi na VVU wawe wamejua hali

zao za maambukizi; asilimia **90** ya waliopima VVU na kugundulika kuwa na maambukizi wapatiwe dawa za kufubaza (ARV) na asilimia **90** ya watu wanaotumia dawa wawe wamefubaza VVU.

***Uratibu wa Maafa***

**165. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kikanda za EAC, SADC, Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Mataifa (UN) na Mashirika yake katika masuala ya usimamizi wa maafa kwa kufanya mafunzo ya vitendo na mazoezi ya pamoja ya kukabiliana na maafa. Vilevile, Serikali imetoa elimu kuhusu usimamizi wa maafa kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yote nchini.

**166. Mheshimiwa Spika**, kama unavyofahamu jirani zetu wa Msumbuji, Malawi na Zimbabwe walipata maafa yaliyosababishwa na kimbunga kikali kiitwacho Idai. Maafa hayo yalisababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa miundombinu na mazingira na watu wengi kukosa makazi katika nchi hizo. Kutokana na athari hizo, Serikali ilitoa msaada wa dharura wa kibinadamu wa tani **214** za chakula, tani **24** za madawa mbalimbali na vifaa vya kujihifadhi. Tumuombe Mwenyezi Mungu awajalie afya njema wale wote waliopata majeraha na azipumzishe mahala pema roho za marehemu. Amina!

**167. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za kuimarisha mifumo ya kufuatilia mienendo ya majanga na utoaji wa tahadhari ya awali ili kujenga jamii iliyo salama na stahimilivu. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali inazingatia vihatarishi vya maafa na hivyo, kuipunguzia gharama kubwa za kukabili na kurejesha hali baada ya madhara kutokea.

**MASUALA YA MUUNGANO**

**168. Mheshimiwa Spika,** Muungano wetu ni matokeo ya mahusiano ya kihistoria ya pande zote mbili, hivyo, hatunabudi kuuheshimu na kuulinda ili uendelee kudumu kwa faida ya watu wetu.

Katika kuimarisha Muungano wetu, Serikali zote mbili zimeendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoukabili.

**169. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika tarehe 21 Januari, 2019 kiliridhia utozwaji wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa kiwango cha asilimia sifuri (0%) kwenye umeme unaouzwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kufuta malimbikizo ya deni la kodi ya VAT lililofikia Shilingi Bilioni 22.9 kwa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwenye umeme uliouzwa na TANESCO.

**170. Mheshimiwa Spika,** kutokana na mafanikio haya yanayoendelea kupatikana katika utatuzi wa kero za Muungano, naomba nirudie kutoa wito wangu kwa Watanzania kuendelea kudumisha muungano wetu ambao ni tunu na mfano wa kuigwa barani Afrika na dunia nzima.

**UHUSIANO WA KIMATAIFA**

**171. Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imeendelea kuimarisha na kuendeleza mahusiano mema baina yake na Mataifa mengine na pia Mashirika ya Kikanda na Kimataifa duniani. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kutokana na jitihada hizo, Tanzania imeendelea kuwa nchi rafiki kwa mataifa yote duniani. Aidha, Serikali imeshiriki katika mikutano na majukwaa muhimu ya kikanda na kimataifa na kutetea maslahi ya Nchi ikiwemo kutoa ufafanuzi pale ambapo baadhi ya watu wa ndani na nje wenye nia mbaya walipojaribu kupotosha ukweli na kuchafua taswira ya Taifa letu.

**172. Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika mwezi Agosti 2018, nchini Namibia ulimteua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na kwa kuendelea

kutekeleza kwa ukamilifu wajibu na heshima hiyo aliyopewa na Wakuu wenzake wa Nchi na Serikali.

**173.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taratibu za SADC Makamu wa Mwenyekiti ndiye anayekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa mwaka unaofuata. Hivyo, mwezi Agosti mwaka huu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli anatarajiwa kuchukua nafasi ya Uenyekiti wa SADC katika mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC utakaofanyika Jijini Dar es Salaam. Napenda kutumia fursa hii kuwasihi wale wote wanaohusika na maandalizi ya mkutano huu mkubwa na muhimu kutekeleza jukumu hilo kwa bidii, weledi na ufanisi wa hali ya juu.

**174.** **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huu utawaleta Nchini Wakuu wa Nchi na Serikali, Mawaziri, Maofisa Waandamizi, wawakilishi wa jumuiya za wafanyabiashara, waandishi wa habari na wengineo kutoka Nchi **15** Wanachama SADC. Hii ni fursa muhimu siyo tu kwa Serikali bali pia kwa sekta binafsi nchini kujiandaa kuwapokea wageni hawa kwa malazi, usafiri, chakula na utalii. Nitoe wito, kwa watanzania kujipanga vyema na kuchangamkia fursa zitakazoambatana na ujio wa mkutano huo.

**175.** **Mheshimiwa Spika,** kama mnavyofahamu, Sera ya mambo ya nje ni mtambuka na ni mwendelezo wa sera ya ndani ya nchi katika nyanja na maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia muktadha huo, nitumie fursa hii kuwasisitiza mabalozi wetu nje kuendelea kutafuta mitaji ya uwekezaji hususan katika miradi ya vipaumbele, masoko mapya ya bidhaa zetu, kutangaza fursa za utalii na kutafuta fursa za mafunzo.

**176.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/2020, Serikali itahakikisha utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi unaendelea kupewa kipaumbele cha kutosha ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Taifa ya Diaspora; kuendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda; kuimarisha ujirani mwema na mahusiano na taasisi za kimataifa; kupigania mfumo wa haki wa utawala, siasa na uchumi na kuunga

mkono juhudi za kulinda amani na utulivu duniani kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu.

**MICHEZO**

**177. Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba imepita takriban miaka **39** tangu nchi yetu ishiriki kwa mara ya mwisho michuano ya mpira wa miguu kwa Nchi za Bara la Afrika maarufu AFCON. Hata hivyo, kusubiri huko kulikoma tarehe 24 Machi 2019 baada ya vijana wetu wa Taifa Stars kupata ushindi mnono wa mabao matatu bila majibu dhidi ya jirani zetu wa Uganda. Ushindi huo, unaipeleka Taifa Stars katika AFCON 2019 huko nchini Misri.

**178. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwapongeza wachezaji, viongozi, benchi la ufundi, kamati za uhamasishaji wa ushindi, mashabiki na watanzania wote kwa kutimiza ndoto yetu ya muda mrefu ya kushiriki michuano hiyo mikubwa kabisa Barani Afrika. Aidha, nitoe wito kwa viongozi, wachezaji na walimu kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye michezo iliyotangulia ili kujiweka sawa na michuano ya mwezi Juni 2019. Napenda mtambue kwamba lengo letu ni kwenda kushindana na si kushiriki. Niwatakie maandalizi mema na mafanikio katika michuano hiyo inayokuja.

**179. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine nchi yetu inaendelea vyema na maandalizi ya mashindano ya mpira wa miguu kwa vijana wenye umri chini ya miaka **17** barani Afrika (AFCON – U17) yatakayoanza Aprili 2019. Katika mazungumzo niliyofanya na viongozi wa Serikali na vyama mbalimbali vya michezo nchini vikiongozwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) wamenihakikishia kwamba maandalizi ni mazuri na timu yetu itafanya vizuri.

**180. Mheshimiwa Spika,** iwapo Serengeti Boys itaibuka na ushindi walau katika michezo yake miwili tu itakuwa imekata tiketi ya kushiriki mashindano ya dunia huko nchini Brazil kwa vijana wa umri huo. Hii inatokana na ukweli kwamba kila kundi litatoa timu mbili ambazo zitaliwakilisha Bara la Afrika kwenye mashindano hayo ya dunia.

**181.** **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kuipongeza timu yetu ya Vijana wenye ulemavu wa akili kwa kuibuka na ushindi wa medali **15** katika Michezo Maalumu ya Olimpiki iliyohusisha riadha na mpira wa wavu huko Abudhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu Machi 2019. Mafanikio hayo ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyowahi kupatikana katika nchi yetu kwenye tasnia ya michezo. Aidha, niipongeze pia timu yetu ya mpira wa miguu kwa wanawake (Twiga Stars) kwa kuibuka mabingwa wa CECAFA mwaka 2018 pamoja na kuwa washindi wa kwanza wa mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Bujumbura, Burundi Julai 2018. Vilevile, nawatakia maandalizi mema na ushindi Twiga Stars katika mchuano wao wa tarehe 5 Aprili 2019 dhidi ya Timu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ikiwa ni hatua ya awali ya kuwania kufuzu kwa ajili ya michuano ya Olimpiki mwaka 2020 huko Tokyo, Japan.

**182.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia nafasi hii kuwahamisisha Watanzania kujitokeza kwa wingi kesho katika uwanja wa Taifa kwa ajili ya kuishangilia timu yetu ili ishinde kwa mabao mengi na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga katika hatua inayofuata. Viingilio vya mchezo huo vimepunguzwa mno. Kwa mfano wanawake ni Shilingi 500 tu na wanaume ni Shilingi 1,000. Lengo ni kutoa fursa kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yetu.Kwa upande wa riadha, timu yetu hivi sasa inashiriki michezoo ya riadha Nchini Rwanda. Ni matarajio yetu kwamba timu hiyo ya riadha itarejea nyumbani na medali za kutosha. Tunawatakia ushiriki mwema na mafanikio katika mashindano hayo.

**183.** **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza mwanamasumbwi wa kitanzania Hassan Mwakinyo kwa kuendelea kuwa mfano bora kwenye tasnia hiyo ya masumbwi. Tarehe 23 Machi 2019 Mwakinyo aliendelea kung'ara katika anga za masumbwi na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania baada ya kumtwanga mpinzani wake Muargentina Sergio Gonzalez, huko Nairobi. Nitoe wito kwa vyama vya michezo kuendelea kuwalea vema wanamichezo hususan vijana ili waweze

kuipaisha vema bendera ya Tanzania kwenye medani mbalimbali za michezo ndani na nje. Huu ni wakati wakila Mtanzania kuthamini michezo na kutambua kuwa michezo ni ajira na michezo inalipa.

**184. Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu vilabu vyetu vya mpira wa mguu vimekuwa havifanyi vizuri katika medani ya michuano ya Klabu Barani Afrika. Hata hivyo, katika msimu wa 2018/2019 Klabu ya Simba ya Dar es Salaam imeweza kututoa kimasomaso baada ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Barani Afrika. Kufanya vizuri kwa Klabu ya Simba kunaongeza uwezekano wa Tanzania kupatiwa nafasi nyingine mbili na kufanya jumla ya vilabu vinne vitakavyoshiriki mashindano hayo makubwa ya vilabu Barani Afrika katika misimu ijayo. Vilevile, ushindi wa Taifa Stars na Simba una manufaa makubwa kwa nchi yetu yakiwemo kuitangaza vyema nchi na kufungua fursa za ajira kwa vijana wetu hususan wanaojihusisha na soka.

**185. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwapongeza wachezaji, viongozi, benchi la ufundi na mashabiki wote wa Klabu ya Simba kwa mafanikio hayo makubwa. Tupo pamoja nanyi. Vilevile, niwatakie kheri, maandalizi mema na ushindi timu zetu zote ikiwemo Serengeti Boys katika mashindano ya AFCON - U17, Taifa Stars katika mashindano ya AFCON huko Misri Juni 2019 na Klabu ya Simba katika hatua ya robo fainali ya ligi ya mabingwa Barani Afrika.

**HITIMISHO**

**186. Mheshimiwa Spika,** wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu hii, nitoe wito kwa Viongozi, Watendaji na watanzania wote kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Nirejee tena kuwakumbusha kwamba dhamira ya kufikia uchumi wa kati itafikiwa tu iwapo watanzania tutaweka mbele uzalendo na maslahi mapana ya taifa letu pamoja na kudumisha misingi ya umoja wa kitaifa.

**187. Mheshimiwa Spika,** lengo la uchumi wa viwanda ni kuharakisha ukuaji wa uchumi jumuishi wenye kupunguza umaskini, kuongeza uzalishaji, ajira na ustawi wa watu wetu. Lengo hilo litafikiwa kwa kufungamanisha sekta ya viwanda na sekta nyingine za uchumi ikiwemo biashara, kilimo na utalii.

**188. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wake Serikali itaendelea kuonesha uthubutu na dhamira ya dhati katika kuhakikisha inatekeleza yafuatayo:

**Mosi:** kuendelea kupambana na rushwa, ufisadi, uzembe na uvivu sambamba na kuimarisha nidhamu kwa viongozi na watendaji wa ngazi zote katika kuwahudumia wananchi;

**Pili:** kusisitiza kwa viongozi, watendaji na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, ubunifu na uzalendo katika kujiletea maendeleo;

**Tatu:** wafanyabiashara na wajasiriamali kuendesha biashara zao kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo pamoja na kujenga tabia ya kuona fahari kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa letu;

**Nne:** kuielekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kujenga mahusiano rafiki na walipa kodi kwa lengo la kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa walipa kodi kuwa Taasisi hiyo inatumia nguvu na vitisho kudai kodi na kwa sababu hiyo kuzorotesha ukusanyaji wa mapato;

**Tano:** kuendelea kujenga mazingira mazuri na wezeshi ya kufanya kazi, biashara, kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi; na

**Sita:** kuwahimiza wananchi kutumia ipasavyo haki yao ya kidemokrasia kwa kujiandikisha na kushiriki katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa Oktoba 2019. Aidha, Serikali itahakikisha Mamlaka zinazosimamia uchaguzi huo, zinashirikiana vyema na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha unaendeshwa kwa amani na usalama.

**189. Mheshimiwa Spika,** ni vema tukatambua kuwa tupo kwenye zama za ushindani wa kiuchumi. Kwa msingi huo, mafanikio yetu katika zama hizi yatategemea pia ubunifu, tija na uwepo wa ufanisi kwenye miundombinu wezeshi ya kiuchumi inayoendelea kujengwa na Serikali. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuhakikisha inasimamia ipasavyo rasilimali za taifa ili zielekezwe katika sekta ambazo zitatuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea pamoja na kuhimili ushindani wa kiuchumi uliopo.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2019/2020**

**190. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Nane, Milioni Mia Nane Themanini na Sita, Mia Tano Ishirini na Tatu Elfu na Mia Tano Themanini na Moja (148,886,523,581.00).** Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Themanini na Sita, Milioni Mia Mbili Tisini, Mia Tatu Hamsini na Tano Elfu (86,290,355,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Sitini na Mbili, Milioni Mia Tano Tisini na Sita, Mia Moja Sitini na Nane Elfu na Mia Tano Themanini na Moja (62,596,168,581.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**191. Mheshimiwa Spika,** naliomba pia, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Ishirini na Nne, Milioni Mia Moja Themanini na Mbili, Mia Tano Thelathini na Saba Elfu na Mia Sita (124,182,537,600.00)** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Mia Moja Kumi na Sita, Milioni Mia Tano Sabini na Tatu na Ishirini na Sita Elfu (116,573,026,000.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Sita na Tisa, Mia Tano Kumi na Moja Elfu na Mia Sita (7,609,511,600.00)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Sasa naomba niwatambue wageni wetu siku ya leo, tutaanza na wageni saba ambao wapo kwenye

Jukwaa la Spika ambao ni ujumbe wa Mufti wa Tanzania unaoongozwa na Katibu wa Ofisi ya Mufti Tawala za Mikoa na Misikiti Tanzania, Sheikh Abdulshakur Mnongane, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo mkuu wa mawasiliano ya umma na mwandishi maalum wa Mufti wa Tanzania Sheikh Harith Nkussa, ahsante sana. Pia yupo Mudir wa Madrasa ya Darul-Mustafa na Mratibu, Sheikh Omary Salum Khamis, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia wamefuatana na wafanyabiashara maarufu nchini akiwemo Ustaadh Osman Hotty, Ustaadh Hassan Omary na Ndugu Rahim Boss. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 61 ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni viongozi kutoka Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni pamoja na Katibu Mkuu (Waziri Mkuu na Bunge) Bi. Maimuna Tarish. Huyu mama ni mchapakazi wa miaka mingi, tunakupongeza sana lakini pia ni mama mlezi mzuri maana ameweza kutulelea mmoja wa Wabunge wenzetu humu ndani Mhe. Zainab Katimba. Mhe. Zainab Katimba yupo leo? Yupo wapi? Kwa hiyo, ahsante sana mama kwa malezi mazuri ya kutulelea Zainab, anafanya kazi nzuri Bungeni. *(Makofi/ Kicheko)*

Katibu Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji Ndugu Dorothy Mwaluko na Katibu Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu Ndugu Andrew Masawe, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia nawaletea Msajili wa Vyama vya Siasa Jaji Francis Mutungi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naona kama hamjaelewa vizuri kidogo. Naomba sasa kumtambulisha kwenu Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi. *(Makofi/Vigelegele)*

Wengine ni Mwenyekiti Mtendaji wa *TACAIDS,* Dkt. Leonard Maboko. Huyu naye ni mtu muhimu kwelikweli, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Athuman Kihamia. Mkurugenzi, wasiopiga makofi wote andika majina na majimbo yao halafu watakufahamu mwakani kwamba unafananaje. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wengine ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Ndugu Rodgers Siyanga; Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ndugu Beng'I Issa; Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa, Ndugu Oliva Vegula; Mwakilishi wa *LESCO,* Prof. Josephat Kanywanyi, oh, karibu sana Profesa, Prefesa wa siku nyingi huyu. *(Makofi)*

Pia yupo Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi za Jamii *(SSRA),* Ndugu Onorious Njole; Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi *(NSSF),* Ndugu William Erio; Mkurugenzi Mkuu wa *PSSSF,* Ndugu Hosea Kashimba; Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF),* Ndugu Masha Mushomba; Mkurugenzi Mkazi Shirika la Kazi la Kimataifa *(ILO)* kwa Nchi za Afrika Mashariki, Ndugu Wellington Chibebe; na Mtendaji Mkuu wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* Ndugu Khadija Mwenda. *(Makofi)*

Wengine ni Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA),* Ndugu Tumaini Nyamuhokya; Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, Dkt. Lucas Luhunde Kija; na Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* kinaongozwa na Ndugu Kabeho Solo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wetu hao wameambatana na wageni wengine 41 ambao ni Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi na Idara mbalimbali zilizopo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na wengine wako nyuma yetu hapa.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji

na Umwagiliaji ambaye ni ndugu yake kutoka Dar es Salaam anaitwa Bilal Saadat Mshihiri**,** karibu sana Bilal, yuko pale. *(Makofi)*

Pia yuko Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, naomba nikutambue uwepo wako, karibu sana. Mnafanya kazi nzuri, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwatum Dau ambao ni watoto wake, Ndugu Zuhura Dau na Ndugu Zubeda Fatihi. Wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambao ni wapiga kura wake, Ndugu Bihagara Nzoya na Ndugu Reuben Miburo, wale pale. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq ambao ni wafanyakazi wa Shirika la *Women Wake Up* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa George Lubeleje (Seneta) ambao ni wapiga kura wake kutoka Mpwapwa Jijini Dodoma, Ndugu Leonida Mkomoya na Ndugu Magdalena Sumbali. Karibuni sana, wale kule wageni wa *Mwaha.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Lubeleje tunamuita Seneta lakini kule Kongwa na Mpwapwa yeye ana jina lake ambalo ukilitaja hilo ndiyo wanamuelewa zaidi, anaitwa *Mwaha,* yaani ni mkubwa, mtu mkuu, kiongozi wa juu kabisa. Kwa hiyo, kule Kongwa na Mpwapwa wa juu kabisa ni Mheshimiwa Lubeleje. Kwa hiyo ukimwambia mwananchi yeyote *Mwaha* wanamjua ni Mheshimiwa Lubeleje. *(Makofi/ Kicheko)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa kutoka Jimboni kwake Longido wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo Ndugu Frank Mwaisumbe. Karibu sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na ndugu kutoka Longido. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa John Heche ambaye ni Katibu wa CHADEMA wa Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Zakaria Thomas. Karibu sana popote pale ulipo. *(Makofi)*

Pia tunaye Mzee ambaye ni Katibu wa Wazee wa Mkoa wa Dodoma, Mzee Makuberi. Yupo pale *Speaker's Lounge,* karibu sana. Wazee hawa ndiyo wenye Dodoma yao hawa. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 200 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* wakiongozwa na Ndugu Mgina Emmanuel. *UDOM please* pale mlipo simameni. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msishangae, tunao Waheshimiwa Wabunge watatu: Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali; Mheshimiwa Mary Deo Muro na Mheshimiwa Anatropia Theonest, hawa wameamua kutokukubaliana na yanayoendelea, kwa hiyo ndiyo maana mnaona tuko nao hapa. Hawa ni watu wazuri sana, wameamua kukataa kabisa yale mambo ya kutokatoka nje na kuzirazira, wao wamekataa hiyo biashara ndiyo maana wako hapa. *(Makofi/ Kicheko)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge tajwa walikuwa wakikataa kwa ishara ya mkono)*

**SPIKA:** Kama kweli hawakubaliani basi tutawaona na wenyewe wakienda nje ili tujue kweli hawakubaliani. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baadhi ya vyombo vya habari na hasa magazeti na baadhi ya redio vimekuwa vinaripoti lile Azimio la Bunge tulilolifanya juzi linalohusiana na masuala ya kukataa kufanya kazi na Profesa Mussa Assad wakichanganya kwa kueleza kwamba Bunge hili limekataa kufanya kazi na Ofisi ya *CAG.* Mambo haya ni vizuri waandishi wa habari wakayaelewa vizuri na kuyaweka vizuri kwa wananchi; hakuna wakati wowote ambapo Bunge hili

limekataa kufanya kazi na taasisi ambayo ni Ofisi ya *CAG.* Bunge hili limekataa kufanya kazi na mtu anayeitwa Prof. Mussa Assad, basi. Kwa hiyo, tusiripoti tofauti tukauchonganisha umma kwa kuuchanganya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo sasa tunaendelea kwa kumuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria aje awasilishe taarifa yake. Anakuja Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Giga, karibuni kwa hotuba yenu. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Moja. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6(2)(a) pamoja na kifungu cha 7(1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba katika kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuanzia tarehe 12 hadi 20 Machi, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilianza kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo nchini iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2018/19, pia Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti za Wizara na taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 21

hadi 27 Machi, 2019 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji ina mafungu sita ya bajeti kama ifuatavyo: Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu; Fungu 65 - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu; Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA);* Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(NEC);* na Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa mradi Na.6581 wa Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini ambao kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 15. Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi huo kwani kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019, Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea kiasi cha shilingi bilioni 12, sawa na asilimia 80 ya bajeti ya mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019. Uchambuzi uliofanywa na Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili, 2018 na kiwango ambacho kimepokelewa kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi huu ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/ 2019 na kiasi cha fedha kilichopokelewa katika mradi wa maendeleo hadi kufika mwezi Machi, 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa mpango

wa bajeti ya mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti ya mwezi Aprili, 2018. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Bunge lako Tukufu liliidhinisha makadirio ya makusanyo ya maduhuli yenye jumla ya shilingi 39,898,030,187 katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari 2019. Kiasi cha maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake ni shilingi19,297,627,950 sawa na asilimia 48 ya makusanyo yaliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, Kamati imebaini kuwa kwa Fungu 37 la Ofisi ya Waziri Mkuu tayari imevuka malengo ya ukusanyaji wa maduhuli kwa kufanya makusanyo ya shilingi 1,139,427,950 sawa na asilimia 114 ya makusanyo yaliyokusudiwa chini ya fungu hilo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko hilo limetokana na hatua ya Serikali kufanyia kazi mapendekezo na ushauri wa Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kuhusu kuboresha mitambo ya utendaji wa Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Aidha, ofisi hiyo, imeongeza ufanisi katika makusanyo kiasi cha kuvuka lengo lililokusudiwa kwa mwaka mzima ndani ya robo tatu ya mwaka. Kamati inaipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa mfano bora na wa kuigwa pamoja na Wizara na taasisi zote za Serikali katika kuongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ya Serikali, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kutoka Hazina. Katika mwaka wa fedha 2018/ 2019, mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake yalitengewa shilingi 66,166,389,698 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh.19,200,572,594 iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mishahara; shilingi 23,136,351,053 iliombwa kwa kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 23,829,466,051 iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019, taasisi hizo zilipokea shilingi 37,528,028,377 sawa na asilimia 58 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya matumizi ya kawaida hadi kufika 2019 umeainishwa katika Jedwali Na.1.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kwa kila fungu. Maoni ya Kamati ni kwamba hali ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya mwaka 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi 58,791,441,000 kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 31 ni fedha za ndani na shilingi 1,027,791,441 ni fedha za nje. Hadi Februari, 2019, fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 36,972,985,789 sawa na asilimia 63 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, yatokanayo na uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa fedha za Mfuko

wa Maendeleo ya Vijana kwa robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019 sio wa kuridhisha sana kwa kuwa Mfuko huo haujapokea kiasi chochote cha fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Maoni ya Kamati ni kuwa pamoja na vijana kuendelea kunufaika na mikopo mbalimbali kupitia Halmashauri nchini, bado kuna kila sababu kwa Serikali kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Vijana kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa Bajeti 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mpango huu wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 umeainisha maeneo 29 ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele vilivyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2019/2020. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinalenga kuboresha na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi, hatua ambayo itatengeneza ajira kwa wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla na hivyo kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 40,913,154,200/=. Makadirio ya Makusanyo yanaongezeka kwa shilingi 1,015,124,013/=, ambapo ongezeko hilo ni sawa na asilimia 2.5 ya bajeti ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kwa kuwa Ofisi hiyo imedhihirisha uwezo na ubunifu mkubwa katika ukusanyaji wa maduhuli kiasi cha kuvuka lengo ndani ya robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa kiasi cha maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 75,884,978,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,881,495,499/= ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 30,702,835,948/= ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa na shilingi 26,300,645,751/= ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeongezeka kwa kiasi cha shilingi 9,718,588,302/= sawa na asilimia 14.7 ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bajeti ya Matumizi ya Kawaida inatokana na sababu za msingi ikiwemo kuongezeka kwa masuala ya uwekezaji ili kukidhi mahitaji ya muundo mpya kutokana na mabadiliko yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kuongeza shughuli za Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, kuanzishwa kwa Kitengo kipya cha Uratibu wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu ni mojawapo ya sababu ya ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri na Mapendekezo ya Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kuanzisha Kitengo kipya

cha uratibu wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu na kukitengea Kasma yake ya kibajeti chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii ni pamoja na kuanza kazi kwa Baraza la Watu wenye Ulemavu kufuatia uteuzi wa Wajumbe wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo inadhihirisha usikivu, utayari na dhamira njema ya Serikali katika kutatua changamoto mbalimbali za makundi maalum ya kijamii kwa maendeleo endelevu ya makundi hayo.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa shilingi 56,639,533,637/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 19 ni fedha za ndani na shilingi 37,639,533,637/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imepungua kwa kiasi cha shilingi 2,151,907,363/=. Pungufu hiyo ni sawa na asilimia 3.7 ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo katika bajeti ya maendeleo pamoja na sababu nyingine muhimu, yanatokana na kukamilika kwa kiasi kikubwa ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu, hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo kwa mwaka huu wa fedha umelenga katika maeneo matano kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati. Naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi

kwa mwaka wa fedha 2019/2020 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

*Mheshimiwa Spika, Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu; Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhishwa na uwezo wa Ofisi hii katika kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa lengo la kupunguza utegemezi, hivyo, Serikali iendelee na jitihada hizo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, hatua ambayo itaongeza makusanyo ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii ni muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza jitihada zake za kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa fedha za nje katika miradi ya maendeleo. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaendelea kuongeza vyanzo vipya vya mapato, kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza kasi ya ujenzi na uendelezaji wa viwanda nchini, hatua ambayo itaongeza fursa za kiuchumi na kuongeza pato la ndani.

(iv) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inaimarisha usimamizi wa masuala ya uwekezaji nchini kwa lengo la kuongeza na kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda nchini kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa; Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iendelee kuchunguza na kufuatilia mienendo ya

Vyama vya Siasa, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi katika usimamizi na udhibiti wa mienendo ya Vyama vya Siasa ikiwemo kuchukua hatua stahiki kwa kila chama kinachovunja misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria nyingine za nchi, kwa lengo la kulinda umoja, udugu, amani, ulinzi na usalama wa nchi kupitia mienendo ya Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF);* pamoja na Kamati kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa chini ya Mfuko huu, Kamati inashauri mfuko uendelee kutoa elimu ya kutosha kwa waajiri na wafanyakazi hususan vyama vya wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa waajiri wote nchini wanazingatia matakwa ya sheria katika kuhakikisha wanajiandikisha kwenye mfuko, wanalipa ada/michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kushauri mfuko kuweka na kuimarisha mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

Mheshimiwa Spika, Fungu 65 - Kazi na Ajira; pamoja na Kamati kuridhishwa sana na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* Kamati inaendelea kushauri kuwa *OSHA* iendelee kubuni mikakati endelevu na kuitekeleza kuhusu kusimamia afya na usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa viwanda nchini katika kulinda usalama wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa na hatua ya Serikali ya kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Masuala ya Watu wenye Ulemavu nchini ikiwemo kuanzisha Rasmi Baraza la Taifa la kuratibu masuala ya kundi hilo kwa ujumla, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inasimamia kitengo hicho na Baraza husika ili vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake kwa weledi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanatatua migogoro mbalimbali

inayoendelea katika vyama vya watu wenye ulemavu nchini. Aidha, mikopo inayotolewa na Halmashari kwa ajili ya makundi hayo irejeshwe bila riba na Serikali isimamie na kudhibiti utoaji wa fedha hizo ili ziwafikie walengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wahakikishe wanaongeza udhibiti wa marejesho ya mikopo ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili mfuko huo uwafikie vijana wengi zaidi. Hatua hiyo iende sambamba na utoaji wa elimu kuhusu matumizi bora ya fedha za mfuko kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali katika kuwajengea ujuzi vijana na makundi mbalimbali ya kijamii kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo mafunzo ya matumizi ya shamba kitalu katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuyawezesha makundi husika kuhusu kilimo chenye tija. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwepo ushirikishwaji wa Wabunge wanaotoka kwenye Halmashauri husika kabla ya Serikali kuanzisha miradi husika kwa lengo la kupanua ushiriki wa vijana wengi waliokusudiwa kupitia wawakilishi wao ambao ni Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Fungu 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha daftari la wapiga kura na kuchukua jitihada za kutosha kwa uangalifu mkubwa katika uboreshaji wa daftari hilo. Hatua hizi zijumuishe utoaji elimu ya uraia hususan uandikishaji wa wapiga kura vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokuwa na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujitahidi kufanya kazi yake kwa weledi ili kuendelea kuaminika kwa wadau wake wa uchaguzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, inawashirikisha wadau

wa uchaguzi wakati wa uhuishaji wa daftari la wapiga kura ili kuepuka migogoro isiyo na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kushauri kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema ili tuwe na wasimamizi walio makini na wanaotambua na kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa wakati ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu masuala mbalimbali ya uchaguzi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu, Mwenyezi Mungu azidi kukuimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama; Waziri wa Nchi, Uwekezaji, Mheshimiwa Angellah Kairuki; Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Antony Mavunde; Mheshimiwa Stella Alex Ikupa; Makatibu Wakuu na wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano

waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini siyo kwa umuhimu wake, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama.

Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Angelina Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndugu Stanslaus Kagisa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, Watu Wenye Ulemavu na Uwekezaji, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za

Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kuanzia tarehe 12 hadi 19 Machi 2019. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 21 hadi 27 Machi, 2019 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-
i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha unaoisha;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambao kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 ulitengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Tano (15,000,000,000/=).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa Fedha za kutekeleza Mradi huo, kwani kwa kipindi cha Julai,

2018 hadi Machi, 2019 Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili (12,000,000,000/) sawa na asilimia 80%** ya Bajeti ya Mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 21 hadi 22 Machi, 2019. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

***Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2018 na kiwango ambacho kimepokelewa kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019.

Aidha, uchambuzi huu ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji

lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2018. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

***Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Tisa, Milioni Mia Nane Tisini na Nane na Thelathini Elfu, Mia Moja Themanini na Saba (39,898,030,187/=).** Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili Tisini na Saba, Laki Sita Ishirini na Saba Elfu, na Mia Tisa Hamsini (19,297,627,950/=)** sawa na **asilimia 48** ya Makusanyo yaliyoidhinishwa na Bunge.

Aidha, Kamati imebaini kuwa, kwa Fungu 37 (Ofisi ya Waziri Mkuu) tayari imevuka malengo ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa kufanya makusanyo ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Tisa, Laki Nne Ishirini na Saba Elfu, Mia Tisa Hamsini(1,139,427,950/) sawa na asilimia 114%** ya Makusanyo yaliyokusudiwa chini ya Fungu hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko hilo limetokana na hatua ya Serikali kufanyia kazi mapendekezo na Ushauri wa Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kuhusu kuboresha mitambo na utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Aidha, Ofisi hiyo imeongeza ufanisi katika makusanyo kiasi cha kuvuka lengo lililokusudiwa kwa Mwaka mzima ndani ya Robo Tatu ya Mwaka.

**Kamati, inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa mfano bora na wa kuigwa na Wizara pamoja na Taasisi zote za Serikali katika kuongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ya**

**Serikali, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.**

***Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina***

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Sita, Laki Tatu Themanini na Tisa Elfu, Mia Sita Tisini na Nane (66,166,389,698/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili, Laki Tano Sabini na Mbili Elfu, Mia Tano Tisini na Nne (19,200,572,594/=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Moja Thelathini na Sita, Laki Tatu Hamsini na Moja Elfu na Hamsini na Tatu (23,136,351,053/=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Laki Nne Sitini na Sita Elfu na Hamsini na Moja (23,829,466,051/=**) iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa.

***Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari 2019 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Tano Ishirini na Nane na Ishirini na Nane Elfu, Mia Tatu Sabini na Saba (37,528,028,377/=)** sawa na **asilimia 58%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge**.** Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 2019 umeainishwa katika **Jedwali Na. 1** .*

**JEDWALI NA. 1: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2019**

| NA. | FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 17, 427,714,000 | 7,834,885,500 | 45 |
| 2 | 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 7,016,012,000 | 4,835,194,549 | 69 |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 13,644,067,698 | 7,751,904,840 | 57 |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,409,941,000 | 12,736,816,350 | 66 |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 3,828,024,000 | 1,983,154,547 | 52 |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 4,840,631,000 | 1,959,814,168 | 41 |
| | **JUMLA** | **66, 166,389,698** | **37,528,028,377** | **58** |

**Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 21 Machi, 2019**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati ni kwamba hali ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ili kurahisisha usimamizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

***Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo

kiasi cha **Shilingi Bilioni Hamsini na Nane, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu (58,791, 441,000/ =)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Thelathini na Moja (31,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu (27,791,441,000/ =)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2019 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Tisa Sabini na Mbili, Laki Tisa Themanini na Tano Elfu, Mia Saba Themanini na Tisa (36,972,985,789/=) sawa na asilimia 63%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

***Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 siyo wa kuridhisha kwa kuwa, Mfuko huo haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Maoni ya Kamati ni kuwa, pamoja na Vijana kuendelea kunufaika na Mikopo mbalimbali kupitia Halmashauri nchini, bado kuna kila sababu kwa Serikali kutoa fedha za Mfuko wa Manedeleo ya Vijana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Bajeti 2018/2019.

**UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 tarehe 21 hadi 22 Machi 2019. Mpango huu na Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao

umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

***Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu***

**Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeainisha maeneo 29 ya vipaumbele yakiwemo;
i) Kuchapa Nyaraka mbalimbali za Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa,
ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;
iii) Kuratibu na kusimamia Maendeleo ya Uwekezaji Nchini,
iv) Kuratibu na kusimamia Shughuli za Baraza la Taifa la Biashara,
v) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;
vi) Kusuluhisha Migogoro sehemu za Kazi,
vii) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji wa Maendeleo ya Vijana,
viii) Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini,
ix) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za Ajira za Watanzania nchi za nje,
x) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, na
xi) Kuratibu Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2019/2020. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinalenga kuboresha na kuimarisha**

**mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itatengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla hivyo, kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya Nchi.**

***Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Tisa Kumi na Tatu, Laki Moja Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (40,913,154,200/=).** Makadirio ya Makusanyo yanaongezeka kwa **Shilingi Bilioni Moja na Milioni Kumi na Tano, Laki Moja Ishirini na Nne Elfu na Kumi na Tatu (1,015,124,013/=),** ongezeko hilo ni **sawa na asilimia 2.5%** ya Bajeti ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuongeza Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa kuwa Ofisi hiyo imedhihirisha uwezo na ubunifu mkubwa katika ukusanyaji wa Maduhuli kiasi cha kuvuka lengo ndani ya Robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2018/2019.**

**Mheshimiwa Spika,** Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37),** Tume ya Taifa ya Uchaguzi (**Fungu 61),** Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, **(Fungu 65)** na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (**Fungu 27).** Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa Maduhuli zaidi ni **Fungu 65** ambalo linahusisha Taasisi mbalimbali zilizo katika Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali **Na.2.**

**Jedwali Na.2. Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu**

| FUNGU | TAASISI HUSIKA | MADUHULI YALIYOIDHINISHWA 2018/2019 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2019/2020 |
|---|---|---|---|
| 27 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 175,000 | 10,300,000 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 1,000,000,000 | 2,000,000,000 |
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 15,000,000 | 20,000,000 |
| 65 | Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu | 38,882,855,187 | 38,882,854,200 |
| **JUMLA** | | **39,898,030,187** | **40,913,154,200** |

***Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Tano, Milioni Mia Nane Themanini na Nne, Laki Tisa Sabini na Nane Elfu (75,884,978,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Nane Themanini na Moja, Laki Nne Tisini na Tano Elfu, Mia Nne Tisini na Tisa (18,881,495,499/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Thelathini, Milioni Mia Saba na Mbili, Laki Nane Thelathini na Tano Elfu, Mia Tisa Arobaini na Nane (30,702,835,948/=)** ni Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita, Milioni**

**Mia Tatu, Laki Sita Arobaini na Tano Elfu, Mia Saba Hamsini na Moja (26,300,645,751/=**) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba Kumi na Nane, Laki Tano Themanini na Nane Elfu, Mia Tatu na Mbili (9,718,588,302/=) sawa na asilimia 14.7%** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inatokana na sababu za msingi ikiwemo kuongezeka kwa Masuala ya Uwekezaji ili kukidhi mahitaji ya Muundo Mpya kutokana na Mabadiliko yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kuongeza shughuli za Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, kuanzishwa kwa Kitengo kipya cha Uratibu wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu ni mojawapo ya sababu ya ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru na kuipongeza Serikali, kwa kutekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kuanzisha Kitengo kipya cha uratibu wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu na kukitengea Kasima yake ya Kibajeti chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii ni pamoja na kuanza kazi kwa Baraza la Watu wenye Ulemavu kufuatia uteuzi wa Wajumbe wa Baraza hilo.**

**Mheshimiwa Spika, hatua hiyo inadhihirisha usikivu, utayari na dhamira njema ya Serikali katika kutatua changamoto mbalimbali za makundi Maalum ya Kijamii kwa Maendeleo Endelevu ya Makundi hayo.**

***Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Hamsini na Sita, Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa, Laki Tano Thelathini na Tatu Elfu, Mia Sita Thelathini na Saba**

**(56,639,533,637/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa (19,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa, Laki Tano Thelathini na Tatu Elfu, Mia Sita Thelathini na Saba (37,639,533,637/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imepungua kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Hamsini na Moja, Laki Tisa na Saba Elfu, Mia Tatu Sitini na Saba (2,151,907,363/=)**. Pungufu hiyo ni sawa na **asilimia 3.7%** ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko hayo katika Bajeti ya maendeleo pamoja na sababu nyingine muhimu, yanatokana na kukamilika kwa kiasi kikubwa Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu, hapa Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo Matano (5)** yakiwemo:-

i) Kutoa Mafunzo ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana ili kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kushiriki katika ujenzi wa Viwanda na kufikia uchumi wa kipato cha kati,
ii) Kuwawezesha Vijana Kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana,
iii) Kuwajengea uwezo wakulima ili kuyafikia masoko yenye tija ikiwemo masoko ya mitaji na pembejeo,
iv) Kuongeza uwezo wa kujiandaa na kukabiliana na maafa nchini, na,
v) Kujenga Mifumo ya utoaji taarifa za hali ya hewa na tahadhari za dharura iliyoboreshwa hapa nchini.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na

Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

***FUNGU 37- Ofisi ya Waziri Mkuu***

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhishwa na uwezo wa Ofisi hii katika kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa lengo la kupunguza utegemezi, hivyo, Serikali iendelee na jitihada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, hatua ambayo itaongeza Makusanyo ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendeleza jitihada zake za kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa Fedha za Nje katika Miradi ya Maendeleo. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaendelea kuongeza vyanzo vipya vya Mapato, kuboresha mazingira ya Uwekezaji nchini kwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza kasi ya Ujenzi na Uendelezaji wa Viwanda nchini, hatua ambayo itaongeza fursa za kiuchumi na kuongeza pato la ndani.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inaimarisha Usimamizi wa Masuala ya Uwekezaji nchini kwa lengo la kuongeza na kuchochea ukuaji wa Uchumi wa

Viwanda nchini kuelekea Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

***Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa***

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iendelee kuchunguza na kufuatilia mienendo ya Vyama vya Siasa, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi katika usimamizi na udhibiti wa mienendo ya Vyama vya Siasa ikiwemo kuchukua hatua stahiki kwa kila Chama kinachovunja Misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria zingine za nchi, kwa lengo la kulinda Umoja, Udugu, Amani, Ulinzi na Usalama wa nchi kupitia mienendo ya Vyama vya Siasa.

***Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)***

i) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa chini ya Mfuko huu, Kamati inashauri Mfuko uendelee kutoa Elimu ya kutosha kwa Waajili na Wafanyakazi hususan Vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajili wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajiandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri Mfuko kuweka na kuimarisha Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

***FUNGU 65 - Kazi na Ajira***

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Kamati inaendelea kushauri kuwa, OSHA iendelee kubuni mikakati endelevu na kuitekeleza kuhusu kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi

kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda nchini katika kulinda usalama wa Wafanyakazi.

ii) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na hatua ya Serikali ya kuanzisha Kitengo cha kuratibu masuala ya Watu wenye Ulemavu nchini ikiwemo kuanzisha Rasmi Baraza la Taifa la kuratibu Masuala ya Kundi hilo kwa ujumla, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inasimamia kitengo hicho na Baraza husika ili vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake kwa weledi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanatatua migogoro mbalimbali inayoendelea katika Vyama vya Watu wenye Ulemavu nchini. Aidha, Mikopo inayotolewa na Halmashari kwa ajili ya Makundi hayo irejeshwe bila riba na Serikali isimamie na kudhibiti utoaji wa fedha hizo ili ziwafikie walengwa kwa wakati.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tamisemi, wahakikishe wanaongeza udhibiti wa marejesho ya Mikopo ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili Mfuko huo uwafikie Vijana wengi zaidi. Hatua hiyo iende sambamba na utoaji wa Elimu kuhusu matumizi bora ya fedha za Mfuko kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada za Serikali katika kuwajengea ujuzi Vijana na makundi mbalimbali ya kijamii kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo mafunzo ya matumizi ya Shamba Kitalu katika maeneo mbalimbali nchini, kwa ajili ya kuyawezesha makundi husika kuhusu kilimo chenye tija. Hata hivyo, Kamati inashauri, kuwepo ushirikishwaji wa Wabunge wanaotoka kwenye Halmashauri husika kabla ya Serikali kuanzisha Miradi husika kwa lengo la kupanua ushiriki wa Vijana wengi waliokusudiwa kupitia wawakilishi wao ambao ni Wabunge.

***FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi***

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Wapiga Kura na

kuchukua jitihada za kutosha kwa uangalifu mkubwa katika uboreshaji wa Daftari hilo. Hatua hizi zijumuishe utoaji Elimu ya Uraia hususan uandikishaji wa Wapiga Kura Vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokuwa na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujitahidi kufanya kazi yake kwa Weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa Uchaguzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, inawashirikisha Wadau wa Uchaguzi wakati wa uhuishaji wa Daftari la Wapiga kura ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija kwa Taifa.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kushauri kwamba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa Uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wakati ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu masuala mbalimbali ya Uchaguzi kwa ufanisi Mkubwa.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia

Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb), Waziri wa Nchi (Uwekezaji), Mhe. Angellah Kairuki, (Mb), Manaibu Waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), na Mhe.Stella Alex Ikupa, (Mb), Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana,Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**
3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb-Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang’ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;

18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb – Mjumbe,
21. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Dkt. Suzan Alphonce Kolimba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

4 Aprili, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga kwa kuunga mkono hoja. Tunakushukuru sana kwa kusoma vizuri sana Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na

Sheria na tunawapongeza kwa kazi kubwa ambayo mmekuwa mkiifanya. *(Makofi)*

Taarifa ya pili ambayo tungeipokea ni ya Kambi Rasmi ya Upinzani lakini walishaweka mezani tangu asubuhi. Kwa hiyo, itakuja kwenye utaratibu wa kitabu. Kwa kuwa hawapo na sina maandishi ya nini kinatakiwa kifuatiwe, kwa hiyo, taarifa hiyo itakuwa mezani na mtagaiwa kama kawaida.

Kwa hiyo, naiita taarifa ya tatu nayo itakuwa ni Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Masuala ya UKIMWI, tafadhali. Nnakupa nusu saa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane, tutakwenda kwa nusu saa zaidi ili ratiba yetu iweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha leo hapa na kutuwezesha kufanya shughuli tunayoifanya. Pia napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Ofisi nzima ya Bunge ukisaidiwa na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein akisaidiwa na Ndugu Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndugu Virgil Mtui, Ndugu Asia Msangi, Ndugu Happiness Ndalu wote kwa kutusaidia kufanya shughuli hii ya mapitio lakini pia mjadala na uwasilishaji wa kazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuanza kwa shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Antony Mavunde na Mheshimiwa Ikupa Alex na pia bila kuwasahau Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile wa Wizara ya Afya kwa sababu wote kwa pamoja wamefanya jitihada kubwa ya kufanya kazi wanazotakiwa

kufanya, lakini na kutoa ushirikiano kwa Kamati kwa ajili ya kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* – Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe tarehe 23 Machi, 2019 Kamati ilipokea na kuijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa mafungu hayo mawili.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa za mafungu hayo, naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua masuala makubwa matano muhimu:-

(i) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

(ii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

(iii) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

(v) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa mafungu hayo mawili; Fungu 91 na Fungu 92.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS).* Kwa Fungu 92 Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Tume hii kwa mwaka wa 2018/2019 na mapendekezo hayo yalikuwa sita.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukulia kwenye baadhi ya mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Kupata Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa UKIMWI *(AIDS Trust Fund - ATF).*

(ii) Kutoa Waraka kwa Halmashauri nchini unaotoa maelekezo ya kujumuisha masuala ya mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kama moja ya majukumu ya Kamati za UKIMWI za ngazi ya Halmashauri na Kata.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ina wasiwasi na kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya maoni na mapendekezo na kwamba endapo hayatatekelezwa mapema, yataathiri jitihada za mapambano ya mwitikio wa UKIMWI.

(i) Kuwa na vyanzo vya uhakika na endelevu vya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa UKIMWI *(AIDS Trust Fund).*

(ii) Mapitio ya Sheria ya UKIMWI hususan katika vipengele vya umri wa mtu kupima maambukizi ya UKIMWI kwa hiari pamoja na mtu kujipima mwenyewe na uwezeshwaji kiuchumi wa watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo haya kwa sababu ni mapendekezo ambayo endapo yatatekelezwa yataongeza kwa kiasi kikubwa kasi ya mwitikio wa UKIMWI hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa namba Fungu 91, Kamati ilikuwa na Jumla ya mapendekezo matano kama yalivyoorodheshwa. Mapendekezo yaliyotekelezwa mpaka sasa ni kutenga fedha ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya Mamlaka, ambapo Serikali imeandaa mradi na mpango wake umewasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya taratibu za kuweza kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2020/2021. Pia kama nilivyosema awali kwa sababu hili lina pande zote mbili pia Waraka wa Serikali za Mitaa kujumlisha masuala ya madawa ya kulevya kama sehemu ya shughuli za Kamati za UKIMWI za Halmashauri na Kata.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati haijaridhika na suala la utekelezaji wa pendekezo la kuipatia Tume ya Madawa ya Kulevya pesa za maendeleo ifikapo mwaka 2020/2021 badala ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuufanya kazi ya kutambua kwamba hilo ni muhimu, lakini bado nina wasiwasi kwamba uahirishwaji wa fedha hizo za maendeleo kwenda mwaka wa mbele zaidi na sio mwaka huu ambao tunauombea fedha ni jambo ambalo bado linaweza likapunguza kasi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Tume ya Kudhibiti UKIMWI (Fungu 92) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91) hakukuwa na Makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Upatikanaji wa Fedha, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Fungu 92. Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ambapo ilitengewa Tume kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama ambavyo ziliidhinishwa na Bunge. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya

shilingi bilioni 12.9. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10.3 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 3.0 na fedha za nje ni shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Fungu 92; hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilikuwa ni shilingi bilioni 10.4**,** sawa na asilimia 81 ya fedha yote zilizopangwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni1.4 ni sawa na asilimia 56.7 zikijumuisha shilingi milioni 500.18 kwa matumizi mengineyo na shilingi milioni 900.6 kwa matumizi ya mishahara. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni Shilingi bilioni 8.9 sawa na asilimia 87 ya fedha za maendeleo zilizopangwa. Hata hivyo, fedha za maendeleo zinaonekana kuwa kubwa mpaka kiwango cha asilimia 87 kutokana na Tume kupata fedha za wadau wa maendeleo ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba fedha iliyopokelewa, kwa kiasi kikubwa ni fedha za Miradi ya maendeleo, ambazo zilitolewa kwa kiwango cha asilimia 87**.**

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Upatikanaji wa Fedha, Mamlaka ya ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91. Mamlaka hii iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 5.7 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 800.06 sawa na asilimia 14 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 4.9 sawa na asilimia 86 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na kwamba Mamlaka haikutengewa fedha yoyote kwa ajili ya maendeleo kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Mamlaka ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 3.9, sawa na asilimia 68.7 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Mwaka wa

Fedha wa 2018/2019. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 5.4 sawa na asilimia 13.9 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 3.4 sawa na asilimia 86 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kama ilivyofafanuliwa kwenye jedwali Na.2.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2018/2019, Fungu 92 na 91. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 10.3 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.3 ni za fedha za wahisani wa nje na shilingi bilioni 3.0 ni fedha za ndani**.** Hata hivyo, hadi kufikia wakati Kamati inapokea taarifa, februari 2019, jumla ya fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo ni kiasi cha shilingi bilioni 7.6 kiasi ambacho ni asilimia 4.6 zaidi ya kilichotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa Bajeti ya Fungu 91 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kulikuwa na matumizi makubwa ya fedha ikilinganishwa na kile kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kiwango hicho kikubwa cha matumizi ni kutokana na fedha zilizotolewa na wadau wa maendeleo ambao ni *DOD* na *GGM* kiasi cha shilingi bilioni 1.8 ambazo hazikuwa katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imepokea kiasi cha shilingi milioni 750 sawa na asilimia 25 tu ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Hali hii imepelekea Tume kuendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa utegemezi wa fedha kutoka kwa wafadhili kwa asilimia 91. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, matumizi ya maendeleo yaliyokwishafanywa na Tume mpaka Februari ni kiasi cha shilingi bilioni 8.3 tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haikutengewa kabisa kiasi chochote cha fedha za Miradi ya Maendeleo. Kamati inasisitiza kwamba, ajenda ya kupambana na dawa

za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyotafsiriwa. Ni maoni ya Kamati kuwa miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika na fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha warahibu kiuchumi kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, stadi za maisha na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, upo ushahidi kwamba watu hawa warahibu wa dawa za kulevya wasipopata mazingira yanayowawezesha na kuwaweka pamoja iko hatari ya kurudi kwenye matumizi ya madawa ya kulevya kwa kipindi kisichozidi miezi sita toka apate tiba. Kwa hiyo, Kamati inaona ni muhimu sana mamlaka kutengewa fedha za maendelo ili kuweza kufanikisha ajenda ya kuwa na jamii isiyokuwa ya matumizi ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba utoaji na utumiaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bila kuambatana na mifumo na mipango ya kimkakati ya muda mrefu ni jambo lenye uwezekano mdogo wa kuleta tija inayokusudiwa. Kwa sababu hiyo ni maoni ya Kamati kwamba fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa Tume kuanza kujenga mifumo itakayo jumuisha jamii nzima katika mapambano hayo na hivyo kuwa na tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo wa kutekeleza Afua za UKIMWI. Ilikuwa ni moja ya shughuli ambazo zilifanyika kabla ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti iliyokwisha na maombi ya Bajeti inayokuja. Kamati ilifanya ziara kwenye mikoa kadhaa na kupitia taasisi kadhaa zikiwemo halmashauri za wilaya na magereza. Malengo ya ziara katika maeneo hayo yalikuwa ni mambo kadhaa yanayohusu mapambano dhidi ya UKIMWI kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mambo yaliyobainishwa na Kamati wakati wa ziara ni kama ifuatavyo:-

i. Katika ngazi mbalimbali, hususan baadhi ya Halmashauri na vituo vya afya, hakuna ufahamu wa kutosha juu ya utekelezaji wa shughuli za mwitikio wa UKIMWI katika muktadha wa 90-90-90. Jambo hili linapunguza uwezo wa Serikali na wadau kufanya tathmini ya matokeo ya hatua zinazochukuliwa.

ii. Kuendelea kuwepo changamoto ya unyanyapaa miongoni mwa watumishi, mahali pa kazi, jambo ambalo lisipofanyiwa jitihada inayostahili bado litaendelea kupunguza nguvu katika mwitikio wa masuala ya UKIMWI katika muktadha wa 90-90-90.

iii. Kuwepo takwimu za kutilia shaka kuhusu hali ya maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu katika magereza nchini. Kamati ilielezwa juu ya magereza nchini kuwa na idadi ndogo sana ya wagonjwa wa Kifua Kikuu ikilinganishwa na wastani unaotarajiwa kulingana na takwimu za Kitaifa pamoja na takwimu za Kimataifa kwenye maeneo mahususi kama magereza.

Mheshimiwa Spika, endapo takwimu hizi zipo sahihi, Kamati haitasita kulipongeza Jeshi la Magereza na Serikali kwa ujumla. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Jeshi la Magereza lishirikiane na Kitengo cha Taifa cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma *(NTLP)* ili kufanya ukaguzi na tathmini ya pamoja katika Magereza yote nchini ili kujihakikishia juu ya usahihi wa hali halisi ya Kifua Kikuu katika Magereza nchini.

iv. Udhaifu katika uchambuzi na matumizi ya takwimu. Kamati imebaini kwamba kuna udhaifu mkubwa kwenye uwezo wa watendaji wa Halmashauri za Wilaya katika kuchambua na kutumia takwimu za UKIMWI katika ngazi zao. Hali hii imejitokeza kwenye Halmashauri zote zilizotembelewa kwenye idara ya afya (inayosimamia mwitikio wa UKIMWI kwa upande wa sekta ya afya) pamoja na ofisi ya mratibu wa UKIMWI ngazi ya Hlmashauri *(Multisectoral HIV Response).*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye Halmashauri mojawapo mratibu wa takwimu wa idara ya afya aliitaarifu

Kamati kwamba yeye binafsi hakushirikishwa kwenye maandalizi ya takwimu zilizowasilishwa mbele ya Kamati, licha ya kwamba yeye ndio mtunzaji wa takwimu hizi. Pia aliitaarifu Kamati kwamba huwa hafanyi uchambuzi wa takwimu kwa ajili ya watumiaji kwenye Halmashauri yake.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri nyingine, takwimu za ngazi ya Halmashauri ziliwasilishwa kwamba, asilimia 50 ya watu wanaotumia *ARV* hawafiki vituoni kuwa ajili ya huduma kama inavyotakiwa *(loss to follow up)* na hivyo hivyo asilimia 79 ya hali hiyo kenye ngazi ya kituo.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaashiria aidha kuna udhaifu mkubwa kwenye uchambuzi na tafsiri ya takwimu au hali halisi ya matumizi ya *ARV* kwa WAVIU ni mbaya sana.

v. Uelewa mdogo kuhusu Malengo ya Kimataifa ya Kupambana na UKIMWI ya 90-90-90 kama ambavyo nimekwishapambanua kwenye paragrafu iliyotangulia.

vi. Afua za UKIMWI na madawa ya kulevya mashuleni. Kamati ilibaini kwamba pamoja na kwamba takwimu zetu za Tanzania *HIV Impact Survey (THIS 2017)* asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15-24 na asilimia 80 ya maambukizi hayo ni miongoni mwa wasichana. Kamati ilibaini kwamba kitengo cha halmashauri cha huduma za afya shuleni *(school health program)* hakifanyi kazi ipasavyo kwenye kufika kwenye mashule hayo na kutoa elimu na maelekezo na hili limeonekana kwenye baadhi ya shule zote tulizotembelea.

vii. Kukosekana hatua mahsusi na za makusudi za kudhibiti maabukizi ya UKIMWI zinazoendana na kasi ya kukua majiji. Maambukizi ya UKIMWI yana sura ya pekee kwenye ngazi ya miji mikubwa na majiji, lakini Kamati kwenye ziara yake ilibaini kwamba kuna upungufu wa mikakati mahususi ya maambukizi ya UKIMWI na jitihada za kuzuia na kushughulika na wale watu ambao tayari wameambukizwa kwenye maeneo ambayo yana sura ya miji kama ilivyofafanuliwa kwenye taarifa yetu.

viii. Mheshimiwa Spika, warahibu wa madawa ya kulevya kukosa namna ya kumudu maisha hata baada ya kukamilisha matibabu ili pia ni jambo mojawapo ambalo kamati ililibaini na kulifanyia uchambuzi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ni Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2019/2020. Vipaumbele vya Tume ya UKIMWI vimeainishwa kwenye taarifa yetu na vipaumbele vya Tume ya Madawa ya Kulevya vimeainishwa kwenye ripoti yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia Fungu 92 linaomba jumla ya Sh.8,769,193,747.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh.5,956,634,747.00 sawa na asilimia 68 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Sh.2,812,599,000.00 sawa na asilimia 32 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, ikijumuisha matumizi ya kawaida *(OC).* Makadirio haya ya matumizi ya mwaka 2019/2020 ni pungufu kwa takriban shilingi bilioni 4.1sawa na asilimia 32.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imekadiria kufanya matumizi ya kiasi cha Sh.7,592,818,000.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 4.9 sawa na asilimia 35 ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 2.6 sawa na asilimia 65 kwa ajili ya mishahara. Kamati inasisitiza kuwa ni umuhimu wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano, ni maoni na ushauri wa Kamati. Moja ni upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI**.** Kamati inasisitiza sana jambo hili katika muktadha wa kuwezesha Mfuko wetu wa UKIMWI. Kamati inashauri Serikali kutenga tozo maalum kwa ajili kuuwezesha Mfuko huu ili mapambano ya UKIMWI yaendelee kwa nguvu zetu wenyewe kwa kiwango kinachostahili ili

tuweze kufanya kazi zetu kwa kujitegemea ingawa bado tunahitaji wahisani kushirikiana nasi, lakini uhuru zaidi unahitajika kwa ajili ya kuweza kusimama kwa miguu yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha ukusanyaji, hifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali za UKIMWI ni jambo ambalo Kamati inashauri Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*, Wizara ya Afya na TAMISEMI kuimarisha usimamizi ikiwa wa ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya takwimu kwa ngazi za Halmashauri na Vituo vya Afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza mipango na Mkakati wa Kimataifa wa Kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90 90 90 kwa sababu bila takwimu upimaji wa mafanikio utakuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Marekebisho ya sheria ya UKIMWI ili kuimarisha Mapambano ya UKIMWI nchini ili yaendane na utekelezaji wa Malengo ya UKIMWI ya 90 90 90. Katika hili tunasisitiza mapitio ya sheria hasa kwa ajili ya upimaji kwa hiari chini ya watu wenye miaka chini ya 18 kwa maana ya watu kupima wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Athari za kutotenga Bajeti ya Miradi ya Maendeleo zinaonekana katika mambo mengi na mojawapo ni ukosefu wa maabara inayomilikiwa na mamlaka yenyewe, jambo ambalo linaifanya mamlaka inategemea kwa kiwango kikubwa matumizi ya Maabara ya Mkemia Mkuu, maabara ambayo tayari ina kazi nyingi sana na hivyo inashindwa kutoa kipaumbele kwa kazi za shughuli ya mamlaka ya kupambana na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, suala la madawa ya kulevya kuwa ni ajenda ya Kamati za UKIMWI katika Halmashauri na Manispaa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa maelekezo kwa Serikali za Mitaa kwa kupitia *GN* Namba 142. Kamati inasisitiza iwepo miongozo kwenye ngazi za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ni hitimisho, nakushukuru wewe binafsi na ofisi yako nzima kama nilivyosema. Naishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista na Manaibu wake, Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Pia napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Nisiache kuwashukuru Wajumbe wa Kamati wote kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha makadirio na matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92 jumla ya shilingi 8,769,192,747 na Fungu 91 Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya jumla ya shilingi 7,592,818,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba ripoti yetu kama tulivyowasilisha mezani iingie yote kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI pamoja na Madawa ya Kulevya na tunakoelekea huko *TB* pia. Tunashukuru sana kwa ripoti yenu nzuri ambayo inatusaidia katika kujiandaa na uchangiaji utakaofuata baadaye leo jioni.

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA NA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba

kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – **Fungu 91** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* **– Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 10 (d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Hivyo, msingi wa maoni yatakayotolewa katika Taarifa hii ni kutoka katika Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe Tarehe 23 Machi, 2019, Kamati ilipokea na kuijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2019/2010, **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Uchambuzi wa kina wa Taarifa za (F**ungu 92 & 91**), naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua masuala makubwa matano (5) yafuatayo: -

1.1 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

1.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

1.3 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

1.4 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020; na

1.5 Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Fungu 92 na Fungu 91

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

### 2.1 Utekelezaji WA Ushauri wa Kamati – TACAIDS

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, kwa Fungu 92, Kamati ilifanya mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Tume hii kwa mwaka wa 2018/2019. Jumla ya Mapendekezo sita (6) yaliyotolewa na Kamati na Mapendekezo yote Serikali imeyachukua na inaendelea kuyafanyia kazi.
Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zilizochukuliwa kwenye baaadhi ya mapendekezo ya kamati ambazo ni pamoja na kumpata Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa UKIMWI (ATF) na kutoa Waraka kwa Halmashauri nchini unaotoa maelekezo ya kujumuisha masuala ya mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kama moja ya majukumu ya Kamati za UKIMWI za ngazi ya Halmashauri na Kata. Hata hivyo Kamati ina wasiwasi na kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya maoni na mapendekezo, na kwamba endapo hayatatekelezwa mapema, yataathiri jitihada za jumla za mwitikio wa UKIMWI.

Baadhi ya maoni na mapendekezo ambayo utekelezaji wake umekuwa na kasi ndogo ni pamoja na pendekezo la kuwa na vyanzo vya uhakika na endelevu vya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa UKIMWI (AIDS Trust Fund), mapitio ya Sheria ya UKIMWI hususan katika vipengele vya umri wa mtu kupima maambukizi ya VVU kwa hiari pamoja na mtu kujipima mwenyewe na uwezeshwaji kiuchumi wa watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo ambayo hayajakamilishwa ili yaweze kutoa matokeo chanya kwa ajili ya kuendeleza juhudi za Udhibiti wa UKIMWI hapa nchini.

### 2.2 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati-Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Fungu 91 na kutoa Jumla ya Mapendekezo matano (5). Mapendekezo hayo yalihusu kutenga bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya Mamlaka, kutoa elimu ya athari za dawa za kulevya kwa jamii,kujenga mfumo wa kitaasisi katika kupambana na dawa za kulevya na hasa katika ngazi za chini hususani katika Halimashauri za uanzishwaji wa vikundi vya watu walioathirika na dawa za kulevya ili kuvitumia kama mfumo wa kuwafikia warahibu wa madawa ya kulevya kwaa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma na uratibu.

Kwa kiasi kikubwa mapendekezo haya yametekelezwa na mengine yapo katika hatua tofauti za utekelezaji. Kuhusu hoja ya kutenga fedha za miradi ya maendeleo Kwa ajili ya Mamlaka, Serikali imeandaa mradi na mpango wake umewasilishwa Wizara ya fedha kwa ajili ya hatua za taratibu za kuweza kutenga fedha katika Mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo Kamati haijaridhika na suala la kuahirisha utekelzaji wa pendekezo hili mpaka Mwaka 2020/2021 badala ya 2019/ 2020. Aidha Serikali kupitia Mamlaka Na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi na Watu wenye Ulemavu, Vijana na Ajira ipo katika mpango wa kutumia fursa ya *skills development levy* ili kuviwezesha vikundi vya warahibu wa dawa za kulevya walio katika tiba na hivyo kuwawezesha kufanya shughuli za kuwaongezea kipato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuufanyia kazi ushauri wa kuweka mfumo wa kuwasaiaida warahibu wa dawa za kulevya kupitia vikundi. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa umuhimu wa kuwa na miradi itakayowezesha waathirika wa dawa za kulevya kuongeza

kipato ndio njia rahisi ya kuwaepusha kurudi katika matumizi ya dawa hizo na hivyo kamati inashauri kuwa ni muhimu kakamilisha kwa wakati muafaka maandalizi ya mpango huu na kuwezesha utekelezaji.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa BajetI kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 (Fungu 92 & 91)

#### 3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 Tume ya Kudhibiti UKIMWI (Fungu 92) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91) hakukuwa na Makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

#### 3.1.2 Upatikanaji wa Fedha Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ( TACAIDS)- Fungu 92

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti (Fungu 92) ambayo ilitengewa Tume kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama ambavyo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuona matumizi yake. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilling **12,909,431,000.** Kati ya fedha hizo shilling **2,609,431,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **10,300,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo fedha za ndani ni shilingi **3,000,000,000** na fedha za nje ni shilingi **7,3000,00,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Fungu 92, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni kiasi cha shilingi **10,477,721,649.96,** sawa na asilimia **81** ya fedha yote zilizopangwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, fedha za matumizi ya kawaida ni **1,478,782,662.52** ni sawa na asilimia **56.7** (zikijumuisha sh.

**518,013,662.52** kwa matumizi mengineyo- OC aidi. **960,769,000.00** kwa matumizi ya mishahara). Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Sh. 8,998,938,987.44,** sawa na **asilimia 87** ya fedha za maendeleo zilizopangwa. Hata hivyo fedha za maendeleo zinaonekana kuwa kubwa mpaka kiwango cha asilimia **87** kutokana na Tume kupata fedha za DoD na GGM ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyopangwa.

Uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba fedha iliyopokelewa, kwa kiasi kikubwa ni fedha za Miradi ya maendeleo, ambazo zilitolewa kwa kiwango cha asilimia **87,** ikilinganishwa na fedha za matumizi mengine ambazo zilitolewa kwa kiwango cha asilimia **56.7**. Aidha kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo zilizopokelewa ni fedha za nje, kiasi cha **Sh 7,632,974,640.61** sawa na **asilimia 105,** ikilinganishwa na fedha za ndani ambazo ni Sh **750,000,000.00** sawa na **asilimia 25** ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kwamba utekelezaji wa shughuli za Tume kwa kiasi kikubwa unategemea sana fedha kutoka kwa wafadhili. Kutokana na hali hiyo ni aidia kuwa endapo ufadhili huu utakoma basi Tume itashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaiomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha hasa za ndani kwa Tume ili iweze kukamilisha utekelezaji wa shughuli zake kama zilivyopangwa kabla aidia wa fedha wa 2018/2019 haujamalizika. **Rejea Jedwali Na. 1**

Jedwali Na. 1: **Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana hadi Mwezi Februari,2019 (FUNGU 92), hadi kufikia Mwezi Februari,2019.**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA | | UPATIKANAJI WA FEDHA | |
|---|---|---|---|
| **MGAWANYO** | **KIASI KILICHOIDHINISHWA** | **Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2019** | **Asilimia %** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)** | | | |
| Mishahara | 1,696,685,000.00 | 960,769,000.00 | 56.6 |
| Kawaida (OC) | 912,746,000,00 | 518,013,662.52 | 56.8 |
| Mfuko wa UKIMWI (ATF) | 0.00 | **0.00** | 0 |
| **JUMLA NDOGO (PE &OC)** | **2,609,431,000.00** | **1,478,782,662.52** | 56.7 |
| **MAENDELEO (MFUKO WA UKIMWI) –ATF** | | | |
| **ATF** | **3,000,000,000.00** | **750,000,000.00** | 25 |
| **MAENDELEO (FEDHA ZA NJE)** | | | |
| DoD | 1,437,044,887.83 (Nje ya bajeti) | 871,592,411.00 | 60.7 |
| GGM Kill Challenge | 150,000,000.00 (Nje ya bajeti ) | 99,488,130.00 | 66.3 |
| UNDAP | 948,062,277.00 | 711,394,980.00 | 75 |
| GLOBAL FUND | 6,551,937,723.00 | 5,950,499,119.61 | 90.8 |
| **JUMLA NDOGO (MAENDELEO)** | **12,087,044,889.83** | **8,382,974,640.61** | 69.4 |
| | | | |

**Chanzo.** ***Taarifa ya Tume (TACAIDS) ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2019/2020***

### 3.1.3 Upatikanaji wa Fedha Mamlaka ya ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ( DCEA)- Fungu 91

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91), iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **5,755,101,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **shilingi 806,549,000.00** sawa na **asilimia 14** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE) na shilingi **4,948,552,000** sawa na **asilimia 86** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Na kwamba Mamlaka haikutengewe fedha yeyote kwa ajili ya maendeleo kwa mwaka 2018/2019.

Uchambuzi WA Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Mamlaka ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **3,954,053,055.00** sawa na **asilimia 68.7** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Kati ya fedha hizo shilingi **549,163,055.00** sawa na **asilimia 13.9** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi **3,404,890,000 sawa** na **asilimia 86 ni** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Rejea Jedwali Na. 2**

Jedwali Na. 2: **Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana 2018/2019 (FUNGU 91) hadi kufikia Mwezi Februari, 2019.**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA | | UPATIKANAJI WA FEDHA | |
|---|---|---|---|
| MGAWANYO | KIASI KILICHOIDHINISHWA | Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2018 | Asilimia |
| MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI) | | | |
| Mishahara | 806,549,000.00 | 549,163,055.00 | 68.1 |
| Kawaida (OC) | 4,948,552,000 | 3,404,890,000 | 68.8 |
| Miradi ya Maendeleo | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **5,755,101,000.00** | **3,954,053,055.00** | 68.7 |

***Chanzo: Taarifa ya Mamlaka Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018***

### 3.1.4 Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2018/2019, Fungu 92 &91

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilitengewa jumla ya shilingi **10,300,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi 7,3000,00,000.00** ni za fedha za wahisani aidi na **shilingi 3,000,000,000** ni fedha za ndani**.** Hata hivyo, hadi

kufikia wakati Kamati inapokea taarifa, februari 2019, jumla ya fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo ni kiasi cha shilingi **7,632,974,640.61,** kiasi ambacho ni aidi kwa **asilimia 4.6** ya kilichotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa Bajeti ya **Fungu 91** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kulikuwa na matumizi makubwa ya fedha ikilinganishwa na kile kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kiwango hicho kikubwa cha matumizi ni kutokana na fedha zilizotolewa na DOD na GGM kiasi cha shilingi **1,866,480,541** ambazo hazikua katika Bajeti ya **Fungu 91.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imepokea kiasi cha **shilingi 750,000,000** sawa na **asilimia 25** tu ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Hali hii imepelekea Tume kuendelea kutekeleza Miradi yake ya Maendeleo kwa utegemezi wa fedha kutoka kwa wafadhili kwa **asilimia 91.** Hii ni kutokana na ukweli Kwamba, jumla ya matumizi ya maendeleo yaliyokwishafanywa na Tume mpaka Februari ni kiasi cha shilingi, **8,382,974,640.61.** Hivyo kiasi cha fedha za ndani ni **asilimia 9** pekee. Ni maoni ya Kamati kuwa, mwenendo huu wa utegemezi wa fedha za Miradi ya Maendeleo siyo jambo sahihi endapo ni nia ya dhati ya Serikali kwamba taifa liweze kudhibiti UKIMWI kwa mujibu wa mipango iliyopo. Kamati inasikitishwa sana na hali hii ya kutotengwa kwa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Tume kwani hii ndiyo Tume pekee inayoshughulika na masuala ya UKIMWI hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haikutengewa kabisa fedha za Miradi ya Maendeleo. Kamati inasisitiza kwamba, ajenda ya kupambana na Dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyotafsiriwa. Ni maoni ya Kamati kuwa miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika na fedha za maenedeleo ni pamoja na kuwawezesha warahibu kiuchumi

kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriammali, mikopo nafuu ya biashara, studi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya aidia kuikinga jamii ili isishiriki katika njia yoyote ya matumizi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa mfumo maalumu kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa madawa ya kulevya na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia ni kikwazo kikubwa katika muitikio wa kitaifa wa kupambana na tatizo hili. Upo ushahidi kuwa watu hawa hurudia baada ya muda mfupi hali yao ya awali ya kutumia dawa za kulevya endapo wataendelea kuwa na ukaribu na watu wanaotumia madawa ya kulevya na endapo watakaa kwa angalau miezi sita bila ya kupata fursa ya kushiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali. Hivyo ni muhimu sana Mamlaka kutengewa fedha za maendeleo ili kuweza kufanikisha ajenda ya kuwa na jamii isiyotumia dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati ni kwamba utoaji na utumiaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bila kuambatana na mifumo na mipango ya kimkakati ya muda mrefu ni jambo lenye uwezekano mdogo wa kuleta tija inayokusudiwa. Kwa sababu hiyo ni maoni ya Kamati kwamba fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa tume kuanza kujenga mifumo itakayo jumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya na hivyo kuiwezesha tume kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

### 3.1.5 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Afua za UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni 10 (b), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili,2016 10(b), inayoitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya,

Kamati ilifanya ziara kati ya tarehe 4 – 9 Machi 2019, kutembelea na kukagua utekelezaji Afua na shughuli zinazotekelzwa na Wizara, Taasisi na Mmlaka za Serikali katika mwitikio dhidi ya mapambano ya UKIMWI na biashara na matumizi ya Madawa ya Kulevya katika Mikoa ya Morogoro, Dar es salaam na Pwani.

### 3.1.5.1 Maeneo na Afua zilizokaguliwa na Kamati

Kwa ujumla, ziara na ufuatiliaji ulilfanywa katika maeneo yafuatayo: -

a) Gereza la Kingolwira Mkoa wa Morogoro;
b) Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Kituo cha Huduma na Tiba- CTC Hospitali ya Sinza na Shule ya Sekondari Makoka;
c) Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Kituo cha Huduma na Tiba- CTC Tandale na Shule ya Sekondari Salma Kikwete;
d) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Kituo cha Huduma ya Methadone –Hospitali ya Temeke na Nyumba ya Upataji nafuu ya nafuu (MUKIKUTE-Temeke);
e) Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti-Pwani na Kituo cha huduma na tiba –CTC- Hospitali ya Songa –Mchukwi-Kibiti

### 3.1.5.2 Malengo ya Ziara katika maeneo yaliyotembelewa

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa kutekeleza ratiba ya ziara, Kamati ilipokea kujadili taarifa za maeneo/ vituo ilivyotembelea, pamoja na kushuhudia utoaji wa huduma mbalimbali za masuala ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya.

Kwa ujumla malengo ya ziara, taarifa zilizowasilishwa na kujadiliwa na ukaguzi uliofanywa ulilenga kubaini mambo makubwa yafuatayo: -

a) Mwitikio wa UKIMWI kwa ujumla kwenye Halmashauri za Wilaya;

b) Hali ya maambukizi ya VVU na upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU pamoja na tiba ya magonjwa nyemelezi kwa muktadha wa malengo ya 90-90-90;

c) Utekelezaji wa afua za UKIMWI mahala pa kazi miongoni mwa Watumishi; mafanikio na changamoto;

d) Udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na huduma ya utoaji Methadon kwa watumiaji wa dawa za kulevya, Mafaniko na changamoto;

e) Ukusanyaji, Usimamizi na matumizi ya takwimu za Masuala ya UKIMWI katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya;

### 3.1.5.3 Uchambuzi wa mambo yaliyobainishwa na Kamati wakati wa ziara

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika maeneo tajwa uliweza kubaini, mambo ya msingi kuhusu mafanikio na changamoto zilizopo pamoja na hatua zinazochukuliwa. Aidha Kamati iliibua hoja pamoja na kutoa ushauri na mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI na adawa ya Kulevya.

Baadhi ya mambo ya msingi ambayo Kamati ilibaini ni pamoja na yafuatayo**: -**

(a) Katika ngazi mbalimbali, hususan baadhi ya Halmashauri na vituo vya afya, hakuna ufahamu wa kutosha juu ya utekelezaji wa shughuli za mwitikio wa UKIMWI katika muktadha wa 90-90-90. Jambo hili linapunguza uwezo wa Serikali na wadau kufanya tathmini ya matokeo ya hatua zinazochukuliwa.

Kutokuwepo na takwimu za makadirio ya wanaokusudiwa kupimwa maambukizi ya VVU ni mojawapo ya mapungufu yaliyobainika katika Halmashauri na Manispaa zotde zilizotembelewa. Jambo hili lina uzito mkubwa kwani ndio msingi wa wa takwimu zote za mkakati wa 90-90-90;

(b) Kuendelea kuwepo changamoto ya unyanyapaa miongono mwa watumishi, mahala pa kazi, ambapo katika Halmashauri zilizotembelewa kumekuwepo na idadi ndogo

sana ya watumishi waliojitokeza na kuweka wazi hali zao za afya ukilinganisha na matarajio.

(c) Kuwepo takwimu za kutilia shaka kuhusu hali ya maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu katika magereza nchini. Kamati ilielezwa juu ya magereza nchi kuwa na idadi ndogo sana ya wagonjwa wa Kifua Kikuu ikilinganishwa na wastani unaotarajiwa kulingana na takwimu za Kitaifa pamoja na takwimu za Kimataifa kwenye maeneo mahususi kama magereza.

**Mheshimiwa Spika, endapo takwimu hizi zipo sahihi,** Kamati haitasita kulipongeza Jeshi la Magereza kwa mafanikio hayo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Jeshi la Magereza lishirikiane na Kitengo cha Taifa cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) ili kufanya ukaguzi na tathmini ya pamoja katika Magereza yote nchini ili kujihakikishia juu ya usahihi wa hali halisi ya Kifua Kikuu katika Magereza nchini.

(d) **Udhaifu katika uchambuzi na matumizi ya takwimu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini udhaifu mkubwa kwenye uiwezo wa watendaji wa Halmashauri za Wilaya katika kuchachua na kutumia takwimu za UKIMWI katika ngzi husika. Hali hii imejitokeza kwenye Halmashauri zote zilizotembelewa kwenye idara ya afya (inayosimamia mwitikio wa UKIMWI kwa upande wa sekta ya afya) pamoja na ofisi ya mratibu wa UKIMWI ngazi ya Hlmashauri (Multisectoral HIV Response). Kwa mfano kwenye Halmashauri mojawapo mratibu wa takwimu wa idara ya afya aliitaarifu Kamati kwamba yeye binafsi hakushirikishwa kwenye maandalizi ya takwimu zilizowasilishwa mbele ya Kamati, licha ya kwamba yeye ndio mtunzaji wa takwimu hizi. Pia aliitaarifu Kamati kwamba huwa hafanyi uchambuzi wa takwimu kwa ajilia ya watumiaji kwenye Hlmashauri yake. Katika Halamashuri nyingine, takwimu za ngazi ya Hlmashauri ziliwasilishwa kwamba, **asilimia 50** ya WAVIU wanaotumia ARV hawafiki vituoni kuwa ajili ya huduma kama inavyotakiwa (loss to follow up) na vivyo hivyo **asilimia 79** ya hali hiyo kenye ngazi ya kituo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii inaashiria aidha kuna udhaifu mkubwa kwenye uchambuzi na tafsiri ya takwimu au hali halisi ya matumizi ya ARV kwa WAVIU ni mbaya sana.

(e) **Uelewa mdogo kuhusu Malengo ya Kimataifa ya Kupambana na UKIMWI ya 90-90-90**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na uelewa mdogo katika muktadha wa wa Malengo na mkakati wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI wa 90-90-90- ifikapo Mwaka 2020. Hii ni kutokana na kwamba, pamoja na takwimu nyingi zilizowasilishwa zililenga kuonyesha mafanikio katika kudhibiti maambukizi VVU/UKIMWI, mafanikio yanayoelezwa hayapimiki kutokana na takwimu kutoonyesha malengo yaliyowekwa na ambayo yanahitaji kufikiwa. Kwa mfano, taarifa nyingi hazionyeshi makadirio ya wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU, haioneshi wanapimwa wangapi kati ya walioakadiriwa, badala yake inaonyesha waliopatikana na maambukizi, Adha takwimu pia hazioneshi idadi ya WAVIU wanaotumia dawa na idadi ya waliofanikiwa kufubaza makali ya VVU. Hali hii, inaathiri kwa kiasi kikubwa maamuzi mbalimbali yanayohusu hatua za kuchukua katika kuimaraisha mapambano dhidi ya UKIMWI.

Kamati ina maoni kuwa, ili kujenga uelewa wa kuondoa dosari zilizobainika katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI, Serikali **(TACAIDS)** iimarisha usimamizi katika ngazi zote kwa kuwezesha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi bora ya takwimu, ili ziweze kutumika ipasavyo katika kuongeza kasi ya kutekeleza mpango Mkakati wa Kimataifa wa kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90 90 90.

(f) **Afua za UKIMWI na madawa ya kulevya mashuleni.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2017) asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15-24 na asilimia 80 ya maambukizi hayo ni miongoni mwa wasichana. Hivyo basi

afua za UMIKWI na madawa ya kulevya mashuleni ni muhimu. Kamati imebaini kutokuwepo mkakati wa uratibu na usimamizi wa mapmabano aidi UKIMWI na matumizi ya madawa ya kulevya mashuleni. Kwa mfano, katika Shule zilizotembelewa na Kamati, wanafunzi waliiarifu Kamati kwamba hawajawahi kusikia kuhusu muktadha wa 90-90-90 kama mkakati wa mwitikio wa UKIMWI nchini na pia waratibu wa elimu ya afya mashuleni waliitaarifu Kamati kuwa hawajawahi kufika katika shule hizo. Kwa maana hiyo, hakuna hatua madhubuti zinazoonekana kutekelezwa kulingana na miongozo iliyopo. Aidha suala la kutekeleza afua kudhibiti dawa za kulevya na UKIMWI limebaki kuwa ni suala la ziada, bila msukumo, mipango, bajeti na bila raslimali fedha.

(g) **Kukosekana hatua mahsusi na za makusudi za kudhibiti maabukizi ya UKIMWI zinazoendana na kasi ya kukua majiji**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Mnispaa ya Kinondoni kuwa na idadi kubwa ya watu takribani 1. 6 Mil, ambao wanajishughulisha na shughuli nyingi za uchumi, likiwa na maeneo mengi ya starehe na viashiria vya ongezeko la maambukizi VVU. Pamoja na viashiria hivyo, hakuna hatua madhubuti za kudhibiti hali hii, kwani idadi ya waliopima ni 305,424 (36%) tu. Aidha, takwimu zilizowasilishwa kuhusu hali ya mambukizi ya VVU/ UKIMWI hazijazingatia Makundi maalum, rika, jinsia, na umri. Hivyo kuzifanya kutoweza kutumika ipasavyo kufanya maamuzi madhubuti ya hatua za kuchukua katika kupambana na VVU/UKIMWI.

(h) **Mahusianisho ya madawa ya kulevya na maambukizi ya VVU**

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa maambukizi ya VVU kwa watumia dawa za kulevya yapo juu ya kiwago cha wastani wa maambukizi Kitaifa. Aidha kumekuwepo na ongezeko la maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu kwa warahibu wa madawa ya kulevya nchini kwa viwango tofauti kutegemeana na sababu mbalimbali. Hivyo Kamati inasisitiza kuwa, pamoja na huduma za methadone kwa warahibu ni

muhimu kuimarisha utoaji huduma za upimaji UKIMNWI, magonjwa ya kifua kikuu na homa ya ini B na C.

(i) **Warahibu wa madawa ya kulevya kukosa namna ya kumudu maisha hata baada ya kukamilisha matibabu**

Waraibu wengi wa madawa ya kulevya hawana ujuzi wa kuweza kujiajiri hali ambayo inawaweka katika hatari kubwa ya kurudia kuyatumia tena madawa hayo baada ya matibabu kutokana na kukosa, makazi maalum, kukosa kitu cha kufanya na kumudu maisha.

(j) **Malalmiko ya warahibu kukewa adhabu ya kusitishiwa dawa ya methadone kwa utovu wa nidhamu**

**Mheshimiwa Spika,** yamekuwepo malalamiko mengi kutoka kwa watumia dawa za kulevya katika Kliniki Methadone ya Temeke, ambapo wanaopata dawa wanalalmikia badhi ya hatua za kinidhamu wanazochukiliwa pindi wakikiuka taratibu zilizowekwa, ikiwa ni pamoja na kunyinwa dawa ya methadone kwa kipindi maalum. Kwa kuwa kamati inaona uwezekano wa uwepo wa malalamiko kama hayo kwingineko, kamati inalichukulia suala hili kwa uzito mkubwa

**Mheshimiwa Spika,** uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa adhabu zinazotolewa zinaleta kuwataka wagonjwa kuzingatia masharti ya kupata matibabu ikiwa ni pamoja na kuwahi muda wa kupata dawa, kuepukana na matumizi ya kilevi chichote wakati wote wa kutumia dawa, kuwa na lugha nzuri, lugha ya staha na heshima kwa watu wote, kutozuzura maeneo ya Kituo baada ya kupata dawa, kutojihusiha na vitendo vya wizi, utovu wa nidha mu na baadhi kusitishiwa dawa kwa sababu moja au nyingine ikiwa ni pamoja na wanaofika wakiwa wametumia vilevi.

Kamati Ina maoni kuwa kwa kuzingatia mazingira halisi ya warahibu, uchukuaji wa hatua za kinidhamu ni jambo la msingi. Hata hivyo adhabu ya kusitisha dawa ya methadone Kwa kipindi Fulani itekelezwe pale tu ambapo ni kwa mujibu wa sababu za kitaalam na si vinginevyo. Kwa mfano pale

mrahibu anapobainika kuchanganya matumizi ya dawa ya methadone na dawa ya kulevya ni budi asitishiwe dawa ya methadone kwa sababu za kitaalamu. Lakini pale ambapo mrahibu anabainika kutenda kosa la kinidhamu kwa mfano kuchelewa au kupigana na mwenzake, Kamati inashauri utengenezwe utaratibu mwingine wa adhabu tofauti na usitishaji wa dawa. Msingi wa pendekezo hili ni kutokana na kwamba, adhabu kuwasitishia dawa ya methadone inawawaweka katika hatari ya kurudi kutumia dawa za kulevya, lakini pia inaisababishia Serikali hasara kwa kuhitaji kuendelea kumtumia dawa kwa muda mrefu aidi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya ikilinganishwa na Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020

#### 4.1.1 Vipaumbele vya Tume ya Kudhibiti UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imepanga kujikita katika kuongeza juhudi za utoaji uongozi wa kimkakati wa mwitikio wa Taifa wa UKIMWI. Tume imeainisha maeneo ambayo itaweka mkazo kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020. Maeneo hayo ni pamoja na;

i. Kutafuta rasilimali za UKIMWI kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi;
ii. Kutayarisha na kusambaza miongozo ya UKIMWI kwenye sekta na mikoa ya kipaumbele;
iii. Kuimarisha majadiliano ya kisekta na wadau wa UKIMWI;
iv. Kuendelea kusambaza matokeo ya tafiti za UKIMWI kwa wadau; na
v. Kujenga uwezo wa watumishi na kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, Tume iliainisha maeneo matatu (3) na kuyawekea mkazo katika utekelezaji wake katika kipindi cha kati yafuatayo:-

i. Kupunguza utegemezi wa wafadhili katika kugharamia programu za UKIMWI nchini;

ii. Kuongeza utumiaji wa huduma za UKIMWI kwa vijana wenye umri wa miaka 15-24 na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi; na

iii. Kuongeza jitihada za kupeleka huduma za UKIMWI kwenye Mikoa 14 ya vipaumbele ukiwemo mkoa wa Iinga, Mwanza, Njombe, Kagera, Katavi, Mbeya,, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Geita na Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia maeneo ambayo Tume iliainisha na kuyaridhia kwa kuwa yalioneka kuwa na tija katika suala zima la uboreshaji wa mapambano dhidi ya VVU/ UKIMWI pia maeneo hayo yanashabihiana na Mipango na Mikakati mbalimbali yakiwemo makubaliano ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijiridhisha kwamba, Tume imepanga kutekekeleza malengo ambayo yameainishwa katika miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo ya Muda wa kati 2017/2018-2020/20121, Malengo ya Maendelao endelevu (Sustainable Development Goals 2030). Aidha, utekelezaji wa shughuli hizo zote unalenga katika kuhakikiasha tisini tatu (90-90-90) zinapatikana ikiwemo hakuna mtu au watu wenye maambukizi wanafariki kutokana na UKIMWI. Kwa kutekeleza haya yote kutapelekea kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi wa jamii ambao utachangia jamii isiyo na maambukizi ya VVU.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2017), ambapo asilimia 40 ya maambukizi mapya ya UKIMWI yapo kwenye umri wa kuanzia miaka 15-24 na asilimia 80 ya

maambukizi hayo ni miongoni mwa wasichana, Kamati inashauri serikali kutoa umuhimu mkubwa katika suala hili.

#### 4.1.2 Vipaumbele vya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imejipangia madhumuni ya kudhibti matumizi ya dawa za kulevya, kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya pamoja na utekelezaji wa masuala ya kinga na tiba kwa watu wanaotumia dawa za kulevya. Mamlaka imepanga kufikia madhumuni hayo kwa kuweka mikakati mitatu (3) ifuatayo;

i. Kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya katika nchi yetu (Supply Reduction);

ii. Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya (Demand Reduction);

iii. Kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya (Harm Reduction);

**Mheshimiwa Spika,** kamati iliijadili mikakati hii na kuona kwamba ina tija kwa taifa zima endapo mikakati hii itatekelezwa kwa wakati. Hata hivyo kwa kuwa utekelezaji wake unategemeana na upatikanaji wa fedha, ni muhimu Serikali ikafanya juhudi kubwa aidi katika kutenga na kutoa fedha kwa wakati. Aidha Kamati inasisitiza upatikanaji fedha za maendeleo kwa ajilii ya miradi ya maendeleo kupewa msukumo wa kipekee kutokana na umuhimu wake.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

#### 4.2.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia **Fungu 92** linatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 5,000,000.00.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia **Fungu 92** inaomba jumla ya kiasi cha shilingi **8,769,193,747.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 5,956,634,747.00** sawa **na asilimia 68** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **2,812,599,000.00** sawa na **asilimia 32** ni kwa ajili ya mengineyo, ikijumuisha matumizi ya kawaida (OC) **shilingi 1,212,747,000.00** na mishahara ya watumishi (PE) ni **shilingi 1,599,813,000.00**

**Mheshimiwa Spika**, makadirio haya ya matumizi ya mwaka 2019/2020 ni pungufu kwa takribani **shilingi 4, 140, 237,253** sawa na **asilimia 32** ikilinganishwa na bajeti ya matumizi ya Tume kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Aidha kwa upande wa Bajeti ya maendeleo ni pungufu kwa takribani nshilingi **4,343,365,253** sawa na **asilimia 42** ya kiasi kilichotengwa mwaka unaoisha. Kamati inasisitiza wasiwasi wake kuwa, upungufu wa fedha za kwa ajili ya shughuli za Tume kwa wastani wa **asilimia 32** ni mkubwa sana. Aidha upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo kwa **asilimia 42** ni jambo la kutizamwa upya, kwani bado mapambano dhidi ya UKIMWI yanahitaji fedha za kutosha ili kuweza kuendelea kupata matokeo tarajiwa, kwani kwa mujibu wa taarifa mbalimbali utekelezaji wa afua nyingi za UKIMWI hazijakamilika na uendelevu wake bado unahitaji fedha za kutosha na kwa wakati.

### 4.2.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya-Fungu 91

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imekadiria kufanya matumizi ya kiasi cha **Shilingi 7,592,818,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4, 948, 552,000.00** sawa na **asilimia 35 ya** fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi **2, 644,266,000.000 sawa** na **asilimia 65** kwa ajili ya Mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi **1, 837,101,000.00** sawa na **asilimia 32**

ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati, ulibainika kwamba Mamlaka haijatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa Fedha wa 2019/2020 kama ambavyo ilijitokeza kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 na 2018/2019. Mwenendo huu wa kutotenga fedha za maendeleo unaashiria kutolitazama suala la madawa ya kulevya kataika mapana yake. Aidha, endapo hatua hazitachukuliwa mapema, linaweza kusababisha hasara kwa kutopata matokeo mazuri ya fedha zinazotengwa na kutumika kwa ajili ya kukabiliana na dawa za kulevya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza kuwa ni umuhimu wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini kwa upana wake ikiwa ni pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevya na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya**.**

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 na Makadirio ya matumzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kupambana na kudhibiti Dawa za kukevya, Kamati ina Maoni, Mapendekezo na Ushauri katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo;

### 5.1 Tume Ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

#### 5.1.1 Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI

Kamati imebaini kuwa, mpaka sasa asilimia kubwa Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Tanzania imekuwa ikitegemea fedha za wahisani. Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi **Bilioni 3** tu sawa na **asilimia 29.1** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tume. Kiasi kilichotolewa ni **shilling 750,000,000**, sawa na **asilimia 25** tu ya kiasi kilichotengwa.

Kamati inasisitiza kuwa, kuendelea kutegemea wafadhili wa nje hakutoi uhakika wa mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI ikizingatiwa kwamba baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI kwa Tanzania.Kwa mfano, PEPFAR wamepunguza **asilimia 23** ya fedha zilizokuwa zitolewe kwa Tanzania kwa mwaka 2019/2020 kiasi cha **USD 119Mil**, sawa na shilingi **282,854,000,000.** Kupunguzwa kwa kiasi hiki cha fedha, kuna athari katika mipango iliyokuwa itekelezwa katika kupambana na UKIMWI nchini**.**

**Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi wake. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vya kujiwezesha kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Itakuwa jambo jema endapo bajeti ya UKIMWI angalau asilimia 75 ya fedha ya maendeleo ya Tume iwe ni fedha za ndani na asilimia 25 tu itokane na wafadhili wa nje.**

### 5.1.2 Kuanzisha Tozo kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (AIDS Trust Fund - ATF)

Kamati imebaini kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutenga fedha katika bajeti kuu, changamoto kubwa imekua ni kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za UKIMWI. Mfuko wa UKIMWI (Aids Trust Fund - ATF) lengo lake ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na janga hili.

**Kamati inashauri Serikali itekeleze sasa kwa vitendo suala hili kwa kuanzisha kisheria chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko huu kama ilivyo kwenye mifuko mingine. Serikali**

**iharakishe mchakato wa tozo maalum kwa ajili ya Mfuko wa ATF. Aidha, Serikali ibuni uwekezaji kwa kushirikisha na Sekta binafsi ili kuwekeza katika miradi ambayo sehemu ya faida itakua chanzo cha mapato kwa ajili ya Mfuko (*Endowment fund*).**

**5.1.3 Kuimarisha ukusanyaji, hifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali za UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika, u**tekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana na ubora wa takwimu zinapatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kuna upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu mbalimbali zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

**Kamati inashauri Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Wizara ya Afya na TAMISEMI kuimarisha usimamizi ikiwa wa ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya takwimu kwa ngazi za HImashauri na Vituo vya Afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza mpango Mkakati wa Kimataifa wa kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 90 90 90.**

**5.1.4 Marekebisho ya sheria ya UKIMWI ili kuimarisha Mapambano ya UKIMWI Nchini ili yaendane na utekelezaji wa Malengo ya Kimataifa ya kutokomeza UKIMWI ya 90 90 90.**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania inaendelea kutekeleza awamu ya kwanza ya malengo na mkakati wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na masuala ya UKIMWI (UNAIDS), ambalo limeweka malengo ya kutokomeza ugonjwa huo ifikapo Mwaka 2020 ambayo yanajulikana kama 90-90-90. Malengo haya yanasisitiza kuwa, ifikapo mwaka 2020, asilimia 90 ya waliokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU wajue hali zao kiafya, asilimia 90 ya watakaopima na kukutwa na maambukizi ya VVU wapate dawa na asilimia 90 wa waliopo kwenye tiba wawe na kiwango kidogo cha virusi kwenye damu

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonyesha utekelezaji wa mkakati huu wa 90-90-90 nchini hauna uwiano linganifu. Katika 90 ya kwanza Tanzania ina **asilimia 61**, 90 ya pili asilimia 93 na 90 ya tatu ina asilimia 87. Hivyo Tanzania ina alama za chini katika 90 ya kwanza. Ikizingatiwa kuwa 90 ya kwanza ndio msingi wa mafanikio ya kutokomeza UKIMWI nchini, hatuna budi kuongeza kasi ya kupima, ili watu wengi zaidi wajue hali zao za afya na kuchukua hatua stahili.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na sababu nyingine, changamoto kubwa ya kutofikiwa kwa 90 ya kwanza ni utekelezaji wa sheria ya UKIMWI, ambayo haitoi wigo mpana kwa watu wenye umri chini ya miaka 18 kuweza kupima kwa ridhaa yao wenyewe, badala yake inataka wapate ridhaa ya wazazi au walezi. Aidha sheria hairuhusu mtu kujipima mwenyewe. Vipengele hivi viaathiri idadi ya wanaojitokeza kupima, hasa ikizingatiwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwepo kwa asilimia 40 ya maambukizi mapya ya VVU kwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15-24. **Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufanya mabadiliko ya kisera na a Sheria pale inapodhihirika kwamba kuna mahitaji hayo ili kuzingatia mahitaji mapya kwa mujibu wa takwimu**

## 5.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

### 5.2.1 Athari za kutotenga Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa miaka mfulilizo Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya imekua haitengewi Bajeti kwa ajili ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotenga fedha za maendeleo ni kukosekana kwa maabara ya Mamlaka ya Kupambana na madawa ya kulevya kwa ajili ya uchunguzi.

**Mheshmiwa Spika,** maabara inayotumika mpaka sasa ni maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo ina

vipaumbele katika utekelezaji shughulia zake. Sio lazima vipaumbele vya Mamlaka ya kupambana na madawa ya kulevya viwiane. Pamoja na kwamba ipo ahadi ya Wafadhili ya kujenga maabara kwa ajili ya Mamlaka, lakini utekelezaji wa ahadi hiyo umekua ukiahirishwa kila mwaka. Vilevile ukosefu wa fedha za maendeleo umepelekea kasi ndogo au kukosekana kwa mfumo maalumu kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa madawa ya kulevya na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia kumudu maisha na kuachana na biashara na matumizi ya madawa hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kwamba, ajenda ya kupambana na Dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyotafsiriwa. Kamati inaamini kuwa, miradi ya maendeleo inaweza kutekelezwa na fedha za maenedeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu kiuchumi kwa kuwaunganisha, kuwapa mbinu za ujasiriammali, mikopo nafuu ya biashara, studi za maisha, uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya na hata kuikinga jamii ili isishiriki katika njia yoyote ya matumizi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maana hiyo ni maoni ya Kamati kwamba utoaji na utumiaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bila kuambatana na mifumo na mipango ya kimkakati inayoweza kuleta matokeo ya kuendeleza mzunguko wa kupunguza idadi ya watumiaji wa madawa ya kulevya na wakati huo huo kuwarudisha kwa kasi ile ile au zaidi watu hao kwenye hali yao ya awali, hakuwezi kuleta matokeo yanayotarajiwa. Kwa sababu hiyo ni maoni ya Kamati kwamba fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa Mmlaka kuanza kujenga mifumo itakayo jumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya na hivyo kuiwezesha Mamlaka kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

### 5.2.2 Kujenga na kuimarisha mifumo ya Kitaasisi katika utekelezaji wa shughuli za Masuala ya Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya udhibiti na upambanaji wa Dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo taasisi zisizo za kiserikali. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, zipo baadhi ya NGOs na Taasisi zinazojihusisha na masuala ya dawa za kulevya nchini ambazo hazina muundo na mifumo rasmi wa jinsi gani zinawasaidia watumiaji wa dawa za kulevya. Badhi zikitekeleza shughuli zake kwa kuwabagua watumiaji wa dawa hizo, mfano zinazo wahudumia wanawake peke yake, wale wanaojidunga kwa sindano na mara nyingine wale wanaotumia kwa kuvuta. Ikizingatiwa kuwa, watumiaji wengi wanaotumia kwa kujidunga ni wale ambao wamepita katika hatua ya kuvuta kwanza na ndipo anakwenda katika hatua ya kujidunga, ubaguzi huu hauna tija katika mapambano dhidi ya matumizi na athari ya watumiaji wa dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, kupitia Mamalaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo chake cha uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, waongeze kasi ya kukamilisha zoezi la utambuzi na uratibu wa asasi zote zinazojishughulisha na Dawa za Kulevya ili kuangalia malengo yao pamoja na kazi zinazofanywa na asasi hizo na kuwawekea mfumo rasmi wa utekelezaji wa shughuli zao ili kuhakikisha kuwa walengwa wanafaidika na uwepo wa asasi hizi kwani fedha zinazotolewa ni kwa jina la watanzania. Aidha mfano mzuri wa uratibu wa aina hiyo ni ule wa wadau wa mwitikio wa UKIMWI nchini.

### 5.2.3 Kuimarisha usimimizi wa nidhamu kwa waathirika wa madawa ya kulevya wanaopata dawa za Metahadone katika Kituo cha Hospitali ya Temeke Jijini Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na wataalamu katika Kliniki ya Methadone Temeke. Na kwamba inatambua umuhimu wa kusimamia nidhamu

kikamilifu kwa watumia dawa za kulevya ambao wengi wao kutokana na matumizi ya muda mrefu na athari za dawa zimewafanya kuwa na mienendo isiyokubalika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Uonngozi wa Kituo, kuendeleza kusimamia nidhamu kikamilifu kwa wagonjwa wanaopata dawa, kwani nidhamu ni sehemu muhimu ya tiba wanayopata kituoni hapo. Aidha Kamati inashauri kuwa, aina ya adhabu zinazotolewa ziendani na hali halisi ya wagonjwa kwa kuangalia kwa mapana maslahi yao na Serikali. Hivyo inapendekeza kuangalia adhabu mbadala kwa wagonjwa wa dawa za kulevya wanaopatikana na mkosa mbalimbali ya kinidhamu kuliko kuwasitishia dawa Methadon, ISIPOKUWA pale inapothibitika kuwa kutumia dawa hiyo kunaweza kumsababbishia athari, mfano kwa wagonjwa wanaofika kituoni wakiwa wametumia vilevi. Hii ni kutokana na kwamba, adhabu ya kutowapa dawa ya methadone, inawawaweka katika hatari ya kurudi kutumia dawa za kulevya, lakini pia inaisababishia Serikali hasara kwa kuhitaji kuendelea kumtumia dawa kwa muda mrefu zaidi.

### 5.2.4 Suala la madawa ya kulevya kuwa ajenda ya Kamati za UKIMWI katika Halmashauri na Manispaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati za UKIMWI katika Halmashauri na Manispa Nchini zimekua zikiratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika Halamshauri na Manispaa kwa ufanisi wa kutosha. Uchambuzi wa Kamati katika ufuatiliaji wa shughuli za mapambano dhidi ya madawa ya kulevya katika ngazi za Halmashari na Manispaa umeonesha kutokuwepo utaratibu au mfumo rasmi wa namna ya kushughulika na suala la madawa ya kulevya. Aidha kwa kuzingatia mahusiano ya karibu yaliyopo miongoni mwa waathirika wa madawa ya kulevya na waathirika wa maambukizi ya UKIMWI, hatua na afua za pamoja katika kudhibiti na kupambana na UKIMWI na Madawa ya kulevya ni muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kukasimisha majukumu ya kudibiti na kupambana na madawa ya kulevya kwenye Kamati za UKIMWI katika

Mamlaka za Serikali za mitaa kupitia GN 142 la tarehe 06 April 2018. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa, ili kuwezesha utekelezaji wa jukumu hili kwa ufanisi, Serikali ikamilishe muongozo na hadidu rejea za namna Kamati hizi zitakavyotekeleza jukumu la kupambana na dawa za kulevya katika ngazi husika.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe binafsi kwa kuipa kamati ushirikiano na ulezi uliotukuka na pia kwa kunipa muda wa kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb) pamoja na Manaibu Waziri Mheshimiwa Antonny Peter Mavunde (Mb) na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa (Mb), vilevile namshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe. Ummy Ally Mwalimu na Naibu Waziri Mhe.Dkt Faustine Ndugulile kwa ushirikiano wao mkubwa wanaondelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu Ofisi ya Waziri Mkuu wa Sera na Uratibu na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anaehusika na Bunge Ndg. Maimuna Tarishi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndg Rogers William Siyanga, na watendaji wote kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii ili kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI , kwa kazi nzuri walioifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Pamoja na ufinyu wa muda wajumbe hawa walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa nomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:

1. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Prof. Norman Adamson S. King, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
14. Mhe.Oliver Daniel Semuguruka, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Susan Anselim Lyimo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb - Mjumbe
17. Mhe.Omary Ahmed Badwel, Mb - Mjumbe
18. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
19. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
20. Mhe Amina Nassor Makilagi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Yussufu Haji Khamisi, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Ester Nicholas Matiko, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Fratei Gregory Massey, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Godfrey W. Mgimwa - Mjumbe
26. Mhe. Mwigulu L. Nchemba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge, Ndg. Athuman Hussein Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Virgil Mtui, Nd. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na msaidizi wa Kamati

Ndg. Grace Mwenye kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania **Fungu 92** jumla ya shilingi **8,769,193,747.00** na **Fungu 91** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya jumla ya Shilingi **7,592,818,000.00**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Oscar R. Mukassa, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

04 Aprili, 2019

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutakaporudi saa kumi na moja jioni tutapokea Taarifa ya Kamati ya Bajeti na baada ya hapo tutaanza uchangiaji kama kawaida na wote ambao mko katika orodha ya uchangiaji mtapata nafasi. Sasa kwa hatua hii niwashukuruni sana kwa uvumilivu wenu nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

*(Saa 7.16 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea, sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Karibu sana Mheshimiwa, anakuja mwenyewe Mheshimiwa George Simbachawene, unaweza kuendelea Mheshimiwa una nusu saa. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika,

maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti wa Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/20. Nitaomba taarifa hii yote nzima kama ilivyo kwenye kitabu chetu iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kwa sababu baadhi ya maeneo nitayaruka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 71(b) cha Sheria ya Bajeti, Na. 11 ya mwaka 2015, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) pamoja na Katibu wa Bunge na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020. Taarifa hii inaeleza kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika kipindi cha hadi Machi, 2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi yanayojumuisha vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya shilingi 125,521,100,000 kati ya fedha hizo shilingi 24,441,023,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 92,764,464,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.8,315,613,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 3,315,613,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida. Hadi kufikia 15 Machi, 2019, Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea fedha za Matumizi ya Kawaida kiasi cha shilingi 73,206,843,427. Kati ya fedha hizo, shilingi 58,085,266,647 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na 63% ya bajeti yote na shilingi 15,121,576,780 kwa ajili ya Mishahara sawa na 62% ya bajeti yote. Kwa ujumla utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida *(OC)* umekuwa mzuri na umewezesha Ofisi ya Bunge na Bunge lako Tukufu kutekeleza majukumu yake vizuri na tunaipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2018, Mfuko umepokea kiasi cha shilingi 6,710,062,500 ambazo ni sawa na asilimia 81 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kutumika katika mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya hizo zilizotolewa, shilingi 4,287,500,000 ni fedha za ndani sawa na asilimia 86 ya fedha za ndani zilizoidhinishwa na shilingi 2,422,562,500 ni fedha za nje sawa na asilimia 73 ya fedha za nje zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mfuko wa Bunge ulipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 61,000,000 ambapo hadi kufikia Machi, 2019, Mfuko ulikuwa umekusanya kiasi cha shilingi 39,983,700 sawa na asilimia 65.5. Maduhuli hayo yametokana na kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2019, Ofisi ya Bunge ilitekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa kama ambavyo yanaonekana katika ukurasa wa 4 hadi 6 na eneo hilo ni majukumu ya kawaida kwa sababu ya muda naomba niyaruke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika

Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/2020, Mfuko wa Bunge umepanga kutumia kiasi cha shilingi 124,182,537,600. Kati ya fedha hizo, shilingi 23,334,462,000 ni fedha za Mishahara; shilingi 93,238,564,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo na shilingi 7,609,511,600 ni fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, kiasi cha shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani na Sh.2,609,511,600 ni fedha za nje. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Bunge inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 54,777,000.

Mheshimiwa Spika, shughuli zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama inavyoonekana kuanzia ukurasa wa 8 hadi 10 ni zile tunazozitekeleza kila siku isipokuwa nitaomba niziseme zile za maendeleo. Kwa upande wa Maendeleo, Mfuko huu wa Bunge utaratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa na pamoja na:-

(i) Ukarabati na ununuzi wa mitambo ya usalama;
(ii) Kusimika Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio*) katika ukumbi wa Bunge;
(iii) Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya viongozi wa Bunge Dodoma;
(iv) Ukarabati wa Ukumbi wa Msekwa, ukumbi wa Bunge pamoja na majengo ya Ofisi ya Bunge; na
(v) Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na watumishi kupitia Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP II) na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma *(PFMRP).*

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri ni kama ifuatavyo:-

(i) Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo na kuziwekea samani ili kurahisisha utendaji kazi wao kwa kipindi wanachokuwa majimboni.

(ii) Kwa mwaka 2018/2019, Ofisi ya Bunge inategemea kutekeleza Miradi muhimu ya Maendeleo kama vile ununuzi

wa Mitambo ya Usalama, Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio),* ukarabati wa Kumbi za Bunge pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi ya viongozi. Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za maendeleo kwa wakati ili miradi hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia niwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Kwa sababu ya muda na wanajulikana nisiwatambue kwa kuwasoma majina yao.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Makamu Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika Kamati na kwa namna tunavyoshirikiana kwa hakika nadhani ni kama kulwa na doto. Napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri wao wa kitaalamu ambapo wamekuwa wakiipa Kamati ambao kwa kweli vijana hawa wanafanya kazi kubwa, ni vijana wadogo lakini kwa kweli wanafanya kazi kubwa wakiongozwa na Ndugu Kadebe lakini mwingine ni binti anaitwa Maombi na mwingine Masabala, kwa kweli wanafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya niliombe Bunge lako Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko wa Bunge Fungu 42 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Jenista Joackim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) pamoja na Katibu wa Bunge na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inaeleza kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika kipindi cha hadi Machi, 2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi yanayojumuisha

vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2019/2020.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya **Sh.125,521,100,000** kati ya fedha hizo **Sh.24,441,023,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Sh.92,764,464,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh.8,315,613,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo **Sh.5,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh.3,315,613,000** ni fedha za nje.

### 2.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 15, 2019 Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha **Sh.73,206,843,427.00.** Kati ya fedha hizo **Sh. 58,085,266,647** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) (sawa na 63% ya bajeti yote) na **Sh. 15,121,576,780** kwa ajili ya Mishahara (PE) (sawa na 62% ya bajeti yote).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida (Mishahara na OC) umekuwa mzuri na umewezesha Ofisi ya Bunge na Bunge lako Tukufu kutekeleza majukumu yake vizuri.

### 2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 15 Machi 2018, Mfuko umepokea kiasi cha **Sh. 6,710,062,500** ambazo ni sawa na **asilimia 81** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kutumika katika mwaka wa fedha 2018/19. Kati ya hizo zilizotolewa, **Sh. 4,287,500,000** ni fedha za ndani (sawa na asilimia 86 ya fedha za ndani zilizoidhinishwa) na **Sh. 2,422,562,500** ni fedha za nje (sawa na asilimia 73 ya fedha za nje zilizoidhinishwa)**.**

### 2.3 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Bunge ulipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha

**Sh.61,000,000** ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Mfuko ulikuwa umekusanya kiasi cha **Sh.39,983,700 (sawa na asilimia 65.5).** Maduhuli hayo yametokana na kodi ya pango.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2019 Ofisi ya bunge ilitekeleza majukumu mbali mbali yaliyopangwa kama ifuatavyo:

i) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Mitatu ya Bunge;
ii) Kuratibu na Kusimamia shughuli za Mikutano Mitatu ya Kamati za Bunge;
iii) Kuwezesha Kamati za Bunge kufanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini;
iv) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);
v) Kugharamia malipo ya stahili za Wabunge (Posho ya Jimbo na Usafiri);
vi) Kugharamia matibabu ya Wabunge;
vii) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;
viii) Kutoa huduma za Utafiti “Information Research” kwa Wabunge;
ix) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni Mwanachama ambayo ni SADC PF, PAP, CPA, Maziwa Makuu, IPU, ACP-EU;
x) Kuwezesha Wabunge kushiriki mashindano ya Michezo kwa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika mashariki;
xi) Kufanya mapitio *(review)* ya Mpango Mkakati wa Ofisi kwa mwaka 2016/2017 – 2020/2021); Mpango wa Usimamizi wa Vihatarishi na kuandaa Rejesta ya Vihatarishi vya Ofisi;
xii) Kuratibu kazi ya utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Kamati na Bunge;

xiii) Kuandaa vipindi vya Televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;
xiv) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala (ununuzi wa vifaa vya Ofisi), malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);
xv) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

a. Kufanya ukarabati na ununuzi wa vifaa ya Usalama;

b. Kufanya ukarabati wa majengo ya Ofisi za Bunge ikiwa ni pamoja na kuongeza ghorofa moja katika jengo la Utawala;

c. Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya Makazi ya Viongozi wa Bunge – Dodoma;

d. Kusimika lifti katika jengo la Utawala na jengo la Utawala Annex;

e. Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi kupitia Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP II) na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP);

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### 4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia kiasi cha **Sh.124,182,537,600.00** Kati ya fedha hizo **Sh.23,334,462,000.00** ni fedha za Mishahara; **Sh.93,238,564,000.00** ni fedha za Matumizi mengineyo na **Sh.7,609,511,600.00** ni fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, kiasi cha **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.2,609,511,600.00** ni fedha za nje.
**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Bunge inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 54,777,000.00.**

## 4.2 Shughuli zitakazotekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2019/20

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama ifuatavyo: -

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Bunge;
b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Bunge;
c) Kuwezesha Kamati za Bunge kufanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini;
d) Kugharamia malipo ya stahili za Wabunge (Posho ya Jimbo na Usafiri);
e) Kugharamia matibabu ya Wabunge;
f) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);
g) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;
h) Kutoa huduma za Utafiti "Information Research" kwa Wabunge;
i) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni Mwanachama SADC-PF, PAP, Maziwa Makuu, IPU, Mabunge ya Jumuiya ya Madola na ACP-EU;
j) Kuwezesha Mkutano wa Maspika wa Jumuiya ya Madola;
k) Kuwezesha Wabunge kushiriki mashindano ya Michezo kwa Mabunge ya Jumuiya ya Afrika mashariki;
l) Kutoa huduma ya mawasiliano ya habari kwa Wabunge kwa kuimarisha Mifumo ya Tehama na Mawasiliano kwa jamii;
m) Kuendeleza marekebisho ya mifumo ya utendaji kazi katika idara na Vitengo ili kuongeza tija na ufanisi (Mfumo wa kielektroniki wa maktaba na kutunza kumbukumbu);
n) Kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za utawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi) pamoja na ukarabati wa Kumbi za Mikutano na ujenzi wa Makazi ya viongozi;
o) Kuboresha utendaji kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi;

p) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

i. Ukarabati na ununuzi wa mitambo ya usalama;
ii. Kusimika Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio)* katika Ukumbi wa Bunge;
iii. Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya Makazi ya Viongozi wa Bunge - Dodoma;
iv. Ukarabati wa Ukumbi wa Msekwa, Ukumbi wa Bunge pamoja na majengo ya Ofisi ya Bunge; na
v. Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi kupitia Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP II) na Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**5.1 Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo na kuziwekea samani ili kurahisisha utendaji kazi wao kwa kipindi wanachokuwa majimboni;

**5.2 Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2018/2019 Ofisi ya Bunge inategemea kutekeleza Miradi muhimu ya maendeleo kama vile ununuzi wa Mitambo ya Usalama, Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio),* ukarabati wa Kumbi za Bunge pamoja na ujenzi wa nyumba za Makazi ya viongozi. Kamati ya Bunge inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za maendeleo kwa wakati ili miradi hii ikamilike kama ilivyopangwa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb– Mwenyekiti
2) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb-M/Mwenyekiti
3) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4) Mhe. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
5) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
6) Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
7) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
8) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
9) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
10) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
11) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12) Mhe. Hasna Sadi Kalunda Mwilima, Mb
13) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
14) Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb
15) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
16) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
17) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
18) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
19) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
20) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
21) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
22) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
23) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
24) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26) Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri

wa kitaalamu ambao wamekuwa wakiipa Kamati ambao umewezesha kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

George B. Simbachawene, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
04 APRILI, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Tunakushukuru sana kwa usomaji mahiri wa taarifa hiyo lakini kupitia kwako tunaishukuru sana Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa sana ambayo mmekuwa mkiifanya *all along* lakini pia kwa kazi kubwa ambayo bado ipo mbele yenu. Tunawashukuru sana kwa kutupa mwanga kuhusiana na bajeti ya Ofisi hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika uchangiaji, kama nilivyosema wale ambao majina yenu ninayo kwa kweli mtapata nafasi ya kuchangia kadri nitakavyowaona humu ndani, kama kuna aliyesahaulika basi mtanikumbusha kwa kuandika ki-*note*. Leo nashauri tuanzie Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, utuanzishie uchangiaji wa bajeti 2019/2020, tafadhali, una dakika 10.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, napenda kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti wa muda mrefu hivi na nikafanya utafiti wa viongozi wa tatu wa Asia na nikabaini viongozi hawa kuna mambo manne makubwa wameyafanya katika nchi zao halafu baadaye nitalinganisha na kile ambacho kwa mawazo yangu nakiona kinafanyika katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi wenyewe ni marehemu Lee Kuan Yew wa Singapore; wa pili ni Mahathir Mohamed wa Malaysia sasa hivi ana awamu pili lakini nitazungumzia awamu ya kwanza; na kiongozi wa tatu anaitwa Deng Xiaoping aliyekuwa Rais wa Taifa la China kuanzia mwaka wa 1978.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo manne wameyafanya, la kwanza, hawa viongozi wote niliowataja watatu ni viongozi ambao wana maono na mipango ya muda mrefu. Pili, sifa yao kubwa ni viongozi wa matendo, wanachokisema ndicho wanachokitenda. Tatu, wanapoteua viongozi na watendaji wanateua wenye uweledi, maarifa, ujuzi, na uzoefu. Jambo la nne ambalo walilifanya viongozi hao ni kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, nikija hapa kwenye nchi yetu kwa nachokiona kwa mawazo yangu kile anachokifanya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinafanana sana kwa asilimia mia moja na hiki ambacho kinafanywa na viongozi hawa watatu niliowataja. Kwa maana hiyo basi Taifa letu la Tanzania katika kipindi cha miaka mitano na miaka kumi inayokuja Tanzania itakuwa miongoni mwa mataifa yenye ustawi mkubwa sana wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya hotuba za Rais Magufuli aliwahi kutuambia kwamba anasikitishwa sana kuona Tanzania bado inaendelea kuwa Taifa ambalo linatembeza bakuli na Taifa ambalo yeye anaamini lina uwezo sana wa kuwa Taifa linalotoa misaada. Mimi bila shaka nakubaliana naye kwamba Tanzania ina uwezo mkubwa sana tukifanya kazi kwa bidii na chini ya uongozi wake bila shaka katika kipindi kijacho si kirefu sana Tanzania itaweza kufikia katika ndoto hiyo. Hata kama hatukufikia Taifa ambalo linaweza

likatoa misaada lakini bila shaka ni Taifa ambalo tutaweza kujitosheleza kwa asilimia mia moja kwa bajeti yetu, ninaamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye yale mambo manne niliyoyaeleza pale mwanzo. La kwanza, Rais wetu Magufuli ni mtu ambaye ana maono, ana mipango ya muda mrefu ya kuliendeleza Taifa hili. Kama kuna jambo ambalo linawafanya Waafrika wadharauliwe duniani, Wazungu wanasema Waafrika kwa kawaida yao wakipanga mipango yao wanapanga mipango ya muda mfupi, pengine miaka miwili na wamekwenda mbali sana miaka mitano lakini tunachokiona Tanzania sasa hivi, tuna mradi huu wa reli ya kisasa ni mradi ambao ukikamilika utadumu kwa takribani miaka mia moja mpaka mia moja na hamsini kama tutaitunza vizuri. Bila shaka inatuonyesha dhahiri kwamba huyu ni kiongozi ambaye ana maono ya muda mrefu. Mradi mwingine ni mradi wa umeme wa Bonde la Mto Rufiji. Mradi huu utakapomalizika bila shaka tukiutunza vizuri utadumu kati ya miaka hamsini mpaka sabini. Kwa hiyo, tunaona bila shaka ni kiongozi wa namna gani, ni kiongozi ambaye ana maono na mipango ya muda mrefu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaona bila shaka ni kiongozi wa namna gani. Ni kiongozi ambaye ana maono na mipango ya muda mrefu. La pili, nimewahi kusikia mahali watu wakilala wanasema ah, Rais Magufuli bwana, anateua Maprofesa, Madaktari; sasa najiuliza, tulitegemea amteue nani? Kiongozi aliye makini, ana ajenda na anajua kwamba kipindi chake cha Urais ni miaka 10, bila shaka unapaswa kuteua watu unaoamini wana uwezo, weledi na maarifa ili wakusaidie kuikamilisha hiyo kazi katika kipindi kifupi. Maana yake miaka 10 katika uhai wa binadamu ni muda mchache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina maana kwamba watu wasio na Shahada za Udaktari wa Maprofesa hawana uwezo, la hasha! Sina maana hiyo. Wapo baadhi ya watu elimu yao ni ndogo sana Mwenyezi Mungu kawajaalia kuwa na uwezo

huo na maarifa, bila shaka wakipewa nafasi hizo sina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nataka kulisema ni la Sayansi na Teknolojia. Bila shaka Rais Magufuli amejitahidi sana katika Sekta ya Afya. Tumewekeza sana katika sekta hii ya tiba. Ni mategemeo yangu kwamba katika Sekta ya Kilimo, kile ambacho tunakiona kinafanyika katika Sekta ya Afya, ningetamani sana nikione kinafanyika katika Sekta ya Kilimo kwa sababu mapinduzi ya kweli ya Taifa la Tanzania linategemea sana katika Sekta hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, najua Serikali inao Mpango wake wa Maendeleo wa Awamu ya Pili lakini nadhani fedha zilizotengwa siyo haba, lakini kama tunataka kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo na hasa kutimiza ndoto yetu ya Tanzania ya Viwanda; na ikiwa kilimo ni sehemu kubwa sana ya maendeleo ya viwanda, naiomba sana Serikali yangu Tukufu ifanye kila linalowezekana tuwekeze sana katika Sekta hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1966 aliyekuwa Waziri Mkuu wa Malaysia aliwahi kusema maneno haya; aliwahi kutembelea Nigeria na Ghana mwaka huo, akasema kwa kile alichokiona Afrika, angepata nafasi ya kuwa mshauri, wa Marais wa Afrika, angewashauri wawekeze kwenye Sekta ya Kilimo. Kwa sababu kilimo ni viwanda na viwanda ni kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwekeza kwenye kilimo, tutapata asilimia 100 ya mahitaji yote tunayohitaji ya kwenye viwanda, tutajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 100. Wanasema katika kipindi cha miaka 10 na 20 inayokuja, dunia itakuwa na upungufu mkubwa sana wa chakula. Bila shaka tukiwekeza kwenye kilimo, Tanzania itakuwa ni Taifa la kupigiwa mfano sana. Naishauri sana Serikali yangu Tukufu na Waziri wa Fedha ananisikia, tujinyime tufanye kila linalowezekana hatutakosa kitu tukiwekeza kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie tu, nasema kwa kile ninachokiona kinafanywa na Rais Dkt. Magufuli, Tanzania inaweza kuwa moja ya Mataifa ya kupigiwa mfano, siyo katika Bara la Afrika, lakini katika Dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kutuwekea msingi wa mjadala wetu. Kwa kweli tukienda hivi, kwa amani na salama, mtu anafikisha ujumbe wake vizuri bila tatizo, bila kukashifu wengine na kadhalika, safari yetu itakuwa ya amani vizuri. Kwa sababu Bunge hili halina nia ya kumzuia mtu yeyote kusema wala nini, lakini kufikisha ujumbe wa Kitanzania. *Whether* unapinga au unaunga mkono, zungumza kama Mtanzania. *(Makofi)*

Sasa anayefuata hapa ni Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na jambo ambalo limezungumzwa sana jana leo na tangu huko nyuma kuhusu udhaifu wa sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hawa wenzetu upande wa pili, katika bajeti ambazo tumekuwa tukipitisha hapa hawajawahi kusema 'ndiyo' hata mara moja. Kwa maana hiyo, wanataka kutuchelewesha kwa kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Kazi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na Waziri Mkuu na Mawaziri pamoja na wewe mwenyewe Spika ambaye unatusimamia kuisimamia Serikali, ni kazi nzuri sana. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo Waziri Mkuu amewakilisha hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo kwenye Jimbo langu la Makambaku, kwa namna ambavyo wananchi wangu wamekuwa wakilia juu ya kulipwa fidia kwa Soko la Kimataifa zaidi ya miaka 18; mwaka 2018 kupitia Ofisi hii inayosimamiwa na Mipango na Waziri, amelipa fidia zaidi ya shilingi bilioni tatu na kitu. Natoa shukrani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba kuna baadhi ya watu kumi na kitu hawakuwepo wakati wa uhakiki, naomba sana watu hawa walipojitokeza watu wa uhakiki walikuwa wameondoka. Kwa hiyo, naomba waweze kuhakikiwa ili nao waingie kwenye kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naiomba Serikali, kuna eneo pale pale Idofyu kuna mpango wa kujenga *one stop center,* sasa napo tunahitaji wananchi wale kulipwa fidia. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, kwenye mpango huu iweze kuwalipa fidia wananchi wangu wa Makambaku.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naishukuru Serikali kwa suala la umeme awamu ya tatu. Kwenye Jimbo langu natoa shukrani kubwa sana, najua na Watanzania wenzangu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni hivyo hivyo. Napongeza sana kwa namna ambavyo wananchi, wameweza kupata umeme katika maeneo yote ya Jimbo langu la Makambaku.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Serikali, kuna kijiji kinaitwa Mtanga ambako umeme umefika kule Kifumbe, pale ni kilometa tano, kimebaki peke yake; naiomba Serikali iwapatie umeme ili nao waweze kufaidi kama ambavyo wenzao wanafaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niishukuru pia Serikali kwa namna ambavyo imeweza kutupa fedha katika vijiji kadhaa kwa ajili ya suala la maji. Kwa kweli naishukuru sana. Ombi, tunataka kujua, fedha hizi za mkopo nafuu kutoka India ni lini mradi huu utaanza ili wananchi wa Makambaku waweze kufaidika na mradi huu mkubwa ambao utatatua

changamoto kubwa kabisa ya maji iliyopo katika mji wetu wa Makambaku na Kijiji cha Ikelu?

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa Diwani kwa miaka 10. Mpango wa afya kwa namna ambavyo Serikali imetoa fedha nyingi kwenye Vituo vya Afya, nami ni mmojawapo nimepata. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa dhati kabisa. Vile vile tumepata fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Rufaa ya Halmashauri ya Mji wetu wa Makambaku, shilingi 1,500,000,000/= na hivi tunakwenda vizuri, naishukuru sana Serikali kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi, tuna Kituo cha Afya ambacho tulikuwa tunakiita Hospitali ya Mji wa Makambaku, tupate *X-Ray* kwa ajili ya huduma mbalimbali katika mji wetu wa Makambaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa *TARURA* tunakwenda vizuri. Tunaiomba Serikali iongezee fedha upande wa *TARURA* ili barabara zinazounganisha baadhi ya kijiji na kijiji ziweze kupitika vizuri. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anayehusika; Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Rais mgombea wakati ule 2015 tuliahidiwa kilomita sita za lami katika Mji wa Makambaku. Mpaka sasa zimetengenezwa mita 150. Ombi langu ni kwamba barabara hii ya kilomita sita iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo. Amezungumza Mheshimiwa Vuai Nahodha hapa; suala la kilimo ni asilimia kubwa sana ya wakulima wetu na mbolea ambazo wanazipata ziko bei juu, haziwiani na mauzo ya mazao yanayozalishwa. Nini kifanyike?

Tunaiomba Serikali ione namna ya kusimamia bei ya pembejeo ili ziweze kupungua ziendane na uzalishaji wa kilimo, lakini vilevile tunaiomba Serikali ilete wawekezaji kwa ajili ya kujenga Kiwanda cha Mbolea ili mbolea hii iweze kuwa bei chini na izalishwe nchini kwetu hapa hapa.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tuna maboma ya Zahanati kwa nchi nzima. Kwangu peke yake kuna maboma ya zahanati zaidi ya 13 katika vijiji. Tunaiomba Serikali, katika mwaka huu wa fedha wa 2019/2020 angalau ione namna ya kutoa fedha nyingi ili maboma haya yaweze kupungua. Kila Jimbo angalau maboma matano au mangapi, tukifika 2020/2021 tunaweka tena bajeti maboma haya tutakuwa tumeyamaliza. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba Serikali iongeze fedha kwenye maboma haya.

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa kipindi kilichopita na leo naomba nirudie; mwenzangu amesema kwamba kiongozi wetu, Rais wetu ana maono makubwa sana, wote hapa tunakubaliana. Mipango hii mizuri iliyowekwa, nilisema hapa kwamba huyu anatakiwa aombewe awe Rais wa kudumu kutokana na mipango aliyoifanya. Sasa kama siyo hivyo, basi ili mipango hii iweze kukamilika vizuri, tuombe angalau aongezewe kipindi kimoja mpaka 2030 ili mipango yake aliyoipanga iweze kukamilika vizuri. Kama ni hivyo, mimi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, 2021 tutatembea nchi nzima, mimi nitakuwa wa kwanza kuwaambia Watanzania tumwombee aongezewe kipindi kingine ili akamilishe mipango na ndoto zake nzuri za maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni shahidi, hata kwenye Jimbo lako unaona namna ambavyo shughuli mbalimbali zinavyofanyika ikiwepo barabara, Vituo vya Afya, na kadhalika. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali na hasa Waheshimiwa Wabunge, tutakapofika 2021 tuanze kutembea kuwaambia Watanzania, kwamba tumwongezee kipindi kingine ili ndoto zake ziweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa ambao sasa wametoka humu ndani, watakuja tena hapa, watapinga hii bajeti ambayo tunaijadili hapa, lakini kwenye Majimbo yao wanahitaji huduma mbalimbali. Kwa sababu Rais wetu alisema maendeleo hayana chama, basi wananchi wapelekewe maendeleo, lakini isingekuwa hivyo, hawa

walitakiwa walambwe na viboko kabisa. Kwa sababu wamekuja hapa kuwakilisha kwenye Majimbo yao... *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, shukrani. Nilishamtaja Mheshimiwa Lijualikali atafuatiwa na Nyina Mtemi, Mama Anne Kilango Malecela.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Sikuwa nimepanga kusema haya maneno, lakini nitasema kidogo. Kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha sana kuona katika Bunge letu kuna Wabunge wana mawazo ya kufanya Rais aliyeko madarakani aendeleze kipindi ambacho kipo katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni jambo ambalo kama tunaweza kuruhusu Katiba yetu ianze kufanyiwa marekebisho makubwa kama haya na kama haya ndiyo mawazo ambayo tunayo, yaani CCM wote ninyi mlioko humu ndani na nje, yaani hamjaona mtu mwingine Tanzania nzima, kwa kweli ni masikitiko makubwa sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI**: Kwa hiyo, kwa kweli ni jambo la fedheha. Mimi binafsi nimesikitika sana.

**MBUNGE FULANI:** Haukuwa mpango.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI**: Aah, kwa sababu hata huo nao haukuwa mpango na alisikika, kwa hiyo, ni vyema mkanisikiliza tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anaongea, alizungumzia maendeleo mengi, mipango ya Serikali ambayo inafanywa na kwenye Sekta ya Barabara ya miundombinu akaizungumzia barabara yangu ya Ifakara Kidatu kwamba inaendelea vizuri na katika moja ya vipaumbele vya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hii barabara ya Ifakara – Kidatu, jambo la kwanza ni barabara ambayo inafadhiliwa na wafadhili mbalimbali na tayari mikataba yake imeshasainiwa na fedha zipo. Rais mwaka 2018 alikuja kule Ifakara, Kidatu akazindua, akaweka jiwe la msingi, lakini hii barabara ni kama vile haifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Spika, *site* yupo Mkandarasi, ni kweli, lakini huyu Mkandarasi ni kama hafanyi kazi yoyote, amekaa tu, analalamika fedha hapati, mambo hayaendi, mizigo yake na vifaa vyake viko kule Bandarini. Akiomba vitoke anaambiwa alipe kodi.

Mheshimiwa Spika, Bunge la mwezi wa Pili, Bungeni hapa niliuliza swali nikamwomba Mheshimiwa Waziri anayehusika twende Ifakara, Kidatu akaangalie maendeleo ya ile barabara na kwa nia, nami niliona kabisa alikuwa na nia njema akasema tutakwenda mbele ya kiti chako, wananchi wakasikia, Taifa likasikia, lakini ukimpigia simu hapokei, ukimtumia *message* hajibu. Sasa hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, ukimwangalia Rais Dkt. Magufuli, ukiwa makini ukamsikiliza vizuri, analalamika sana. Huyu Rais wetu amekuwa Rais wa kulalamika. Tena imefikia hatua analalamikia mpaka Mawaziri. Juzi hapa alisema Mawaziri ham-*communicate.* Sasa hii maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafikiri labda sijui kuna kitu Mheshimiwa Rais watu wanamtegea hawamuungi mkono, kwa sababu kama tuna Mheshimiwa Waziri anakubali atakwenda Jimboni kwenda kutekeleza kitu ambacho Rais wake alikwenda tena nchi nzima ikawa *live* kwenye *TV,* watu

wote wanaona kabisa, Mheshimiwa Rais anasema kabisa, “natoa miaka mitatu barabara hii iwe imeisha” na akasema fedha zipo.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kule kazi haziendi, Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba twende tukaone. Mheshimiwa Waziri hapokei simu, hajibu *message,* anaingia mitini. Maana yake nini? Sasa sijui ni kumgomea Mheshimiwa Rais, sijui ni maneno ya kampeni tu, sijui maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kweli kukomboa Taifa letu, kuna vijitabia kama hivi lazima tuviache. Sisi ni viongozi humu ndani, tabia hizi nami niseme kabisa kutoka moyoni, mimi Rais Dkt. Magufuli namwonea huruma sana. Mheshimiwa Spika ni shahidi, Rais Magufuli kila anaposimama ni kulalamika, anasema Wizara hii, Wizara hii, jambo hili, jambo hili, hili niliagiza, hili nilisema, hili nilisema, watu wote hawa hivi Rais wenu hamumpendi, mbona analalamika sana, ninyi manafanya kazi gani, mbona hamsaidii? Kila siku ni kulalamika tu yaani vitu ambavyo anatakiwa alalamike Mbunge, analamika Rais, mpo Mawaziri, kuna Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wote mpo. Nyie Magufuli hamumpendi ila tu hamsemi ukweli, kama mnapenda kwa nini hamumsaidii?

Mheshimiwa Spika, niombe, kama fedha za barabara hii hakuna mseme, hizi fedha hakuna, kama fedha zimeenda kwenye *Stiegler’s Gorge* mseme, zimekwenda *Stiegler’s Gorge,* kama zinafanya kazi mseme, watu wa Ifakara, watu wa Kilombero, watu wa Kidatu, watu wa Mkula, watu wa Sanje tumechoka. Tunahitaji barabara hii ijengwe, kama fedha hakuna mseme, sisi tumechoka jamani, mbona nyie mna raha, mnakaa kwenye lami sisi tumewakosea nini? Kwa upande huu nilikuwa na hili.

Mheshimiwa Spika, ukija kuangalia kwenye Wizara ya Kilimo, nimeangalia randama ya kilimo, lakini fedha ya pembejeo, hakuna. Rais Dkt. Kikwete ameondoka madarakani kwenye bajeti ya 2015/2016 aliweka bilioni 78, bajeti hii kwenye randama ya Wizara ruzuku ya pembejeo

*nil,* hata mia hakuna, yaani wanataka kuwaambia Watanzania kile ambacho Rais Kikwete alikifanya wao kwa miaka miwili wameshindwa tayari, yaani wameshashindwa. Mwaka 2016/2017 asilimia 89 ya bajeti ya Kilimo haikutoka, wamepeleka *only* 11, halafu sasa wanahuburi nchi inakwenda mbele, nchi inasonga, pembejeo tu zimewashinda, wataweza kweli.

Mheshimiwa Spika, kama Rais wetu hawamsaidii kumwambia ukweli kwenye haya mambo, hii nchi ilipofikia inategemea *with due respect* tunaongea hapa unasikia sauti za kunikejeli, *is not fair,* sisi tukifanya vitu kama hivi kidogo tu kama hivi toka nje, ondoka, lakini Msukuma na mwenzake wanaongea kejeli kabisa, *as if* mimi hapa naongea ujinga, lakini kwa sababu mnasema nchi ni ya kwenu, lakini nataka niwambie jambo moja CCM, hamtakaa hapa milele, hamtakaa milele, mtatoka na tutawatoa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali kidogo tu, utaratibu wa humu ndani unaongea na mimi, wewe hao usiwasikilize, wewe niambe mimi tu, utajikuta hugombani nao, endelea kuchangia ili dakika zako zisipokee.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, naongea na wewe na hata sisi wakati tunaongea na wewe, watu wanapofanya mambo kama haya, wewe unatakiwa unilinde, ni haki yangu kuwaambia wanyamaze niseme, lakini wewe kuwaachia *is not fair*.

**SPIKA:** Sasa nimekupa nafasi ya kusema na unapaswa kusema na mimi, badala lake unanifokea, unanifundisha si ndio hapo tunapokosana na ninyi ndugu zangu. Wewe umepewa nafasi changia hiyo bajeti, ongea na mimi usisikilize watu wangine, wewe ongea na mimi.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika ninachosema ni kwamba kama unahisi, kama unafikiri...

**SPIKA:** Hivi ngoja nikwambie, unajua kwenye Bunge hubishani na Spika mnafahamu, ndio haya yanafanyika,

kujua kwingi ndio tatizo, yeyote anayesimama hapa anaongea na Spika. Ongea na Spika kama una cha kuongea, kama huna cha kuongea, pumzika.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika naomba unisamehe kama ambacho nimekiongea, unadhani kwamba nimekufokea au nimekusema, sio lengo langu wala sio kusudi langu. Naomba unisamehe kwa hilo, lakini ambacho mimi namaanisha, naomba kwamba mtu anapoongea watu wote tuheshimiane. Hilo ndio ombi langu, naomba hili litusaidie ili twende vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nasema, ruzuku ya pembejeo 2000 kwenye randama ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, inaonekana ni *nil,* haipo. Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete aliondoka akacha bilioni 78, sisi miaka miwili tu ya Rais Magufuli akiwa madarakani, miaka miwili tu, wameshindwa kutenga bajeti ya pembejeo, maana yake wanawaambia wakulima kule mtaani, wapambane wenyewe. Sasa huko mtaani ajira hakuna, vijana hawajaajiriwa kwa 98%, kitu pekee labda ambacho kingeweza kuwasaidia kilikuwa ni kilimo na utaratibu wa nchi ulitenga ruzuku, wao wametoa, hawa watu wanafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, wanasema wanakwenda katika nchi ya viwanda, sijui nchi ya nini, mimi nimeangalia *style* nyingi, wakati wenzetu wanafanya *revolution* za uchumi, walianza na *agriculture revolution,* walianza kupata kwanza mazao, kilimo kikaimarishwa ndio viwanda vikaja, sasa kilimo kinakufa, wategemee kutakuwa na viwanda, vitatoka wapi? Hivyo viwanda vita-*feed* kitu gani? Yaani unakuwa na kiwanda cha nini kama hakuna *raw materials* na lazima kuwa na mkakati wa nchi. Kuna siku nilisema hapa *development* lazima kwanza ingalie watu na 89% au 80% ya Watanzania wapo kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika jambo ambalo naamini lilikuwa zuri ambalo pengine lilifanyika, ile sheria ambao tuliipitisha hapa ya tani moja kwa mkulima apite bila ushuru, wale wakulima wadogo kabisa, nilijua kwamba itakomboa

na *sincerely* kabisa naamini hivyo, lakini ukienda *field* wakulima hawa wanafanya nini? Wanafanyiwa nini, ni kweli kwamba ile tani moja wakipita hawatozwi ushuru? Ni kweli unakuta wakulima wanatozwa ushuru, vibibi, vimama, ambavyo wanalima heka moja, heka mbili kupata *substance,* tumetunga sheria hapa Bunge ya kazi gani? Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli alikuja Ifakara, nilimwambia kwamba Rais ile sharia, ile amri yako hapa haitekelezeki, akasema marufuku nchi nzima, nini kinafanyika? Wakuu wa Mikoa wapo, Mawaziri wapo, Wakuu wa Wilaya wapo, Serikali ipo, *as if* hamna mtu anayeona, yaani hatuumii.

Mheshimiwa Spika, jana ulisema hapa Lema alipata mkopo milioni mia sita na ngapi, ni kweli kapata kwa sababu hiyo ni haki yake, hawa wakulima wa nchi hii wanapata nini? Mbona hatuwapendi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nashukuru na Mungu akubariki, uendelee vizuri, ufanye kazi zako vizuri, ingawa Mwenyekiti wangu wa chama leo hakufanya kazi yake hapo ya kuwasilisha bajeti yetu ya Kambi, lakini kwa sababu alitoka Bungeni na wewe ukatoa ile amri yako, lakini anasikitika sana. Nashukuru. (*makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lijualikali. Hii ndio demokrasia tuliyonayo unaongea. Unaona umeongea kwa uhuru, nimekulinda, wamesema taarifa, nikawambia aaa, ukasema, umetoa nyongo yako vizuri, ndio Ubunge huo. Tunatumaini na wewe utakaa kidogo usikie majibu kidogo, huenda majibu mengine wanayo, sasa nyie shida yenu mnakimbia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mama Anne Kilango, tafadhali, atafuatiwa na George Malima Lubereje.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukumshukuru Mungu kwamba nimeweza kusimama katika Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ipo mbele yetu. Naomba nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya

kuchangia, lakini nimshukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametoa hotuba nzuri iliyosheheni miradi mingi ya maendeleo, iliyofanywa na Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukianza kusema kazi zilizofanywa na Awamu ya Tano utamaliza siku tatu unazungumza tu. Kwa hiyo, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano, nampongeza Rais na Mawaziri wote na Wakuu wa Mikoa, nchi inasonga mbele. Naona kila mtu ana mtazamo wake katika mambo. Baada ya Rais kufanya mambo mengi sana, kuna jambo sasa hivi ameamua kama mnaangalia mambo vizuri, ameamua kuweka misisitizo kwenye uwekezaji. Kwa nini nasema hivyo? Mheshimiwa Rais ameangalia vizuri akaona uwekezaji ndani ya nchi haujakaa vizuri, akaamua kuteua Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Angella Kairuki ambaye mimi namwamini sana, amempa Wizara hii na ameiweka chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa nini ameweka msisitizo kwenye Wizara hii ya uwezekezaji? Dira ya nchi yetu ni kwamba ifikapo 2025 tuwe tumefikia kuwa kwenye Taifa ambalo ni la uchumi wa kati, lakini tuliangalie Taifa la uchumi wa kati na tulipo. Ili tufikie kwenye uchumi wa kati, tunahitaji tuboreshe viwanda kwenye nchi yetu, lakini viwanda tutaviboreshaje, lazima tusimame imara kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ili Rais asisitize zaidi katika uwekezaji amewaita Mabalozi wote Ikulu akafanya dhifa, akala nao chakula, lakini akatoa tamko kwa wale ambao mnasomasoma magazeti, kwamba ni mwaka 2019 ni mwaka wa uwekezaji. Mheshimiwa Rais alizungumza kwa wale Mabalozi, lengo lake ni kwamba Mabalozi wote wachukue tamko lile kwenye nchi zao kwamba Tanzania imeamua mwaka 2019 ni wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba dakika zangu zote nichangie kwenye uwekezaji. Mimi ni Mwalimu ndugu zangu na Walimu tunaamini unafanya vizuri ukisimamia *specialization.* Nisingependa kuzungumza mambo mengi sana nitazungumzia uwekezaji na nitachangia kwa maandishi pia nikizungumzia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naifahamu nchi yangu vizuri na nimekuwa Bungeni hapa kwa muda wa kutosha. Tumezungumza sana kuhusu pamba na naomba Waheshimiwa Wabunge wanaolima pamba mnisikilize kidogo. Tumezungumza sana kuhusu zao letu la pamba, lakini nikiri bado hatajatumia pamba vizuri kwenye nchi hii. Kuna mikoa minne mikubwa inayolima pamba, Mkoa wa kwanza Simiyu, Mkoa wa pili Shinyanga, Mkoa wa Tatu ni Mwanza pamoja na Geita na wengine wanajaribu jaribu, lakini hii ndio mikoa minne inayolima pamba vizuri. Ukiangalia Mkoa wa Simiyu ukisoma vizuri utaona, Simiyu pekee inalima zaidi ya 40% ya pamba inayolimwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hapa nimezungumzia pamba ndani ya nchi, twende kwenye zao la pamba Tanzania katika Afrika na pia twende kimataifa. Tanzania katika kilimo cha pamba ni namba nane, inachukua nafasi ya nane katika nchi 30 za Afrika zinazolima pamba. Hiyo ni upande wa Afika, lakini Tanzania katika kulima pamba Tanzania inashika nafasi ya 22 duniani katika nchi 77 zinazolima pamba. Kwa hiyo, tunaweza Watanzania tukajipambanua kwamba tunalima pamba. Kama dunia nzima nchi zinazolima pamba zipo 77, Tanzania tunashikika nafasi ya 22; kama Afrika zipo nchi 30, Tanzania tunashika nafasi ya nane Waheshimiwa hatulimi pamba? Tunalima pamba.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kama Mbunge mzoefu kusema bado hatujatumia zao za pamba vizuri. Nilipomsikia Mheshimiwa Rais ametangaza 2019 ni mwaka wa uwekezaji, naomba Serikali waende wakajitikite kwenye kuwekeza kwa kutumia zao la pamba, kwa nini nasema hivi? Kwa sababu kuna nchi ndogo hapa Asia inatiwa Bangladesh, mnaifahamu, Bangladeshi hana umaarufu katika kulima pamba hata kidogo, soma vitabu vyote hana, lakini Bangladesh anaongoza kwa kuwa na *textile Industry,* anaongoza kutuvisha watu wote duniani. Mmarekani anauza nguo sana duniani, lakini viwanda vyote vipo huko Vietnam. Bangladesh ni namba *one,* anatumia pamba ya ku-*export,* sasa sisi tuko namba 22 duniani, tuko namba nane Afrika, tuna uwezo wa kufanya vizuri kama

Bangladesh na kumzidi. Hivyo, ni lazima Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji aende akamsaidie Mheshimiwa Rais, hakumchagua kwa sababu nyingine, amemwamini. Uwekezaji ndio utakaotupeleka kufika kwenye Taifa uchumi kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu katika uwekezaji iwapo Serikali wata-*invite* mataifa mengi kuja kuwekeza katika *textile Industry,* tutafika mbali, tutakuwa kileleni, tutafika mbali, nina imani kabisa. Naona vibaya kweli kale kanchi ka Bangladesh hakana umaarufu lakini kila nguo unayonunua Marekani *made in* Bangladesh, Bangladesh, Bangladesh, hawana umaarufu ni kanchi kadogo kenye takribani *square* mita laki moja hamsini elfu, kitu kama hicho, lakini kanaongoza duniani kwa kutuvisha mavazi ni *number one* akifuatiwa na China.

Mheshimiwa Spika, niinyenyekee Serikali, sasa ni wakati wa kusimamia uwekezaji, Mheshimiwa Rais amefanya vizuri sana tangu ameanza, jamani kuna ambaye hawatakubali? Rais anafanya kazi nyingi sana, sasa namwomba Mheshimiwa Rais kwa unyenyekevu mkubwa, nampigia na magoti, aipeleke nguvu yake kwenye uwekezaji na uwekezaji huo aende akaitumie pamba ya nchi hii, tutumie pamba ya nchi hii, tutafika mbali sana.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kusema sana kwa sababu nataka kusimama kwenye pamba na Mheshimiwa Waziri naomba niseme nachangia nitampelekea faili lenye *data* akamsaidie Mheshimiwa Rais kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono haja na nakushukuru sana. (*Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa Wabunge wazoefu huo ndio uchangiaji, yaani uchangiaji wa hapa asikudanganye mtu ni barabara, kisima changu pale, kilimo, zahanati, bado sijui maji, yaani Mbunge unachagua eneo moja au mawili *utmost* katika dakika 10. Dakika 10 Mbunge

unabaki ayeyeye, yeyeyeye, haiwezekani, yaliyobaki si unachukua karatasi, yaliyobaki ndio zahanati kule Nyanghwale sijui wapi, Nyanshimo sijui nini, hiyo sasa unampelekea Waziri vile vitu vingine vingine vile. Mheshimiwa Mbunge ukitaka watu wakuelewe hata mtu mwingine akiuliza, wote tuliokuwepo hapa, jana Mheshimiwa Anne Kilango alichangia nini Bungeni, utamwambia, alichangia kuhusu uwekezaji wa pamba, lakini wewe unayesema eeeh sijui nini, mtu aulize hivi jana, hata wewe ukiulizwa ulichangia nini jana, hata hukumbuki, sijui ilikuwa, niliongelea sijui nini na nini lakini hiari ya moyo. Kwa kweli ukipewa dakika tano, kumi kwenye *issue* yoyote utaongea machache yale ambayo unayaamini kabisa kwamba haya ndiyo msingi wa hoja yako, mengine yanaweza yakawa mifano na kadhalika. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mama Seneta kwa kutuwekea misingi lakini uhuru wenu jamani msiseme Spika kasema, uhuru wenu kutumia dakika kumi mnavyoona inafaa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mansoor Shanif.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru umenipa nafasi na mimi nisimame leo Bungeni hapa nizungumze. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya niweze kusimama kwenye Bunge hili Tukufu kuzungumza kuhusu hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti aliyowasilisha leo asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri sana ambayo inaifanya. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imesema mambo mengi sana, naomba nipongeze mambo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nipongeze Serikali kwa maamuzi ya kujenga reli ya kisasa ambayo ni ya historia, kwa Afrika nzima itakuwa ni reli ya kwanza ambayo inatumia umeme. Pili, ni *Surrender Bridge*

ambalo ni kero kubwa kwa wananchi kwa sababu ya msongamano wa magari. Kwa kweli hilo daraja pia litapunguza msongamano wa magari. Mambo mengi sana yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, tuna mradi wa *Stigler's Gorge* na sera ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala ambalo nitalichangia hapa ni ajira. Nchi yetu tuna changamoto kubwa sana ya ajira. Jimboni kwangu hata nchi nzima tuna changamoto ya ajira ni za aina mbili. Jimboni kwangu Wilaya ya Kwimba changamoto ya ajira ni kwanza ya wale vijana wanaomaliza *form four* ambao wanashindwa kuendelea na masomo kwa sababu hakufaulu kwenye mtihani wake au hana uwezo wa kuendelea na masomo.  Changamoto nyingine ni wale ambao wamepata digrii, wamesoma mpaka chuo lakini hawana ajira. Kwa hiyo, kuna aina mbili ya vijana ambao hawana ajira.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya ajira ni kubwa sana, natambua Serikali ina mipango mingi kupunguza kero ya ajira lakini kero ya ajira Jimbo la Kwimba ni kubwa sana. Mara nyingi utaona ajira zinatangazwa kwenye Mikoa na Miji mikubwa, vijana wa Jimbo la Kwimba hawana uwezo wa kufuta ajira hizo kwenye Miji mikubwa wanabaki pale pale, wanadumaa hawana pa kwenda.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ingefanya utaratibu wa kuwa na mpango mkakati wa kusaidia vijana vijijini ambao hawana uwezo wa kwenda mijini kutafuta ajira. Tuwe na mpango mkakati ambapo kuna mambo mawili, nashauri Serikali itusaidie Jimbo la Kwimba. La kwanza, tuna maombi ya miaka mingi sana tujengewe Chuo cha *VETA*. Vijana wengi ambao wanafeli masomo na kurudi nyumbani hawana pa kwenda kusoma wangeenda kwenye Chuo cha *VETA,* wangepata ufundi na wangejiongezea ujuzi wakajiajiri wenyewe wakasaidia familia zao. Hiyo ni kero kwa wananchi wa Jimbo la Kwimba ya miaka mingi sana. Eneo lipo, tunaomba Serikali itufikirie itujengee *VETA* itapunguza kero ya ajira kwenye Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, pili, tuna utaratibu wa kutoa asilimia 10 kutoka Halmashauri kwa ajili ya vijana, akina mama na walemavu hizo fedha hazitoshi hasa kwa sisi Wilaya Kwimba kwa sababu mapato ya Halmashauri yetu si kubwa sana. Ukiangalia Mkoa wa Dar es Salaam wana mapato ya shilingi bilioni ya 12 kwa vikundi vya akina mama, vijana na walemavu, sisi Wilaya ya Kwimba hatufiki hata shilingi milioni 300. Ukiangalia ukubwa wa Wilaya ya Kwimba ambayo ina majimbo mawili vijana ni wengi sana wanatafuta mitaji lakini mitaji ambayo inatoka Halmashauri haitoshi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itafute mikakati mingine ya kutafuta mitaji ya kusaidia vijana ambao wako vijijini kupata mikopo ili waweze kufanya biashara. Kusubiri fedha za Halmashauri ni ndogo sana, hazitoshelezi mahitaji ya wananchi au vijana wa Jimbo la Kwimba.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni changamoto ya maji. Jimbo la Kwimba tuna matatizo mengi sana ya maji. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana alifanya ziara kwenye Jimbo la Kwimba, aliagiza Serikali ya Wilaya na Mkoa kwamba kuna Mradi wa Maji wa Kijiji cha Shilima ambao unategemea kupeleka maji kwenye vijiji takribani 14, kata takribani tatu kwamba ukamilike ndani ya miezi mitatu lakini mpaka sasa maagizo ya Mheshimiwa Waziri bado hayajatekelezwa. Kwa unyenyekevu mkubwa Watendaji wananisikia, maagizo ya Waziri Mkuu hayajatekelezwa, naomba angalau wafuatilie ili yatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya afya, nashukuru Serikali kwenye Kituo chetu cha Afya cha Mwambashimba tumeletewa shilingi milioni 400, tumeongeza majengo matano, sasa hivi tutakuwa na *Ultrasound* na majengo ya mama na watoto. Naomba nichukue nafasi kuishukuru sana Serikali kwa mradi huu wa kuboresha kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Serikali kwenye Wilaya ya Kwimba, Makao Makuu yetu ambayo ni Ngudu

tuna Hospitali yetu ya Wilaya ambayo ilianzishwa kama Kituo cha Afya lakini tunakitumia kama Hospitali ya Wilaya tuna changamoto ya *X-ray*. Tuna *X-ray* ambayo ni ya zamani sana ambayo inatumia gharama kubwa sana na kila mara inaharibika na ni *analog,* tunaomba tupate *X-ray* ya kisasa ili tuweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia Hospitali yetu hiyo ya Wilaya hata mashine ya kufua nguo haina, tuna watumishi wanafua mashuka kwa kutumia mikono. Sasa kwenye Hospitali ya Wilaya mnaosha shuka kwa kutumia mikono kwa kweli sidhani kama inaweza kuwa ni salama.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mansoor Shanif. Sasa twende kwa Mheshimiwa Hamidu Hassan, amechelewa sana kuja, nianze waliokuja mapema, Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa, niseme mwanzo kabisa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, napenda niseme maneno machache ya utangulizi. Cha kwanza tunatoa pongezi kubwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa inayofanya. Sote tumeshuhudia Waziri Mkuu ametembea karibu mikoa yote Tanzania akifanya kazi kubwa za kuleta maendeleo ikiwepo kuhamasisha shughuli za maendeleo na usimamizi mzuri wa fedha za umma na hiyo imeleta ari kubwa kwa wananchi kuona kwamba Serikali yao inafanya kazi nzuri na kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna msemo unaosema Roma haikujengwa kwa siku moja, sasa watani zetu kila wakisimama

hapa wanasema jambo hili halijafanyika, tunakwenda polepole lakini katika miaka hii minne sote tumeshuhudia kazi kubwa ambayo imefanyika. Hivi tunavyozungumza Rais alikuwa Kanda zile za Kusini alikuwa anafanya kazi kubwa ya kuhamasisha maendeleo na kufungua miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ziko kazi kubwa zimefanyika ambazo zimeshazungumzwa na kwenye kitabu zimeandikwa kwa hiyo sina sababu ya kuzirudia lakini Watanzania wote wanaona kazi hizo. Napenda kuzungumza jambo moja kwa msisitizo sana nalo ni kilimo kwa ujumla wake. Watanzania wengi zaidi ya asilimia 70 wanategemea kilimo, sasa tunapozungumza kwenda kwenye uchumi wa kati na chenyewe kinatakiwa kibadilike, tupate ukombozi wa kilimo. Ili tupate ukombozi wa kilimo tunaelewa uchumi wa Watanzania, tunao wakulima wadogo wadogo wanalima kwa jembe la mkono na sehemu zingine wanalima kwa kutumia ng'ombe, kwa hiyo, hawawezi kujikombo katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba limezungumzwa suala la kuimarisha Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo. Napenda kushauri kwamba benki hiyo iimarishwe na tuione vijijini kwa sababu unakuta benki hizi zinanufaisha baadhi ya watu wa mijini ambao pia siyo wakulima. Kwa hiyo, benki hii ikifika vijijini tutaweza kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala zima la mazao ya kimkakati. Tumeona Waziri Mkuu ameweka juhudi kubwa kuhimiza kilimo cha pamba, korosho lakini pia alikwenda Kigoma kushughulika na mambo ya michikichi. Sasa uko umuhimu tupige kampeni kubwa sana kuimarisha zao la alizeti kwenye mikoa hasa ya kati ambapo zao hili linastawi.

Mheshimiwa Spika, pia tuangalie namna ya kuwasaidia hawa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo wanaokaa na mafuta barabarani. Waziri wa Viwanda aangalie namna anavyoweza kuwasaidia mafuta hayo yakakusanywa lakini yakawekwa kwenye mzunguko

yakiwa na viwango. Jambo hili tumekuwa tukilizungumza sana kwenye Wizara ya Viwanda tunasema kwamba mafuta ya kula yanatumia fedha nyingi za kigeni, jambo hili likifanywa vizuri tunaweza tukaokoa fedha za kigeni lakini pia tukainua uchumi wa Watanzania na Taifa letu likawa limekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukijikomboa katika sekta ya kilimo, tutakuwa tumepunguza pia umaskini. Kwa hiyo, dhana ya umaskini na yenyewe itakuwa imepewa suluhisho la kudumu. Tumeona juhudi mbalimbali zimefanyika, kuna mradi ule wa matrekta pale Kibaha, ingeangaliwa namna ya kuweza kusaidia wakulima wetu wa vijijini na pia tuweze kuwapanga vizuri ili waweze kulima maeneo makubwa kidogo na walime kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni sekta ya elimu. Tunaipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika. Sisi tunaotoka majimbo ya vijijini hiyo kazi tunaiona. Kwa hiyo, mtu anayesimama hapa Bungeni akasema hajaona kazi hiyo wengine sisi tunamshangaa.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa pamoja na kuendelea kutoa Elimu Bila Malipo yako mambo makubwa ambayo yamefanyika, kwa mfano, ujenzi wa maabara lakini baadhi yake bado hazina vifaa. Kwa hiyo, naomba vifaa vya maabara vipatikane, *technicians* na walimu kwa sababu tunasema elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Kwa hiyo, sekta ya elimu tukiimarisha tutaweza kupiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu bali iko mikoa na jamii ambazo ziko nyuma kielimu, kuna maeneo ambayo hata hayafikiki. Kwa hiyo, tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye tathmini na kuona maeneo hayo yanasaidiwaje na hizo jamii zinasaidiwa kwa kiwango kipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano rahisi tu, kuna pesa ambazo Serikali inatoa kusaidia kwenye shule kuboresha miundombinu lakini utakuta zile sehemu ambazo ziko nyumba hazipewi kipaumbele, unakuta mtu anacho halafu

anaongezewa. Nashauri utengenezwe mkakati wa makusudi ili kuwe na uwiano wa elimu na jamii zingine zisije zikaachwa nyuma.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo hilo, niipongeze Serikali kwa sababu Mkoa wa Singida tumepata kama shilingi 1.3 ambazo ziligawanywa katika kila Jimbo ili kufunika maboma. Hata hivyo, bado tunasisitiza kwamba Serikali iangalie namna ya kutenga pesa zaidi ili zile nguvu za wananchi zisiweze kupotea. Tumeona miradi kama hiyo ni mizuri sana, Mwenge umepata fursa ya kufungua miradi hiyo, viongozi wanakuja, Mawaziri, Waziri Mkuu, Rais, Makamu wa Rais wanapata nafasi ya kufungua miradi hiyo ambayo inasaidia kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya nishati, kazi kubwa imefanyika, tunapongeza upatikanaji wa vyanzo vya umeme, ujenzi wa *Stigler's Gorge,* Kinyerezi, Rusumo na maeneo mengine, kazi kubwa sana imefanyika na umeme huu ndiyo pia utasaidia viwanda. Kuna huu utekelezaji wa Mpango wa REA III wa usambazaji wa umeme vijijini na yenyewe imekuwa ni changamoto kubwa, yako maeneo ikiwepo Mkoa wa Singida ambao utekelezaji wake unasuasua sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa ujumla wake iweze kuangalia jambo hili, Waziri mhusika ameahidi kwamba atafika na tunaamini kwamba atafika ili umeme huo uweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo napenda niseme tu *comment* moja kwamba mimi kwa mtizamo wangu wako watu ambao wamepewa madaraka hawaisaidii sana Serikali kwa maana ya kwamba Mawaziri wanapokuwa wanafanya ziara, Mawaziri wa sekta zote, yanafanyika maandalizi mazuri na wanapofika pale wanapata taarifa nzuri lakini sasa wakiondoka utekelezaji wake unakuwa ni changamoto. Kwa tunaomba jambo hilo liweze...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Naam!

**WABUNGE FULANI:** Muda umeisha.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikwishamtaja Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Raza, twende Zanzibar kidogo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayofanya lakini niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la maji, maji ni uhai, maji ni maendeleo, maji ni uchumi wa nchi yetu. Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa tuna matatizo makubwa ya maji. Kuna miradi ya maji inayoendelea mpaka sasa lakini bahati mbaya sana imesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi niliuliza swali hapa kwamba kwa nini Serikali haiwalipi wakandarasi? Kuna miradi inachukua miaka kumi haijakamilika, kwa nini? Kwa mfano miradi kutoka Kijiji cha Bumila, Iyoma, Mima na Mnzasa, ni zaidi ya miaka kumi haijakamilika. Wakandarasi hawalipwi kwa nini na hapa Bunge tunapitisha bajeti, kama tunapitisha bajeti hiyo hela kwa nini isiwalipe wakandarasi? Kwa hiyo, nashauri wakandarasi wote nchi nzima walipwe ili miradi ya maji iendelee ili wananchi waweze kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni ujenzi wa Vituo vya Afya katika Majimbo yetu au katika Wilaya zetu. Hili ni jambo

jema, kwa sababu tunawasogezea wananchi huduma katika maeneo yao. Kwa sababu ukishajenga Kituo cha Afya, Wataalam kwa mfano Madaktari watakuwa pale, Manesi watakuwa pale hata hizo *minor operations* labla, mama ameshindwa kujifungua, kwa hiyo, zile *operations* ndogo ndogo zinafanyika pale badala ya kuwapeleka Hospitali ambako ni mbali. Kwa hiyo, hili ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa shilingi milioni 500, kujenga hivi vituo, lakini nilikuwa nashauri TAMISEMI mjitahidi basi, mtoe kila Wilaya angalau fedha kidogo za kujenga Zahanati. Tusiishie tu kwenye Vituo vya Afya, hapana. Tunaomba sana, kwa sababu Vituo vya Afya viko mbali na Vijiji vingine havina Zahanati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba pamoja na na kutoa shilingi milioni 500 kwenye ujenzi wa Vituo vya Afya, kwa mfano kama kwangu pale wamejenga Kituo cha Afya Mima na pale Jimbo la Kibakwe, pamoja na Pwaga. Kongwa vilevile wamejenga Kituo cha Afya pale, wamekarabati maana yalikuwa ni majengo ya zamani kwa hiyo, wamejenga mpya pale maeneo ya Mlali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru sana, ni mpango mzuri sana. Mjitahidi sasa mwanze mpango wa kutoa fedha kidogo kidogo kwa ajili ya ujenzi wa zahanati. Zahanati ni muhimu sana, hasa maeneo ambayo hayana huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, tunajenga zahanati; wananchi wameambiwa kila Kijiji kiwe na zahanati, lakini tatizo ni kwamba wahudumu hawatoshi kabisa. Lengo la Wizara ya Afya ilikuwa ni ku-*train* Watabibu Wasaidizi na Tatibu, yaani *Clinical Officers* na *Clinical Assistants,* lakini mpango huo umesimama na watumishi bado wanaendelea ni wale wale, ambao tunasema kwamba hawa *Medical Auxiliary* wanafanya kazi nzuri sana, lakini *Medical Auxiliary* amekuwa *trained* kwa ajili labla ya kugawa dawa na mambo mengine. *Medical Auxiliary* huyo ndiye atibu, huyo ndiye achome

sindano, huyo ndiye a-*prescribe* dawa. Kwa hiyo, inakuwa ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Afya mwendelee na utaratibu ule wa ku-*train* wale *Clinical Officers* na *Clinical Assistants* na kuwasambaza katika zahanati zote nchi nzima. Kwa hiyo, itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa ni Serikali kamili. Katiba Ibara ya (145), (146) inatambua kabisa kwamba tutakuwa na Serikali za Mitaa hapa Tanzania. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali jambo moja, mnapochukua vyanzo vya mapato vya Serikali za Mitaa, basi mshauriane na wale wenye vyanzo vile, itasaidia kuwapa ushauri. Juzi tumepitisha Sheria ya Kukusanya Kodi ya Majengo, ni jambo jema, hatupingi sisi, lakini Kodi ya Majengo *TRA* wakusanye mwaka mzima, halafu ukiisha mwaka ndiyo Halmashauri zianze kupewa fedha. Hiyo miradi ya Halmashauri itakuwa imesimama! Kwa nini?

Mheshimiwa Spika, maana yake miradi inatolewa taarifa *quarterly* kila miezi mitatu. Sasa fedha gani ukusanye halafu uziweke mpaka mwaka uishe?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri kwamba angalau wangejitahidi kukusanya miezi sita halafu wazipatie Halmashauri ili ziweze kutekeleza miradi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, sisi Wabunge tuko hapa miezi mitatu kwa ajili ya kupitisha bajeti ya Serikali, lakini jambo la kushangaza, bajeti tunayopitisha na fedha inayofikishwa kwenye Wilaya zetu na Mikoani, kuna fedha mahali pengine hata asilimia 50 haifiki. Ndiyo maana kunakuwa maboma. Kuna miradi mingi sana imelala tu, haijatekelezwa. Maboma ya shule, zahanati, yamelala wala hayatekelezwi kwa sababu fedha hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Bajeti ambayo tunapitisha Bungeni hapa, basi Serikali ijitahidi

kufikisha pesa mapema. Kwa mfano, kama Wilaya ya Mpwapwa imetengewa shilingi bilioni kumi, basi ziende shilingi bilioni kumi siyo zipelekwe shilingi bilioni nne, haiwezekani. Shilingi bilioni nne utatekeleza nini? Kwa hiyo, nilikuwa nashauri sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hali ya hewa katika Mkoa wa Dodoma. Wote ni mashahidi mnapita barabara hii…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hasa kule mwisho kule, sitaki kuwataja majina Waheshimiwa mliosimama na nini, mmeanzisha *club* huko, naomba make.

Halafu pili, naomba yaani wewe mwenyewe ukiona sauti imekuwa kubwa, unaanza kwa kushusha ya kwako kidogo. Tuelewane. Pia kuwa ma-*back bencher* siyo ruhusa ya kuwa ni vituo vya vikao visivyokubalika. Niendelee. Nyie mmenichonganisha eeh! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Lubeleje, endelea. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, niendelee...

Mheshimiwa Spika, la mwisho nimesema hali ya hewa. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Dodoma, kwa kweli mwaka huu hatutegemei kama tutavuna chochote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama tutakuja kuomba msaada Viongozi wa Mkoa wa Dodoma, msije mkafikiria kwamba wananchi wetu hawakulima, hawakufanya kazi, hapana. Mvua analeta Mwenyezi Mungu, lakini bahati mbaya mvua zimekatika mwezi wa Pili, mimea yote imekauka. Kwa hiyo, naomba sana, hili suala ni muhimu, lazima tupate chakula cha kutosha katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie na kama muda wangu bado kidogo, nimalizie la mwisho… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, niendelee!

**SPIKA:** Nakushukuru sana, inatosha. Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, dakika kumi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo iko mbele yetu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii. Naomba niseme kwamba naipongeza Serikali kwa masuala ya afya kwa kuhakikisha kwamba wameweza kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa katika kufunga vifaa vya kisasa katika hospitali mbalimbali hapa nchini, lakini zaidi kabisa kuweza kufunga mashine za kisasa za *MRI, CT-SCAN Digital X-Ray* na *Modern Ultrasound,* katika Hospitali ya Moi Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, nilisema tena wakati tumeletewa Mpango wa Bajeti na nikaiomba Serikali kitendo cha kuweza kufunga vifaa vya kisasa kwenye Hospitali ya Muhimbili kimeokoa sana sana watu wengi ambao walikuwa wanaumia na kupoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuweza kuimarisha huduma kwenye Taasisi ya Moyo ya JK Kikwete. Cha kwanza nipongeze sana utendaji mzuri wa Taasisi ya Moyo ya JK Kikwete. Kama hujauguliwa au hujaugua huwezi kujua

umuhimu wa Taasisi hii. Kama umeuguliwa au umeugua unaweza kuona umuhimu wa Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati *Director* wa ile Taasisi, Profesa Jinabi na Dkt. Kitenge na watumishi wengine wote na Madaktari wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kama unataka kwenda kujifunza huduma ya upendo wa dhati, huduma inayomponyesha mgonjwa kabla hajaipata, basi watumishi waende Taasisi ya Moyo. Kwa kweli, nisiposema haya, mawe yatasimama yatasema na nitaonekana sina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoiomba Serikali, baada ya kuhakikisha kwamba kuna huduma hizi za msingi kwenye ya JK pamoja na Hospitali ya Moi na maeneo mengine, naomba vifaa vya kisasa viende kwenye hospitali zote za Mikoa ya Tanzania, tuwekeze kwa mara moja. Serikali imesema iwekeza karibu shilingi bilioni 12. Ukiwekeza shilingi bilioni kwa mara moja kwa miaka zaidi ya kumi ijayo hujapoteza chochote. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwa makofi haya yaliyopigwa humu ndani kuhusiana na Taasisi ya Jakaya Kikwete, basi kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge tutaandika barua rasmi ya pongezi kwa Uongozi na Wafanyakazi wa Taasisi hiyo kuwapa moyo kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge wote. Endelea Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa hatua hizo. Naiomba Serikali tuhakikishe tunatafuta fedha tuwekeze kwenye vifaa tiba na vifaa vya kisasa kwenye Hospitali za Mikoa. Inakuwa ni ngumu mtu kutoka labda Ruvuma au kutoka Tabora mpaka Muhimbili kufuata vifaa hivi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwekeza kwenye hospitali zote za Rufaa za Mikoa, tukihakikisha tumeweza kuweka vifaa vya kisasa kuhakikisha tunakuwa na uchunguzi wa kisasa, tutaweza kupunguza idadi ya watu wengi

wanaokuja Muhimbili. Pia tutaokoa sana wananchi wetu ambao wengi walikuwa wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, leo tumeokoa gharama kubwa ambazo watu walikuwa wanaenda India na maeneo mbalimbali, lakini leo huduma ambazo zilikuwa zinapatika India leo ziko ndani ya Tanzania pale Hospitali ya Moi. Nashukuru sana kwa ajili ya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema kwamba inajenga hospitali katika maeneo mbalimbali, nami napongeza kwa hatua hiyo. Naomba juhudi ziendelee. Pamoja na kuwa tunaongeza vituo, katika hotuba Mheshimiwa Waziri amesema wameongeza vituo 441, lakini kwa *speed* ya ongezeko la Watanzania, *speed* yetu ni kubwa kweli kweli, tunaongezeka sana na niliwahi kuomba mwongozo hapa kwamba angalau tuweke *standard* ya watoto, Serikali ikasema imeachia *free* watu wazaane tu. *Speed* yetu ni kubwa sana. Kwa hiyo, tunavyozidi kuongezeka ndivyo mahitaji ya Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba bado *speed* ya kuongeza vituo vya iendelee kuongezeka. Nashukuru kwamba Serikali ilitoa agizo kupitia TAMISEMI miaka kama miwili iliyopita kwamba kila baada ya Kata mbili wajenge Kituo cha Afya kimoja. Sisi Kaliua tumeanza kujenga vituo vinne kwa mpigo. Tunaomba Serikali iongeze nguvu kwenye vile vituo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alipokuja Kaliua, alitoa shilingi milioni kumi kama mbegu kupanda kwenye Kituo kimoja cha Afya cha Usinge. Kwa hiyo, naomba Serikali isadie vile vituo ambavyo vimeanzishwa ili yale maboma yasibaki wazi, likamilike tuendelee kuongeza huduma za afya lakini pia kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imesema kwamba inaendelea kujenga hospitali, imekarabati hospitali nyingi na ina hospitali nyingi sana kwa ajili ya kujenga. Wilaya ya Kaliua

tunajenga hospitali ya kisasa ya Wilaya kwa fedha za ndani, iko karibu asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja ametupongeza, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametupongeza, Mheshimiwa Rais ametupongeza; naiomba Serikali iongeze nguvu pale kwenye ile hospitali. Tumemaliza jengo la *OPD,* la ghorofa tumemaliza, jengo la akina mama na mtoto la kisasa tumemaliza mwaka huu. Tunaiomba Serikali itusaidie, kuweza kujenga jengo la wanaume na jengo la uchunguzi ili huduma pale ziweze kufunguliwa, hospitali ile ifunguliwe kazi ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru sana. La pili, naomba niende kwenye suala la mifugo. Watanzania tumejaliwa kuwa na mifugo mingi, lakini kiukweli hatujaweza kutumia fursa ya mifugo Tanzania kuongeza pato la Taifa inavyotakiwa. Hiyo ni wazi kabisa. Leo mifugo yetu mingi inakwenda kunufaisha Taifa la nje. Mimi mwezi wa 12 nilienda Nairobi kwa kutumia basi, kupitia Namanga. Nimefika pale Namanga niliweka mikono kichwani, nimekuta malori tisa yamebeba ng'ombe, mbuzi, kondoo.

Mheshimiwa Spika, nikawauliza wale watumishi wa pale, wakasema huu ndiyo utaratibu, kila siku malori tisa au kumi yanakwenda Nairobi. Sasa nikawa nasema mifugo kuanzia ngozi ni mali, kwato ni mali, damu ni mali, kila kitu ni mali. Leo yale yote yanakwenda kutoa faida kwenye Mataifa mengine, sisi tunabaki tu tunaambulia ile kodi kidogo inayotolewa pale.

Mheshimiwa Spika, bado tunahitaji kufanya mambo makubwa sana kwenye Sekta ya Mifugo, hatujaweza. Leo Mikoa ambayo inazalisha mifugo kwa wingi hatuna viwanda vya kuchakata masuala ya mifugo. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alizindua machinjio ya kisasa pale Ruvu.

Mheshimiwa Spika, niiulize Serikali leo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tujue yale machinjio ya kisasa pale Ruvu ambayo yalipewa karibu shilingi bilioni mbili tangu

mwaka 2008 mpaka leo yamebaki ni magofu, nini kinaendelea pale?

Mheshimiwa Spika, lazima tuwekeze kwenye viwanda vya mifugo, lazima tuhakikishe kwamba rasilimali ya mifugo inanufaisha Taifa. Leo kwa baadhi ya maeneo ya Mikoa mingine, mifugo inaonekana ni changamoto, inaonekana ni kero na siyo fursa, wakati hii ni mali. Tunatumiaje uwezo wetu Watanzania wa kuwa watatu kiafrika kuwa na mifugo mingi kuweza kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwenye Sekta ya Mifugo tuhakikishe tunawekeza vizuri. Leo Tanzania nzima, nilikuwa nazungumzia habari ya viwanda vya *Tanganyika Packers*, ni historia. Viwanda vyote ni historia. Mwanza kulikuwepo na viwanda vya nyama, leo ni historia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, ili tunufaike vizuri na pato hili; mimi nilijaribu kupiga mahesabu ya haraka haraka: Je, pale Kenya kwa kupokea magari tisa kwa siku, wanapata nini? Sisi tunakosa nini? Hiyo ni mifugo, bado maziwa, wanachukua. Sisi tumekuwa ni *collecting Center.* Pale Arusha ambapo kuna mifugo mingi imekuwa ni *collection Center* wanakusanya wanapeleka Nairobi.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, tunakwenda kwenye uchumi wa kati, hatuwezi kwenda huko kama hatuwekezi vya kutosha. Ndiyo maana nashukuru sana mchango wa mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango, Sekta ya Uwekezaji, dada yangu Mheshimiwa Kairuki umepewa jukumu zito, ni lazima utumie nafasi hiyo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Rais alivyoweka hii Sekta chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hii Wizara iliyoko chini ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamjua utendaji wake wa kazi, tumwambie asimamie kikamilifu lakini walio chini yake wafanye kazi kikamilifu, wahakikishe wanaitendea haki Wizara hii. Hatuwezi kwenda

kwenye uchumi wa viwanda, kwenye uchumi wa kati kama hatujaweza kusimamiwa vizuri suala la uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano mmoja, kwanza tumekuwa wazito sisi Watanzania kwenye suala la uwekezaji na tumekuwa tuna vikwazo vingi, tumekuwa na urasimu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Nakuongezea dakika tano uweke vizuri uwekezaji huo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tumekuwa na urasimu ambao saa nyingine hauna tija kabisa, urasimu ambao unakatisha tamaa wawekezaji, urasimu ambao unafanya mtu anazungushwa mwaka mzima; amekuja na mtaji wake au anakopa benki anataka awekeze, mwaka mzima anapigwa dana dana, nenda rudi nenda rudi, ameshapata ardhi, anaambiwa mpaka *Environment Impact Assessment,* inachukua miezi sita, anaambiwa sijui hiki, miezi sita.

Mheshimiwa Spika, wale wanaokuja kuwekeza wanakata tamaa, hawawezi kuwaambia walioko huko kwamba njooni. Kwa hiyo, ni lazima tuweke *conducive environment* kuhakikisha kwamba mwekezaji anapokuja tunampokea vizuri, akiwekeza anapiga simu, njooni Tanzania inawekezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 ulitutuma kwenda *South Africa*, bahati nzuri tukapata bahati ya kumtembelea Balozi wetu wa *South Africa*, tukajaribu kumwambia mojawapo ya tatizo katika nchi yetu, hatuna wawekezaji. Vile vile kazi mojawapo ya Mabalozi ni kuwa na *diplomacy* ya kuvutia wawekezaji kwenye nchi yetu. Wewe umefanya nini kuhakikisha kwamba tunapata wawekezaji kutoka *South Africa*?

Mheshimiwa Spika, alisikitika sana, akatuambia ndugu zangu mimi nasikitika sana. Nimepata wawekezaji *South Africa.* Kwanza alipata wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza Tanzania kwenye mashamba ya kulima parachichi Iringa, ametuma barua *TIC* mwaka mzima hakujibiwa. Wale wawekezaji wamesubiri mwisho wamekata tamaa wameondoka zao. Akapata wawekezaji wengine hata ile ku-*reply* kwamba tumepata barua yenu jamani tuna-*respond, no response.*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji wawekezaji; lakini akapata wengine, akahangaika baba wa watu, kapata wawekezaji wa kuwekeza kwenye kiwanda cha ku-*assemble* Volkswagen hapa Tanzania, walitaka kuja hapa kuwekeza Tanzania. Walitaka kuweka kiwanda cha magari ku-*assemble Volkswagen.* Wamepigwa dana dana nenda rudi hawajibiwi; na wenzetu Wazungu wanakwenda kwa muda. Watu wana-*invest* kwa muda. Huwezi kuwa unataka uwekeze leo, unaambiwa kaingize mwakani. Mipango inabadilika, watu wanakwenda kwa malengo, ya jana siyo ya leo.

Mheshimiwa Spika, wamepigwa dana dana, Tanzania *Investment Center* imezubaa, haikujibu kwa wakati, wale wawekezaji wamekwenda kuwekeza kiwanda cha *Volkswagen* Kenya pale. Leo tayari uchumi ambao ungeingizwa na kile kiwanda kimoja cha *Volkswagen,* umekwenda Kenya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ni mifano hai, ni namna gani ambavyo hatutumii fursa kama Watanzania. Kwa hiyo, Sekta ya Uwekezaji ni sekta muhimu sana. Hakuna Taifa lolote duniani linaweza kuendelea bila wawekezaji usidanganywe na mtu. Ukiona leo China imeendelea, ni wawekezaji, Malaysia, Singapore, kila mahali, hata Nairobi hapa ni wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni lazima kama Taifa tuhakikishe kwamba tunaweka nguvu ya kutosha kwenye suala la uwekezaji ili lengo letu la kwenda kwenye uchumi wa viwanda, uchumi wa kati liweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la kilimo. Wenzangu wamechangia sana suala la kilimo, lakini kwa kuwa ni sekta muhimu sana kwenye uchumi wetu na hasa uchumi kwenda uchumi wa kati, kwenda uchumi wa viwanda, naomba nami niweke *inputs* zangu.

Mheshimiwa Spika, bado uchumi wetu hatujaweza kuwekeza kikamilifu. Nilikuwa nasoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema kwamba benki yetu ya *Tanzania Agriculture Development Bank* imeweza kukopesha shilingi bilioni 100. Mimi naona ni kidogo sana kwa wakulima wa Tanzania nzima, ni kidogo bado. Kwa sababu kuna watu ambao wana ekari 1000, kuna watu ambao wana ekari 2000 mpaka ekari 100,000. Ukiangalia hii shilingi bilioni 100 ni kidogo kwa watu hao, lakini tunataka ku-*transform* kilimo chetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE.MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Sakaya kwa kweli mchango wako *class one* pia, wanawake wanaweza kwa leo tunavyokwenda. *(Makofi)*

Kasema sijui wangapi wamesikia Kaliua pamoja na ule wizi mkubwa uliofanyika kule Kaliua lakini wanejenga Hospitali ya Wilaya kwa kauznai wao wenyewe na tayari wameeleza ni majengo ya aina gani ambayo wanajenga. Wengine ni Wabunge wenye Halmashauri zenye mapato makubwa kuliko wao lakini mnajenga nini? Sisi tukija hapa Waziri, nani, nani sasa wewe hapa kwanza anzia hapa, weka mambo sawa sawa sasa tunajifunza humu ndani miongoni mwetu.

Lakini pia hili la uwekezaji alilozungumzia Mama Kilango na Mheshimiwa unaona jinsi ambavyo tunaisaidia

Serikali yetu ni *direction* gani ichukue tupate mapato mengi zaidi, tukipata mengi zaidi tunaweza kumwambia Waziri wa Afya geuka kushoto, geuka kulia, songa mbele, kama kwenye kihenge hamna kitu utalia tu, hii kwa nini hii haijafanyika imekuwa, imekuwa, kwa hiyo nakushukuru sana nimesimama kwa kweli ku-*acknowledge* na uwekezaji huu tunaozungumza ni wa ndani na wa nje. Mheshimiwa amejitahidi kuuelezea tu ule wanje na mifano iko mingi kweli yaani inasikitisha kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Kidogo sekunde moja na mimi kidogo Waziri wa Uwekezaji, sheria zetu na vikwazo vyetu vya uwekezaji wawe wa ndani, wawe wa nje bado ni vilevile. Amesema *NEMC* miezi sita naweza nikapinga na wewe, ni *certificate* gani inayoweza kutoka ndani ya miezi sita? Hakuna. Ni mwaka, miaka miwili nani atasubiri muda mrefu namna hiyo? Nenda *EWURA* hivyo hivyo, wanakwambia uki-*lodge* kitu fulani hapa *60 days,* ukimaliza hicho ki-*lodge* cha pili *40 days,* nani yuko tayari na *60 days, 40 days? (Makofi/Kicheko)*

Tuangalie vile vitu vinavyochelewesha wawekezaji wetu wa ndani na wa nje na wawekezaji wa ndani hata wale wadogo wadogo ni wawekezaji pia. Inakwaza kweli kweli na mifano ni mingi wala hatuna haja ya kueleza sana mifano ni mingi sana na mingine hatupendi kusema hapa, lakini tunaomba hebu Serikali kama ni vikwazo vya kisheria mtuletee hapa tukwamue ule uwekezaji ambao Mheshimiwa Rais na Serikali yake anataka uweze kwenda kwa *speed* kubwa zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Ibrahim Raza nilikwishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hi kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ameisoma Bungeni leo hii asubuhi.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi zake mimi kusimama hapa nikiwa mzima. Nichukue

nafasi hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake iliyojaa busara na matumaini ya Watanzania. Kwa kweli naweza kusema katika timu aliyokuwa nayo Rais Mheshimiwa John Pombe Magufuli basi siyo vibaya tukampa Mheshimiwa Waziri Mkuu jina la mchezaji mashuhuri duniani kama Messi kwa sababu Messi kama anavyojulikana basi na Waziri Mkuu naye anafanyakazi nzuri sana kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze vilevile Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa sababu hayo maendeleo ambayo tunayaona katika nchi hii ni moja katika jitihada zake kubwa anazochukua kuwasaidia Watanzania wanyonge na ni mashahidi wetu Watanzania pamoja na sisi Wabunge kwamba kazi anayoifanya Mheshimiwa John Pombe Magufuli ni kazi kubwa sana na kwa kweli anastahili pongezi katika miaka yake mitatu hii amefanyakazi, *extra job* au *extra miles* amekwenda Mheshimiwa Rais, kwa kweli tuzidi kumuombea Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nije katika changamoto sasa katika Wizara hii au katika mambo ambayo yataweza kusaidia kutupeleka mpaka 2019/2020. Changamoto iliyokuwepo mwanzo kwamba ni ajira *(permit work). Permit work* imeleta vilio kwa wale wawekezaji. Wanapokuja watu wao kutaka kufanyakazi katika nchi hii basi kupata *permit work* imekuwa kazi ngumu sana na hii inarudisha maendeleo ya Mheshimiwa Rais. Kuna watu wanapanga hujuma ya kurejesha maendeleo ya Mheshimiwa Rais na sisi hatutakubali kuona hayo yanafanyika katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu nina ushahidi ya kwamba mtu ana kitega uchumi ambacho ame-*invest billions of shillings* halafu anaomba kupeleka *permit* yake ya *engineer* wake anakataliwa wakati katika kile kitega uchumi ana wafanyakazi 150 ambao wanategemea kupata riziki zao. Sasa kwa ajili ya mtu mmoja hiyo nafasi inakuwa inafungwa, wale wafanyakazi 150 ambao ni Watanzania wanakuwa hawana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka Wizara hii ambayo inahusika na *work permit* kidogo walegeze kamba, tusiwavunje nguvu watega uchumi wetu wanaokuja kuleta maendeleo katika nchi yetu ili vilevile Mheshimiwa Kairuki ambaye sasa ameteuliwa karibuni kuwa Waziri wa *investors protocol* ningemuomba na Mheshimiwa Kairuki atusaidie katika masuala haya kwa sababu ni moja katika kuleta maendeleo katika nchi yetu na kuwavutia wawekezaji na ninamuamini sana huyu Dada Kairuki atatusaidia katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine tukija katika masuala ya mawasiliano, mimi nashukuru kwamba *terminal III* imemalizika kwa *95 percent,* niishukuru sana Serikali, lakini kuna changamoto mbili, tatu katika uwanja wa ndege ambao sasa hivi tunatumia *terminal II.* Utakuta wale ma-*porters* ambao wanasaidia abiria ambao wanakuja nchini, hakuna hata *porter* mmoja ambao yupo uwanja wa ndege wote wameondolewa. Sasa nauliza kwamba watu wazima ambao ni walemavu au watu wazima watawezaje kuchukua mabegi yao kuchukua kwenye ile *belt* kutia kwenye *trolley* na kupeleka nje? Hii kidogo inaleta picha mbaya sana katika Uwanja wetu wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere ambao sisi tunatumia *terminal II* lakini tusijetukafanya makosa haya ambapo tunakwenda katika *terminal III* ambayo tunataka kuiboresha zaidi ili kuvutia watalii ambao watakuja nchini kutumia uwanja wa ndege wetu huu mpya ambao umekamilika kwa asilimia 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nataka wenzetu hawa wa *ATC* wajipange vizuri kwa sababu ushindani umekuwa mkubwa na wasipojipanga vizuri watakuja kuwa katika hali ngumu kutokana na haya mambo ya ndege inatakiwa mkakati maalum wa kupanga *programs* kwamba ndege ziende sehemu gani ili mapato ya nchi yaongezeke na kuinua Shirika la Ndege ya *ATC.*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lingine lipo katika Halmashauri zetu hapa nchini, Halmashauri nyingi sana katika mikoa mingi sana hazikufanya vizuri katika asilimia 10 ya

vijana, akinamama na walemavu. Kuna Halmashauri nyingine katika hizo asilimia 10 ya hizi pesa wanazipangia kuzitumia kwa kazi nyingine ambapo hizi asilimia 10 tumepitisha katika Bunge hili tukufu kwamba zinakwenda kwa vijana, akinamama na walemavu, sasa Halmashauri nyingi sana hazikufanya vizuri, lakini tunaomba Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi watusaidie kuhusu masuala haya ya asilimia 10 ili hii itakuwa ni changamoto kwa vijana, akinamama na walemavu katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nikija katika masuala ya madini, mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli katika kukutana na wadau wa madini ambao kwa kweli ameyatatua matatizo mengi sana. Lakini pamoja na kwamba Serikali imeweka mkakati maalum wa kuuza hizi dhahabu kwa kutumia utaratibu utakaotambulika, lakini bado madini yanasafirishwa nje kwa njia za panya. Bado dhahabu zetu, *Tanzanite* zetu zinasafirishwa nchi za nje kwa kutumia njia za panya.

Nilikuwa naomba sana wahusika ambao wapo katika *boarders* zetu wawe wanalifanyiakazi hili na mimi nitakaa na Mheshimiwa Waziri wa Madini ili nimpe changamoto ambapo mimi nafahamu vipi haya madini yanasafirishwa, kwa sababu tukiachia madini yasafirishwe, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakosa mapato mengi sana na sisi tuna kazi kubwa sana ya kuwapelekea maendeleo wananchi wetu ambao wengi ni wanyonge na wanategemea hizi pesa za maendeleo zifike katika shughuli za maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika kumalizia kwangu, katika kuwasaidia wafanyabiashara ambao wanataka kufanya biashara ambapo hiyo inaongeza changamoto, inaongeza mapato katika Halmashauri zetu, wenzetu wa *TFDA* na *TBS* kwa kweli wamekuwa na urasimu mkubwa sana, inavunja moyo. Mtu anataka kuanzisha biashara ya kuleta maziwa au kuleta dawa ya mbu, miezi mitano hajapata *report* kwamba anafaa kuruhisiwa kuleta au haruhusiwi. Sasa kwa kipindi cha miezi mitano inakuwa Serikali kwanza inakosa

mapato ya ndani, Halmashauri inakosa mapato. Kwa hiyo, wenzetu wengine wanataka kama kumuhujmu huyu Mheshimiwa Rais ambaye kwa kweli mimi siwezi kueleza mfano wake kwa kazi anayoifanya, anaifanya kazi kwa imani kubwa sana Mheshimiwa Rais na anataka nchi hii iendelee, isonge mbele lakini kuna watu makusudi wanamkwamisha.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanakuwa wanamkwwmisha Mheshimiwa Rais lakini watajibu kwa Mwenyezi Mungu wanajua wao. Lakini mimi naomba *TFDA* na *TBS* msiwakwaze wafanyabiashara ambao wana nia ya kuleta mali kuuza Tanzania. Hakuna urasimu wa miezi mitano, miezi sita sijawahi hata kuona katika nchi nyingine ambazo nimetembelea mimi sijapata kuona urasimu huo naona hapa tu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nichukue fursa nyingine ya kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana iliyojaa matumaini ya Watanzania na sisi *In Shaa Allah* Wabunge tutafanyanae kazi Mheshimiwa Wazitoi Mkuu kumsaidia kuona kwamba hii bajeti yake inapita na tunakwenda mbele mwaka 2020 na vilevile kumsaidia Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli ili kazi ya mwaka 2020 kushika hatamu Tanzania iwe kazi rahisi kwetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nichukue fursa hii vilevile niwapongeze Mawaziri wote ambao wako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, niwapongeze kwa jitihada zao wanazofanya na Mungu atawasaidia, lakini haya niliyoyazungumza nimeona bora nitoe changamoto hii ili tupate kusogea mbele siyo katika kumlaumu mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nakushukuru sana, ahsante sana, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Raza.

Waheshimiwa Wabunge nimepata taarifa hapa nadhani siyo wote mnafahamu kwamba mwenzetu

Mheshimiwa Riziki Lulida amefiwa na mtoto wake Hospitali ya Benjamin Mkapa leo, kwa hiyo kwa niaba yenu tunampa pole sana Mheshimiwa Riziki Lulida kwa msiba huo mkubwa wa mtoto wake, mazishi huwenda yakawa Dar es Salaam kesho, lakini kama kuna taarifa nyingine tutaendelea kuwapatia.

Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala nilikuwa nimekutaja.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:**Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia hoja muhimu iliyo mbele yetu. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kujielekeza katika eneo moja muhimu, nalo ni eneo la uwekezaji. Najielekeza katika eneo hili ili Tanzania tuweze kupiga hatua kuingia kati ya nchi zilizo katika uchumi wa kati kama walivyosema walionitangulia kwa vyovyote vile lazima tujitahidi tuhakikishe tunapanua uwekezaji, tunavutia wawekezaji wa ndani na wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa makusudi wa kuanzisha Kitengo cha Uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu, ni jambo muhimu sana na nampongeza sana. Na siyo tu kwamba kahamasisha kitengo hicho Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia kateua Waziri wa kusimamia sekta hiyo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Nimesoma kitabu kilichowasilishwa mbele yetu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikaona kwamba kutoka nje tumeweza kuhamasisha, kuvutia wawekezaji kwa ujumla wake kwa ndani na nje dola bilioni 1.84 lakini pia kwenye kitabu hiki kinatuonesha kwamba Tanzania tumeweza kuvutia kutoka nje kuja Tanzania uwekezaji wenye dola bilioni 1.18; kwa hiyo, kwa hesabu ya haraka haraka, nilipochukua ule

uwekezaji kwa ujumla tuliohamasisha wa jumla wa ndani na nje *1.84 billion US dollars*, nikaondoa dola bilioni 1.18 ambazo zimetoka nje, nikabaini kwamba ndani ya nchi tumeweza kuhamasisha uwekezaji *0.66 billion dollar.*

Mheshimiwa Spika, sasa takwimu hazina maana kama hujazifanyia tafsiri. Tafsiri ya haraka haraka ni kwamba wawekezaji wa ndani bado hatujafanya kazi kubwa ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani kwa sababu ili Tanzania tuweze kupiga hatua lazima pia tuwe na wawekezaji wa ndani ya nchi. Sasa ili tuweze kuongeza wawekezaji wa ndani ya nchi kutoka dola bilioni 0.6 angalau tupande angalau ifike dola bilioni moja au dola bilioni mbili lazima tufanye kila kinachowezekana siyo kuhamasisha tu wawekezaji wanaotoka nje, lakini pia na wawekezaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa moja ambalo umelizungumza vizuri ni kuhusu kuangalia hivi vikwazo vilivyopo na tukavifanyia kazi. Sote tunafahamu kwamba kwa muda mrefu Serikali imefanyakazi nzuri kupitia Wizara ya Biashara kuandaa ile *blue print. Blue print* inaonesha ni changamoto zipi zipo, ni mambo yapi yapo yanatakiwa kufanywa, lakini changamoto kubwa iliyopo ni kwamba ukiisoma ile *blue print* utagundua kwamba kuna mambo mengi yanahitaji kutungiwa sheria, kuna sheria nyingi zinahitaji kufanyiwa *rationalization,* sasa naomba kupitia kwako tuishauri Serikali ifanye kila linalowezekana ndani ya muda mfupi ituletee hapa Bungeni sheria zote zinazotakiwa kurekebishwa ili kuendana na *blue print* ambayo imeandaliwa vizuri na kwa muda mrefu ili hiyo *blue print* iweze kufanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ili tuhamasishe vizuri ndani maana Tanzania kama Tanzania tunasema Tanzania ni *gateway* ya Afrika Mashariki, lakini nichukue nafasi hii nitangaze ndani ya Bunge hili wakati Tanzania ni *gateway* ya Afrika Mashariki, Wilaya ya Misenyi na Jimbo la Nkenge ni *gateway* ya Tanzania kwenda Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji ambaye nimemualika tarehe 05 Julai,

2019 aje kuwa mgeni rasmi katika kongamano kubwa la kimataifa la kutangaza uwekezaji na amenikubalia namshukuru sana na nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu ukisikia Mheshimiwa Waziri Angellah naomba kwenda Misenyi kufanya kazi hiyo umruhusu aje aifanye kwa sababu ni kazi muhimu sana katika kuvutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii nitoe jambo moja la tahadhari. Sote tunafahamu hali ya hewa si nzuri sana kwa sasa, katika maeneo mbalimbali hali ya mvua haikwenda kama tulivyotarajia lakini tuna *National Food Reserve Agency* taarifa tulizonazo na za uhakika wana tani kati ya 78,000 mpaka 100,000 za chakula tu. Kwa takwimu tulizopewa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza vizuri tu kwamba Tanzania tumezalisha tani milioni 16, matumizi ni tani milioni 13, kwa hiyo, tumebakiza *surplus* tani milioni 3.32.

Mheshimiwa Spika, hali ya hewa isipokuwa nzuri kama ambavyo imeanza kuonekana maana yake tutakuwa na upungufu wa chakula ndani ya nchi. Kama itakuwa hivyo litakuwa jambo la hatari kama huyu *National Food Reserve Agency* ataendelea na mipango yake ya kuuza *reserve* kidogo ya chakula aliyonayo ili kuweza kupata fedha ya kuongeza *reserve* ya chakula. Kama una tani 78 kama *reserve* unataka uuze hicho ili upate fedha za kununua kingine ni changamoto. Nichukue nafasi hii kuomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ajaribu kuliangalia eneo hilo ili tuweze kujipanga vizuri kwa sababu ukishakuwa na matatizo ya chakula hata upange mambo yoyote yale hayawezi yakaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niipongeze Serikali kwa sababu imetoa tangazo maeneo mbalimbali ya Ranchi za Taifa ambayo yalikuwa hayatumiki vizuri sasa yapate wawekezaji wapya, ni jambo jema. Hata hivyo, natahadharisha wale wawekezaji walio wengi wameshindwa kuwekeza kwa sababu ya migogoro mingi kutokana na ukweli kwamba ranchi hizo zilivamia vijiji na kwa hivyo mara kwa mara wawekezaji hao wamejikuta kwenye migogoro ya

muda mrefu na migogoro hiyo haijaisha. Kwa hiyo, hata Serikali ikitangaza upya ikapata wawekezaji wapya bila kumaliza migogoro iliyopo yatakuwa yale yale. Kwa hiyo, nishauri tu kwa nia nzuri kwamba ile Kamati iliyoundwa ya Mheshimiwa Rais ifanye kazi yake na ihakikishe ranchi inabaki tu maeneo yake na vijiji vyetu waachiwe wananchi ili hizo ranchi mpya zitakazotangazwa zisianze na migoogoro.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Diodorus Buberwa Kamala. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze kwa shukrani na kupongeza hatua ya Serikali ya kutatua tatizo la umeme kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kiukweli kabisa mimi nimekaa kule karibu miezi miwili sikuwahi kushuhudia hata siku moja umeme ukiwa umekatika tena kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambasamba na hilo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati atusaidie, najua Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja mwezi Februari katika Mkoa wa Lindi na alisema kwamba mkandarasi wa *State Grid* anafanya kazi zake taratibu sana, yuko *very slow.* Ni kweli kabisa katika Jimbo la Mchinga nakotoka mimi katika kipindi chote cha *Phase II* na *III* huyu mkandarasi hajawahi kabisa kuonekana. Viko vijiji ambavyo vimeingia kwenye mradi lakini miaka yote tangia 2016 mpaka leo 2019 hajawahi kuleta hata nguzo moja.

Kwa hiyo, naomba jambo hili lichukuliwe kwa kipaumbele sana kwa sababu hivi vijiji viliingia kwenye mradi na tulishawaeleza wananchi na wananchi wamejiandaa kwa siku zote kusubiri umeme lakini umeme haufiki. Kwa bahati mbaya sana wakienda kwenye vijiji jirani ambako umeme unafika wanaukuta na haukatiki. Tuna umeme wa uhakika sana lakini kuna vijiji ambavyo havijapata hiyo stahiki ya umeme…

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji, huyu *State Grid* anayemzungumza hatufahi kabisa kwa Mkoa wa Lindi kwa sababu mimi kwenye Jimbo langu la Liwale ameweza kuwasha umeme katika vijiji viwili kwa muda wa miaka miwili sasa. Kwa hiyo, huyo mkandarasi hatufai.

**SPIKA:** Unaipokea taarifa hiyo Mheshimiwa Bobali?

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimeipokea taarifa hiyo. Ni kweli Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi tunamlalamikia mkandarasi huyu na hata Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira Mgalu alikuja na yeye akamlalamikia.

Mimi nafikiri ifike wakati hatua zichukuliwe kwa sababu kama mkandarasi yuko *site* miaka mitatu hajawahi kwenda hata kwenye kijiji kimoja kupeleka nguzo mkandarasi huyo hafai, lakini siku zote yupo, ukifika Lindi pale Mkoani unamkuta, ana makabrasha yake, kubwa analokuambia sijalipwa, lakini taarifa za Serikali zinasema kwamba amelipwa. Naomba sana Serikali walichukue hili jambo huyu mkandarasi kwa kweli hatufai kabisa watubadilishie watupatie mkandarasi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia juzi nimemsikia Mheshimiwa Rais akiwa Mkoani Mtwara ametupongeza Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara namna tulivyosimamia na namna tulivyolisemea zao la korosho. Nashukuru kwa sababu Mheshimiwa Rais ame-*recognize* juhudi yetu ambayo tulikuwa tunaifanya ndani ya Bunge na sisi tunashukuru na tunapongeza kwa hatua zilizochukuliwa na Serikali kulipa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili la mwaka huu liwe fundisho kwetu wote. Kwenye suala la korosho kuna changamoto nyingi sana. Nafikiri Mheshimiwa Rais mwenyewe amejionea na zingine amekuwa akishangaa kama zinatokea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako watu wengi wamekatwa fedha zao, mtu badala ya kulipwa ile fedha yake halali analipwa anakatwa Sh.300. Yako maagizo mengine Mheshimiwa Rais ameyatoa lakini nachosisitiza jambo lililotukuta kwenye msimu wa korosho uliopita liwe fundisho kwetu sote. Jambo hili kwa kweli limetupotezea fedha nyingi. Mimi nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais ame- *recognize* na ametambua juhudi zetu namna Wabunge tulivyolisemea zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambasamba na hilo kuna zao la ufuta, ndiyo ile hoja ya uwekezaji ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa, ufuta unalimwa kwa wingi sana Mkoa wa Lindi. Ukizungumza na matajiri wanasema ule ufuta wa Lindi ambao kwa jina unaitwa *Lindi White* ni ufuta bora sana kwa sababu una mafuta mengi. Mafuta ya ufuta ni miongoni mwa mafuta bora na ni mazuri yanatumiwa na watu wenye fedha zao. Hapa Tanzania sidhani kama tuna kiwanda cha kukamua mafuta ya ufuta. Ufuta wote ambao unazalishwa kwenye nchi hii unasafirishwa kupelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa naposema tayari wakulima wanakaribia muda wa mavuno, najua tayari matajiri wameshajiandaa kuja kuchukua ufuta, tunapoteza fedha nyingi sana za kigeni kuagiza mafuta ya kupikia, kwa nini tusifanye mpango ufuta unaozalishwa ukawa umewekewa utaratibu pale Lindi tukapata kiwanda cha kukamua mafuta, tukaongeza ajira, kuna tatizo kubwa la ajira ingesaidia pia kupunguza tatizo la ajira la vijana. Kwa hiyo, hili jambo la uwekezaji ni muhimu sana na nashukuru umekuwa ukisimama zaidi ya mara mbili kulisisitiza. Jambo hili linahitaji lichukuliwe kwa tahadhari kubwa sana kwa misingi ya kutaka kupata maendeleo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai pia viongozi wetu, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wasifanye *harassment* kwa wawekezaji. Kuna jambo la kusikitisha lilitokea hivi karibuni katika moja ya Mikoa ya Kusini mwa Tanzania, Mkuu wa Mkoa anaonekana anaweka ndani mwekezaji, anachukuliwa anasekwa mule, mambo kama haya yanaharibu taswira nzima ya uwekezaji na mtu mwingine ambaye alikuwa ana nia ya kutaka kuja Tanzania hawezi kuja. Kwa hiyo, jambo hili lazima lichukuliwe kama ni *sensitive* na iwe ni ajenda ya Taifa kwamba tunakwenda kwenye kuvutia wawekezaji, sheria zibadilishwe, miongozo iwekwe sawa ili wawekezaji warahisishiwe namna gani wanaweza wakaja wakafanya shughuli zao vizuri kabisa lakini bila kubuguziwa, kuwekwa ndani saa 24 na kadhalika. Mambo haya kwa kweli yanatutia doa wote.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali kwa mchango wako mzuri sana. Sasa ni zamu Mheshimiwa Anatropia atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Edward Mwalongo ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushuruku kwa nafasi hii. Nichukue nafasi hii kutoa masikitiko yangu kwa niaba ya Kambi yetu kwamba hatujaridhishwa na mambo mengi. Napenda kutoa hayo masikitiko yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna mchango kutoka kwenye hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambao nimeambiwa tumepewa humu ndani na nitaeleza. Sisi kama Kambi ya Upinzani au kama CHADEMA hatujaridhishwa na mwenendo wa Tume ya Uchaguzi ambavyo imekuwa ikifanya kazi zake. Kumekuwa na upungufu mkubwa sana katika Tume ya Uchaguzi ambayo kimsingi tunaiona kwamba Tume haiko huru. Inasikitisha kwamba tuko kwenye nchi ya kidemokrasia, tuna *referee* ambaye anapaswa kuwa Tume huru ya Uchaguzi na badala yake siyo Tume huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, tuna Tume ambayo Mwenyekiti wake ni mteule wa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa chama fulani. Tunajiuliza, je, wengine wanafanyaje? Ni kwa nini yule ambaye ni Mwenyekiti wa chama ndiyo anatuchagulia refa ambapo sisi wengine hatuko kwenye chama chake? Kama hiyo haitoshi kwa maana ya muundo wa Tume, uongozi wake, Mwenyekiti wake, wasaidizi wake, Makamishna wanajikuta ni wateule wa Mwenyekiti wa chama fulani, *automatic* wanapoteza kile kinachoitwa kuwa huru katika kusimamia mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sisi wote hapa tumekuwa tunashangilia ukitaja Simba au Yanga, ukimwambia *referee* ana maslahi na Yanga na aende kuchezesha mechi ya Simba watu wataandamana usiku kucha. Ni kwa nini sisi tuone ni *fair* tunakuwa na Mwenyekiti ambaye anaenda kupiga kipenga, ambaye anapaswa kusimama katika lakini ni mteule wa chama fulani.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, tuna wasimamizi wasaidizi...

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu kumpa taarifa mchangiaji kwamba Tume hii ya Uchaguzi na uteuzi wa viongozi wote waandamizi wa Tume iko kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hii kwa uhalali huo huo iliweza pia kumtangaza hata yeye Mheshimiwa Anatropia kuwa Mbunge na yuko ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wako ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niendelee tu kumkumbusha Mheshimiwa Anatropia anapodai kwamba Tume hii siyo huru ina maana basi hata Ubunge wake yeye sio halali. Kama Ubunge wake ni halali na yuko ndani ya Bunge basi Tume hii imeendelea kufanya kazi yake kwa maadili na kwa kuzingatia Katiba na kwa sababu hawa viongozi wote wako kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Theonest pokea hiyo.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nadhani siyo lazima niipokee, kuna msemo wanasema *the means justify the end* na mimi ndiyo nachoeleza leo na kwenye Kambi yetu tumeshauri tulete hapa mabadiliko ya sheria husika tuwe na Tume huru. *The means justify the end.* Kama unavyonileta hapa Mbunge wa CHADEMA unategemea nitakaa kutetea CCM? Amekuja hapa Msajili wa Vyama vya Siasa ameshangiliwa sana na kuna mtu mmoja aka-*post* sitamtaja jina akasema wale ambao hamshangilii shauri yenu, hiyo inaonesha *to what extent* ile *level* ya *independence* ipo *questionable, the means justify the end. (Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, angekuwa ni huyo ambaye wewe unasema awe angeshangiliwa ingekuwa ni mbaya? Sioni uhusiano wa kumshangilia mtu na *role* yake, endelea tu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pili, tuna Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kwa maana ya Wakurugenzi wa Halmashauri kwenye Wilaya zetu. Ukiangalia *composition* ya watu wengi *majority* tunaweza kutaja hata majina wameshiriki kwenye kura za maoni za Chama cha Mapinduzi, baada ya kuachwa ndiyo wameenda kuteuliwa kuwa Wakurugenzi, *to what extent* wale watu wanaweza kuwa *so independent?* Hiyo yote inaleta *questionability* ya Tume *whether* ni huru au siyo huru.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi kuna *funding* yenyewe ya Tume, tuna Tume ambayo inategemea busara

za Mwenyekiti kwa maana ya Mheshimiwa Rais hatuna namna ambayo tunaweza ku-*finance* Tume yetu zaidi ya kutegemea ...

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ruksa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tukiendelea kuacha haya maneno yatakuwa yanachukuliwa kama ni maneno sahihi lakini si kweli. Kwenye hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunayo *Vote* maalum kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi na inatengewa bajeti na Bunge lako kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya Uchaguzi inapofika kwenye suala la uchaguzi, kisheria na Kikatiba fedha za uchaguzi zinatolewa na Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ni lazima atenganishe hayo mambo mawili, tusiendelee kuacha watu wanazungumza tu vitu ambavyo wakati mwingine siyo vya kweli. Vinginevyo nitakuja kuomba kanuni ya utaratibu na mwongozo ili Mheshimiwa Anatropia athibitishe kama Tume hii inapewa fedha kwa hisani. Tuna *Vote* hapa tutaipitisha na fedha za uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Katiba zinatengwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, taarifa nimeipokea lakini *amount* inayokuwa *allocated* kwenye *Vote* inaamuliwa na nani? Tutakuja hapa tutaongea, inaamuliwa na nani?

Mheshimiwa Spika, tunakuja kwenye uandikishaji wa *BVR.* Kumekuwepo na changamoto ya uandikishaji wa *BVR*

tunakumbuka 2015 lakini hebu tuangalie tangu 2015 ni mara ngapi imekuwa *updated* na tumekuwa na chaguzi ngapi zilizofanyika hapa katikati. Ina maana *assumption* ni kwamba wale waliojiandikisha 2015 ndiyo bado wana *exist* kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ni kwa nini haiwi *updated* na kwa nini tunaendelea ku-*maintain* kwamba wale watu bado wako wote lakini wale ambao hawapo kwa nini hawatolewi na waliofikisha miaka 18 wako *eligible* ku-*vote* kwa nini wanakuwa hawaingizwi kwa wakati. Hiyo pia inatilia shaka uhuru wa Tume huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, tuje kwenye suala lingine, Tume imeendesha chaguzi kadha wa kadha na nyingine zimekuja hizi mpya za *voda faster* ambazo hazioneshi uhalisia. Uhalisia wa uchaguzi unauona kwenye mchakato husika. Mchakato wa kwanza ni pamoja na watu kuchukua na kurudisha fomu, tuna wagombea niongelee Korogwe, mgombea amepiga kambi kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Msaidizi wa Uchaguzi siku nzima, Mkurugenzi hatokei na *deadline* imefika na unaambiwa amekosa vigezo kwa sababu hajarudisha kwa wakati. Unaweza ukaona ni michakato ambayo inakuwa *manipulated* makusudi sijui ni kwa nia gani kwa sababu nchi inayoamini kwenye demokrasia nikiingia kwenye uchaguzi naamini nitashinda au utashindwa lakini ikifikia wakati mna mifumo ambayo haipo *independent*...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Unajua Mheshimiwa Anatropia unajiweka kwenye eneo ambalo nashindwa hata kukulinda lakini umechagua mwenyewe kujiweka kwenye eneo hilo ndiyo linakupa shida kidogo. Duniani hapa kama huyo mgombea wenu alipata matatizo fulani si alikuwa aende Mahakamani tu. Sasa ukituambia sisi Bunge hapa tufanye nini? Kama alifanyiwa jambo ambalo siyo sawa angeenda tu Mahakamani. Hizi taarifa unayosikia na nini wala yasingejitokeza. Endelea tu kuchangia muda bado ni wako, mtunzieni muda wake.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ushiriki wa vyombo vya dola na kwa kiwango kikubwa katika mchakato mzima wa uchaguzi, tukianzia kupiga kura na kutangaza matokeo. Unaona nguvu kubwa inatumika lakini kama haitoshi kuna *incidence* ambapo Polisi wamekimbia na maboksi ya kupigia kura, imetokea Kinondoni. Nayaongea haya kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiyo msimamizi anapaswa kukumbusha watu wajibu wao, anapaswa kuangalia, je, taratibu zinafuatwa na kama hazifuatwi yeye ndiyo anasimamia. Ninaongea kwenye hotuba yake kwa sababu yeye ndiyo mtu anayehusika katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mauaji na ugomvi mbalimbali, tuna Katibu wetu wa Kata ya Hananasifu aliuawa katika uchaguzi wa Kinondoni mpaka leo hatupewi taarifa uchunguzi umefikia wapi na aliuawa kwa nini? Hayo ni maswali ya kujiuliza, kama tuliamua ku-*embrace* demokrasia na tumeamua kuiweka pembeni na kucheza na mifumo tuliyonayo kwa ajili ya kupata matokeo, tunaiweka nchi yetu katika mazingira ambayo siyo sahihi. Tunaiweka nchi yetu katika mazingira ambayo sisi wenyewe tunai-*push* ambako wengine hawataki kwenda.

Mheshimiwa Spika, kugoma kutoa viapo vya Mawakala, huo ni mchakato wa kawaida wa uchaguzi, inakuwaje Wasimamizi Wasaidizi, Maafisa Watendaji wasitoe viapo kwa wakati? Kwa nini chama kimoja kipewe na kingine kisipewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naweza kuongea mengi, lakini mnapaswa kujua, kama tunaingia kwenye mchezo, naamini mnajinasibu kwamba Serikali yenu inafanya vizuri, imepeleka miradi, imepeleka maji, imepeleka shule, hebu twende kwenye uwanja sawa wa uchaguzi, tuwaache Watanzania wachague kati ya mliyoyatenda na sera zetu. Kati ya mlichowapelekea na sisi tutakachokuwa tunawaambia, kuliko kubaki nyuma kutumia vyombo vya dola vilivyopo, kucheza na Tume, kucheza na mfumo kwa ajili ya kupata

matokeo. Tuacheni, naamini mmefanya mazuri, twendeni tukapige jaramba, wananchi wenyewe wataamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye hoja yangu ya pili, naongelea uminywaji au mifumo ya utoaji haki isiyoridhisha. Leo kupewa dhamana katika Kituo cha Polisi au Mahakamani nimekuwa ni hisani siyo tena haki. Nitatoa mfano wa kilichomtokea Mwenyekiti wa CHADEMA, Mheshimiwa Aikaeli Mbowe. Sitaeleza chote kilichotokea, lakini Jaji Rumanyika alisema, kilichofanyika katika shauri hili ni sawa na kuchukua mzigo ukaufunga mbele ya mkokoteni, kwa maana ni mambo ambayo ni ya aibu. Akasema, masharti ya kufuta dhamana yanapaswa kuwa magumu kuliko masharti ya kutoa dhamana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Theonest, unajua unachojadili ni mambo ya Mahakamani ambayo tena kesi yenyewe bado inaendelea na pia, Jaji wa Mahakama ya juu anakosoa vitendo vya Mahakama ya chini yake. Sasa unataka Bunge tuingiliaje? Endelea tu Mheshimiwa Theonest, naona leo kidogo haujajipanga vizuri.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa kinachopaswa kusimamiwa. Ninaeleza kilichotokea, ninaeleza wajibu wetu kama watunga sheria. Ninaeleza umuhimu wa kutoa haki kwamba, ukienda Magerezani wamejaa watu ambao wangeweza hata kupatiwa dhamana tuka-*save* fedha nyingi za Serikali kuliko kuendelea kuweka watu ndani.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo kupandikiza kesi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naambiwa ni kengele ya pili, lakini kwa kuwa ulikatizwa katizwa sana, nakuongeza dakika tatu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kumekuwepo tatizo la Polisi kubambikiza

kesi kwa wananchi likiwepo suala zima la *money laundering.* Sasa hivi ndiyo umekuwa mtindo wa kisasa. Ukitaka kupigwa kule ndani na usitoke, kesi unayobambikizwa ni ya *money laundering* ambayo upelelezi wake unachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuangalie hata vyombo vyetu vinavyofanya kazi. Nadhani ni kama wiki mbili au tatu zimepita tumepata taarifa ya mtu aliyebambikizwa kesi na Askari, lakini upelelezi ulivyokuja kujulikana ikaonekana alibambikizwa kesi na katika mazingira ambayo imeonekana siyo *fair.* Ni lazima tuangalie mifumo yetu, ni lazima tuangalie, nasi tunatoa rai kwa mujibu wa sera za chama chetu kwamba, kupatiwa haki haitakuwa tena hisani, haki ni lazima ipatikane na ipatikane kwa wakati. Siyo tu kupatikana kwa wakati, ni lazima ionekane inatendeka.

Mheshimiwa Spika, ninamaliza kwa kusema, sisi kama Chama cha Demokrasia na Maendeleo, tunaamini amani na utulivu wa nchi yetu utapatikana katika mifumo iliyopo ikiwa inasimiwa kwa amani. Nimetoa mfano mkubwa wa Tume ya Uchaguzi, kama tuki-*temper* na Tume ya Uchaguzi; kwa mfano, tunaenda kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa, tuki-*maneuver* na chaguzi za Serikali za Mitaa tunaenda kuwasha moto ambao hatuujui.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawako tayari kuzidi kuonewa kwa sababu ukweli wanaujua, haki zao wanazijua na ukweli wanaujua.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Yaani Mheshimiwa Anatropia la maendeleo hata moja hamna, yaani wewe! *(Kicheko)*

Nilikutaja Mheshimiwa Mwalongo, utufungie pazia.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote niseme naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napende kusema kwamba, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya. Katika Jimbo la Njombe tumepata maendeleo ambayo toka dunia kuumbwa haijawahi kutokea. Nitoe mfano mmoja tu, tumepelekewa maendeleo na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika Kata ya Utalingolo katika Kijiji kijulikanacho kwa jina la Ihalula, mpaka leo nilipokuwa nafuatilia, maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni mbili, haijawahi kutokea. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejengewa zahanati mahali pale ya shilingi milioni 500, tumepelekewa vifaa vya hospitali vya zaidi ya shilingi milioni 300, lakini tumepelekewa umeme kwa thamani ya shilingi bilioni moja. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya katika nchi yetu, lakini ni pamoja na maendeleo mengine makubwa yanayofanyika ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, yako mambo ambayo tungependa sana Serikali yetu ifanye. Ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC.* Tunakushukuru sana umetuwezesha tumefanya ziara nyingi sana katika Kamati yetu. Jambo kubwa nililoliona ni tatizo kubwa la maji katika nchi, lakini ni pamoja na Jimbo la Njombe Mjini, lina tatizo kubwa la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya maji katika nchi yetu ukiiangalia imekosewa *design.* Kikubwa kinachofanyika ni kwamba, ndani ya Halmashauri husika hakuna wataalam wa maji. Halmashauri wanatafuta Mkandarasi au Msanifu wa mradi, anakuja msanifu wa mradi anasanifu mradi, baada ya kusanifu mradi anaikabidhi Halmashauri. Halmashauri inaupokea ule mradi haijui chochote. Ina Mhandisi pale naye hajui chochote. Vinaandikwa vitu ambavyo ikifika wakati wa kutekeleza mradi, mradi hautekelezeki. Hilo ndiyo tatizo kubwa katika Halmashauri zilizo nyingi ikiwemo Halmashauri yangu ya Mji wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Mji wa Njombe uko mradi unaitwa Igongwi, ni mradi wa vijiji sita kwa ajili ya maji, lakini mradi ule umesanifiwa na umeanza kutekelezwa na una *lots* kama tano au sita, lakini *lot* ya kwanza ni ya uzalishaji maji kwenye chanzo. Kwenye chanzo, kutokana na umbali na milima ilivyo, Msanifu ameweka mabomba ambayo hayawezi kufika kule. Sasa unajiuliza huyu Msanifu alifikaje kule aka-*design* mabomba mazito kiasi hicho ili yaweze kwenda kule?

Mheshimiwa Spika, nimeenda Halmashauri ya Ilemela, Mwanza, Msanifu amesanifu mradi wa maji wa kijiji uchimbwe mtaro kwenye mlima wa mawe. Matokeo yake imekuwa haiwezekani, Mkandarasi ameshindwa kufanya vile, imebidi ifanyike *variation.* Kwa hiyo, unajiuliza, hivi tuna Wahandisi wa Maji kweli katika Halmashauri zetu? Tuna wataalam wa maji kwenye nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeenda Halmashauri ya Ngara, Msanifu amesanifu tenki la maji lijengwe kwa matofali. Mkandarasi amejenga kwa mawe, tenki linavuja na kuna Mhandisi wa Halmashauri. Tumeenda Halmashauri ya Mheshimiwa Mwijage, mradi wa maji umekamilika hakuna mita inayoonesha kiasi gani cha maji kilichopo kwenye tenki. Unamwuliza Mhandisi wa Halmashauri anasema labda Mkandarasi ali-*overlook.* Sasa unajiuliza, yeye kama Mhandisi wa Halmashauri alikuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ya Maji ifanye utaratibu mpya wa kupata Wahandisi sahihi wa Maji ili kusudi Wasanifu wanaposanifu miradi ya maji, ile miradi ikifika kwenye Halmashauri, wakiiwasilisha kwenye Halmashauri Mhandisi wa Maji mwenyewe auone ule mradi ni nini kimeandikwa na nini kinatakiwa kufanyika? Vinginevyo tutalalamika matatizo ya maji, fedha itapotea, Wakandarasi watashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye miradi ya maji, pamoja na upungufu ambao upo, Wizara na yenyewe inachelewa mno kufanya marekebisho. Wakandarasi

wanaweza wakaleta taarifa kwamba hapa hili jambo halitekelezeki, lakini unaona kabisa Wizara inachukua muda mrefu sana kufanya marekebisho. Naomba sana Wizara ijitahidi kufanya marekebisho mapema ili miradi ya maji iweze kwenda.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la biashara. Katika Halmashauri ya Mji, Njombe sisi sio wafanyabiashara *per-se,* lakini sisi ni wakulima, lakini mazao yetu ndiyo hayo tunayoyafanya kuwa biashara. Nizungumzie suala la mazao ya misitu hasa mbao, miti, nguzo na majengo.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kwamba mazingira ya kufanya biashara Tanzania ni magumu, sisi wakulima wa miti Njombe tunayaona hayo. Tunayaona kwa namna ipi?

Mheshimiwa Spika, sisi zao la miti ni zao la kawaida kama yalivyo mazao mengine kama korosho, wanaolima mpunga, mtama, mbaazi, na kadhalika. Inapokuja kwenye zao la miti kumewekwa sheria na taratibu nyingi sana. Taratibu ya kwanza ambayo inachelewesha maendeleo kwa wananchi hawa, ukitaka kuvuna miti yako, baada ya kuivuna, ili usafirishe mbao kuna kitu kinaitwa *TP (Transit Pass).* Sasa kama umeshavuna na unataka kusafirisha, ile *Transit Pass* inapatikana Makao Makuu ya Halmashauri. Kwa hiyo, mwananchi anapaswa kusafiri kilometa kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuchukulie mwananchi anayetoka mwishoni kabisa mwa Jimbo la Njombe Mjini, kwa mfano Kata ya Makoo ambayo iko kilometa 70, lazima aje Njombe Mjini, akate *TP* ambayo thamani yake haizidi shilingi 3,000/= au shilingi 4,000/=, arudi kijijini akatafute usafiri asafirishe. Hiyo safari peke yake inamgharimu zaidi ya shilingi 20,000/=. Hiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ya pili, mazao haya ya misitu pamoja na kwamba jana Serikali ilizungumza hapa kwamba itaweka utaratibu rasmi, lakini mwananchi yule haruhusiwi

kusafirisha ule mzigo kutoka kule kijijini kuleta sokoni baada ya saa 12.00 jioni. Sasa ukiangalia haya ni mazingira ambayo yanachelewesha maendeleo. Wananchi wanashindwa kusafirisha mazao yao ya kawaida kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Njombe, kama Mkoa, idadi yetu tuko 700,000 tu, lakini wenye nafasi ya kuchangia maendeleo, nguvu kazi, siyo zaidi ya 400,000. Sasa ukiangalia watu 400,000 tunachangia maendeleo, tunafanya nchi iweze kupata mbao, ipate nguzo, ipate miti, lakini vilevile tunachangia chakula, tunalima mahindi kwa wingi sana, tunalima viazi kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana, idara inayohusika na mambo ya misitu iangalie upya jambo hili. Inapokuwa inazuia wananchi wasiweze kufanya biashara eti kwa sababu saa 12.00 imefika, huku ni kuchelewesha maendeleo kwa makusudi. Niombe sana sisi wenye misitu ya kupandwa turuhusiwe kufanya biashara, zao letu la miti liwe kama zao la kawaida kama vile zilivyo mbaazi, pamba, mpunga, na kadhalika ili kusudi *speed* ya maendeleo iweze kupatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mnapotuwekea mazingira ya kuweka sijui vibali, utaratibu, kama hiyo *TP* hatukatai, iwepo, lakini ikatwe kijijini, kwa sababu kule kuna Mtendaji wa Kijiji ambaye ni Mtumishi wa Serikali. Idara ya Misitu ikasimu kwamba akitokea mwananchi ana miti yake anataka kusafirisha, mkatie *TP* kuliko asafiri kilometa 70 akakate *TP* arudi kijijini akaanze kusafirisha, inafika saa 12.00 hawezi kuondoka, asubiri siku ya pili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie hilo na ilione kwamba ni jambo linalochelewesha maendeleo wakati mahali kwingine tunakwenda haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia jioni ya leo katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni suala la elimu. Elimu

yetu inapata shida, inapita wakati mgumu. Tunafanya elimu ipite wakati mgumu kwa sababu ya kutokutaka kubadilika. Kuna vitu tunavisimamia haviko sahihi.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha Shule za Kata. Shule za Kata leo zimekuwa bora sana na *performance* inaonekana kwenda kuwa juu sana. Nimekuwa nikishauri hapa na Wajumbe wengine walikuwa wakichangia hapa kwamba, katika Shule zetu hizo za Kata, tuanzishe michepuo ya ufundi. Jambo hili limekuwa gumu sana. Yaani limekuwa gumu. Kila mtu akisimama hapa anasema *VETA,* Serikali yenyewe ikisimama inasema *VETA;* lakini hizo *VETA* ukiangalia jinsi zilivyo, zitaweza kuchukua watoto wote hawa wanaohitimu Kidato cha Nne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ugumu wa kubadilisha shule angalau moja kila Halmashauri kuwa Shule ya Ufundi. Naomba sasa Serikali ilione hilo na iweze kusaidia hawa vijana. Vijana hawa wakipata Elimu ya Ufundi tutakuwa tumewasaidia, tutakuwa tumewapa ajira na tumewapa ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nina mashaka nalo sana, miaka ya nyuma wakati tuna Shule za Ufundi kama *Ifunda Tech, Moshi Tech, Tanga Tech, Mtwara Tech,* Ihungo na nyinginezo, kulikuwa na Chuo kinaitwa *Dar es Salaam Technical College,* lakini kilikuwa kinatoa Diploma ya Ualimu wa Ufundi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hilo la Sekondari za Ufundi inabidi liangaliwe vizuri, tusije tukaishia kutoa mafundi mchundo.

Hata zile *Ifunda Tech* na nini zilikuwa zinawaanda vijana kwenda *Dar Tech, Arusha Tech, Mbeya Tech,* vitu vya namna hiyo. Yaani ile ilikuwa ni *transit,* haikuwa kwamba ukimaliza pale sasa unafungua *garage* wewe mwenyewe, *unless* ujiendeleze tena kidogo.

Kwa hiyo, umuhimu wa *VETA* kila Wilaya na kadhalika bado uko pale pale ili vijana wetu siyo tu wachemshwe chemshwe hivi, wapate ufundi wa kweli kweli. Ufundi wenyewe tunashauri sana Serikali, huu mtindo wa sasa wa kumfundisha mtu anakuwa seremala peke yake, yaani anajua umeme tu, seremala tu, fundi bomba tu, fundi kujenga tu, kidogo umepitwa na wakati.

Safari moja nilikuwa naongea na rafiki yangu, Balozi wetu wa China, akaniambia kulikuwa na nyumba fulani pale kwenye eneo lao la Ubalozi wakataka kubadilisha makochi, yalikuwa yamechakaa kidogo, kupata sura mpya. Wakampata kijana. Alipokuja katika muda wa saa chache tu akawa ameshafanya ile kazi ya kurekebisha yale makochi kuweka ngozi mpya au hivyo, nafikiri mnanielewa.

Alipomaliza wakamwambia hebu tutafutie kijana mwenzako kuna mabomba fulani yana shida ya maji kwenye hii nyumba tunataka turekebishe. Akawaambia aah, hiyo mimi naweza kufanya. Akaya-*check* akawaambia kifaa hiki na hiki na hiki, wakamletea, aka-*fix* mabomba. Wakamwambia, lakini kuna *line* za umeme zinasumbua hapa na taa nyingine haziwaki, nini na nini, akawaambia haina shida ngoja niangalie, nunueni hiki na hiki na hiki, aka-*fix*. Mwisho kabisa, kuna mmoja akawa na simu yake sijui ina shida gani, akamwambia lete, akachukua kitambaa akaweka, kafungua cha, cha, cha, simu yako hii hapa nzuri. Huyo ndio fundi tunayemtaka. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, haya mawazo ya sekondari, nini haya, tuondokane nayo. Yaani vijana wetu waende *VETA* wafundishwe tena *diverse,* yaani akitoka pale yeye ni fundi wa vitu vitatu, vinne, vitano. Hawezi kukosa ajira huyo. Kuliko yeye anasubiri mbao tu. Yaani akiona umeme, haelewi kitu;

akiona sijui bomba limefanyaje, hajui aanzie wapi, na kadhalika.

Vile vile na Walimu. Tuna Walimu wanafundisha sijui Kiswahili na Historia, basi. Kwa nini? Wakati Sekondari unasoma masomo saba, kwa nini usiweze kufundisha masomo matano Mwalimu mmoja? Eeh! Unafundisha Hesabu, *Biology*, *Physics,* na kadhalika. Inawezekana, wenzetu wanafanya hivyo. Kwa hiyo, unaweza ukawa na Walimu kiasi fulani, siyo kikubwa kiasi hicho, lakini sasa sisi lazima uwe na Walimu wengi. Uajiri wengi, maana kila mtu anajua vitu viwili, kimoja; nani kasema hiyo ndiyo *correct?* Tu-*diversify* kwenye vyuo vyetu, tutoe watu ambao wanajua mambo mengi zaidi. *(Makofi)*

Napiga michapo kidogo kwa sababu nilikuwa na dakika mbili, tatu. *Otherwise* leo ndiyo tumeanza, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuanzishia na ninawashukuru wote kwa mjadala mzuri, *informative,* ambao ni msingi sasa wa mijadala inayofuata. Ningeshauri sana tuendelee kuisaidia Serikali, tuchangie vizuri, tuwakosoe, tuwasifie pale walipofanya vizuri, tuwaoneshe njia pale ambapo wenzetu wamepotea kidogo.

Sizuii kumlaumu Mheshimiwa Waziri wala nini, wala siko katika eneo hilo, lakini lazima kujua saikolojia ya binadamu. Binadamu yeyote yule ukishaanza kwa kumlaumu, wewe Bwana Bobali wewe Wizara yako wewe hufai kabisa, kawaida ya binadamu anafunga masikio na akili yake, yaani anafunga nge! Ndiyo hakusikilizi kabisa! Nawe umekuja hapa na shida za wananchi.

Kwa hiyo, lazima u-*balance,* kama kuna kizuri amefanya, unamwambia kuna mazuri moja, mbili, tatu unafanya. Ahaa, kumbe, lakini kuna maeneo mawili hivi wewe bwana wewe, atachukua kalamu yake utamwona anasubiri aone maeneo gani a-*improve.* Tukienda na ile *methodology* ile, ile imepitwa na wakati, ndiyo hiyo ku-*diversify* kidogo ili mambo ya wananchi wako yaweze kufika vizuri na salama. *(Makofi)*

Basi ndugu zangu nawashukuru tena tumeanza vizuri, tutaendelea kesho Saa 3.00 asubuhi. Naomba niahirishe shughuli za Bunge sasa.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*